# Velten, Safari za Wasuaheli

# Safari za Wasuaḥeli

von

**Dr. C. Velten,**
Lehrer des Suaheli
am Seminar für Orientalische Sprachen.

Göttingen.
Vandenhoeck & Ruprecht.
1901.

LOAN STACK

Eine deutsche Uebersetzung erscheint gleichzeitig im gleichen Verlage. Preis gebunden 5 Mk.

PL8704
A2V39

Seiner Königlichen Hoheit

dem

**Grossherzog Friedrich von Baden**

mit allerhöchster Genehmigung

in tiefster Ehrerbietung gewidmet

vom Verfasser.

508

# Vorwort.

Die Suaheli-Litteratur steht noch in ihren Anfängen. Wir besitzen in den „Swahili tales“ von Steere, den Erzählungen in Dr. Büttner's „Anthologie aus der Suaheli-Litteratur“ und den „Märchen und Erzählungen“ vom Herausgeber dieser Reiseschilderungen eine Anzahl guter Prosatexte, während von der Poesie, die im Lande der Suaheli sehr gepflegt wird, nur Weniges uns bis dahin überliefert worden ist. Jede Bereicherung der Suaheli-Litteratur kann uns daher nur willkommen sein.

Afrikanische Reiseschilderungen von Europäern sind in stattlicher Zahl vorhanden. Von den Eingeborenen selbst besitzen wir noch keine. Um so interessanter dürfte es sein, auch einmal die Afrikaner selbst als die besten Kenner ihres Landes über das Reisen daselbst und die Sitten und Gebräuche der verschiedenen Stämme zu hören. Besonders schwierig ist es nicht, den Suaheli zum Erzählen zu bewegen, sobald er einmal Vertrauen zum Europäer gewonnen hat, und die meisten von ihnen besitzen ein gutes Erzählertalent.

Den Anlass zur Aufzeichnung und Sammlung dieser Reiseschilderungen gab mir der Erzähler der ersten, nämlich Sleman bin Mwenyi Tshande. Im Jahre 1893 lernte ich ihn zufällig in Daressalam kennen und gewann bald Gefallen an seinen lebhaften und interessanten Erzählungen, die hauptsächlich seine einige Jahre vorher gemachten Reisen ins Innere Ost-

Velten, Safari za Wasuaheli

und macht uns mit den Sitten und Gebräuchen der Wazaramu auf's genaueste bekannt.

Die letzte Reiseschilderung verdanken wir wiederum Selim bin Abakari. Er begleitete Dr. Bumiller auf dieser Reise nach Russland und Sibirien im Jahre 1896. Die ganze Erzählung deutet auf den mit europäischen Verhältnissen nunmehr vertrauten Afrikaner hin, dessen grosse Beobachtungsgabe jeden Europäer in Staunen setzen muss.

Sprachlich sind die Berichte von Mtoro bin Mwenyi Bakari die besten. Er hat sie erst nach reiflicher Ueberlegung und allmählich niedergeschrieben. Alle übrigen Schilderungen sind mit Ausnahme der von Abdallah bin Rashid im Erzählerton gehalten und von mir nach dem Dictat der Erzähler niedergeschrieben worden.

Was die Schreibweise des Suaheli anbelangt, so verweise ich auf die Einleitung zu meinen „Märchen und Erzählungen der Suaheli" Band XVIII der Lehrbücher des Orientalischen Seminars. Die Interpunktion habe ich, um auch dem Anfänger im Suaheli das Lesen des Textes zu ermöglichen, so gestaltet, dass er sich mit Leichtigkeit in der Construction der Sätze zurechtfinden kann.

Berlin im August 1901.

**Dr. C. Velten.**

# Safari yangu ya barra Afrika

ya

**Slēmān bin Mwenyi Tshande bin Mwenyi Ḥamisi esh-Shirazi.**

Áuwali safari yangu ya barra nimekopa mali kwa Mhindi. akanambia: „vema, utapata mali, tafuta wapagazi". nikenda kambini kutafuta wapagazi, nikapata wapagazi mia na wanyampara watano. nikarudi kwa Mhindi, nikamwambia: „hawa wapagazi nimepata, haya funga mali sasa". nikafunga mali thenaʿshara mia, nikawapa wapagazi upagazi wao, kulla mpagazi jora sitta na nguo tano rangi, wakaniuliza: „ʿáhadi yetu tutapeleka ḥatta wapi mizigo"? nikawambia: „ʿáhadi yangu Tabora".

siku ya kuondoka nikamwambia kirongozi wangu: „haya kirongozi, toa safari, peleka shamba". tukenda ḥatta shambani, tukalala pale. aṣ-ṣubuḥi siku ya pili tumekwenda mtoni Ruvu, tukamwita mwenyi mitumbwi, tukamwambia: „haya, lete mitumbwi tuvushe mizigo yetu". tukapakia mizigo katika mitumbwi, tukavuka wote pia wapagazi na wanyampara na tájiri.

tulipotoka Ruvu, tulikwenda Bigiro kambi moja. tulipofika nikawambia wapagazi: „haya, Wanyamuesi, pangeni mizigo". wakaleta mizigo wakaipanga maḥali pamoja. nikawambia tenna: „haya, jengeni ḥema; haya,

wanyampara, twaeni nguo, mukahemere vyakula. haya wengine wapagazi jengeni boma, hapa pana wevi wengi".

siku ya pili tumekwenda Viranzi, ya tatu tukenda Kengeni, pana ziwa kubwa la maji, ndipo kambi ya tatu. kambi ya nne tumekwenda Mbuyuni kwa Wakwere. mkubwa wa Kikwere Mwene Mtaimbo. tulipofika, nikatoa nguo tatu, nikampa ḥéshima yake. naye akatoa unga chakula na kuku kitoweo, chakula cha tájiri ya msafara. na yule Mwene Mtaimbo mtu mbaya sana. maneno yake mengi kama mtu mwenyi wazimu.

tukatoka hapa Mtaimbo, tukaenda Mbiki. pana mto mkubwa wa maji hapo Mbiki. na mkubwa wa mji wa Mbiki jina lake Sādi, huyu mtu mzuri. tukampa nguo mbili, akatupa unga na mpunga na kuku. tumetoka kwa Sādi, tukaenda Sagati porini. hapana mtu wala hapana nyumba. tukalala porini.

tulipoondoka tukenda Msua, na mkubwa wa mji Msua Tshamulungu, qabila yake Mkwere. na mkubwa wa pili Tongo, ndio wakubwa wa mji ule wa Msua. tukatoa gharama nguo mbili hongo.

kutoka Msua tulikwenda Kisemu, uko mji, na mkubwa wa mji jina lake Kibarrabarra. tukatoa gharama nguo tatu, tukampa, naye akatupa chakula unga na kuku.

tukatoka Kisemu, tukenda Rungerengere. na mkubwa wa Rungerengere Masʿūdi. tukajenga boma kwa ḥáḍari ya simba, sababu simba Rungerengere wakali sana kulla mwaka. ḥatta usiku tulipolala, wakaja simba, wakakamata watu wawili wapagazi. tukaamka wote kwa makelele yao, tukawafuata simba, tukapiga bunduqi, tusiwapate.

aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukenda Yangeyange. na mkubwa wa Yangeyange Magembe. tulipoqaribia akasema: „nipeni hongo, kama hamkutoa hongo, ntafanya vita, niwanyanganye mali yenu yote pia". tukatoa nguo kumi

hongo, tukampa, akakataa. na sisi tukakataa vilevile kumpa záyidi. akaleta vita, tukapigana naye. wakaua watu wawili kwetu, wakachukua mizigo miwili ya biḍa'a, na sisi tukaua watu watatu kwake.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukenda Mikesse. na mkubwa wa mji wa Mikesse Matitu. akatwambia: „nileteni hongo, mali mengi nataka". tukatoa nguo khamso u 'asherīn, tukampa. naye mtu mbaya sana, maneno yake ya ukali.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaondoka, tukenda ḥatta Mrogoro kwa Simba Mwene. akatwambia: „leteni hongo, ndipo mpate rukhṣa ya kuhemera vyakula". tukatoa nguo arba'īn, tukampa, akatwambia: „sasa rukhṣa kutafuta vyakula mpate kula".

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda Viranzi. na mkubwa wa Viranzi Libega. tukampa hongo nguo sitta. na usiku ule tulipolala, akaja fissi, akamkamata Munyamuesi, akaondoa pua yake. aṣ-ṣubuḥi ya pili tukafika Mkata, mto mkubwa, mamba wengi na viboko vingi wako. na mkubwa wa Mkata jina lake Kigongo. tumempa hongo lake nguo tatu. na siku ile alitoka mwanamke moja, anakwenda kuteka maji katika mto ule wa Mkata, akakamatwa na mamba. tukenda mbio kumkamata, hatukumpata, mamba amemchukua.

tukaondoka tenna tukenda Mgomberenga. na mkubwa wa Mgomberenga jina lake Waziri. maji hapo yako mbali sana, yapata záyidi ya sa'a mbili kunako maji. na siku ile mpagazi mmoja akaugua. wanyampara wakasema: „na tushinde hapa leo". lakini mimi nikakataa kushinda, kwa sababu maji yako mbali sana. tukaondoka tukenda Mkondoa. na mkubwa wa Mkondoa Sēfu bin Slēmāni bin Juma' Reami. tumefika pale pa Sēfu, akatufanzia ḥéshima kama tuko pwani. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda kwa Mwinyi Msagara. tukampa nguo

kumi na tano hongo lake, naye akatupa ñgombe mkubwa sana. siku ya pili tukashinda kwa Mwinyi Msagara — ḥatta mchana wakaja Wahehe, wakapiga mji wa pili qaribu na Mwinyi Msagara, marra wakenda zao na mali waliyoteka.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda Kilossa. hapo hapana kutoa hongo. hapo twalilala, aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukapanda kilima kikubwa sana, yapata sa'a sitta ḥatta kwisha kilima. tukenda ḥatta Kidete porini, hapana nyumba wala watu. aṣ-ṣubuḥi tukaondoka tukenda Tubugwe, pana mto mkubwa sana. kufika kupanga mizigo yetu, tukajenga na ḥema, mpagazi moja akenda akeba mahindi na maboga. wakamkamata wenyi maboga, wakamfunga, wakamleta ḥatta kambini. tukatoa nguo mbili, tukawapa, maneno yamekwisha.

siku ya pili tukafika Mpāpua. tukataka kujenga ḥema yetu, sulṭani akasema mwenyewe: „marufuqu, hakuna kujenga“. tukamwuliza: „kwa nini hakuna kujenga?“ akasema: „mpaka mhonge, ndio mpate kujenga“. tukatoa nguo settin, tukampa sulṭani, akasema: „rukhṣa sasa, jengeni“. tukalala, ḥatta usiku akaja mwevi, akaingia ndani ya ḥema, akeba sufuria moja. tulipoondoka usingizini, wakamkutia watu mwevi huyu, wengine wakampiga riṣaṣi. yule mwevi akafa. ḥatta aṣ-ṣubuḥi maneno yakenda kwa sulṭani. akafanya ḥokumu yake sulṭani kawambia: „huyu amekwenda kwiba usiku kwa wangwana, amepigwa — bassi — hapana maneno“. ndivo alivowambia watu wake.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda mpaka mji wa Kambi. pana vilima vingi, na chini ya kilima pana maji ya chumvi. khalafu tukaingia ndani ya pori la Chunyu, pori kubwa sana. tukakaa mle siku tatu, hatujapata mji. siku ya nne tukafika Kinyazungu. na mkubwa wa Kinyazungu Nyagaru. hiyo ndiyo mwanzo

wa Ugogo. huyu Nyagaru akaleta wanyampara wake kambini, wakatwambia: „mbūkūa [1]), wangwana"? tukatikia: „mbūkūani [2])"? tukawauliza: „mkasaka chichi [3])"?. wakatujibu: „tukasaka mahongo ya mtemi [4]), sulṭani wetu". wakasema: „mumpele mienda, ni kusaka magana matatu" [5]). na sisi tukawajibu: „magana matatu nyingi". wakajibu: „mumpele tauli [6])"? tukawambia: „tutawapa igana" [7]). wakakataa, wakasema: „iaye miangu [8])". baʿada tukawapa nguo igana na khamsīni, wakatwambia: „maneno yote sasa yamekwisha". wakatuletea mawele [9]), tukapokea.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda Msanga, na sulṭani wa Msanga jina lake Mabokera. akaleta munyampara wake kambini, akatwambia: „leteni hongo langu". khalafu tukatoa nguo mitēni na ʿesherīn, tukazipeleka kwa sulṭani, maʿana ndio lázima, sababu tupate maji na chakula. sulṭani akatwambia: „nguo hizi kidogo, nataka mkatoe na ningine kama hizi". tukatoa jumla nguo arbaʿ mia u arbaʿīn, tukapeleka watu kwake, tukataka maji na chakula. akatunyima chakula, akasema „hapana".

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu Madako. na mkubwa wa Madako jina lake Tshayaya. tukapeleka nguo mia na tano hongo lake, tukanunua maji ya kunywa kwa nguo ʿesherīn, sababu hapana maji kabisa.

hapa tukasikia khabari ya simba. kulikuwa na simba, killa siku hukamata watu. siku qabla ya kufika kwetu wakaondoka watu wengi kwenenda kumvizia ku-

---

1) wie geht's? — 2) wie geht's euch? — 3) was sucht ihr? 4) Häuptling. — 5) Gebt ihm Stoffe, er will 300 Tücher haben. — 6) Wieviel wollt ihr ihm geben? — 7) Hundert. — 8) Nein, meine Freunde. — 9) Hirsenart.

taka kumwua. walipofika katika mwitu, wakamwona yule simba, sababu hakwenda mbali na mwanamke yule aliyomkamata jana. wakajigawa wale watu, mmoja akampiga yule simba, lakini risasi haikumpata sana. marra simba akamrukia. na huyu mwenziwe alipomwona amekamatwa na simba, naye akataka kumpiga yule simba, risasi isimpate simba, akampiga mwenziwe. simba alipomwona yule hana nguvu, akamwacha, akamrukia yule aliyopiga bunduqi. naye alipokamatwa, akapiga kelele nyingi. yule mwenziwe wa tatu alipomwona mwenziwe anapiga kelele kwa ghadabu za simba, naye akapiga bunduqi yake, isimpate simba, ikamfikia yule mwenziwe, aliyokamatwa na simba. yule ikawa amelia kelele nyingi sana, simba akamwacha akenda mbio. na yule akafa, na mwingine alikuwa na majeraha, baʿada ya saʿa haba akafa vilevile, na simba amekimbia.

as-subuhi tukenda zetu mpaka Ungomvia. na mkubwa wa Ungomvia jina lake Mabokera. tumetoa nguo mitēn na khamsīn mahongo yake. hatta el-ʿasiri wakaja Wamassai, wakawapiga wenyewe Wagogo, wakachukua n̄gombe zote za Wagogo, wakenda zao mbio kama walivokuja. na sisi hatukulala kwa kuogopa Wamassai, kwa sababu tumechukua mali mengi. hatta as-subuhi tukenda zetu Mtoni Bubu, hapana nyumba wala mtu — porini. tukajenga boma kubwa sana kwa kuogopa Wamassai.

siku ya pili tukafika Unyangwira. sultani wa Unyangwira jina lake Makenge, mzee sana. akatwambia: „nileteni mahongo“. tukatoa nguo sitta mia, tukampelekea. akatwambia: „kesho hapana rukhsa kuondoka wangwana“. tukamwambia: „kwa nini kutuzuia, na mahongo tumekupa? sababu gani?“ akasema: „nataka mjenge boma langu“. tukamwambia: „tumekuwa watumwa wako“? akasema: „bassi hamjui kama watumwa

wangu? mimi si sawasawa kama na sulṭani wenu wa Unguja?“ tukamwambia: „hewallah, tutajenga“. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka na mashoka yetu kwenda 'kukata miti ya boma. tukenda tukakata, ḥatta el-ʿaṣiri tukarudi. siku ya pili na siku ya tatu tukajenga boma, kwa siku ya nne tukapata rukhṣa, tukenda zetu ḥatta Mtiwe. na sulṭani mwanawe yeye Makenge. tukatoa nguo mia mahongo yake.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu Kilimatinde. na mkubwa wa Kilimatinde Massomoka. akatwambia: „wangwana, toeni nguo elfu mahongo yangu, ndipo mpate rukhṣa ya kuondoka“. tukakataa, tukatoa nguo khamso mia, tu kampelekea. akasema: „shurṭi mnipe ṣanṭūr [1]). tukamwambia: „hatuna ṣanṭūr“. akasema: „kama ṣanṭūr hapana, mnipe vitambi bora ʿesherīn“. tukampa.

tukaondoka aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu ḥatta Muhalala. huu ndio mwisho wa Ugogo. na yule sulṭani wa Muhalala mwanawe huyu Makenge. tukatoa nguo thalatha mia na arbaʿīn, tukampa mahongo yake. siku ya pili tukafika Mabunguru Mtoni, hapana nyumba wala mtu — porini. siku ya tatu tukenda Mwale. na huyo mkubwa wa mji jina lake Kilunda. ametaka mahongo, lakini sisi tumemnyima, hatukumpa. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukafika Jiwe la Singa, na sulṭani wa Jiwe la Singa jina lake Wamba. tukatoa nguo mitēn mahongo yake.

tukaondoka tukenda Malwa. qábula hatujapanga, tukakuta Warugaruga, wanatoka kwake yeye Wamba. zile nguo tumempa, hazikutosha, ataka kuja kunyanganya. tukapigana nao, tukaua watu sitta, hawakupata kitu kutwaa. tukateleka, lakini hatukulala pale, tukenda tukalala Malwa Madogo porini.

aṣ-ṣubuḥi tukafika Mgunda Mkali porini, siku ya

1) Spieluhr.

pili tukenda Bimbisanda, na siku ya tatu tukenda Tshaya porini. pana ziwa kubwa la maji na mamba wengi na viboko vingi. wakaja Warugaruga, wanatoka kwa sulṭani Nyungu ya Mawe. tukapigana nao siku tatu. wakachukua mitumba ya nguo sitta, wakachukua mizigo ya baruti miwili, wakaua na waungwana watatu kwetu, wakenda zao.

tulipotoka pale tukafika Tula, sulṭani jina lake Maganga. hapo hatukutoa mahongo, tumekataa sababu yeye sulṭani mdogo, hana nguvu. tukaondoka tenna kwenda Ziwani Nyahua porini. siku ya pili tukenda Lubuga, na mkubwa wa Lubuga jina lake Nsilatali. hatukuhonga kitu. siku ya tatu tukafika Kigwa, na mkubwa wa Kigwa jina lake Mabokera. siku ya nne tukenda ḥatta mtoni Wala. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda Kwihala. na mkubwa wa mji huu jina lake Kasui. mji huo ndio mwanzo wa Unyanyembe.

tukapumzika pale, ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaingia Tabora. áuwali Tabora Kanyenye, mji wa Mwʻarabu, jina lake Muhina bin Slēmāni Leʻúrubi pamoja na Saʻīdi bin ʻOthmāni. na mji wa pili unakwitwa Bahareni, wa Mwʻarabu, na mwenyewe jina lake Saʻīdi bin ʻAli. mji wa tatu unakwitwa Lufita, mwenyewe Saʻīdi bin Sālum pamoja na Mwenyi Mlenda, mtu wa mrima. mji wa nne unakwitwa Mkowani. mwenyewe Mwʻarabu Saʻidi bin Ḥabibu el-ʻAfīf. na mji wa tano unakwitwa Bomani, wa Mwʻarabu, jina lake Seti bin Jumaʻ. na mji wa sitta unakwitwa Mbugani, na Mwʻarabu mwenyewe Sālum binʻAli. na mji wa sabaʻ Tshemtshem, mwenyewe Mhindi na jina lake Jumaʻ bin Dina. na mji wa nane unakwitwa N̄gambo, wa Mwʻarabu, na jina lake Muḥammed bin Naṣur. na mji wa kenda unakwitwa Mbirani, mwenyewe Mwʻarabu ʻAli bin Sulṭani. na mji wa kumi jina lake Malolo, wa Mwʻarabu, mwenyewe Rashid

bin Sālum. na mji wa kumi na moja unakwitwa Kwihara, mwenyewe Mw'arabu, na jina lake 'Abdallah bin Nasibu. na mji wa kumi na mbili unakwitwa Gange, mwenyewe Mw'arabu, na jina lake Thāni bin 'Abdallah. na mji wa kumi na tatu unakwitwa Miemba, mwenyewe mtumwa wa Mw'arabu, anakwitwa Farḥani bin 'Othmani. na mji mwingine unakwitwa Ituru, wa Mw'arabu, mwenyewe Moḥammadi bin Juma', baba ya Tipu Tip (Ḥammed bin Moḥammadi), na ndugu yake Moḥammed bin Sa'īd el-Wardi.

Wa'arabu kwanza walikaa mrima wote. khalafu wamekopa mali kwa Wahindi, wakala mali yote pia, ndio wamekwenda zao Tabora, wakenda wakajenga miji, wakanunua watumwa, wakalima. wengine wamekwenda kana mkuu wa msafara wa Wahindi, wakachukua feḍḍa ya Mhindi, wakakaa Tabora, wakamsahau Mhindi na mali yake kabisa. kazi yao khalafu kulima mpunga na ngano kule Tabora.

khalafu Wahindi wakashitaki kwa Seyyid Barghash. Seyyid akapeleka luwali, jina lake Sa'idi bin Sālum el-Lemki. akenda akamwambia, kawakamate Wa'arabu, watoe mali ya Wahindi, kwa sababu wenyewe Wahindi wakafanya makelele sana. alipokwenda luwali, akawambia Wa'arabu: „toeni mali ya Wahindi" — wakamwambia: „hatuna kitu sisi kabisa". wakamfanzia ḥéshima kubwa sana, kulla mmoja akampa kitu, akazidi kukaa luwali, akastareḥe.

khalafu ndio imekuja vita na sulṭani Mirambo kuja kupiga Tabora. luwali akapeleka barua kwa Seyyid Barghash, na Seyyid akamjibu akamwambia: „pigana naye mshenzi, baruti na bunduqi na riṣaṣi kwangu". ḥatta wamepigana vita vya Mirambo sana, wameuawa Wa'arabu wengi sana, ḥatta na sulṭani wa Tabora amekufa, jina lake Mkassiwa. ba'ada ya kufa kwake

Mkassiwa Wa'arabu wakaona: „tu pekeyetu, tutafanyaje sasa? na tumweke Silanda katika usulṭani wa Tabora!“ na mwenyewe akasema: „jina langu ndio Issike“ [1]).

khalafu ndio ameleta vita tenna Nyungu ya Mawe. anatoka kwenda inchi yake Kiwere, maqṣudi kunyanganya usulṭani Issike. Wa'arabu wakasimama wakapigana sana ḥatta wakamfukuza Nyungu ya Mawe. akenda kwake, wakakaa kitako Wa'arabu pamoja na Issike wao.

khalafu amepanda Amiri Pasha [2]) pamoja na amri ya jerman [3]). akafika kwa Issike, akamwambia Issike: „lete mizinga yetu sisi na viasi vyetu, ndipo tufanye udugu“. ma'ana Issike amevitwaa vitu hivo kwa misafara ya Mabeljiki [4]) na ya Madeutschi. Issike akakataa, akakusanya 'askari wake wengi sana, akenda akapeleka vyakula vingi sana na ñgombe wengi sana na mbuzi wengi sana. Amiri Pasha akasema: „sitaki chakula chako, tunataka mali yetu, utuletee, pamoja na huu mlingote wa Séyyidi, tutundikie bendera ya jerman“. mlingote akampa, walakini mzinga na viasi hakumpa. khalafu Amiri Pasha akenda zake.

nyuma ya Amiri Pasha akaja bwana Prinzi, akapigana naye Issike ḥatta akamwua na watoto wake, na 'askari wakamwagika wote, na watu wake wakatawanyika wote.

ndio tenna Wa'arabu nguvu zao zikawa ndogo, sasa wako chini ya miguu ya jerman. wengine wamekwenda Manyema, wengine wakaenda Uganda, wengine wakaenda Ruemba, wengine wakashuka pwani. wako mojamoja sasa, hawajui la kufanyiza. ile stareḥe yao

---

1) Issike hiess dieser Sultan richtig, nicht Sikki. — 2) Emin Pascha. — 3) engl. german. — 4) Belgier.

ya Tabora imeondoka. wanatafuta chakula, wale washibe — hawapati, sababu wale washenzi hawalimi kwao kama kwanza. hulima kidogo cha kutoshea wao, ndio sababu chakula kidogo na yote ghali.

tangu tulipowáṣili Tabora, tumekaa miezi miwili, kwa sababu ya kutafuta wapagazi wengine. ḥatta tulipowapata wapagazi, umekuwa mwezi wa tatu. na kulla Munyamuesi upagazi wake nguo kumi. ḥatta siku moja tukaondoka, tukenda zetu na safari yetu ḥatta kwa sulṭani Mtimsi. siku ya pili tukafika mji wa Kassekera. na huyu mkubwa wa Kassekera jina lake Mayole. siku ya tatu tukaondoka tukenda zetu Talikwa. na huyu mkubwa wa Talikwa jina lake Mualabu, Munyamuesi. tukalala usiku akaja mwevi kambini, lakini hakupata kitu. tukampigia kelele, akenda mbio.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukafika mji wa Kuigunda, sulṭani wa Ugunda, na jina lake Ndisha. tukatoa nguo saba'īn, tukampa mahongo yake, akasema: „nguo hizi kidogo, kama hamtanipa nguo nyingi, hamtapata rukhuṣu ya kanunua vyakula kwenu ninyi na watu wenu“. ḥatta tulipotoa nguo themanīn mahongo yake, akapokea, lakini yeye hakutupa kitu, ametupa kuku moja na viazi kidogo. bassi ndio kitu alichotupa.

ba'ada ya kulala tukaondoka tukenda Issimbiri. na mkubwa wa Issimbiri jina lake Sigimbi, mtu wake yeye Ndisha. siku ya pili tukafika mpaka Kakoma, mji wake yeye Ndisha. siku ya tatu tukenda Kinywa Simba, vilevile mji wake yeye Ndisha. na siku ya nne tukafika Kassinde, sawasawa mji make Ndisha. huu ndio mwisho wa inchi yake Ndisha.

tulipotoka inchi ya Ndisha, tukenda mto wa Ugala, mto mkubwa sana, lakini porini, hapana nyumba wala mtu. tukakata miti, tukaweka ndani ya mto, ndivyo

tukapata kuvuka. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaingia auwali inchi ya Ugala. na sulṭani wa inchi ya Ugala anakwitwa Kassagura. tukatoa nguo kumi na tauo, tukampa, ndio mahongo yake. naye hakutupa kitu, ametupa asali kidogo ya nyuki ndani ya kibuyu.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaingia tenna mji wa pili wa Ugala, wake yeye Kassagura. yuko mkubwa wa mji ule, jina lake Mwana Mlimka, alikuwa anamwia mpagazi wetu. tulipoingia mjini akamkamata, qábula hatujapata chakula wala maji ya kunywa. tukaqaṣirika sana sisi waungwana. kwa nini akatuonea sana mshenzi huyu? hatupigani naye? wengine wakasema: „haifai kupigana naye, wacheni tufanye maneno taratibu“. tukakaa ḥatta usiku, yule mpagazi akatoroka, sababu hana mali ya kumlipa.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi mshenzi akaleta maneno kwetu sisi: „waungwana, mmepoteza mtu wangu, sasa mali mtalipa ninyi?“ na sisi tukamwambia: „mali yako qiäsi gani tutakulipa?“ akasema: „mali yangu nguo saba‘“. tukamwambia: „vema“. tukatoa nguo saba‘, tukampa. khalafu tukamwambia: „siku ya pili usifanye hivi. mtu hajafika mjini — marra na kumkamata? jana umefanya vibaya sana. kuwa watu wabaya — tungalipigana nawe, walakini sisi hatutaki kelele. sasa mali yako imewáṣili“. akasema: „mimi ni raḍi, mali yangu imefika“.

tulipopumzika, tukaondoka tukenda zetu mpaka Ukalala, pia inchi ya Ugala, na mkubwa wa inchi ile jina lake Mweru Mpambara. akasema: „nipeni mahongo“. tukamwambia: „vema, tutakupa aṣ-ṣubuḥi“. ḥatta usiku tukatoroka, sababu mali yamekwisha kwa mahongo. tukaenda usiku kucha ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukafika mtoni Mtambo. huu ndio mwisho wa inchi ya Ugala.

katika safari yetu tukafika Ussauwira. na mkubwa wa inchi ya Ussauwira jina lake Simba. tulipofika, akapiga ngoma. tukamwuliza: „ngoma hizi za nini, sulṭani?“ akasema: „mke wangu amekufa“. bassi wale wapagazi wetu wakafanya oga kwa zile ngoma alizopiga sulṭani. wakatoroka Wanyamuesi saba', wakatwachia mizigo. tukamwuliza: „sasa mkeo amekufa — wataka nini?“ akasema: „mnipe sanda ya kuzikia mke wangu“. tukamwuliza: „sanda qiasi gani?“ asema: „kama mtakavyo wenyewe kunipa, mimi ntaqubali“. tukampa nguo mbili. akenda akazika.

ḥatta usiku tukamwambia: „sulṭani, watu wetu wamepotea, utatupa wengine, wachukue mizigo yetu?“ naye akatujibu: „laleni ḥatta aṣ-ṣubuḥi, mkesha honga — ndio tutatengeneza maneno ya wapagazi.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukapeleka nguo khamsīn, akasema: „hii kitu gani?“ tukamwambia: „ndilo hongo lako“. akatwambia: „mnasema kweli ao mnasema ḍiḥaka? mimi bado nna kilio cha mke wangu, na ninyi mnanambia uwongo? mimi nataka nguo elfu mahongo yangu, ndipo mpate rukhuṣa kwenda zenu“. tukamwambia: „unataka mahongo ao unatunyanganya?“ asema: „kama nataka kuwanyanganya, nisingaliwanyanganya[1]) toka jana?“ wakaja wanyampara wake, wakasema: „bassi ninyi wangwana hamtoi mahongo ya kweli? tukamsikiliza sulṭani maneno yake, walakini mnatoa nguo khamsini, mnafanya mchezo, mnasahau — huyu si sulṭani?“ tukatoa nguo mitēni, tukampa mahongo yake. akatwambia: „nimequbali; sasa moto umeḥaribika, kwa sababu ya huyu mke wangu

1) nisingalinyanganya, usingalny., asingaliny. kommt neben der Form singaliny. hungaliny. hangaliny. vor und zwar scheint erstere Form beliebter zu sein als letztere.

amekufa, bassi, hamnipi kidogo, nikafanzia dawa, nikapata kufanya moto mwingine? waqati wa kurudi hamtaki kupika ninyi? huu si mji wenu?“ tukamwambia: „vema, sulṭani“. tukatoa nguo tatu, tukamwambia: „hizi, upate kufanzia moto mwingine.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda Ussense. na mkubwa wa Ussense jina lake Kalimba. akatwambia: „waungwana, Tabora kwema? luwali hajambo?“ tukamwambia: „hajambo“. „Issike amepigana na Jerman sababu nini?“ tukamwambia: „sababu — Issike amejifanya sulṭani, naye si sulṭani. ataka kushindana na Jerman, atamweza wapi? Jerman baruti kwake tele, mizinga kwake ṭayyari, bassi huyu mtu wa kuwezekana?“ akasema: „sisi watumwa wa Jerman, kwa sababu hatuna nguvu. bassi ndugu zangu hamtaki kunipa ʿada kidogo, kwa sababu mimi sitaki mahongo kama wenzangu. nitake mahongo, anisikie bwana mkubwa aje nipige? mkanipa kidogo, ijapokuwa kidogo sana — chanitosha“. tukampa nguo ʿasherīn. tukaona ḥéshima yake kubwa sana, ametuḥeshimu sisi ḥatta bwana mkubwa, kwa sababu anamwogopa bwana mkubwa qábula hajaenda kwake.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu mpaka Gongwe. na mkubwa wa Gongwe jina lake Kakamba. na sisi ametufanzia ḥéshima kubwa, ametupa vyakula vingi na kitoweo, akatupa samaki. naye hakutaka mahongo kwetu, tumempa kwa ḥéshima kwetu nguo ʿasherīn. hio ndio mwisho wa Ukonongo.

tukaondoka pale tukenda zetu Mbugani, panapo mizimu[1]) yao, na jina la mizimu yao inakwitwa Katawi. ndipo porini, hapana nyumba wala mtu. pana nyama wengi sana, simba wengi, na chui wengi, na

1) Seelen der Verstorbenen.

fissi wengi, na mbogo wengi, na punda milia wengi, na viboko vingi.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu, tukawáṣili mji wa Kawende. na mkubwa wa mji jina lake Soloma. tulipofika mjini, akatufungia lango. „ninyi wangwana", akatuuliza, „mmekuja na viṭa?" tukamwambia: „sisi wasafiri". asema: „ḥasha, huo uwongo wenu. ninyi mmekuja na Mzungu. mmetangulia maqṣudi, yeye mmemwacha nyuma. ḥatta mkafika mjini, akija yeye marra moja, atapigana". tukakataa, tukamwambia: „hatukuja na Mzungu, na kama huṣadiqi — tule kiapo". akasema: „wangwana, kiapo kitawafaa wapi? mji wangu sitaki mwingie. kwa nini msijenge kambi hapo nje, na vyakula wataleta hukohuko? walakini kuingia mjini mwangu sitaki".

tukapanga mizigo yetu nje, tukajenga na ḥema yetu, tukawambia na wapagazi: „jengeni boma jema sana, kwa sababu mshenzi huyu mbaya, kazi yake kunyanganya mali ya watu". akatuletea vyakula kulekule, tukanunua. tukapika, tukala ḥatta tukashiba, tukalala, lakini haikujiri neno.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu mtoni. na huo mto jina lake huitwa Mfune — porini, hapana nyumba wala mtu. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda Kafissa, na inchi jina lake Kawende. na huyu sulṭani wa mji huu Kafissa, jina lake Tshata, akatufanzia ḥéshima kubwa sana, akatupa na majumba ya kulala na vyakula vingi. hatuna khabari, kama atufanyizia khadaʿa ya kutunyanganya mali zetu. tukalala ḥatta usiku, akaleta watu, wakaizunguka nyumba, akatwambia: „wangwana, amkeni!" tukamwambia: „sulṭani, kuna nini usiku huo? kama una maneno, sababu hungojei aṣ-ṣubuḥi?" akasema: namtaka mkubwa wa msafara atoke nje, tuje tuonane, na maneno yangu nataka nimwambie". tukasema: „ḥasha lillah,

maneno yako ngoja aṣ-ṣubuḥi". marra watoto wake wakafanya ḥaraka, wakapiga bunduqi. tukajua — kweli hivi vita. na sisi tukajifunga silaḥa zetu na bunduqi zetu, tukatoka nje, tukaona washenzi wengi na bunduqi zinalia kwao, na sisi kwetu tunapiga bunduqi. wengine wa washenzi wakazunguka nyuma ya nyumba, wakapiga moto ile nyumba yetu sisi. tukasema: „jama'a, tutapigana vita viwili — moto na watu! sasa tufanye shauri gani? na tujigawe, wengine wateke maji, wazime moto, tupate kutoa mali yetu, na wengine tupigane na watu". tukapigana ḥatta aṣ-ṣubuḥi, na moto ukazimika. tukapata nuṣṣ ya mali zetu. na washenzi wamekufa watu 'asherīn na wawili, kwetu sisi wamekufa watu kumi.

sulṭani akatwita akasema: „sasa hapana vita, ninyi na tufanye urafiqi, na mali yenu iliyopotea nitalipa, kwa sababu haya sikufanya mimi, wamefanya watoto wangu. kama hamniamini, na tule kiapo cha kwetu sisi washenzi". na sisi tukakhada'ika, tukathanni maneno yake kweli. tukaqubali kufanya urafiqi na yeye Tshata. tukatia mizigo yetu nyumbani mwake, akasema: „kaeni kitako, wageni wangu, na bunduqi zenu nipeni mimi zote pia, kwa sababu nakataa watoto wangu, wasifanye gházia, wakesha waona na bunduqi — roḥo zao watafanya oga, watakwenda porini na waanawake wote. chakula atatupikia nani? na ninyi mmekwisha kuwa ndugu zangu, mna ḥofu nini?" tukampa bunduqi zetu zote pia, ḥatta na pembe tukamvulia tukampa, akatia nyumbani mwake, akasema: „wangwana, sasa uhodari wenu uko wapi? silaḥa zote nimekwisha twaa, mtapigana na nini? hamjui mali yenu nimekwisha wanyanganya, sasa mnataka roḥo zenu ao hamzitaki? kama mnataka roḥo zenu, msiseme — kwangu yako mali. kama mnataka kufa,

kaeni kitako hapa pangu, ntawaua wote pia, kwa sababu waungwana jeuri sana“.

„alikuja mungwana mmoja hapa, jina lake Matuumla, akaja, akanifanzia ḥila, akachukua mali zangu pembe ʿesherīn, akanambia: „ntakuletea mali mengi“. nimekaa mwaka mzima, sijamwona ḥatta sasa. na leo muungu umenipa kutwaa kwa mkono wangu. tenna mniachie mimi mjinga kama nani? ao mimi mnafanya si sulṭani? kama mnataka mali zenu, kaniletee Matuumla, tuje tufanye ḥesabu ya mali zangu, alizochukua Matuumla, na ninyi ndipo niwape mali zenu. na watu waliokufa — enda walipa wote pia, na mali zilizopotea — nazo ntalipa, walakin shurṭi mje na Matuumla, ndio mpate yote hayo kwangu. na kama hamkuja naye — hayo hampati. labda mje kwa vita! na mkileta vita kwangu mimi, shurṭi mniambie — kwa kuwa: „sisi tunakuja, ukae ṭayyari!“ waanaume hawafichani; kwetu sisi washenzi vibaya sana kufichana, sijui nini waungwana kwenu. hayo ndio maneno yangu; kama mmesikia — sikilizeni sana, na kama hamkusikia — mali yenu mmepotea“. na sisi tukamjibu yule sulṭani tukamwambia: „sisi huyu Matuumla hatumjui, walakini umetunyanganya mali zetu kwa kutuonea, kwa sababu hatuna nguvu. weye — kwa sababu sulṭani — ndipo ukanyanganya mali ya watu. na sisi tungalikuwa na nguvu kama wewe — nasi tungaliweza kunyanganya. walakin haiḍuru, baḥati yako, kula mali yetu, yalale ndani ya tumbo lako“. akatujibu: „bado — tenna mnasema — roḥo zenu haziogopi? hamfanzi safari mkenda zenu? maneno mengi yote ya nini? manamme hufanya maneno mengi sana? kama mnaweza kupigana — piganeni. sikupigana?“ na sisi tukamjibu: „tutapigana na fimbo? na bunduqi zote zetu umetwaa? kama wataka tupigane na weye —

tupe bunduqi zetu, utazame kama tutapigana ao hatutapigana!“ akasema: „mimi nna wazimu, niwape bunduqi — khalafu mnipige mimi? kama mnaweza, tafuteni nyingine, mje mpigane na mimi. hivyo tenna ondokeni, kwa sababu hawajaja watoto wangu, wenyi kichaa, watazidi kuwamaliza“.

tukafanya mashauri: „jamaʿa, hatwendi zetu? tunasema — na mshenzi hasikii! labda roḥo yake itagheiri, atafute kutuua? mali zetu zimepotea, na roḥo zetu hazipotei?“ wengine wakasema: „hatwendi zetu Karema, tukampe khabari Mzungu, kwa kuwa Tshata ametunyanganya? sasa tutaondoka waqati gani hapa? kuondoka mchana haifai, labda watatufuata washenzi, wakapata njiani watuue — afaḍali tumwendee sulṭani, tumwambie: „maneno yako tumequbali, mali zetu weka vema, nasi tunakwenda mtafuta Matuumla“.

tukapatana tukenda kwa sulṭani tukamwambia: „maneno yako kweli, sulṭani, tukikuletea Matuumla, utatupa mali zetu?“ akasema: „bassi mimi nnasema uwongo?“ tukamjibu: „bassi, sasa tunataka rukhuṣa kwako, tulale usiku kucha ḥatta aṣ-ṣubuḥi tutakwenda zetu, sulṭani, inshallah tutakuletea Matuumla“. akasema: „hayo si ndio niyataka hayo? haya, twaeni nyumba mkalale, nanyi msifanye ḥofu. laleni ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tuagane vyema, na chakula ntawapa njiani ḥatta mfike kwenu“. tukenda zetu ḥatta kule nyumbani alipotuonyesha. tukakaa kitako na masikitiko yetu ya kusikitikia mali zetu, zilizopotea, na ndugu zetu, waliokufa. hapana sababu, wala Matuumla hatumjui.

tukalala ḥatta usiku tukatoroka, tukenda zetu Karema. kupata njiani mwenzetu mmoja akakamatwa na simba. tutamfanya nini simba — hatuna bunduqi?

tutampiga na nini? tutafanya kelele tu? akamchukua mwenzetu, akampeleka mwituni, akenda, akamla.

na sisi aṣ-ṣubuḥi tukawáṣili Karema, tukamkuta Mzungu amelala bado. tukawambia watu wake: „bwana yuko wapi?“ wakasema: „amelala, walakini qaribu ataamka“. tukakaa kitako mlangoni. ḥatta sa'a mbili u nuṣṣ ilipopata ya tatu bwana akaamka, akauliza: ēē boi, kuna nini huko?“ akasema: „wamekuja waungwana, wanatoka Tabora“. bana akasema: „wameleta barua yangu mimi? hela — nenda kawaulize“. tukamwambia: „sisi hatukuleta barua, sisi tumepigwa Kafissa na huyu sulṭani Tshata, ndiye aliyetupiga, akatunyanganya mali zetu zote, na ndugu zetu amewaua. bassi — twamtaka bwana, tumwambie maneno yetu“. boi akatujibu: „bwana sasa yuko mezani, kaeni kidogo, mumngojee, atakuja sasa hivi“.

ḥatta alipokuja bwana, tukamwambia: „bana, tumepigwa? akauliza: „nani aliyowapiga?“ tukajibu: „Tshata“. akatwambia: „walakini mimi nimesema, kama waungwana wote kwanza wafikie kwangu! mmekwenda fanya nini kwa mshenzi? walakini haiḍuru, ntapeleka 'askari, waende wakaulize „umenyanganya waungwana sababu nini?“ na nyīe toeni mtu moja kwenu, afuatane na 'askari wangu, akasikilize maneno anayosema 'askari wangu pamoja na Tshata, na nyīe wenyewe mpate sikia“.

wakafanya safari, wakenda zao ḥatta kwa Tshata. 'askari wakamwambia: „weye Tshata sasa umekuwa mwanamume wa kunyanganya mali za watu? huogopi amri ya serkali?“ akasema: „mimi sikuwapiga burre, nimewapiga kwa sababu yangu ya Matuumla, kachukua mali zangu — pembe 'esherīn“. 'askari wakamwambia: „ḥasha, sisi hatuqubali, lete mali ya waungwana yote, ndivyo alivyotwambia bwana mkubwa“. alipoona nguvu

zimezidi, akatoa mali mshenzi, akawapa ʿaskari. wakaja nayo ḥatta Karema, mali yetu yaliyobaqia.

walipofika Karema, Mzungu akatwita: „ēnye wangwana, njooni huko, mje mtazame mali yenu, ndio haya aliyotwaa Tshata?“ tukatazama tukamwambia: „ndio bana, mengine yamepotea na moto“. akasema: „ḥaiḍuru, chukueni haya yaliyosalia“. tukamwambia tenna: „hewallah bana, lakini sasa tunataka mitumbwi. tuvukẹ na mali zetu, twende zetu Marungu“. akatwambia: „mimi sina mitumbwi, nna mashua yangu moja, nayo imekwenda Marungu. mkitaka mitumbwi, nendeni kwa washenzi, ndio wenyi mitumbwi“. tukamwuliza: „washenzi gani?“ akasema: „wenyi mitumbwi si Wafipa“? tukamwambia: „huyu mkubwa wa Wafipa nani?“ akasema: „sulṭani wao si Kapofi?“

tukalala, ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukamwaga bwana mkubwa: kwa ḥeri, tunakwenda zetu“. tukafika ḥatta kwa Wampembe, ndio mizimu yao Wafipa. wanakuja kutambika [1]) siku zote hapo. na mitumbwi yote ndipo ilipo hapo. tukenda tukawambia wenyewe: „twataka paḥali tupange“. wakatwambia: „ingieni mjini, sisi na waungwana ndugu zetu. sulṭani wetu anawapenda sana waungwana“. tukaingia mjini wote na mizigo yetu yote. wakatupa nyumba ya kulala.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukawambia: „tunataka mitumbwi“. wakatuuliza: mitumbwi ya kwenda wapi?“ tukasema: „tunakwenda n̄gambo Marungu“. „mnakwenda fanya nini?“ tukawambia: „tunakwenda fanya biʿashara ya pembe“. wakatwambia: „ndio, lakini sisi hatuna amri ya kutoa mitumbwi, mwataka — nendeni kwa sulṭani Kapofi, huyu ndiye mwenyi mitumbwi. akesha toa amri

1) die Seelen der Verstorbenen anrufen.

yake, bassi tutakuja wapa hiyo mitumbwi mwitakayo". tukawambia: „bassi, tupeni mtu moja, atupeleke ḥatta kwa sulṭani, twende tukatake mitumbwi".

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, wakatupa mtu moja, tukafuatana naye ḥatta kwa sulṭani Kapofi. akamwambia mtu wake: „hapa inchi wamekuja na wageni, wanakutaka wewe, uonane nao, wakwambie maneno yao waliyo nayo". akamwambia: „bassi, nenda kawete, nisikilize khabari yao waliyo nayo". akaja ḥatta nje pale tulipokaa, akatwambia: mnakwitwa na sulṭani, walakini msiende watu wengi, nendeni watu wawili ao watatu, kwa sababu huyu si sulṭani mdogo, ni sulṭani mkubwa sana, wanamjua watu wote inchi zote". tukaondoka watu watatu, tukamfuata yule mshenzi. tukenda ḥatta kwa sulṭani, tukamkuta amekaa kitako juu ya kiti. ameweka waanawake wawili na huku wawili, na mbele yake wawili, na nyuma yake wawili. na watu wamemzunguka, mwenyewe kattikatti. ameweka kibuyu cha pombe, ameshika mwanamke mmoja, ndio anampa pombe sulṭani. ḥatta tulipokwenda, akatwambia: „wangwana, hamjambo sana?" tukamjibu: „hatujambo, sulṭani". „pombe mnakunywa? niwape, na nyie mpate kunywa?" tukamwambia: „hatunywi sulṭani". akasema: „mnaogopa kwa sababu mnaṣali; ndipo msinywe pombe?" tukamwambia: „ḥasha, mioyo yetu haipendi kunywa pombe, tunaogopa kulewa, kwa sababu mtu akisha lewa — hupiga kelele, hutaka labda na kupiga na watu, na hayo mtu mgeni haifai? yataka mtu mgeni akae vyema na watu". akasema: „bassi, sasa mnataka nini? niwape ugali?" tukamwambia: „hatutaki, kama unga twataka, tupike wenyewe namna yetu ya mrima". twaliogopa sumu, lakini hatukumwambia mwenyewe kwa sababu ataqaṣirika, ḥatta mitumbwi atatunyima. bassi akatupa unga na kuku, akatuonyesha na nyumba. aka-

tupa na vyungu vya kupikia ugali wetu, tukapika ule ugali, tukala.

tulipokwisha kula, tukamwambia yule mshenzi tuliyokuja naye: „tupeleke kwa sulṭani, kwa sababu hatujapata kumwambia khabari yetu ya mitumbwi. bassi sasa tunataka tumwambie, na yeye apate kujua, kama tutapata kwake mitumbwi, tupate kujua, roḥo zetu zifuraḥi“. tukenda zetu kwa sulṭani, tukamwambia: „sulṭani, tunataka mitumbwi kwako, tunataka kuvuka kwenda ñgambo Marungu“. akatuuliza: „Marungu mnakwenda kwa nani?“ tukamwambia: „tunakwenda kwa sulṭani jina lake Mlilo, huko ndio tunakokwenda“. akasema: „haya bassi, tupatane újira wangu wa mitumbwi mnayoitaka. mtanipa qiasi gani?“ tukamwambia: „qiasi unakijua wewe mwenyewe mwenyi mitumbwi yako“. „khaṣṣa mnataka mingapi?“ tukamwambia: „sisi twataka mitumbwi sitta“. akasema: „mitumbwi sitta hiyo — mnipe nguo mitēni“. tukamwambia: „pamoja na baḥaria?“ akasema: „ḥasha, na themani ya baḥaria nayo mbali“. tukamwambia: „bassi utupunguzie, sulṭani wetu, na sisi wanao“. asema: „bassi, nipeni ninyi qiasi mnachoweza“. tukamwambia: „tutakupa nguo khamsīn“. akasema: „ēé, mnafanya ḍiḥaka, kama mnataka mitumbwi, semeni kweli“. tukamwámbia: „tutakupa nguo settīn, na baḥaria tutapatana nao kwâ themáni nyingine. hizo settīn ni zako wewe pekeyáko“. akasema: „vema, nimequbali, walakini mnipe bunduqi moja“. tukamwambia: „sulṭani unatukumbusha kilio! bunduqi tuipate wapi? bunduqi katunyanganya Tshata zote“. ákasema sulṭani: „hivi Tshatâ amekuwa mtu m̃baya? hawáogopi? hakusikia kitendo walichotenda Issike, mwana Kiungi? naye átaka hivohivo? bassi wanangu, sikujua kama bunduqi mmenyánganywa. nipeni bassi nguo zangu settīn“. tukafungua mtumbâ

tukampa nguo settīn. akasema: „haya, sása pataneni na baḥaria, wapate kuwavusha, wawapeleke ḥatta ñgambo, mfike kwa Mlilo, nà wao wapâte kurudi upesi“.

tukâweta baḥaria wote pia, na mkubwa wa baḥaria jina lake Makunganya. akasemà: „pataneni na waungwana hawa újira wenu wa kuwavusha ḥatta ñgambo“. mkubwa wao akasemà: „watoto wangu nguo ńneńne, wote pia, na mimi mwenyewe nguo tano na vitambaa vya kufungia kichwa. watupe na posho yetu“. tukawapa nguo ńneńne wote pia, na mkubwa alivotaka.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukapakia mali yetu ndani ya mitumbwi na sisi wenyewe. wakavuta makasia. ḥatta sa'a heda'shara ikaja ḍaruba kali, tukaona twataka kufa. Wafipa wakatwambia: „upesi upesi kunako mizimu yetu, twende tukatambike, labda upepo utaregeza“. tukenda upesi upesi ḥatta tukafika kisiwani. tukashukà wote pia na mali zetu. Wafipa wakátwambia: „toeni nguo mojá nyeusi, mtoe na bendera mojá, mtoe na shuka moja nyeupe, mtoe na ushanga kidogo mweupe, na ushanga kidogo mwekundu, tupeleke mizimuni“. tukafungua mizigo upesi upesi, tukatoa vitu walivyotaka, tukapeleka mzimuni. na huo mzimu jina lake Wampembe. tukapeleka vile vitu vyote, tukamtajà kwa jiná lake, tukamwambià: „weye ndiye Wampembe, tumekuletea zawadi zako hizi, twataka utupe salāma ya safari, twende salāma, tukarudi salāma“. tukakaa robo' sa'a — upepo ukaregeza.

tukamwambia: „haya, upesi tupakie mali yetu“. tukapakia, nasi wenyewe tukajipakia. baḥaria wakashika makasia yote pia, tukasafiri. ḥatta sa'a sitta za usiku tukawáṣili ñgambo ya Marungu kwa sulṭani Mlilo. walakini hatukufika mjini kwa sa'a ile, tumelala mitumbwini.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukashuka, tukenda mpaka kwa sulṭani, tukaonana naye. akatuuliza: „waungwana huko

kwema? nanyi nyote hamjambo?“ tukamwambia: „hatujambo sulṭani“. „kwa nini hamwendi leta mizigo yenu, mkaje mkingia mjini?“ tukarudi ḥatta pwani, tukenda tukatwaa mizigo yetu. tuliporudi, tukamkuta sulṭani katutafutia nyumba ṭayyari. tukatia mizigo yetu ndani. akatuuliza: „waungwana, mnataka nini?“ tukamwambia: „tunataka biʿashara ya pembe, kama zipo — lete tufanye biʿashara“. akasema: „baruti na bunduqi mnazo?“ tukamwambia: „baruti hatuna, kwa sababu tumenyanganywa na Tshata, sasa tumepakia na biḍaʿa tupu“. akasema: „vyema, laleni ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tutazidi kuonana“. tukenda kulala.

aṣ-ṣubuḥi akaja, akutwita, tukamkuta ameweka kalasha mbele yake, akasema: „wangwana, mnataka hii mnunue?“ tukamwambia: „twataka, sulṭani, kuna mali mabaya?“ akasema: „haya, fanzeni biʿashara“. tukainunua kalasha, themani yake nguo ʿasherīn, tukapeleka nyumbani kwetu. akatoa na bori moja palepale, qabla hatujaondoka, akasema: „mnunue na hii“. tukamwuliza: „themani yake qiasi gani“? akasema: „nataka nguo khamsīn“. tukamwambia: „hizo nyingi sana“. tukainunua kwa nguo khamso u thalathīn, tukaipeleka nyumbani kwetu. akatuonyesha pembe moja kubwa, babu Ulaya, kwa sababu nzuri sana. tukamwambia: „qiasi gani themani yake?“ akasema: „nataka nguo mitēni“. sisi tukampa nguo mia. akasema: „n'ongozeni“. tukamwongeza nguo kumi. tukainunua, tukaipeleka nyumbani kwetu. akatoa na pembe moja — imeoza. tukamwambia: „hii ya nini? mbayambaya“. akasema: „nunueni kwa ubaya wake. mtanipa nguo ngapi“? tukamwambia: „tutakupa nguo kumi“. akasema: „nipeni“. tukainunua. akasema: „kwa ḥerini, sasa nimechoka, labda kesho tutafanya biʿashara“.

aṣ-ṣubuḥi akaja, akatwita, asema: „wangwana,

bamnipi pipa moja la baruti, niwape watoto wangu, waende porini?" tukampa, tukaagana naye kutupa pembe, ndio themani ya pipa letu. khalafu akatoa pembe ningine, akatwambia: „fanzeni bi'ashara". tukainunua kwa nguo saba'īn, tukapeleka nyumbani kwetu.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi jua la kupata sa'a mbili — watoto wake, waliokwenda porini, wamerudi, wakasema: „tumepiga tembo wawili". tuliposikia vile — tukajuta, kwa sababu tumeagana naye pembe moja, na leo baruti yetu imechuma, imeleta pembe nne. akatwambia sulṭani: „wangwana, baḥati yetu njema, baruti yenu imepata fayida". tukamwambia: „inshallah, sulṭani".

tukalala, ḥatta aṣ-ṣubuḥi wakarudi na pembe zote nne, wakaingia mjini kwa furaḥa kwa kucheza ngoma, na kunywa pombe nyingi. akaja akatwita sulṭani, akasema: „wangwana, njooni mtwae pembe yenu ya baruti tulivoagana". tukachukua pembe moja, tukenda tukaiweka nyumbani. tukamwambia sulṭani: „na hizi hutuulizi? akasema: „miye bassi nakataa? leteni mali, tufanye bi'ashara". tukanunua moja kwa nguo mia, tukapeleka nyumbani kwetu, tukanunua ya pili, na themani yake nguo mia, tukaipeleka nyumbani kwetu. na moja ndogo tukainunua kwa nguo khamsīn na tano.

bassi biḍa'a yetu imekwisha. sasa tufanye mashauri gani? na deni yetu pwani kubwa sana. na mali nyingi yamenyanganya Tshata! afaḍali tuchuuze, tukatwae ile pembe kubwa, tuliyoinunua kwanza, twendee tukaiuze kwa huyo Mzungu, aliyo Marungu. tukafanya hivyo, tukapata biḍa'a na baruti na bunduqi na ushanga, tukauza pembe yetu. tukarudia mpaka nyumbani kwetu kwa yule sulṭani wetu, tukafanya bi'ashara tenna. akaleta pembe moja nzuri sana, sababu ameona biḍa'a yetu na baruti na bunduqi na ushanga — akazidi kufuraḥi,

nguo kumi". tukayanunua, tukampa nguo kumi, tukapeleka, nyumbani kwetu.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukamwambia: „sulṭani, bi'ashara tenna hapana?" akatwambia: „nguo zenu zipo tu bado?" tukamwambia: „zipo". akaleta pembe moja ndogo. tukainunua kwa nguo 'esherīn na nne na shindano khamsīn, tukaipeleka nyumbani kwetu. akaleta na pembe moja ndogo, tukainunua kwa nguo kumi na nane na shindano mia. sasa biḍa'a yetu imekwisha. tukamwaga sulṭani: „kwa ḥeri, tunakwenda zetu bendarini kwetu kwa Mlilo". akasema: „vema, nimesikia, mtaondoka leo?" tukamwambia: „leo hatuondoki, kwa sababu jua limekuwa kali, tutalala, tutaondoka aṣ-ṣubuḥi".

tukalala ḥatta äṣ-ṣubuḥi, tukàfungafungà mizigo yetu, tukaondoka. kupata njiani yule sulṭani wa Kabwire akatuletea watu, kujà kutupiga porini. tukapipigàna naò, tukaua mtu moja, hawa wengine wakenda mbio ḥatta kwao. na sisi tukenda zetu, tukawásili Tshoma kwa yule sulṭani, aliyokopa mali yetu. tukafika pale tukalala.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukamwambia: „sulṭani, tupe mali yetu, twàtaka kwendä zetu". akasema: „shindeni leo, wanangu, kwa sababu pembe ziko porini, ntapeleka watu, wende wakazilete, ḥatta jioni watawáṣili hapa". tukàmwambia: „vema, walakini wasiende lala porini huko, kwa sababu tuna hamu ya kwenda zetu, kẁenda kutazama mali yetu kwa Mlilo, kwa sababu tumeondoka siku nyingi". tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, jua kupata sa'a tatu, waliokwenda porini — wakarudi, wakaleta pembe mbili, zile tulizoagana naye yule sulṭani wa Tshoma. akatupa mwenyewe pembe zetu, akatwambia: „mali yenu yamewáṣili?" tukamwambia: „yamewáṣili". „mulikuwa mkanifanya mwevi! sasa mali yenu sikuwapa mwenyewe? nimenyanganya nini? aliyewanyanga-

nya — si sulṭani wa Kabwire?“ akaleta meno matatu ya ngiri, akasema: „chukueni waungwana; maqṣudi kuwanyanganya“.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu ḥatta Kissanso. siku ya pili tukafika bandarini kwetu kwa Mlilo', tulikoacha wenzetu. tukapiga bunduqi, wakaja, wakatufuraḥia, wakatuuliza khabari ya Kabwire. tukawambia: „kwema, walakini mchenzi huyu alitufanzia ḥila sana, lakini muungu hakusimama naye, kwa sababu alitaka kutunyanganya. bassi, na sasa tumefika salāma, tupeni ninyi khabari ya huko“. wakatwambia: „huku kwema; zama mlipoondoka, tukapata khabari, kwa kuwa mmepigwa njiani na washenzi. bassi khabari hiyo kweli ao uwongo?“ tukawambia: „uwongo“.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi mkubwa wa safari akatukusanya wote pia, katwambia: „nipeni khabari yenu, biḍaʿa zimekwisha, sasa tufanye shauri gani?“ tukamwambia: „hapana mashauri illa ya kupima pembe zetu, tupate kuzijua frasila ngapi“. akatwambia: „wambieni watu bassi wapate kuzitoa pembe, tuzipime“. tukatandika mizani, tukapima pembe. jumla ya pembe zote, kubwa na ndogo, njema na mbaya, zikatokea frásila waḥed u thalathīn. baʿadaye akatuuliza: „ēē, pembe hizi mwazionaje? zitalipa mali za Wahindi?“ tukamwambia: „zitalipa wapi? na mali nyingi tumenyanganywa!“ „sasa bassi tufanyeje? si khēri tukenda tukabadili? tukatafuta njia ningine ya kwenenda, tukazidi kuelemea mbele?“ tukamwambia: „mashauri yote pia yako kwako, wewe, mkubwa wa msafara, likawa jema — tutafuata, na likawa baya — tutafuata“. akatwambia: „moyo wangu mimi unanidanganya kwa hivo, kwa sababu kwenda pwani — nawaogopa Wahindi kwenda nishitaki na kunifunga, moyo wangu umefanya oga. sasa bassi tutaondoka kabisa? ao watu wengine watabaqi hapa?

na tukae bassi, ḥatta jioni tumwendee sulṭani wetu, tumwage, tusikilize mashauri yake. atatupa rukhuṣa, ao atatuziwia? kwa sababu washenzi watu wa ḥila". tukamwambia: „vema".

tukakaa ḥatta jioni, tukamwendea sulṭani, kwenda kumwaga, tukamwambia: „sulṭani, tumekuja kwako qáṣidi kukuaga". akasema: „mwaenda wapi?" tukamwambia: „twaenda kwetu, kwa sababu biʿashara zetu zimekwisha". akasema: „kwa ḥerini, wageni wangu, mtaondoka leo ao kesho?" tukamwambia: „tunaondoka aṣ-ṣubuḥi".

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu sisi sote pia na pembe zetu, tukenda ḥatta Sumbu. na mkubwa wa Sumbu jina lake Mwenyi Tereka, mtu wa mrima. tukiwáṣili, kwake akatuuliza: „wageni, mmekuja hapa ao mwaenda mbele?" tukamwambia: „tunakwenda mbele". ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu ḥatta Iyendo. na sulṭani wa Iyendo jina lake Kitimbo. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukachukua pembe zetu zote pia ḥatta kwa Mzungu, tukamwambia: „bwana, pembe hizi tumenunua". akatwambia: „vema, na tupatane". tukapatana kulla frásila reale khamso u tissaʿīni kwa themani ya barra. tukamwuliza pembe zetu zote pia. tukafunga biḍaʿ, nuṣṣ tukatwaa baruti na bunduqi, nuṣṣ tukaṭwaa ushanga, mizigo yetu pia jumla mizigo khamso u settīni.

akatwambia mkubwa wa safari: „na tuulize sasa — tutakwenda njia gani?" tukamwita mshenzi, tukamwambia: „unajua wapi na wapi?" asema: „naijua inchi ya Lunda, ḥatta Luemba kwa Kitimkuru, ḥatta Itawa kwa Samma, ḥatta kwa Kafimbi, ḥatta kwa Mamba, ḥatta kwa Mkalikali, ḥatta kwa Kasembe". tukamwuliza: „biʿashara njema záyidi wapi?" akatwambia: biʿashara njema záyidi, kama mwataka kuchuma kweli, mpate furaḥi nyoyo zenu, mwende Kissinga kwa

Mkalikali". tukamwambia: „mbali sana?" akasema: „mbali, lakini hamtaki kupata mali? japokuwa mbali — si kuenenda?" tukamwambia: „utatupeleka?" akasema: „tunapopatana — ntakwenenda". „twambie újira wako qiasi gani?" akatwambia: „nipeni nguo kumi na tano, walakini sitachukua mzigo, kazi yangu mimi rubani kutangulia mbele ya njia. mnipe na ushanga kidogo, nimpe mwanamke wangu pamoja na wanangu, sababu nna watoto watatu". tukafungua mzigo, tukampa nguo kumi na tano, alizozitaka, na ushanga wake tukampa. tukauliza: „safari leo ao kesho?" akatwambia: „mtakapo popote wenyewe". tukamwambia: „leo tutafute vyakula, ḥatta kesho tufanze safari".

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaondoka, tukenda ḥatta Pumpe. na sulṭani wa Pumpe jina lake Tshungu. tulipowáṣili akatwambia: „waungwana, mnatoka pwani ao hapa kwa Mzungu?" tukamwambia: „tunatoka hapa kwa Mzungu". kwa sababu tulimficha maqṣudi, akesha jua kama tunatoka pwani — atatunyanganya. akasema: „qaribuni". tukatoa nguo tano tukampa.

tukalala, ḥatta usiku akaja mwevi kutaka kwiba. wenyewe tukaamka, tukampigia kelele, ḥatta tukamkamata, tukamfunga. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukampeleka kwa sulṭani, tukamwambia: „sulṭani weye huna ḥaya? wageni, tuliokuja kwako, na ḥéshima yako, tuliyokupa, ḥatta usiku unamleta mtu wako maqṣudi kuja kutwibia mali zetu? weye huogopi?" akatwambia: „waungwana, ḥatta kumjua simjui. na kama hamṣadiqi — mtendeni kitendo, mnachotaka ninyi wenyewe, ndipo mpate kujua, kama huyu sikumwamrisha mimi". tukamwambia: „vema, tumesikia". tukarudi ḥatta kambini kwetu.

tulipofikia tukafikiri: „sasa tutamfanyaje huyu mshenzi?" mkubwa wa safari akatwambia: mpigeni bakora kumi, kwa sababu tumepata rukhṣa kwa sulṭani

wake. mkesha mwacha aende zake, kwa sababu hakutoa kitu". tukampiga bakora kumi, tukamwambia: „nenda zako! siku ya pili usifanyize kama hivi. ukifanza — — utakufa. leo umekuja kwetu sisi watu wema, kesho utakwenda kwa wabaya, watakuua, kwa sababu watu si wamoja".

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu ḥatta Mtoni Kavubu. na huyu sulṭani wa Mtoni Kavubu jina lake Kapoma, ni mtoto wake yeye Tshunga. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu tukafika áuwali ya Luemba. na mkubwa jina lake anakwitwa Porokosso, mwana wa Kitimkuru. tulipofika, hatujaingia mjini, akapiga ngoma, akakusanya jeshi kubwa. akawagawia baruti, akawapa na riṣaṣi, akawapa na mishare. mnyampara wake akamwuliza: „sulṭani, vita hivi tunakwenda wapi?" akamwambia: „huoni waungwana wamekuja? hao hawakuja pekeyao, wamekuja pamoja na Mzungu, maqṣudi kunipiga mimi. wametangulia wao mbele, Mzungu wamemwacha nyuma, maqṣudi tuamini roḥo zetu, tupate kufungua mlango, waingie mjini — usiku Mzungu atupige. hio ndio khadaʿa yao. ʿaqili zao zote nazijua". mnyampara akamwambia: „bassi tupeleke watu, wakenda wakauliza, kama kweli wamekuja na Mzungu ao pekeyao?" sulṭani akamwambia: „bassi, nenda weye na watu wawili watatu wakupeleke".

aliposikia waziri, akatoka yeye na watu wake, akaja ḥatta kwetu sisi waungwana, akatwambia: „waungwana, nipeni khabari yenu, iliyowaleta huku kwetu, mpate 'nambia mimi, nipeleke khabari kwa sulṭani. walakini msiseme uwongo, semeni kweli". tukamwambia: „sisi tumekuja kutafuta biʿashara ya pembe, na kama hamṣadiqi, tupeni vyapo vya kwenu vya kishenzi, tupate kuwaapia, kwa kuwa — sisi hatuna shari". akatwambia: „nimesikia maneno yenu, ngojeni nikampe khabari sulṭani wangu".

alipokwenda kwa sulṭani, akampa khabari zote pia, kama tulivyomwambia. akamjibu akamwambia: „nimesikia maneno, yaliyotoka kwa waungwana, wambieni, wazunguke nyuma ya mji, wende wakapange. kuingia mjini hawana rukhṣa". akaja akatujibu. tukamwambia kirongozi: „ondoa safari, twende tukapange tusikilize khabari vyema. miaka hii washenzi wote wameta'addi kwa kutaka kudanganya mali za watu". tukaenenda ḥatta tukapanga, tukajenga ḥema yetu, tukawambia wapagazi: „shikeni mashoka, tujenge boma kubwa, tukae kwa ḥážari". tukajenga boma letu ḥatta ilipokwisha".

wakaja washenzi watatu wakatwambia: „tunatoka kwa sulṭani, ametutuma kuja kwenu kutaka mahongo. mtampa ao hamtaki?" tukamwambia: „tukatae sababu nini? mahongo yake qiasi gani?" wakatujibu: „hatuijui themani yake, toeni kama mnavotoa wenyewe. tuondoke sisi na ninyi, tuwapeleke kwa sulṭani, mkapate kusikia anavosema mwenyewe sulṭani". tukachukua nguo 'asherīn, tukenda ḥatta langoni — tukazuiwa, wakatwambia: „mnaingia hivi billa rukhuṣa? mnafanya jeuri hii?; kawambia nani?" tukawajibu: „siye tumekuja pekeyetu? hatukufuatana na wenyeji?" wakatwambia: „simameni hapo, ḥatta tupeleke khabari, mpate rukhuṣa yake sulṭani, ndipo mwingie ndani, mpate onana naye sulṭani". tukamwambia: „vema, nendeni".

wakenda zao ḥatta kwa sulṭani, wakampa khabari: „waungwana wako mlangoni, wanataka kuja huko kwako. iko rukhṣa ya kuja ao hapana?" akauliza: „wamechukua nini?" wakamwambia: „wamechukua nguo". akawambia: „wacheni wapite. watu wawili watatu watafanya nini?" marra tukawaona wakaja ḥatta pale mlangoni, wakatwambia: „twendeni zetu, mkaonane na sulṭani". tukaenenda ḥatta kwa sulṭani, tukaingia ḥatta ndani, tukamkuta amebarizi, amekaa juu ya kiti. huko

waanawake watatu, na huko watatu, na nyuma ya mgongo watatu, na mbele ya tumbo watatu, na mmoja ameshika kibuyu cha pombe, anamnywesha sulṭani. na mtu mwingine anampepea mainzi sulṭani. alipotuona akawambia watu wake: „ondokeni mkae upande moja, huko mwapishe, wakae waungwana“. akatuuliza: „waungwana, mmeletea nini?“ tukamwambia: „tumeleta nguo za mahongo kuja kukuhonga“. akatuuliza: „nguo ngapi?“ tukamwambia: „nguo ʿasherīn“. akatwambia: „zatosha, leteni mweke hapa mbele yangu“. tukampelekea ḥatta mbele yake, akatuuliza: „sasa mmekuja hapa, ao mnakwenda mbele?“ tukamwambia: „sisi nia yetu tunakwenda Kissinga kwa Mkalikali, kwenda tafuta biʿashara ya pembe. na wewe — pembe kama ziko kwako, tunataka tununue“. akatwambia: „pembe nizipate wapi? mimi maskini, kazi yangu kulima mtama tu. wakipita waungwana, wakanipa nguo moja mbili — nikapata kuvaa, kama mlivonipa mimi, na wenzenu hunipa vivihivi“. tukamwaga sulṭani huyu, tukenda kambini.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda ḥatta porini. na hilo pori jina lake Dshaga, hapana nyumba wala mtu. tulipofika tukapanga mizigo yetu, tukajenga ḥema, tukawaamrisha Wanyamuesi: „kateni miti, tupate kujenga boma, kwa sababu maḥala hapa pabaya sana, pana simba wengi na mafissi mengi na chui wengi. na washenzi wengi huja kuwanyanganya watu“. tukajenga boma, ḥatta likesha, kwa miti mikubwa sana, tukachimbia, tukafunga fito na kamba.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka tukafika Kissinga kwa Mkalikali. tukatua mizigo yetu njiani, tukapeleka khabari watu wawili: „nendeni ḥatta kwa Mkalikali, mkampe khabari — kwa kuwa „njiani tumewacha waungwana, kuja kupasha khabari mwenyi inchi yako, utoe rukhuṣa yako, wapate kuingia mjini wageni wako“. akafuraḥi

sana, aliposikia vile, akaondoka mwenyewe sulṭani, akawaita watu wake watatu kwenda kutwaa wageni njiani. akawambia: „mniletee wageni wangu upesiupesi". wakaja wale watu ḥatta njiani, wakatukuta tumekaa kitako, wakatwambia: „haya waungwana ondokeni, twende zetu mjini, mnakwitwa na sulṭani, anahimiza upesiupesi mpate kuonana naye".

tukaondoka tukachukua mizigo yetu. ḥatta tukaingia mjini, akatuonyesha majumba, tukatia mizigo yetu. tukakaa tukaweta watu wakubwa mjini, wanaokaa chini ya sulṭani, tukawambia: „tunataka mtu, atupeleke kwa sulṭani, tupate kuonana naye, ndipo roḥo zetu zitulie. kama hatukuona na sulṭani — tutafanya wasiwasi". wakatwambia: „vema, ngojeni tupeleke khabari". wakenda ḥatta kwa sulṭani, wakamwambia: „waungwana wanataka kuonana nawe, bassi tupe rukhṣa waje, ao wasije?" akawajibu sulṭani: „wana ḥaraka ya nini? mādām wamekwisha kuwáṣili mjini — hatuna buddi tutaonana. nendeni mkawape khabari". wakaja wakatwambia: „sulṭani anena „pumzikeni kwanza, mtaonana naye tartibu". tukawambia: „hiyo si qawaʿida ya mgeni ya kufika maḥala kutoa kuonana na mwenyeji — haifai. illa kwa kuonana naye, tukapata kuuliza khabari naye, ndio roḥo zetu zipate kutulia". wakatwambia: „bassi, tutarudi tenna marra ya pili, tukampe khabari".

wakenda ḥatta kwa sulṭani, wakamwambia: „waungwana hawaqubali illa kuonana nawe". akawambia: „bassi kawaiteni, tupate kuonana, wanipe khabari zao, walizokuja nazo, wameletwa na nini". wakaja ḥatta tulipo, wakatwambia: „jē waungwana, m ṭayyari, mpate kwenda onana na sulṭani?" tukawambia: „sisi ṭayyari". wakatwambia: „bassi sisi tutakwenda mikono mitupu?" wakatwambia tenna: „tafuteni nguo moja mbili mpe-

leke, zilizo kubwa za kuonana naye sulṭani". tukafungua mtumba, tukatwaa debwani moja na kitambi bora kimoja, tukawambia: „twende zetu". tukenda ḥatta ndani, tukamkuta sulṭani amebarizi, amekaa juu ya kitanda, amekusanya na watu wengi, wamekaa chini ya sulṭani. na sulṭani amevaa ngara ya simba, ameshika na shoka ndogo mkononi, na mkuki ameshika pamoja na shoka, na mkono wa kushoto amezuia kiko cha bangi — anavuta.

ḥatta tulipowáṣili, akatwambia: „kaeni kitako". tukakaa kitako. „jē waungwana, nipeni khabari yenu, huko mlikotoka, mmepita salāma? ḥatta maporini hamkupatikana na neno baya?" tukamwambia: „bassi — msafiri hana buddi na kupatikana na mabaya". akatuuliza: „sasa mnakwenda wapi? mmekuja hapa kwangu mimi tu, nambieni, nipate kujua, kama wageni wangu?" tukamwambia: „sisi wageni wako. yakitupata mema na mabaya kwako — hatuna maḥala pengine pa kwenda". akatwambia: „marḥaba, ni vema, wageni wangu". tukamwaga: „kwa ḥeri, tunakwenda kambini". akasema: „nendeni', záyidi ya khabari tutaulizana kesho, kwa sababu hamjapumzika, wala hamjala chakula". tukenda zetu ḥatta kambini tukalala.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi akaleta watu kuja kutwita. tukenda ḥatta kwake. tukamkuta sulṭani emeshughulika, tukamwuliza: „Mkalikali una nini?" akatwambia: „nimepata khabari mbayambaya — kwa kuwa vitakuja vita leo hapa mjini petu kuja kutupiga. bassi waungwana, kaeni vema". tukamwambia: „vema, tumesikia". tukenda ḥatta kambini kwetu, tukamwambia mkubwa wa msáfara: „tufanyeje sasa? tupe mashauri yako sasa, kwa sababu weye ndio mtu mzima! tumekuja hapa — na vita vinatujia". akatujibu: „ntafanzaje bassi, ndugu zangu? sisi tumefuata mali — tupate ao tukose! kheri

na shari itatukuta hapa na hapa, sisi na mwenyeji wetu, kwa sababu hatutakufa pekeyetu — tutakufa sisi na wenyeji. mali yetu yakipotea — na yao yatapotea na ya watoto wao“.

aṣ-ṣubuḥi na mapema ilipopata sa‘a mbili — bunduqi zikalia. na huyo aliyokuja na vita kuja kumpiga Mkalikali, jina lake anakwitwa Kigongo, ni mtu wa Msiri. tukashika bunduqi, tukatoka nje, sisi na wenyeji wetu, tukachanganyika pamoja kupigana na vita vilivokuja. tukapigana nao ḥatta sa‘a sitta, tukawashinda, wakenda mbio. tukaua watu arba‘īn na wawili, na sisi waungwana tukafa watu sitta, jumla wote pamoja na washenzi watu khamso u saba‘ini, ndio waliokufa katika mji wa Mkalikali.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi sulṭani akatwita: „waungwana, nipeni mashauri yenu; roḥo zenu zaweza kujizuia, ao mnaogopa, kwa sababu tumepigana na Kigongo?“ tukamjibu: „sulṭani, kama tunaogopa — tunaweza kupigana? na watu wetu wakafa — hujui kama tunaweza?“ akasema: „kweli waungwana, ninyi hodari, ḥatta mkaweza kunisa‘idia vita — hamnijui wala siwajui!“ tukamwambia: „sulṭani bassi, hapana bi‘ashara? kama ipo, tupe tufanyize, kama hapana, pia twambie, tupate kujua. na tukipata kukaa, tuṭama‘ini roḥo zetu — kwa kuwa tutapata bi‘ashara, tufuraḥi roḥo zetu“. akatwambia: „mtafanza bi‘ashara“.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukamwendea sulṭani kwenda mwamkia. tukakuta pembe moja kubwa, ameiweka mbele yake. tulipokwenenda akatwambia: waungwana, bi‘ashara mliyotaka si hii?“ „haya bassi na tupatane, qiasi gani pembe yako?“ akatwambia: „nataka nguo mia na pipa mbili za baruti na bunduqi mbili na qarṭasi mbili za ushanga“. tukamwambia: „hivo vitu vingi sana, sema kweli, tupatane“. akasema: „bassi —

hamsemi na nyie mnavotaka?“ tukamwambia: „tutakupa nguo khamsīn na bunduqi moja na pipa la baruti moja na qarṭasi mbili za ushanga“. akatwambia: „leteni mali nitazame“. tukafungua mzigo, tukampelekea mali. akatwambia: „biʿashara imekwisha“. tukaichukua kwetu, tukenda tukaipima, ikatokea frásila tatu. mkubwa wa safari akasema: „mshenzi mpumbavu, pembe tumeipata vema hii, tumeipata rakhiṣi“.

siku ya pili tukaenenda kwake kumwamkia, tukakuta pembe mbili, ameweka mbele yake. akatwambia: „waungwana, nalitaka kutuma mtu sasa hivi kuja kuweta mtazame pembe. sasa mmekwisha kuja wenyewe — kaeni kitako, tufanye biʿashara“. tukazifanyiza zote mbili kuwa pamoja na themani yao, tukazinunua kwa nguo mia na pipa mbili za baruti na bunduqi moja na qarṭasi mbili za ushanga, tukazipeleka kwetu.

ḥatta tulipokwisha, akaleta pembe ningine kubwa, akatwambia: „fanzeni na hivi“. tukamwambia: „qiasi gani?“ akasema: „ninyi mnataka qiasi gani?“ tukamwambia: „twataka kwa nguo settīni na pipa la baruti na bunduqi“. akatwambia: „leteni mali“. tukafungua mizigo, tukampelekea mali, kama tulivosema. akatwambia: „bassi — biʿashara imekwisha, chukueni pembe yenu“. tukaichukua kwetu.

tukenda kambini kulala. ḥatta aṣ-ṣubuḥi akatwita: „waungwana, mali yenu yote nikopesheni mimi, nitawapa pembe kuwa pamoja“. tukamwambia: „sulṭani, hii khabari gani? kuna sisi maskini — tukakukopesha weye mtu wa inchi yako?“ akatwambia: „nipeni, msifanze khofu, wala mimi siwanyanganyi, ntawapa mali zenu“. tukaenenda ḥatta kambini kufanya mashauri yetu.

mkubwa wetu akatwambia: „na tumpe, tubakhatishe, hawezi kutunyanganya sisi“. tukakusanya mali yetu, iliyosalia yote, tukampelekea, tukamwambia: „la-

kini sulṭani tufungue upesi upesi, usituweke siku nyingi, kwa sababu tumetoka kwetu kuwa siku nyingi sana, na haya mali si yetu, mali ya wenyewe Wahindi. sisi hukopa, tukaja tukafanya biʿashara, maqṣudi kuṭumaʿini fáyida". akatwambia: „hamtakawia, ntawapa pembe sasa hivi kwa siku mbili zizi hizi, wakesha rudi watu wangu, waliokwenda kwa mwanangu, nilikopeleka khabari zangu. watakuja na pembe, hawatakuja burre". tukamwambia: „vema, tumesikia".

tukakaa siku mbili, ya tatu tukamwendea: „sulṭani, ʿáhadi yetu imekwisha, tupe pembe zetu, tupate kwenda zetu". akatwambia: „hivi hamna khabari?" tukamwuliza: „khabari gani?" akatwambia: „yule mpagazi wenu siku moja alikwenda kunya kunako maqaburi yetu, hamjui kama vibaya? ao kwenu hakuna vibaya? bassi, mtapata kitu kwangu? si kwa sababu hii?" tukamwambia: „bassi, hapo alipokunya, usingalitwambia tukalipa? sasa ndio unafanya ḥila, wataka kunyanganya mali yetu, kwa sababu umekopa, huna pembe za kutulipa". akatwambia: „si kwa sababu hiyo, nawambia, kwa sababu vibaya tu". tukamwambia: „bassi vibaya mtoto akiḥaribu — si kuruddiwa?" tukafanya mashauri yetu.

usiku tukatoa watu watano, wakenda ḥatta kwa sulṭani Kigongo kule Msiri, wakenda wakampa khabari yetu yote — kwa kuwa: „Mkalikali ametunyanganya mali zetu, tumekuja kumshitakia wewe sulṭani, tuletee watu upesi, waje watudaʿie ḥaqqi yetu kwa Mkalikali".

baʿada ya siku mbili wakatutokea watu, wanatoka kwa Msiri pamoja na watu wetu, wakapiga bunduqi, wakaingia ḥatta mjini, wakamwendea sulṭani, wakamwambia: „Mkalikali umenyanganya waungwana, wape mali yao sasa hivi, wala hatutaondoka sisi". akawambia: „bassi, ntawapa mali yao". akaingia nyumbani,

akatoa pembe kubwa na ndogo, zote pia tano, akatwambia: „haya mali ya waungwana". tukachukua pembe zetu ḥatta kambini.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukapima pembe zetu zote pia, zikatokea frásila arbaʿīn na manni mbili. mkubwa wetu akasema: „sasa safari ya pwani tenna, kwa sababu naona, tutalipa mali ya Wahindi, na siye tutapata fáyida, japokuwa kidogo". tukamwambia: „sasa tupite njia gani?" akatwambia: „tupite njia ya Iramba". tukenda zetu ḥatta Iramba. na huyu sulṭani wa Iramba jina lake Gongotembo. tukakakaa siku moja, tukenda ḥatta Kikuyu porini, hapana nyumba wala mtu. tukapita porini, tukafika Kidete, na siku ya pili tukaenda ḥatta Tshaga porini. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukafika áuwali ya Luemba, na huyo mwenyi mji jina lake Mkorefumo. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu ḥatta kwa Tshewe. akatuuliza Tshewe: „waungwana mnapita njia gani? mtapita njia ya kwa baba?" tukamwuliza: babako nani?" akatwambia: „hamnijui kama mtoto wa Kitimkuru?" tukakaa kwake, akatufanzia ḥéshima nyingi.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu, tukafika Makomba. pana ziwa kubwa porini, lakini hapana mtu wala nyumba. siku ya pili tukenda zetu ḥatta Mweru, pana paḥali pakubwa, mna viboko vingi na mamba wengi, kwa kulla namna ya samaki imo, ḥatta daga limo, ḥatta ushimba umo. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukafika kwa Kitimkuru, kwa mwenyewe sulṭani mwenyi inchi yake.

tulipowáṣili mjini mwake, akatupangisha nyumba, akatwita: „wambieni waungwana waje tuonane. wanatoka wapi huko? wanaacha njia, zinazopita watu, wao wanatokea njia ya pekeyao?" tukaenenda ḥatta kwake, tukamkuta jeshi na watu wake. akatwambia: „waungwana jambo? khabari ya huko mmesikia?" tukamwam-

bia: „hatukuisikia“. akatwambia: „mwanangu amekufa, nnataka sanda kwenu, nizikie mwanangu“. tukamwambia: „sanda itatoka wapi? nasi tunatoka barra, wala hatutoki pwani“. akasema: „bassi, mtafanyaje? na huyu mwanangu amekufa, nendeni mkafanye shauri. msinifanzie kelele hapa, upesi upesi mniletee sanda upesi“.

tukenda zetu kambini, tukafanya mashauri: „jē, sasa tufanyeje?“ tukatoa ʿaqiba yetu nguo tano, tukampelekea. akatwambia: „waungwana nyie wapumbavu — ḥatta ʿaqili hamna! mimi sulṭani mkubwa — mnamletea nguo tano?“ tukamwambia: „tufanyeje? biḍaʿa zimekwisha“. akatwambia: „kama zimekwisha, nije nitwae kwa mkono wangu mimi mwenyewe?“ tukenda zetu kambini, tukatoa bori ya pembe, tukampelekea, tukamwambia: „hii sanda yetu sulṭani, upate zikia mwanao“. akafuraḥi, akawa raḍi.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu, tukafika mwisho wa Luemba. siku ya pili tukafika Mambwe. na sulṭani wa Mambwe jina lake Fambo. tukalala salāma, hatukuona kelele. na vilevile tukapanga vema kwa Tingamanda na kwa Kassonso na kwa Kakungu. hio ndio mwisho wa Mambwe.

tulipotoka hapa, tukaingia Unyamwanga. na sulṭani wa Unyamwanga jina lake Kanamlilo. kwanza akatufanzia vema, lakini ḥatta aṣ-ṣubuḥi na mapema qaribu na alfajiri akatupigia ngoma na bunduqi zikalia. tukapigana. wakafa watu wawili kwetu. tenna wakachukua na pembe moja, wakachukua mzigo moja wa vyakula. ilipopata saʿa sitta, vita vimekwisha. tukenda zetu ḥatta kwa Sambi, na siku ya pili tukafika kwa Serengeni, ḥatta siku ya tatu tukafika kwa Mtanga Holile. hio ndio mwisho wa Unyamwanga.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukenda zetu ḥatta Ubungu. na sulṭani wa Ubungu jina lake Mamsanya. siku ya

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukachukua mashoka, tukenda tukakata miti, tukarudi nayo. tukamwuliza sulṭani: „tuonyeshe boma tulijenge wapi?“ akatwambia: „mji wangu si huu? zungusheni mji“. tukasimama kujenga boma, mudda wa siku tiss'a boma limekwisha. tukamwambia: „kwa ḥeri, twende zetu, kwa sababu kazi yetu imekwisha“. akatwambia: „baṣsi, hamnipi zawadi?“ tukamwambia: „tukupe nini? nasi tumeagana kujenga boma, na leo boma limekwisha, si bassi?“ akasema: „nipeni walau majembe, japokuwa kidogo“. tukampa majembe 'asherīn, akawa raḍi.

tukalala, ḥatta usiku mpagazi wetu mmoja akakamatwa na chui. akachukua shikio lake, sababu tukapiga kelele — mtu akamtupa.

tukenda zetu ḥatta kwa Mawala. tukapanga, tukapeleka mahongo, akakataa. tukamwambia: „unafanya uqorofi wa nini tenna?“ akatwambia: „nataka mwende mkanisa'idie kupiga Wahehe, ndio mahongo yangu, kwa sababu Wahehe huja usiku, wakachukua ñgombe zangu, ḥatta zimekwisha zote“. tukamwambia: „sisi vita hatuwezi. tumetoka kwetu kwenda kuchuma mali, hatukujia kupigana sisi“. akasema: „hampati rukhṣa ya kuondoka“.

tukenda kambini, ḥatta usiku tukatoroka, tukenda zetu ḥatta Marwa porini. tukaingia Marenga Makali porini, hapana nyumba wala mtu. tukenda zetu porini ḥatta Kilimatshanenge. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukafika Tutumi, ndio áuwali ya Kutu. siku ya pili tukafika Mgazi. na huyu sulṭani wa Mgazi jina lake Muhunzi. naye akatufanzia ḥéshima. tukaondoka tukenda zetu ḥatta Kiperepetu. na mkubwa wa Kiperepetu jina lake Kirengawana. siku ya pili tukafika ḥatta Mniyombo. na mkubwa wa Mniyombo jina lake Mangwatwa. tukenda zetu ḥatta Mbamba. na mkubwa wa Mbamba jina lake

Kiratu. kisha tukafika Kole porini, na tenna Mbwiga. na mkubwa wa Mbwiga jina lake Mzeremela. tukenda zetu ḥatta Kirengwe. na mkubwa wa Kirengwe jina lake Mkunguze. na humo mote hamna mahongo. mahongo yamekwisha inchi ya Ugogo, sababu hao washenzi walimwogopa sasa Mzungu kutoza mahongo. nao Wadeutschi wamekwisha ingia barrani, wamejenga maboma pale, kuwaangalia hao masulṭani, walionyanganya safari njiani mali yao, wakakamata na watu wao, wakawatozea mahongo. na sisi tulipopita sasa humo — kazi yetu kula na kulala tu bassi, hatuna gharama kabisa.

tukenda zetu Kidunda. na mkubwa wa Kidunda jina lake Mgumba. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukafika Rufiji, mto mkubwa sana, una mamba wengi na viboko vingi. na huyu mkubwa wa Rufiji jina lake Korogero. tukakaa pale, sababu mkubwa wa msafara akawa hawezi. tukashinda siku saba‘, ya nane akapata hajambo kidogo. tukamtiȧ njiani, akenda akachechema kidogokidogo. tukenda zetu ḥatta Mvuha. na huyu mkubwa wa Mvuha jina lake Makuka. siku ya pili tukafika mpaka Luguru, tukapanda vilima vingi sana, tukapoteana. tukalala mbalimbali, wengine wakalala juu ya mlima, wengine wakashuka bondeni. hatukuonana illa kwa siku ya pili kwa sa‘a tatu, ndipo tulipoonana wote pia.

aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukawáṣili Ziwa la Manse, ziwa kubwa sana, limekaa kama baḥari. na viboko vingi na mamba wengi na samaki wengi. na kattikatti ya ziwa pana nyoka mkubwa sana, na jina lake huyu nyoka anakwitwa nondo. ḥatta mtumbwi hauthubutu kuingia hapo, kwa sababu ya kumkhofu huyu nyoka.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaja zetu ḥatta Lowela. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukageuza njia ya kwendea Ba-

gamoyo. tukenda zetu ḥatta Sungwi. siku ya pili tukawáṣili Mtoni kwa Kidunda, siku ya tatu tukenda zetu ḥatta kwa Mpangile, siku ya nne tukavuka mto wa Ruvu. tukavukia chini — maji yametufika kiunoni. tukaja zetu ḥatta kwa pazi Mrombwa.

kisha kulala tukaondoka, tukaja zetu mpaka Yombo. tukapumzika pale. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukenda zetu ḥatta Dunda. na huyu mkubwa wa Dunda jina lake Djaha. pana mwitu mkubwa sana. ḥatta majumba yao wamejenga ndani ya mwitu, na mashamba yao wanalima ndani ya mwitu. akija mtu, hatajua kama pana mji, illa atajitukia yuko mjini.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaja zetu ḥatta Nsole. tukandika barua kupeleka pwani kwa tájiri yetu — kwa kuwa: „sisi tumewáṣili Nsole, qaribu tutafika pwani. upesi tuletee vyakula na nguo za kuvaa, kwa sababu tu uchi, tunatoka mbali". tukashinda siku mbili, ya tatu tukaondoka, tukenda zetu ḥatta Kanga. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukawásili mashamba áuwali ya Bagamoyo Sanzale. tukaondoka tenna, tukaja zetu ḥatta Tshemtshem, alipojenga daraja bana mkubwa. tukavuka daraja, tukapanga kambi. watu wanakwenda wakarudi, wanaotoka mjini kuja kututazama na vyakula kutuletea. tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaingia mjini Bagamoyo.

tukakuta wametoa ngoma kuu, wameweka uwanjani kutupigia — siwa na zumari. wakatufuraḥia sana. pembe zikenda ḥatta forḍani, na sisi tukenda nyumbani kwetu. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukawaendea wenyewe Wahindi, tukawambia: „twendeni mkatazame mali yenu". wakenda wakapima pembe ḥatta zikesha, zikapigwa chapa ya serkali. khalafu wakachukua ḥatta nyumbani kwao Wahindi, tukawambia: „tufanye ḥesabu, tupate kuwalipa mali yenu". tukafanza ḥesabu

mwanzo ḥatta mwisho, zikakusanyika daftari zote pia. wakajilipa mali yao yote pia, haikusalia kitu juu yetu. tukapata fâyida reale khamso mia. akatwaa mkubwa wa msafara, akatugawia. wa reale mia akampa, wa khamsīn akampa, wa thalathīn akampa, wa ʿasherīn akampa, kulla moja kwa qâdiri yake, ḥatta tukesha wote pia.

hio ndio safari yetu, tuliyokwenda mwaka juzi. na taʿabu yetu iliyotupata ni kubwa. kulla maḥala tulipokwenda, tulipopigana — tumepigana, tulipohonga — tumehonga, tulipojenga maboma — tumejenga, tulipolima mashamba — tumelima, tulipokufa — tumekufa. wala hatukufika qaribu, tenna tumefika mbali. safari ina taʿabu kulala na njaa, kushinda na kiu — hapana raḥa ḥatta marra moja. na mtu, kama hajasafiri barra, haijui taʿabu ya dunya. utaona kulla siku raḥa na stareḥe yako nyumbani mwako — kwa nguo njema, kwa kitanda chema, kwa chakula chema. hujui taʿabu kama watu wanataʿabika — mpaka uende barra, ndipo utapojua, kama kweli barra taʿabu. haiwi kulala chini, na mwendo mchana kutwa — hapana kupumzika — hio ndio khabari ya barra.

# Safari yangu ya Nyassa

**waqati bwana Major von Wissmann alipopeleka stima[1]) katika juto la Nyassa**

ya

**Selim bin Abakari.**

katika mwezi sitta u ʿasherīn märz sene elfu themānie mia tisaʿīn na moja nikaondoka na bana wangu doktor Bumiller Mannheim, tukasafiri Berlin na khalafu Hamburg. kutoka Hamburg katika meli tukafika Amsterdam, Lisbao, Napoli, Port Said, Suezi, Aden, Tanga na khalafu Unguja.

kuondoka Unguja tukasafiri mpaka Mzumbiji[2]), na toka hapo ḥatta Quilimane na Shinde. tukashuka Shinde, tukafanya kambi kubwa sana min ájili ya mizigo yetu, tuliyopakia katika meli „Peters“ na „Wissmann“, kazi ya meli tunayoipeleka baḥari ya Nyassa. na sisi tulipofika Shinde, tulikuwa na kazi nyingi ya kushusha vitu na kuvitengeneza, na kutengeneza namna ya safari itakapoondoka, kwani taʿabu sana zile safari katika mto wa Nyassa. siye hatupiti inchi kavu, lakini mtoni. na mizigo mizito, maṣanduqu ya chuma, na

1) engl. steamer. — 2) Mozambique.

matishali[1]) yaliyokongolewa vipande, na meli[2]) yote ilikongolewa vipande.

kule Shinde tumekaa miezi miwili kutengeneza safari yetu. nasi hatukuwa na wapagazi, tuna ʿaskari tu, Wasuaḥeli na Sudani na Wasomali. kwanza kusafiri kwetu tumeondoka bana Wissmann na bana Bumiller na bana Eltz kutangulia mbele kutafuta kambi. tukasafiri katika matishali na stima yetu inayokwitwa „Pfeil". tukenda panga kambi ya pili paḥali panapokwitwa Msongwe. na Msongwe tumekaa mwezi u nuṣṣu, kungoja vitu vingine vinavyotoka pwani, na tenna kuʿallimisha ʿaskari.

na katika qabila kule ya Msongwe wanakwitwa Wachegunda. nayo qabila hii wengi ni Wareno, wamechanganyika sana na Wareno. nao hujua sana lugha ya kireno. mavazi yao kama Mabanyani. na maakuli ya kule kuna mitama na mahindi na ndizi, na nyama ya kule kondoo na kuku, shidda huona n͠gombe. lakini kuna nyama msituni wengi na mitoni mamba wengi sana. majengo yao ya watu hawa ni kama majengo ya kizaramu, lakini nyumba zao kubwa kidogo.

tulipoondoka hapo, tukenda Msange, ndio mji wa Wengereza. na hapo paḥali hugawana Zambesi na Shire, khaṭari sana kwa nguvu za maji. imepotea watu wengi sana, wamekufa. na mtu akitumbukia katika maji hayo, hapatikani tenna. na siye tumepoteza mtu moja hapa. kule Msange tumekaa qádiri ya mwezi. na hapo ʿaskari wetu Wangoni wametukimbia, kwani waliogopa kufanya kazi, wakakimbia na Wasuaḥeli watatu.

na katika Msange, mtu akiwa na nguo kidogo, yapata żiraʿa nne, hupata kuku thenáʿshara amma kondoo.

1) Stahlboote. — 2) engl. mail.

hapo Msange ndipo paḥali nilipoona mtu aweza koga katika mto, hapana khofu, mamba wa hapa hawaḍuru watu. lakini katika mto wa Zambesi mtu hawezi koga kwa kuogopa mamba wengi. na katika mamba, tuliowapiga, tukaona vikuku vya watu ndani. mtu akiondoka aṣ-ṣubuḥi sana, waqati jua linatokea, kulla paḥali unapokwenda, utakuta mamba na viboko wengi sana.

kuondoka Msange tumepita inchi kavu ḥatta Chiromo, vitu vyetu vimepita mtoni. Chiromo ni mji mzuri kidogo, máthaḷi kama pwani. pale pana Consul wa Wengereza, wako tenna ʿaskari wa Unguja. na aliyokuwa hobsa[1]) wao ni Slemān Maulidi. hapo tulikuwa na furaḥa kidogo, na kazi ilipungua kidogo. waqati ule vitu vyote tumefanza kambi tatu, na vitu mikononi mwa bana Eltz.

Chiromo tumekaa mwezi moja vilevile, tukenda kupiga nyama sana. na kule Chiromo ukenda katika mbuga, huweza kuona nyama wa mwitu kwa marra moja hupata elfu, nyama wa mwitu namna nyingi sana. kuna mbogo wengi sana, kuna chui, kuna simba.

siku moja tumekwenda kupiga mbogo na doktor Röver pamoja. tumekwenda katika mbuga waqati wa maghribi; ilikuwa ilifanya jiza kidogo, khalafu mbaamwezi ikatoka. mbaamwezi ilivotoka, tukajongea mbele kidogo, marra tukaona weusi kama boma lililojengwa, bana Bumiller kasema: „nini hii?“ Washenzi wakatwambia: „mbogo“. hatukuṣadiqi. bana Bumiller akamwamrisha ʿaskari moja Mgazija, jina lake Saleḥ, kamwambia: „nenda katazame“. yule Saleḥ akachukua bunduqi yake, akapiga magoti, akenda ḥatta akafika qádiri ya żiraʿa tisʿa, akawakuta kweli ni mbogo.

---

1) farbiger Offizier, verstümmelt aus dem engl. officer.

akarudi, akaja, akasema: „mbogo“. bana Bumiller kasema: „haya tupige“. tukajongea kidogo ḥatta hapo walikuwako. walipotuona wakatawanyika, wakabaqi wawili. marra bana Bumiller akaamrisha bunduqi sitta zikapigwa. kupiga — wale mbogo huzidi kuingia ukali kutujia mbele. doktor Röver alipoona, wametujia qaribu, alitupa bunduqi, akakimbia juu ya mti na boi wake vilevile. bana Bumiller alisimama na ʻaskari moja Jumaʻ bin Mwinyi, naye hodari sana. bana Bumiller akápiga moja, akazidi kuamrisha kupiga bunduqi, khaláfu yule mbogo mwingine akakimbia. ndio siku niliyojua, kama kweli mbogo mkali sána. hapana kitu khaṭari kama kupiga mbogo, khaṣṣa ákiwa pekeyake.

tukaondokä Chiromo safari ya Katunga. tukapita inchi kavu, mwendo wa siku nne tukafika Katunga. ndio mji wa Wengereza. hapo tukajenga kambi ya nguvu min ájili kungojea safari nyingine ya nyuma, inayoleta stima na mashua na mizigo. na Katunga tumekaa sana, na kazi ya hapo ilikuwa ngumu sana. ʻaskari pale lázima wachukue matishali kuyapeleka Blantyre. ndio użia sana, sababu kupanda kilima, na kipande kimoja lázima kuchukuliwa na watu sittaʻshara. yapata kuchukua siku nne wakichukua vile vipande, na mtu akienda hana mzigo huenda siku moja u nuṣṣ. bana Bumiller alikuwa na kazi sana, maʻana kazi ya kupeleka vitu juu yake, ḥatta miye nilikuwa nikimwona ḥuruma jissi alivotaʻabika.

mizigo mingine walikuwa wakichukua hao Wangoni, walioʻajiriwa katika Katunga na Blantyre. kulla mtu hupewa żiraʻa nane amma ushanga kwa safari moja toká Katunga ḥatta Blantyre, amma toka Blantyre ḥatta Mpimbi. waanawake wa Wangoni wakachukua nao vilevile pâmoja na waanaume. wale wakubwa wao huitwa capitano. siku moja huja wapagazi

mitēn, siku nyingine wapagazi khamso mia ḥatta sitta mia, haina qawā'ida. na ushanga wa kule hufa'a ushangá „kijani kiviti" nà „maji ya baḥari". watu wa kule hupenda sana ushanga, ndio uzuri wao.

tulipokaa Katunga, ilikuwa ikiingia ghấfula ya 'askari wa Sudani, walitaka kutoroka. na sababu — 'askari moja ndio aliyofanya fitna hii, jina lake Ibrahīm. kazi yake ilikuwa akimsa'idia bana doktor Röver kazi yà daktari. akiwambia 'askari wengine: „tukimbie, sababu kazi hii kazi ngumu, hatuwezi kuchukua mizigo". na katika mizigo ile huchukuliwa si kwa nguvu, lakini matájiri wetu waliwanáṣiḥi 'askari wetu kwa tafaḍḍali, ya kuwa wachukue zile mashua, wapeleke upesi, safari ipate kwenda mbele. ma'ana wangechukua wapagazi, wangaliḥaribu, ma'ana hawàjui, ya kuwa zile màshua ni mali. lakini 'askari walijua kama mali, na tenna manfa'a kwetu zikifika salama. 'askàri wengine katika ile tafaḍḍali walifuraḥi, nao wametambua, ya kama wakichukua wapagazi — zitaḥaribika, bassi afaḍḍali hii ta'abu tupate wenyewe na mali ifike salama. walakini wale Sudani walisikia khabari ya fitna, ikawaingia kichwani, wakafanya shauri moja kutoroka. siku waliyotaka kutoroka, alikuwa 'askari moja katika jama'a ya hawa Sudani, alikuwa hawezi sana. naye áṣili yake ni Bárbar, jina lake Murjān, naye àlikuwa mpishi wa matájiri wetu. alikuwa rafiqi yake ya yule Ibrahīm, akamwambia: „utafanya shauri gani sasa na weye huwezi? 'askari wote wa Sudani watakimbia". yule akaingia khofu, akamwita mkalimani 'Othmani bin Sa'id, akamwelezea khabari zote. 'Othmani akenda akamwambia bana Bumiller. marra bana Bumiller akaamrisha tarumbeta [1]),

1) **Trompete.**

akakusanya 'askari wote. wakaja wakafunga kulla namba[1]) mṣafa wao. akawambia: „leteni silaḥa zote“. wakatoa silaḥa. akamwita effendi[2]) wa Sudani Faraji na mashaushi[3]) wote, akawauliza shauri waliyo nayo. wakataka kutuficha. bana Bumiller akawaelezea khabari zote, ya kama amesikia walitaka kutoroka wote. wakasema: „kweli, lakini fítina hii ameileta mtu moja“. akawauliza, wakamwambia: „Ibrahīm ameleta fitna hii“. bassi bana Bumiller akawambia: „kama mkiona neno msilolipenda, bassi nambieni, lakini kukimbia haifai, ma'ana kazi hii hatuwezi kuwashuruṭiza kwa nguvu, illa kwa tafaḍḍali na ḥesani. na nyie mnajua, ya kama mtapata ḥéshima juu ya kazi hii, na mshahara utazidi. na nyie mnaona wenzenu Somali na Wasuaḥeli hufanza vilevile. na siye Wazungu tunasumbuka vilevile kama ninyi katika kazi hii, hapana mwenyi stareḥe hapa ḥatta moja, si mtu mweusi, mala Mzungu, wala Mw'arabu — wote tunasumbuka katika kazi hii“. mwisho yule Ibrahīm akachukuliwa akafungwa.

na siku ile sisi watu wanne tukafanya zamu kwa bana Bumiller, sababu tukaogopa wale Sudani wasije kufanya shauri kumpiga bana Bumiller. ḥatta siku ya tatu, tulipoona imewaelea ile khabari, hatukulala zamu tenna.

zile mashua zikachukuliwa zote pamoja na mizigo ya vyakula kupeleka Blantyre. bana mkubwa akatangulia Mpimbi kufanya kambi, yeye na bana Fuchs, na bana Bumiller akakaa na mizigo. waqati ule kazi ilikuwa nyepesi, sababu hapana vilima. na Blantyre kulikuwa kuzuri sana, tumekaa kama kule pwani. kuna maduka ya Wäzungu, kulla kitu unachokitaka hupata.

---

1) engl. number. — 2) farbiger Offizier. — 3) farbiger Unteroffizier.

ḥékima nyingine kuchukua mashua ndogo kufungasa matishali ná kuyavuta. ḥatta jioni siku ya tatu tukawáṣili milangoni mwa mto, unaokwenda Fort Johnston. na pale ḥatta Fort Johnston ni siku moja. siku ile tukafanya kambi nyingine, siku ya nne tukafika Fort Johnston.

tulipofika tukaona furaḥa kidogo. tukaona jamaʿa wa Unguja, waliofuatana Wengereza kama ʿaskari. nao wamekaa kule kama ndio kwao, wameoa Washenzi, wamezaa nao. na yule sulṭani wa kule huitwa Mponda, na kule kwake mji wake huitwa vilevile Mponda. naye amepiga sana na Wengereza, lakini sasa wamemshinda.

na pembe kule nyingi sana, pembe inatokea Hiyao na Nyassa na Utonga. na Wangoni huleta kule pembe nyingi. nako kuna neʿema sana ya mtama na mchele na mahindi na muhogo na viazi. tenna kuna kondoo na kuku wengi sana, na nyama wa mwitu wengi mno. na watu wa kule hulewa pombe sana. katika inchi hizi zote, tulizozipita katika safari yetu, hupenda kulewa pombe.

Fort Johnston hatukukaa sana, yapata labda siku sabaʿ. tukasafiri katika stima ingereza, wakafungasa matishali yetu kutupeleka Konde. na baḥari ya kule mbaya sana, ina mawimbi, ikichafuka — mtu hawezi kula chakula. afaḍali baḥari ya chumvi, mtu huweza kustaḥamili kuliko baḥari ya Nyassa.

kutoka Fort Johnston ḥatta siku ya tano tukapata chombo cha Waʿarabu, waliopakia watumwa. na siku ile hatukuingia katika sitima ya Wengereza, tumetweka wenyewe matishali yetu. tulipoona kile chombo cha Waʿarabu, tukawambia watue. wakakataa, tukaweta marra tatu — hawakusikia. marra ya nne tukaweta — hawakujibu — tukapiga mzinga, nao wakajitupa ba-

ḥarini wote wakavukia pwani. hatukuwapata, wámekimbia wote, na kuwapiga wenyewe hatukutaka.

tukaondoka tukenda tukajenga kambi nyingine katika kisiwa cha Watonga. wale Watonga hupenda kukaa visiwani, sababu wanaogopa Wangoni. ma'ana Wangoni huja wakawapiga Watonga, wakiwachukua, wakiwafanya watumwa wao. na mno ukimwona Mtonga humkuta na tundu za kingoni mashikioni — bassi mtu hujua, ya kama huyu amechukuliwa na Wangoni. ukitaka kumqaṣiri Mtonga, humwambia — ya kama „weye mtumwa wa Wangoni“, huqaṣirika sana. na machezo yao ya kivita ya kimafiti. na 'ajabu yao hujigeuza majina ya ki'arabu, na jina lake, alilolipewa na wazee wake, halitaji. atakwambia „miye Seyyid Barghashi“, mwingine „miye Seyyid 'Ali“, mwingine „Moḥammed bin Salim“ amma „Moḥammed bin Khalfān Rumaliza“. wao hawajui ma'ana ya majina, wanataka majina ya ukubwa tu.

nao Watonga welevu sana. wakikaa na watu wa pwani siku kidogo, hujua upesi maneno yao. na khabari ya amri wakifundishwa, hujua upesi. nao hodari ya kazi. na siye tulipofika kule Rumbira [1]), bana Bronsart ameleta Watonga, ili kuja kufanya kazi ya upagazi. nao walikuwa hodari sana. nao tenna hodari kuchukua machera [2]). ikabidi ya kuwa mtu akiwa hawezi katika safari humchukua siku nyingi na miezi mingi katika machera. nao sasa ndio 'askari wanaotumika kule Konde kwa Wadeutschi na Wengereza.

siku tuliyofika Rumbira, tukashuka tukafanya kambi pwani. na wale Washenzi, waliokuwa pale, walistuka, wakat͟hanni vita. tukajenga kambi yetu. tukakaa ḥatta siku ya pili, ili kutafuta paḥali pengine pazuri tujenge,

1) Langenburg. — 2) Hängematte.

lakini hatukupata, palepale tuliposhukia ndipo tulipojenga. tenna vikashuka vitu vyote katika matishali, tukaanza kujenga mabanda.

ḥatta siku ya tatu usiku walipolala, ilikuwa mvua sana na ḍarba. na ʿaskari, waliokaa zamu kutazama matishali, hawakuangalia vema, matishali mawili yamevuta nanga, yamekwenda baḥarini. shaushi alipoona matishali hayapo, akapiga kelele. marra akaondoka bana Major na bana Bumiller kuwambia watu wote, ya kama matishali yamepotea. bana Major ameqaṣirika sana. marra ʿaskari wakachukua tishali lililobaqi na mashua ndogo, wakavuta wakenda kutafuta yale matishali. ḥatta qaribu na al-fajiri wakayapata wakayaleta. tenna tangu siku hiyo matishali hapana rukhṣa kukaa pekeyao illa kulaliwa kulla tishali watu wawili.

tukakaa pale Rumbira, tukajenga boma. tukesha tukajenga na mabanda ya ʿaskari na majumba ya kutia mali. qádiri ya mwezi moja tumejenga pale. mwezi wa pili bana Major akaamru, yeye na bana Bumiller wagawe safari, wende wakatazame inchi kwenyi amani na kwenyi ukháṣama. bana Bumiller ikabidi, ya kuwa yeye kupanda vilima kwenda Ukinga.

waqati ule tulioondoka pale, hatukujua, ya kama pale inchi, inayokwitwa Ukinga, illa tulipokwenda, wakatwambia wao wenyewe, waliozaliwa kule, ya kama wao Wakinga. na kutoka Rumbira ḥatta kufika Ukinga siku tatu vilimani, hapana áṣili ya mtu, huoni mtu wala nyumba, vilima vitupu, wala hapana bonde, hupanda hushuka vilima tu. na paḥali pa kupigilia ḥema hapana. tukitaka kulala, huchimbia udongo amma hujengea mawe — mtu akalala, kwani khofu mtu asije kuporomoka chini.

siku ya tatu tukafika Ukinga. na kule hapana mji, kulla mtu hufanza kibanda chake katika shamba lake.

inchi ya kule nzuri sana kwa kutazama kwa macho na vilevile kwa kulima, sababu udongo wake wa inchi hii mwema sana, hufa'a kulla maakuli kupanda. na n̄gombe na kondoo wengi sana kule. na miti ya huko mianzi mingi sana na tenna mizuri. nyumba zao miti wanayojengea mianzi. hufunga mianzi sitta ḥatta saba' majukwaa [1]), na miamba miwili huzungusha kama boma, yatosha kwa watu wawili amma watatu kulala. na mtu akiwa mbali, hatambui kama ndio nyumba ya bin Adam, huthanni kama majani yamewekwa, lakini kinachotambuza ni moshi wa moto.

hawa Wakinga hawakupata bado kuona Mzungu. walipoona matájiri wetu weupe, walishituka, wakaogopa sana. tukawauliza wakatwambia, kama ndio Wazungu wa kwanza, walioingia katika inchi yao. nao hawana nguo, lakini nguo zao hutwaa majani, huweka mbele ya utupu. na waanawake hupandisha winda wa majani. na katika bi'ashara, tuliyofanya, hutwaa nguo hukata qádiri ya nyanda [2]) tano, ndio tunanunulia vyakula na kuku, nao hupandisha winda na zile nyanda tano.

na mtu akiwapa kitu kidogo kama nguo, amma kitu kingine, aḥsante yao hucheza kama nyani, hufanya é-é-é, hukuna vilevile mbavuni kama nyani. nao hukaa qádiri ya robo' sa'a kwa furaḥa yao kucheza kama nyani.

kwanza waliogopa sana kuja kwetu kambini, ḥatta mwisho wakatuzoea min ájili ya kupata vitambaa. nao wakikimbia hukimbilia vilimani wote, hupiga makelele, huitana wote pamoja. na ukisimama kilimani, ukapiga kelele, watu wote bondeni husikia. ukelele wao vizuri sana kusikia, hupiga kelele na ṣauti kubwa mfano wa kwimba.

---

1) Gerüst. — 2) Fingerdicke.

ba'ada ya siku tano ao sitta tukaondoka, tukauliza njia ya kwenda Usango. wakatupa mkalimani moja, anayejua kisango na maneno ya Ukinga, kutupeleka tufike Usafa. tukapita tenna inchi ya Ukinga. na katika 'ajabu, iliyotupendeza katika ile inchi, ina maji mengi. ukenda mwendo wa nuṣṣu sa'a, hupata bonde la maji, na ina ne'ema sana. na maakuli wanayopanda wenyewe: mbaazi za kizungu na kunde na mawese [1]) na nyangwe [2]) na mahindi mengi sana. mtu mwenyi 'aqili akipita hapa, anajua inchi nzuri ya kulima na 'afya.

tumekwenda mwendo wa siku nne tukafika Usafa. katika mpaka wa Usafa na Ubena, paḥali tulipojenga kambi yetu Usafa, palikuwa nyumba kidogo. tukakuta na kambi ya Wahehe, waliotoka siku hiyo katika kambi yao, wakanyanganya ñgombe ya Wasafa hao. na hawa Wasafa wakatwambia, kama leo amma kesho aṣ-ṣubuḥi watarudi hapa. siye tukalala katika kambi yao. ilikuwa zamu kubwa siku ile min ájili kuwakhofu Wahehe. hapana mtu aliyolala, kulla mtu silaḥa mkononi. ḥatta usiku wakaja hawa Wasafa wakatwambia, Wahehe watakuja sasa hivi. na siye tulikuwa na bunduqi arba'īn na tano na mzinga moja na bombom moja. 'askari wakaondoka wote, wakawekwa maḥali pao. na Wazungu hawakulala ḥatta kidogo. tukaangalia sana, lakini ḥatta aṣ-ṣubuḥi hatukuona mtu.

ikaondoka safari tenna, tukaingia kattikatti ya inchi ya Usafa. na katika inchi ile vilevile vilima kama kule Ukinga, lakini vikubwa kuliko kattikatti ya Ukinga. watu wa kule huwakuta mojamoja huvaa nguo. inchi yake vilevile nzuri sana, ina maji tele, ina ne'ema ya mtama na mahindi na viazi na migomba ná mawese

---

1) kleine schwarze Kornfrucht. — 2) Batatenart.

mengi. na salāmu zao watu wa kule wakikutana, hukaa robo' sa'a huamkiana, hukusanya mikono pamoja, husema robo' sa'a „āje, āje". wao hujua kidogo khabari ya pwani, kwani wako katika ura'ia wa Merere wa Konde huona Wa'arabu waliotoka pwani.

nyumba zao kama nyumba za Wakonde, hujenga na mianzi na miti. kuna miti mingi na mikubwa sana. mtu akiingia mwituni, hawezi kuona jua. na kule mwituni kuna tumbiri wengi sana. tumepiga tumbiri wengi, waliokaa mitini. nao wakitutisha, killa siku wakitwambia, kàma Wahehe wanakuja. wale wanaogopa sana Wahehe. watu wa kule Usafa wanaqubali kazi ya upagazi, lakini Wakinga hawaqubali kabisa.

tukaondoka Usafa kushuka kwenda Usango. tukàkaa siku mbili njiani, siku ya pili tukafika paḥali qaribu na Uténgure. napo pana mji mdogo. tukafanya kambi pale. tukakuta mtu moja wa pwani pale, jina lake Mwenyi Tshande, naye mkalimani wa Merere. tukamwuliza: „unatoka wapi?" akasema: „natoka Uténgure". tukamwuliza: „hapa ḥatta Uténgure sa'a ngapi?" katwambia: „huchukua sa'a mbili". tukamwuliza: „tutaweza kufika leo?" akatwambia: „afaḍali laleni hapa ḥatta kesho, sababu hamkupata rukhṣa ya Merere ya kufika Uténgure. nami ntatangulia nikampasha khabari, ya kuwa wamekuja Wazungu, nao Madeutshi, wanataka kuonana nawe. labda atanipa rukhṣa kuja kuchukua ninyi, ma'ana hiyo ndiyo kazi yangu kupeleka wageni kwake". khalafu akaondoka, akenda zake Uténgure kumkhubiri Merere.

ḥatta usiku wale wazalia pale mjini wakataka kututisha wapate kutunyanganya. waliondosha watu, waliwapeleka nje, ili kattikatti ya usiku waje watwambie „Wahehe wanakuja sasa hivi". na wale watu walikuwa watatu. hutokea mojamoja, hujifunga silaḥa zake,

huja kwa ghâzia na kutoka jasho, hutwambia: „Wahehe tumewacha hapo qaribu, sasa hivi wanakuja". sisi tuliamka, tukachukua bunduqi zetu, tukazungusha boma letu, tukakaa ṭayyari. lakini siye tulikuwa tukijua, kama uwongo, wanatutisha, wapate kunyanganya. na ile ʿaqili yao haikuongoka.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi akatokea yule Mwenyi Tshande, katumwa na Merere kuja kutuchukua. tukenda mwendo wa saʿa mbili tukafika Uténgure. tulipoqaribia mjini, tukaona bendera ya kideutschi, tukafuraḥi sana tulivoiona. kufika mjini Mwenyi Tshande akatuonyesha paḥali qaribu ya mji, akatwambia: „jengeni kambi hapa, na miye nakwenda mjini kumkhubiri sulṭani, kama umekwisha fika". akenda zake mjini, akakaa mudda wa saʿa, akarudi akaja kambi akatwambia: „ngojeni kidogo, atakuja wakili wa Merere kuja kumchukua bana Bumiller, akaonane naye". ilipopita saʿa moja, akaja mtu moja, akatwambia, kama Merere leo hawezi kuonana na Wazungu. marra bana Bumiller akamwambia Mwenyi Tshande, ende akamwambie Merere — kama: „sisi hatuwezi kungoja hapa siku nyingi, bassi afanze leo tuonane, mudda wa saʿa moja nataka majibu yake, amma kama hataki, ntakuja miye mjini billa rukhṣa".

akenda Mwenyi Tshande mjini, akenda kamwambia Merere, — kama: „Wazungu hawataki kungojea sana hapa, wanataka shauri yao ishe upesi. bassi wâjibu wako kuwaqurubisha kwa ḥéshima billa kuingia wenyewe mjini, ndio mrua[1])". Mwenyi Tshande akaamrishwa na Merere na mawaziri watatu, kuja kutuchukua kwenda kuonana na Merere. bana Bumiller akafuatana na bana Illich na ʿaskari tisʿa. tukaingia mjini, tukenda katika tembe lake. na kattikatti tembe lake

1) Achtung, Respekt.

imezungushwa boma na kattikatti majumba. na majumba hayo ni nyumba zake mwenyewe na masuria yake. tulipokwenda tumewekwa ukumbini, naye bado hakuja katika ule ukumbi. tukakaa qádiri ya nuṣṣu sa'a ili kumngojea. bana Bumiller akaužika, akamwuliza Mwenyi Tshande: „yuko wapi Merere?" na kulla akiuliza, husema: „sasa hivi atakuja". akamwambia: „kama sasa hivi haji, mimi taondoka, sitaki kuonana naye, bassi mwambie upesi". akaingia ndani, akenda akamwambia. marra tukaona watu wanakuja, wakamleta katika baraza. akaja akakaa kitako akatwamkia. lakini kutwamkia ni kisango „āje mwanamtwa! āje, āje, āje", watu wote kuamkia kwa qauli moja „āje, āje". wakageuza „tuhongeje, tuhongeje, ā ā ā ā!" na katika salamu hiyo huchukua sa'a nzima ḥatta watakápokwisha.

walipokwisha kuamkia, akawanza kutuuliza khabari. naye akiuliza, hamwulizi mkalimani wake, la, lakini humwuliza wakili wake. na yule wakili wake humwuliza mkalimani, na yule mkalimani huniuliza mimi, mkalimani wa bana Bumiller, na mimi nikamwambia bana wangu kwa kideutschi, na maneno yake ya bana Bumiller hujibiwa vilevile.

naye alianza kwa kufuraḥi, ya kwamba amekuja Mzungu, na bado Mdeutschi, ma'ana tangu Wadeutschi walipoingia katika barra ya Afrika hakupata kwenda Mzungu Uténgure, illa hawa mapadri [1]), alikwenda mtu mmoja. naye alikuwa na hamu sana kuonana na mtu wa sirkali. bana Bumiller akamwambia — ya kuwa: „mimi nimeondoshwa na bana mkubwa Wissmann kuja hapa kukutazama na kutazama inchi nyingine, tusizozijua, na watu wengine, wasio na bendera ya kideutschi,

1) **Missionare.**

tuwape bendera. nami nimefuraḥi nilipokuja hapa, marra nimeona bendera ya kideutschi, marra nimejua weye ni rafiqi ya sirkali deutschi". bassi waqati ule akasema Merere: „tafáḍḍal nna mashauri nataka kusema nawe. tafáḍḍal ngoja ḥatta kesho, uje mchana tuonane tufanye mashauri haya". khalafu tukaondoka tukenda zetu kambini.

ḥatta siku ya pili tukarudi kwa Merere. na tulipokwenda hatukumkuta ṭayyari, lakini lázima kumngojea saʿa nzima. na bana Bumiller hastaḥamili. lázima kumtuma mkalimani, akenda akamhimiza. ḥatta ilipopata saʿa, akatokea barazani. alipokuja barazani, kaanza salām yake, nayo yaḥitaji siku ile nuṣṣu saʿa ḥatta yakisha. akamwuliza bana Bumiller, ya kwamba ataka sikiliza khabari ya Uhehe, shauri gani? maʿana amesikia khabari ya bana Zelewski, ya kwamba amepigwa na Wahehe. nao ulikuwa mṣiba mkubwa wa Madeutschi, na yeye Merere vilevile ana mṣiba, maʿana hawa Wahehe kháṣimu zake tangu zamani. akamwambia tenna: „wamenifukuza katika inchi ya babangu, wamenileta ḥatta huku Usafa, maʿana huku Uténgure ni Usafa. nami naomba duʿa kurudi katika inchi ya áṣili yetu, bassi iwapo mtaweza nyie Madeutschi kunitilia msaʿada, twende tukapigane na Wahehe. miye ntaweza huu upande wangu kuzuia, na nyie mwanze pande nyingine, lakini nileteni qadri ya ʿaskari mitēni na Wazungu wanne, na miye ntaweza kuwapitisha ḥatta waingie Uhehe". khabari ile kamfuraḥisha bana Bumiller, akamwambia: „aḥsante sana, shauri hili tunataka, lakini lázima niende nikamkhubiri bana mkubwa Rumbira".

akatufahamisha tenna na mshenzi moja, áṣili alikuwa ḥádimu yake, jina lake Kimaraunga, akatwambia, kama anataka kwenda kumpiga. maʿana sasa ametakabbari yule ḥádimu, ḳichwa chake kikubwa, sasa ame-

pata mali, amejitenga mbali, anataka kumpiga bana wake. bassi bana Bumiller, kama ataweza, atafaḍḍali siku hiyo tuondoke tukampige Kimaraunga. bana Bumiller akamwuliza: „itachukua siku ngapi toka hapa ḥatta kufika huko kwake?“ asema: „huchukua siku tano“. akamjibu: „siwezi kwenda huko, lázima nirudi kwa bana mkubwa kwanza, kwani hakunipa amri ya kupiga watu billa sababu. bassi nieleze khabari yake vema, nikamkhubiri bana mkubwa. akitoa rukhṣa, tarudi kwenda kumpiga amma kufanza ṣuluḥu mpatane“. lakini katika ʿaqili ya Merere hakutaka ile ṣuluḥu, ázima yake ni kutaka mpiga Kimaraunga, amnyanganye pembe, yateke, na watu wake afanye watumwa. hakujua, kama Wazungu hawataki kunyanganya.

akazidi kuleta mashauri mengine piga Washenzi wengine, waliomo qaribu ya inchi yake, wasio nguvu. akatwelezea na mshenzi moja, aliyo qaribu ya Uténgure, mwendo wa saʿa mbili tu, akatwambia, mshenzi huyu humżarau, bassi ataka amwondoshe katika mji wake, amma amwadabishe awe chini ya miguu yake. na yule mshenzi anamsumbua Merere sana. maʿana katika mji wake Merere hawezi kuingia — imezungushwa kwa ḥandaqi mbili za maji, ni áṣili kutafaḍḍali sisi kwenda kumpiga. walakini katika ʿaqili ya bana Bumiller alijua, kama yule Merere hataki wale Washenzi wadogo wenyi miji yao pekeyao kujikalia billa kwa ḥokumu yake, ataka yeye ḥokumu pekeyake katika barra hii yote. na bana Bumiller humwitikia: „vema, lakini amri shurṭi itoke kwa bana mkubwa. akisha toa amri bana mkubwa, lázima ntapiga. lakini vibaya miye kuletwa huku kuja kufanya ṣuluḥu na kuweka bendera — kuja kuwapiga watu burre, nao hawana sababu waliyonitenda“. Merere akashika ṭamaʿa, ya kuwa bana Bumiller arudi Rumbira, atakwenda kum-

tengenezea maneno mazuri kwa bana Wissmann, apate kuwapiga Washenzi, waliomo katika pande za Usango.

tukakaa siku nne kwa Merere. na kulla siku huleta chakula cha 'askari ñgombe na unga, na Wazungu wakaletwa kondoo wanne na kuku na mayayi. tukamwaga, tukamwambia: „tunataka rudi Rumbira". akatoa watu na pembe mbili, kulla moja frásila tano, kwenda kumwamkia bana mkubwa Wissmann. akamwamrisha yule mkalimani wake Mwenyi Tshande na watu wake heda'áshar, ili kutwonyesha njia kuturudisha Rumbira.

ametupitisha vilima vya Usafa kushukia Konde. na katika njia, aliyotupitisha, ilichukua siku sitta ḥatta kufika baḥari ya Ñyassa. njia hiyo ina mianzi sana na mitu ya miti mingine mikubwa sana. na mtu akitoka na mitu hii ya mianzi na miti mingine hushukia Konde.

na siye tulipokuja Konde, ilikuwa inchi nzuri sana tuliyoiona. na watu wa kule watu wa nguvu sana, lakini hawavai nguo. katika nyumba zao naḍifu. wao na ñgombe wao hulala katika nyumba moja, lakini mchana, mtu akiingia katika nyumba, akiona ule unaḍifu, hajui kama kulikuwa ñgombe. nao wana ñgombe na kondoo wengi wa 'ajabu. kulla mtu huwapenda ñgombe wake kama mtoto wake, ndio sababu hutwaa ñgombe akawalaza katika nyumba. naye haoni uchafu ya kuwa haya mavi, anaona bora kama lulu, hutwaa mavi akajengea nyumba yake. na ñgombe wao, akimwona bwana wake, humtambua.

nao chakula chao mno maziwa na ndizi za kuchoma. tenna kuna vyazi vingi sana, kuna magimbi [1]), kuna mahindi, kuna mtama na mawese na vyazi vikuu vingi sana na muhogo na mbaazi na kunde na chooko na chooko za kizungu.

---

1) Batatenart.

lakini chakula chao kizuri wanachopenda sana ni ndizi. vyakula hivo vyote hufa'a katika inchi, udongo wake ni mwema, haukatai vyakula. kulla waqati hulima, ikiwa jua hulima, ikiwa mvua hulima. na tenna vyakula vyao vyote rakhiṣi. mkono wa nguo hupata mikungu miwili ya ndizi, huwezi kuichukua pekeyako. amma hupata pakacha la vyazi, huwezi kuvila siku kumi. na malesi mizigo miwili ya watu wenyi nguvu hupata kwa mkono na nuṣṣu, na mbuzi hupata kwa upande wa nguo, na kuku hupata wawili kwa mkono moja, na mayayi thalathini kwa mkono moja. wao wenyewe hawali mayayi, hufuga bassi. wageni, wanaokuja katika inchi, ndio wanaokula kama Wazungu na Washenzi wengine, wanaotoka katika inchi nyingine. wao wanakula samaki na nyama ya n̄gombe na nyama ya kondoo na nyama ya mbogo na nyama ya kiboko na mamba wanakula. hula nyama mbichi kabisa ao ya kuvunda, ma'ana wanaacha nyama hii, wakichinsha siku mbili tatu, hawatii chumvi, na nyama huvunda. hawana chumvi katika inchi yao. wakiona chumvi hupigania ile chumvi. hubugia chumvi, hawataki kuunga. chumvi ndio ghali. ukiwa na chumvi, utapata kulla kitu utakacho katika inchi ya Konde. ukitaka n̄gombe utapata kwa chumvi, ukitaka mbuzi utapata, ukitaka mtumwa utapata kwa chumvi, ukitaka pembe utapata kwa chumvi. ukitwaa gao [1]) la chumvi, utapata chakula cha siku tano.

inchi ile ina ne'ema sana. hapana inchi nzuri katika inchi ya kideutschi ya Afrika yote kama Konde. inchi yenyewe ina udongo mtupu, na popote maji mengi sana. kulla kitu chafa'a kupanda kule Konde. na mtu akiwaona wenyewe, waanaume na waanawake, jissi wa-

---

1) Handvoll.

livo na nguvu na ṣura nzuri, hujua kama kweli inchi ya ʻafya. nao tenna wakubwa sana Wakonde. na umardadi wao katika mikuki, huichukua qádiri ya mikuki mitano, mikuki minne huwa mkononi moja na mkuki moja huwa mkono wa kulia.

huzuka nywele zao, hutwaa mafuta hujipakaa mwili mzima. bassi mwili wake hun͠gara kama chupa. na akenda mtu, huthanni anatoka jasho, lakini ni mafuta yanayochiririka. nao wakenda katika njia, huenda kwa tartibu na majivuno kwa mguu mojamoja kupiga mguu chini sana kutingisha inchi.

na machezo yao hupiga ngoma, hucheza manamme na mwanamke. mwanamke hutingisha kifua na mwanamme huruka akitingisha kifua na kupiga miguu chini na mikuki yake mikononi. na mtu akiwa mbali, akisikia machezo yao Wakonde husikia inchi kutingishika jissi wanavopiga miguu chini kwa nguvu. nao hawembi, lakini hunguruma tu, kwa jissi wanavoona nguvu. na ukimkuta Mkonde katika migomba, hatazami mtu kwa kiburi chake, husema dunya yao pekeyao, sababu huona hapana inchi kama inchi yao.

na mtoto akizaliwa kwao, kwa siku ya pili hutoka nje kwa ájili hawana stara. hutwaa udongo mwekundu, wakampaka mama yake, humfungia huyu mtoto mgongoni. kwa siku ya kumi ya kuzaliwa mwanamke anakwenda zake huko mashamba, akenda kulima na mtoto. na mwanamke akichukua mimba, ijapokuwa mwezi wa tisʻa, hana stara. hana nguo illa majani ya mgomba. hana chakula kilicho ni cha mgonywa, chakula chake hageuzi. na chakula cha mtoto ni maziwa na ugali na ndizi na malesi. mtoto huyu huchukuliwa mgongoni wa mwanamke ḥatta khátima yake. akisha kua hasomi, kazi yake kuchunga n͠gombe na kulima. waanawake na watoto hulima, waanaume huchunga n͠gombe bassi.

wakioa hufanya karamu ya pombe la ndizi na maziwa ya ndizi za kuchoma. hucheza machezo yao, hutwaa ngoma, wakajizungusha uanjani, watu wawili huwa katti. hupiga ile ngoma, na mwanamme hucheza na mikuki, na mwanamke hucheza kwa mabega. mwanamme hupiga mguu chini, akatingisha na mabega. wakisha mchezo wao hutoka, wakavaa kengele miguuni vijana wa ḥerīm moja. huchukua mikuki wakicheza wakipinduka na kwenda mbio. na mwendo wao sawasawa, miguu hupiga chini mshindo moja. huenda kulla paḥali palipo jamaʿa yake. na wao hufaraḥiwa hutoa n̄gombe na maziwa. hii ni furaḥa yao. wakesha kukusanya, wakenda zao, hugawa nuṣṣu kwa nuṣṣu, wakampa bana ʿarusi na nuṣṣu huchukua wao. nao hawapendi mtu mwingine aoe watoto wao, shurṭi wao wenyewe kwa wenyewe waoane.

hawafanyi vita na watu wengine, hupigana wao kwa wao. silaḥa zao mikuki, hawana bunduqi, hawana mishare. lakini wao hodari sana, hawaqubali kujenga boma, wameṭumaʿi mikuki yao. wamekaa katika migomba yao, wanasema „hapana watu kama sisi kwa uhodari". wakitokea waungwana hurudi nguvu zao. huwaṣiḥi husema „hapana watu kama waungwana", kwa ájili wanaona zile bunduqi, wanaogopa kuliko radu. wanasema: „waungwana tusiwapige, kwa maʿana hawana daʿawa, huleta vitu tukinunue, na neʿema katika inchi tuwafanze, ni ndugu zetu". wakiona mshenzi anapita katika inchi yao, hawaqubali, humpiga, husema: „hawa wanakuja kutuchukulia n̄gombe wetu, na wakitupigia inchi yetu na n̄gombe wetu tutakula nini?" n̄gombe wanaona bora kuliko inchi, kuliko watoto wao.

na katika khabari za watumwa sulṭani wao husema: „watu wangu wote watumwa wangu". lakini

watu wengine wana watumwa wenyewe, hupigana wakawateka, ao hununua kwa ñgombe kwa wenzi wao. hununua mtumwa moja kwa ñgombe moja. na ñgombe moja utanunua kwa doti mbili za nguo. be'i ya mtumwa mwanamke sawasawa na mwanamme, ma'ana hawajui ma'ana ya mwanamke na mwanamme, husema „wote wamekhuluqiwa na mtu moja".

na katika inchi zao wako nyama tele. kulla nyama iko, ḥatta tembo wako, na vifaru viko na mbogo wako na viboko viko na mamba wako.

mpiga tembo hupiga na bunduqi, lakini wenyewe hupiga na mikuki. humwandamia maḥali alipo, humwendea kwa tartibu, ḥatta akifika qaribu — humpiga mkuki wa sumu mbavuni. akesha hukimbia, sababu wanaogopa ḍaruba za tembo. na tembo huenda akafia maḥali pengine. wao humfuatia kinyumenyume ḥatta maḥali atakápofia. akisha kufa huchukua pembe, wakakata na nyama yake, huenda kuuza, na pembe huenda kuza vilevile. frásila moja utapata kwa jora sitta.

na kiboko hupiga na mkuki. mkuki huu huwa na kamba na kamba huwa ndefu sana. wakimpiga huwachia ile kamba, akenda ḥatta akachoka kurudi nguvu zake, nao wanamvuta wakampandisha inchi kavu. huchukua nyama yake, na ngozi huitupa na kichwa hukitupa. na mamba vilevile wanapiga na mkuki.

mtu akifa shurṭi watu wote waalikwe. wakisha kuja, huja katika nyumba wakaondosha killa kitu chake cha huyu aliyekufa. wakaḥesabu ñgombe wake, wakaḥesabu mbuzi wake, na kulla kitu, kilichomo nyumbani, chaḥesabiwa. humwamru mtoto wake na mama yake, humwambia — ya kuwa: „tunataka kuzika". wao hutoa rukhṣa, hutoa ñgombe na mbuzi, ñgombe nne amma ṭano amma sitta, akaamru na mashamba yake: „nendeni mkaḥaribu vitu vilivyoko katika mashamba, kulla

chakula kilichoko, nendeni mkavikate vyakula". sababu anaona uchungu, anasema: „sioni kitu kuwa bora kuliko mume wangu, nimemkosa mume wangu — na vitu vyote nivikose". huchukua zile ñgombe wakachinsha, wakafanza karamu na machezo. khalafu wakisha kula na kucheza huenda kuzika. watu wote huchukua mikuki, huenda mbio na wengine wanarudi. wakifika penyi qaburi lake humzika. huchukuliwa na nguo zake zote. wakisha mzika, hurudi katika mashamba yake kuḥaribu vyakula vyake vya huyu aliyekufa. wanaḥaribu migomba na mahindi na vyazi na malesi na magimbi, yote wanaḥaribu, ḥatta nyumba yake hutia moto. na mkewe huenda zake kwao na watoto wake, huchukua na ñgombe zao. nuṣṣu ya mali ya ñgombe huchinsha, huwapa watu, na nuṣṣu huchukua mtoto wake na mamake.

na yule mke akitaka kuolewa tenna — huolewa, hana mṣiba. mṣiba wanasema wale ñgombe, waliochinshwa, na mashamba yaliyoḥaribiwa, na nyumba iliyotiwa moto, husema hutosha mṣiba.

turudi sasa katika safari yetu. siku hiyo tulivofika Konde, tukauliza katika mission ya Wazungu. wakatwambia, mwendo wa sa'a thená'shara tutafika mission. ilikuwa sa'a sitta za mchana, tukenda mwendo ḥatta sa'a thená'shara za jioni. 'askari wakachoka, ikalázima 'askari kujenga kambi. bana Illich na bana Krause wakakaa na 'askari pamoja. bana Bumiller akaniamrisha kuchukua mizigo mitatu yake na wapagazi watatu na Mwenyi Tshande na 'Othmani. tulikuwa bunduqi sitta, illa kufuata usiku wa jiza na vilimani na mito, lázima tufike katika mission siku ile. Mwenyi Tshande akasema: „haifai, ma'ana hapa kambini ḥatta kufika penyi mission, tukenda upesi, lázima sa'a sitta itachukua. na huku khaṭari kwa hawa Wa-

shenzi, wajinga bado, wakisikia watat͟hanni vita. na nyama huko wengi, na simba na chui wengi, afaḍali tulale hapa“. bana Bumiller akasema: „sitaki, lázima nifike katika mission leo“. ikatulázima kwenda usiku katika usiku wa jiza na njia mbaya. tukenda katika njia hizo, kazi ya kupanda kilima na kushuka na kuvuka mito. ḥatta tukafika qaribu ya mission, ilikuwa sa'a tano u nuṣṣu ya ki'arabu usiku. marra tukasikia Washenzi wanakuja, waketa kwa maneno ya kikonde. wakauliza: „watu gani nyie?“ tusiwajibu. wakauliza marra ya pili. Mwenyi Tshande akawajibu akawambia: „huu msafara wa Mzungu, tunakwenda katika hii nyumba ya mission“. ndio ma'ana waliotupisha.

ḥatta ilipopiga sa'a then'áshara wa robo', tukafika penyi mission. nao hawakujua, kama pana kuja Wazungu. wakaamka na bunduqi zao, wakat͟hanni vita, wakauliza kwa maneno ya kikonde. Mwenyi Tshande akawajibu: „wanakuja Wazungu“. na bana Bumiller akaweta kwa kideutschi: „siye rafiqi yenu“. khalafu waliposikia ṣauti ya kideutschi, wakazidi kujongea kwetu kuja kutuchukua. wakafuraḥi sana walivoona mtu jama'a yao, na bado mtu wa sirkali. wakafanya ḥéshima sana, wakaongea naye sana. akawambia: „nangoja msafara wangu, kesho ntaondoka“. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tulivoamka, tukakaa ḥatta sa'a tano, ndipo msafara ulipokuja. marra tukaondoka tukenda mbele katika mission nyingine. na kutoka pale ḥatta kufika mission nyingine huchukua sa'a kumi.

tangu tulipoondoka, tumeingia katika mashamba ya migomba ḥatta kufika mission nyingine. hapana mti mwingine illa mgomba, nayo mwendo wa sa'a kumi. mtu akiingia pale, haoni jua kwa migomba. tukafika katika mission ya pili, na bado 'askari hawajafika. ḥatta siku ya pili wakafika aṣ-ṣubuḥi.

tukaondoka kwenda mission ya tatu. tenna pale qaribu ya baḥari ya Nyassa, mwendo wa siku moja. pale ndipo tulipopata khabari, ya kama bana Wissmann amekwisha reje'a Rumbira katika safari yake ya Mafiti. na kutoka hapo mission ya tatu tumeondoka aṣ-ṣubuḥi, tumekwenda ḥatta sa'a sitta, tumepumzika na kutelekeza.

wale Wakonde wa kule ni ba'aḍi nyingine. na mkubwa wao mwingine, jina lake Makenya. na Wakonde wote wanamwogopa Makenya kwa ukali wake. naye huwafanzia użia wale mission. na mission akatwambia, tuangalie sana katika inchi hii ya Makenya, ma'ana yeye khaṭari sana.

na siye kufika kule mchana, hapo tulipotelekeza, tukenda mbele watu sitta vilevile na bana Bumiller, ma'ana msafara unakwenda polepole, hatuwezi kufuatana nao. tukenda ḥatta sa'a hedá'shara jioni, tukafika paḥali penyi mto kungojea msafara, waje walale pale, na siye twende mbele. msafara ukafika wote. bana Bumiller akawambia bana Illich na bana Krause — ya kuwa: „jengeni kambi hapa mlale, na miye nakwenda kulala kwa Makenya, ma'ana nimesikia hapa na kwa Makenya sa'a tatu, na nyie hamtaweza kwenda mmechoka. bassi nachukua watu wangu na vitu vyangu kidogo, nende nikalale huko kwa Makenya. na mkisikia bunduqi imelia — mjue, ya kama kuna vita. kama hamkusikia bunduqi — hapana neno. na mkiondoka aṣ-ṣubuḥi, msinitafute, ma'ana ntachukua mitumbwi nivuke Rumbira upesi, nipate kuleta matishali yaje yachukue msafara".

tukawacha msafara wetu nyuma, tukenda mbele, ili kwenda kwa Makenya. tulipokwenda mwendo wa s'aa, kulla mtu tunayomwuliza „Makenya qaribu", husema „Makenya papo". yule Mwenyi Tshande akam-

tuma Mkonde kamwambia: „upesi nenda kwa Makenya kamwambie, kama anakuja Mzungu wa sirkali, bassi asije kufanya gházia yake, kama anavofanzia mapádiri. hawa hawaqubali, akifanza wazimu kidogo — watampiga, wachukue na mali zake zote. bassi afanze tartibu, aje akutane naye katika njia, amchukue kwa ḥéshima qabla hakufika penyi nyumba yake".

yule Mkonde akenda akamwambia Makenya. Makenya akaogopa, akaja upesi, akatukuta njiani. na alipokuja, hapana mtu aliyomtambua, kama ndio Makenya mwenyewe — jissi alivoogopa. alinyenyekea kama mtoto mdogo. akaja akatuchukua, akatupeleka penyi nyumba yake, akatwambia: „laleni katika nyumba yangu, na miye ntalala paḥali pengine". vile ni kuogopa pia. lakini na siye hatuqubali kulala katika nyumba yake, afaḍali tulale nje katika ḥema yetu, maʿana tuli<u>th</u>anni alitaka kufanya ʿaqili kutia nyumba yake moto. bana Bumiller akampa rukhṣa, akamwambia: „nenda kalala, kesho aṣ-ṣubuḥi nataka mitumbwi kutuvusha twende Rumbira, walákin watu wangu walioko nyuma, ʿaskari wangu, na Wazungu wengine watazame vema, wasije kuḍurika. na weye fanza safari katika siku hizi, wende ukamwamkie bana mkubwa. na wewe ukituletea vyakula ukituuzia, maʿana tuna watu wengi katika mji wetu Rumbira, na nyie mtapata manufaʿa mengi, nguo na ushanga, killa kitu mnachokitaka mtapata". bana Bumiller akenda kulala, lakini Makenya hakuaminisha kwenda kulala, kwani asije kuja Mkonde mwingine akatuḍuru sisi, khalafu taʿabu ataipata yeye. bana Bumiller amempa rukhṣa kwenda kulala, lakini yeye hakwenda, akakaa nje mpaka aṣ-ṣubuḥi. tulipokwenda kulala, ilipopata saʿa moja, ikaja ḍarba na mvua, ikatwangushia ḥema. hakuweza mtu kulala kwa mvua na upepo na mbu wengi sana.

siku ya pili aṣ-ṣubuḥi tukaondoka kwenda kuingia katika mitumbwi kwenda Rumbira. na hapa ḥatta Rumbira yapata sa'a tatu. tulipoqaribia Rumbira, wale hawakujua, ya kama ni siye, sababu tulitokea upande mwingine. ḥatta tulipofika, ndipo walipojua, ya kama sisi. tenna wakafuraḥi sana, ma'ana walithanni kama tulipotea, kwani tangu tulipoondoka Rumbira, hawakupata khabari yetu.

bana Bumiller akaamrisha matishali kwenda kuchukua msafara wetu. tenna tukakaa Rumbira siku sitta'shara. na katika siku hizi Washenzi wakaja kufanya bi'ashara. nao wakaleta vyakula vingi sana, na n̄gombe na kondoo na kuku, killa kitu walicho nácho wakaleta, nasi tukanunua. na hawa wafalme wakaja wakamtazama bana mkubwa, lakini hawana nguo kabisa, huvaa winda tu.

tukakaa siku kidogo kule Rumbira. bana mkubwa akaamrisha safari, ya kuwa bana Bumiller asafiri ende Usango kwa Merere, min ájili ya kupatana naye atutafutie wapagazi. tukasafiri na bana mkubwa pamoja, ili kupitia Konde, ende akapige nyama kwanza, ndipo wagawe safari. tulipokwenda Konde, tumekwenda mwendo wa siku mbili, tumefika katika mji wa mission, ndio waliotuelezea penyi simba na faru. wakatupa kirongozi kutupeleka. kutoka hapa mission ḥatta kufika penyi simba — siku moja u nuṣṣu. tulipofika huku kwa siku ya pili, tukajenga kambi katika mwitu, ili kungoja usiku, ya kuwa simba atakuja amma chui. na siku hiyo hatukulala, tumeingia mwituni kuandamia simba na chui, walákin hatukuwaona, tumesikia wakilia.

na hapo tulipojenga hiyo kambi yetu, pana maji ba'aḍi mbili, moja maji ya baridi na moja maji ya moto — yanachemka, yanatoka katika arḍi, nayo hu-

ruka sana jissi yanavochemka. mtu hayawezi kuyakamata. na mtu mwenyi funza, akitia miguu yake ndani ya maji haya — matekenya[1]) hufa. na maji haya nathanni mazuri kuyakunywa, lakini hatukuyajaribu. lakini Ulaya nimeona maji kama hayo, yana 'afya kwa watu wagonywa, kama watu walinambia, ma'ana mtu akinywa huendesha kama msahla[2]).

tumekaa siku tatu katika kambi hiyo, hatukupata kupiga simba. tukarudi kwenda kule mission. qaribu ya mission tumejenga kambi, ndipo tulipogawana safari yetu. bana mkubwa alitaka kwenda piga faru, na bana Bumiller kwenda kwa Merere. bana Bumiller akachukua 'askari kumi na saba', na bana Oehm kwenda naye pamoja.

tukaachana tukenda zetu mwendo wa sa'a sitta. mpaka sa'a moja ya usiku tukafika pahali penyi mji wa Konde. nao watu wa pale wakali sana, na ujinga wao mwingi. bado bawakuelewa khabari ya Wazungu. walipoona bendera yetu wakashituka. wakaja wale Washenzi wote kuja kuzungusha kambi yetu kutazama mavazi ya 'askari. khalafu akatokea yule ndugu yake ya yule mkubwa wa mji ule, naye pande la mtu, akatokea pale na kiburi chake na majivuno yake, akachukua mikuki sitta mikononi. mkalimani wetu 'Othmani bin Sa'id akamwambia mkalimani wa kikonde, kama awambie hawa, watupe kuni tupikie, amma watuuzie. wale Washenzi wakakataa, wakatwambia: „tafuteni kuni wenyewe. amma nani aliyoweteni kuja huko? siye hatuogopi Wazungu, wala bendera yenu. bassi msiwe mkijivuna sana, siye hatujui Mdeutschi na bendera yenu na sultani wenu, tunamjua sultani wetu

1) in kikonde Sandfloh. Die Suaheli sagen funza und wadudu wa Kepu (Kapstadt). — 2) Abführmittel.

tu“. ʿOthmani alivosikia vile, na ʿaskari Saleḥ, Comore, akamkamata yule mshenzi mrefu, akamtupa chini kumnyanganya mikuki. ʿOthmani akaamrisha na ʿaskari wengine kumsaʿidia Saleḥ. ḥatta ʿaskari wengine walikuja, yule mshenzi akainuka juu. Saleḥ akamkamata akamtupa vilevile. ʿaskari wakamchukua, wakamleta kambini kwa bana Bumiller. marra ikaamrishwa „shika bunduqi mikononi“, „bunduqi ṭayyari“. tukazungusha kambi zetu, kwani Washenzi wote wataka kutupiga. alipoona vile tulivozungusha kambi kwa bunduqi zetu, na yule mshenzi akafungwa — bana Bumiller akamwuliza ʿOthmani — ya kuwa: „sababu mlivomfunga huyu mshenzi?“ ʿOthmani akamwelezea khabari zote, ya kuwa ametukana bendera yetu, asema hawajui bendera ya kideutschi. bana Bumiller akaużika vilevile, akamsaili — ya kuwa: „kweli umesema?“ yule mshenzi akasema: „ndio nimesema, lakini nisámeḥe sasa“. ikalázima kufungwa siku hiyo ḥatta aṣ-ṣubuḥi na kuleta n̄gombe kumi na wawili, waje wanunue bendera, wapate kuijua.

lakini jissi walivoogopa Washenzi wote — ni kwenda usiku wakifika hapo penyi mkubwa wao, wakifanya mashauri ḥatta waje wamwondoshe yule mwenzi wao katika kifungo. katika saʿa sabaʿ ya usiku, tukasikia watu wanakuja. alikuwa yule mkubwa wa Washenzi, anakuja kutaka raḍi kwa bana Bumiller, awasámeḥe, naye aqubali kuleta n̄gombe thenʿáshara, wanunue bendera, naye amrudishe ndugu yake. bana Bumiller akamwambia: „mimi singalimfunga, lakini yeye amejifunga mwenyewe. maʿana miye sikuja huko kuja kutaka n̄gombe amma mali, lakini nimetumwa kutazama inchi hii, na kufanya ṣuluḥu watu wasiopatana, na kuweka bendera sulṭani wetu. na huyu ameitukana bendera yetu. lakini kama angalikuwa

mtu mwenyi ʿaqili, akajua ni ʿaibu kutukana bendera — ningalimpiga riṣaṣi, lakini huyu mjinga hajui. ndio maʿana mlete n̄gombe thenʿáshara, mpate kujua, ya kama haifai kutukana bendera. na khabari hii isipite marra nyingine". akaqubali, wakaleta n̄gombe.

tukaondoka katika safari ya kwenda kwa sulṭani moja, jina lake Maisote. na tangu tulipoondoka pale ikawanza mvua ya masika. tukapigwa na mvua — ḥatta mwendo wa siku moja hatuwezi kwenda kwa siku mbili, kwa jissi maji yalivokuwa mengi. maʿana ikinya mvua sana Konde, lázima mtu aogelee. na nyumba zao vilevile huogelea kwa maji mengi.

tukenda mwendo wa siku tatu, tukafika paḥali pana mtu mkubwa, walákin hatujui upande gani unakokwendea, kama unashukia upande wa Nyassa, amma unakwenda upande mwingine. bana Bumiller akamwambia ʿOthmani: „nenda panda katika kilima, ukatazame huo mto unashukia wapi?" ʿOthmani akawacha bunduqi yake na pistole yake kwetu, akenda kutazama. na siye tukenda mbele. ḥatta aliporudi, haukuta msafara, umekwisha ondoka. akatufuatia nyuma, asitupate. alipokwenda mwendo wa nuṣṣu saʿa, akakuta Wakonde wawili, nao wana mikuki. akataka kuwauliza, kama hawakuona msafara wa Wazungu, wanaokwenda mbele huku. na wale Washenzi ʿázima yao wanataka kumnyanganya ʿOthmani. wakaja wakamkamata wakamwambia: „lete koti[1]) lako". akataka kusita kidogo, lakini wao wakamwambia: „kama hutatoa tutakupiga". akawapa ile koti. „vua na kanzu yako", wakasema. akakataa. na wale Wakonde wakubwa sana, watu wa nguvu, nao hawana nguo, walikuwa utupu. walipomkamata ʿOthmani, walitaka kumwangusha chini. aka-

1) engl. coat.

pigana nao ḥatta yapata nuṣṣu sa'a. 'Othmani akachoka. wakamtupa chini, wakamchoma mkuki katika mguu. alivoona wamemtupa chini, akafikiri „tafanyaje sasa“? akapata ḥékima, akamkamata moja utupu sana, akavuta, akamtupa chini. 'Othmani akachukua mkuki wa yule, aliyoanguka chini, kupigana na yule mwingine. yule mwingine akakimbia. alivokimbia marra atokea yule mkalimani wa Merere, Mwenyi Tshande, amemjia 'Othmani. lakini yule Mwenyi Tshande hakumjua, ya kama ndiye mtu wa bana Bumiller, illa alivoqurubia ndivo alivotambua, kama huyu ndio mkalimani wa bana Bumiller. tenna akaja akamchukua 'Othmani, wakafuatana wakaja hapo tulipojenga kambi yetu.

wakaja wakatuelezea khabari zote, ya kuwa 'Othmani alipigwa na Washenzi, wamemchoma mkuki. ikabidi kutafuta yule sulṭani wa ile inchi, atafute watu hao. tukamwambia: kama hukuwatafuta, siye tutafanya vita“. yule sulṭani akasema, kama hawezi kuwatafuta, sababu hawajui. na siye tukawacha khabari, lázima awatafute, ḥatta tukirudi kwa Merere — lázima atupe watu hao.

tukaondoka kwenda kwa mfalme Maisote, aliye chini ya amri yake Merere. tulipofika katika inchi yake, akatushika kwa ḥéshima. tukakaa siku tatu kwake, kwa sababu bana Bumiller hawezi. kuondoka hapo bana Bumiller amechukuliwa ndani ya machera kupanda juu ya vilima, na mvua nyingi. tumekwenda mwendo wa sa'a tisa' kupanda kilima kimoja. kule juu ya kilima tukajenga kambi yetu. ilikunya mvua sana. tukakaa mudda wa sa'a mbili, wakatokea Wasafa, waliotoka Usafa, wakaja wakatwambia, kama njia haiendeki, kwani Wahehe wanakuja. na bana Oehm, alivosikia khabari hiyo, akamwambia bana Bumiller — kama: „turudi twende zetu Nyassa, kwani

hatuna watu wa kupigana na Wahehe". bana Bumiller akakataa, akasema: „sirudi nyuma, mpaka niwaone, lakini sikimbii vita nisivyoviona". hawa Washenzi wakazidi kututisha, kama wanakuja Wahehe wengi sana, lakini bana Bumiller hakusikia maneno yao.

tulivoondoka aṣ-ṣubuḥi, tukafuata njia kwenda Usafa. naye akachukua wale watu wawili, waliotwambia khabari hii, ya kama watuonyeshe hapo Wahehe walipo. wakatangulia. tukenda mwendo wa sa'a tisa' — hatukuona mtu, wala hatukuona 'alama ya mtu mbaya kupita. tukazidiwa na mvua, ikabidi kulala kule mwituni kwa mvua nyingi. hapo tulipojenga kambi, tuliwasha vibiriti vingi, havikuwaka kwa mvua nyingi na baridi.

tukakaa ḥatta siku ya pili tukaondoka tukenda Usafa kuuliza hawa Wasafa — ya kuwa: „kweli Wahehe wamekuja huku?" wakatujibu — ya kuwa: „hatukuwaona Wahehe kupita". ndipo tulipojua, ya kama wale walitaka kututisha kweli.

tukakaa Usafa siku mbili kupeleka khabari kwa Merere, ya kuwa tunakuja. alipopata khabari, akaleta watu kutuchukua ḥatta tukafika Uténgure. tulipofika kule Uténgure, akatushika kwa ḥéshima, akatupa nyumba mjini kukaa. lakini katika sisi kukaa Uténgure na yeye kutupa nyumba kukaa mjini — alikuwa ana khofu, Wahehe wasije kutujia usiku kambini, ndio ma'ana aliyotwita mjini. tukakaa siku nane kwa Merere. kulla siku ni kufanza shauri ya wapagazi, lakini yeye hawezi kukataa. na bana Bumiller hawezi. ḥatta siku moja bana Bumiller akamwita katika nyumba yetu kufanya shauri, tupate kuondoka. na siku hiyo alikufa mpagazi wetu. akakataa asema: „siji huku, ma'ana amekufa mtu. naye bana Bumiller asije nyu-

mbani kwangu mpaka zipite siku nne, sababu amekufa mtu, na miye haifai kuona mtu, aliyoona maiti".

ikawa siku ya pili bana Bumiller akamtuma mtu, akamwambia: „nenda kwa Merere, mwambie, nakuja kwake". akamkataza. na siye tunataka kuondoka. alipokuja majibu, ya kuwa yeye asiende, akamrudisha mkalimani, akamwambia: „nenda mwambie — vema, siji leo, lakini kesho lázima aje kwangu. na kama hakuja — khabari itakayopita — asinilaumu".

aliposikia vile Merere, akakhofu sana. siku ya pili aṣ-ṣubuḥi akaja kwetu. wakafanya mashauri ya wapagazi. ḥatta ilipopata nuṣṣu sa'a, akamwambia, mudda wa siku tatu atatoa wapagazi. bassi tukakaa pale siku tatu, akatupa watu arba'īni, akatwambia: „wengine watakuja nyuma". tukawachukua, ili tupitie njia ya kwendea Unyika.

na katika njia tunayopitia, kulla mji tunaofika, hukata mfalme mwingine. na wale Wanyika mali yao mbuzi na n͠gombe. na vitu wanavyopanda kule mawese na mtama. na mtu akifika katika mji, wakijua, kama pana kuja wageni, hufunga lango la boma, hukimbiza n͠gombe zao na mbuzi zao kwa sababu ya kuogopa.

mji tulipofika kwanza katika inchi ya Unyika, huyo mfalme huitwa Karondo. wakatufungia lango, na siye hatuna vyakula. bana Bumiller akamwamrisha mkalimani — ya kuwa: „nenda mjini, ukamwambie mkubwa wa hapo, kama afungue mlango, atupitishe mjini, amma kama hataki, walete vyakula hapa tununue, ma'ana watu wangu hawana vyakula". akaja yule mwenyewe mji, akatwambia: „hatuna vyakula, na siye hatuna mbuzi wala n͠gombe". alivosema vile, bana Bumiller akasema „kama huleti chakula, bassi fungua mji tuingie, tukae sote tufe na njaa". akatutia mjini.

tulipoingia tukakuta wote wamekimbia, wako watu kidogo tu. na vyakula wamevificha. tukakaa mudda wa nuṣṣu sa'a, akatokea 'askari mmoja nje kutafuta kuni. alipoingia mwituni, akakuta mbuzi na ñgombe na kondoo wote kule mwituni. akarudi 'askari, akaja akasema, kama wako ñgombe na mbuzi wengi. marra ikaamrishwa bunduqi sitta, wakakusanya mazizi ya ñgombe na mbuzi kuleta. walipozileta, bana Bumiller akamwambia yule mkubwa pale mjini: „ñgombe hizi si zako?“ akasema: „zetu“. akamwuliza: „mbona unasema huna mbuzi huna ñgombe?“ akasema: „hizi za watu wengi, si za miye pekeyangu“. lakini bana Bumiller hakuzitaka burre, alitaka kuzinunua. ikabidi siye kuchukua zile mbuzi na ñgombe, tuondoke pale mjini, ili kumtaka kumtisha yule mshenzi na kumwadabisha, asiseme uwongo tenna. msafara ukaondoka, na yule mwenyewe akatufuatia na watu wake kututafaḍḍali tuwarudishie mbuzi zao na ñgombe zao. na ḍámiri yetu twataka kuwatisha ḥatta siku ya pili tuwarudishie.

tulipofika mwituni, tukajenga kambi, tukachinsha ñgombe moja na mbuzi wanne. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukawakuta wale Washenzi walilala qaribu ya kambi yetu, hawana roḥo kabisa kuwachia mazizi yao. bana Bumiller akaamrisha 'askari — kama: „rejesheni mali zao hawa Washenzi“. na mkalimani akäwaelezea: „akipita Mzungu ao mgeni mwingine hapa, lázima mshike uzuri, mpe kula na kunywa. kama mkifanya kama mmefanya leo na sisi, mtakuja kupata adabu yenu“. wakafuraḥi sana, wakasema „aḥsante“. na zile tulipochinsha tukalipa nguo.

tulipokwenda mji wa pili, wakataka kutufanya vile, lakini hawakuwaḥi kuficha, ma'ana marra tulikwenda kufika mjini. kulla nyumba tunayoingia huwa-

kuta wanafunga vitu wanataka kukimbia, ma'ana walithanni tumekuja kuwapiga na kuwanyanganya mali yao. na ñgombe zao ziko bomani, vilevile wakataka kuziondosha. tukawambia: „kwa nini mnaondosha ñgombe?“ wakasema: „twataka kwenda kuchunga sasa“. tukawambia: „hapana rukhṣa kuondosha, wacheni hapa, ma'ana nyie mnaogopa. siye hatunyanganyi, lakini kitu tunachokitaka hununua“. waqati ule wakaziacha. wakatunzia ñgombe wawili na unga na mahindi, na bana Bumiller wakamletea kuku. na kule wote wakitaka kumpa mtu ḥéshima, humletea kuku na unga na mayayi amma pombe, hawana kitu kingine.

nao majengo yao hujenga mwituni. na maboma yao huzungusha ḥandaqi za maji. na kama wamepigana vita paḥali, wakiua mtu, huchukua kichwa, wakatungika katika boma lao. na akifa mtu — hawaziki, hutupa. na nyama akifa — hawatupi, hula.

tukaondoka safari ya hapo kwenda Karonga. tukenda mwendo wa siku mbili, tukafika qaribu ya Karonga. pana mji wa Mw'arabu na mtu wa mrima. na kule kote huitwa Mlozi. na Wakonde wote humwogopa Mlozi. tulipofika huko, wakatwambia Washenzi: „tazameni sana, ma'ana huyu Mlozi mkali, hapatani na Wazungu, na nyie watu kidogo“. wale wanathanni tunamwogopa kama wao. tulipofika tukajenga qaribu na ule mji wa Mlozi. na yeye ana gházia nyingi kutisha watu. usiku walikuwa wakipiga ngoma na bunduqi za machezo. na katika machezo yale walithanni, labda siye tutaogopa, lakini sisi tukalala kambini mwetu.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukapitia njia ya kwendea kwa Mwakilima. tulipofika kwake, tukakaa pale penye nyumba yake. akatushika kwa ḥéshima sana. naye mshenzi mrefu, kasimama uzuri na kuum-

bika kwake kuzuri. nyumba yake naḍifu sana. naye kaipakaa chokaa kama nyumba ya pwani. na mtu akiingia ndani, vilevile naḍifu.

na kule kutushika uzuri — ataka tumsaʻidie tumpige mshenzi mwingine, anayemwużi, jina lake huyo mshenzi Mwakiyusa. naye mpaka moja na inchi yake. akatuchukua aṣ-ṣubuḥi yake, ili kutuvusha katika inchi yake, mtu asije kutuḍuru, amma kutufanzia ujuvi katika inchi yake. ḥatta tulipofika mpakani, akatwambia: „sasa nnarudi, maʻana hiyo si inchi yangu. nikiingia na nyie pamoja, Mwakiyusa atasema, nampelekea vita, na miye sitaki maneno naye“. tukamwambia: „njoo, tufuatane“. akakataa kabisa kuingia katika inchi hiyo. tukaagana.

tukaingia katika migomba ḥatta tukafika kwa Mwakiyusa. tukajenga kambi pale. tukauliza huyu Mwakiyusa — kama: „yuko wapi?“ wakatwambia — ya kama: „hayupo, amekwenda tembea“. bana Bumiller akawambia: „ondosheni watu wakamwite, nataka kuonana naye“. wakatucheka wale Washenzi. na kutucheka kwao ni kiburi tupu, wanatużarau — sisi kuja katika inchi yao, marra kutaka kuonana na yule mfalme wao. wasipeleke mtu, wakasema: „yeye mwenyewe atakuja, wala haiḥitaji kupeleka mtu“. tukawambia: „leteni vyakula na maziwa na n̄gombe na kulla kitu, tunataka kununua, maʻana hatuna vyakula“. wakakataa, wakasema: „hatutaki“. tukawambia: „kama hamkutuuzia, tutachukua kwa nguvu“. wakazidi kutucheka, wakaona upuzi kabisa, kwa sababu wao wakajiona na nguvu sana na mikuki yao. tukangoja mudda wa saʻa tano, hawakuleta vyakula. ikabidi ʻaskari waingie majumbani wachukue wenyewe vyakula. nao wamezunguka katika kambi yetu yapata watu themānie mia, na siye

bunduqi saba'ṭ'ashara na Wazungu wawili. wakapiga makelele majumbani, kama wananyanganywa vyakula. wakaja wakatwambia: „kama akiingia mtu katika nyumba — tutampiga mkuki“. bana Bumiller akawajibu — kama: „nyie watu, mliozunguka kambi hii yote, na waliono mjini humo wote — akaonyesha kwa mkono — jua likifika hapo — nataka kulla mtu awáṣili hapo, alete na kitu kidogo ḥéshima yangu. kama hamkuleta, nitatia inchi hii yote moto, siogopi mikuki yenu. hizi bunduqi mbili zangu zitanitosha kupiga katika inchi hii yote“. wakaondoka kwenda kufanya shauri. ilivopata nuṣṣu sa'a, akaja yeye mwenyewe Mwakiyusa, akaja kuangukia tumsámeḥe. wakaleta na vyakula, wakaleta na n̄gombe then'áshara na kondoo 'asherīn, na ndizi nyingi, na kulla 'aina ya vyakula ya Konde huleta, ili kutuhonga sisi. waqati ule tukafanya urafiqi. tukampa na bendera ya kideutschi, tukamwambia, yeye lázima aje Rumbira kwa bana mkubwa, aje amwamkie. akatupeleka yeye mwenyewe ḥatta kwa Makenga.

na yule Makenga ni rafiqi yetu. tulipofika kule, akafanza gházia ya machezo na kuleta n̄gombe na kuku, vitu vingi akaleta. naye mwenyewe akaingia na sisi pamoja katika mashua kutupeleka Rumbira. tulipofika Rumbira, ikawa furaḥa sana tuliyorudi salama.

hatukukaa sana Rumbira, tumekaa siku arba'ṭ'ashara, ili kufanya mizigo ya safari ya Tanganyika. bana Wissmann na bana Bumiller na bana Fuchs na bana Oehm ndio wanaopeleka safari Tanganyika. tukachukua matishali mawili, tukaingia na 'askari wetu kuvukia Karonga. siku tuliyosafiri Rumbira, tukafuata chanjari matishali yote mawili. tukatweka mpaka mwendo wa sa'a tatu. marra tunaona ḍarba inakuja. lakini tishali, aliloingia bana Wissmann, limekwisha kwenda mbele. ḥatta mudda wa nuṣṣu sa'a hatuku-

mwona. siye tukatweka ḥatta kattikatti ya usiku, tukafika qaribu na inchi ya Mwakaringa. tishali letu likafunguka misumari yake, ikafanya kama linataka kukatika vipande viwili. likajaa maji, na siye tumo kattikatti ya baḥari. na shehena nyingi, watu na maṣanduqu. hatukulala, illa kazi yetu kuteka maji kwa zamu. ḥátta ilipofika al-fajiri, tukavutia qaribu na pwani. lakini siye hatuwezi kushuka kwa mawimbi, min ájili maji yanakupwa. ikabidi waqati ule kutupa vitu baḥarini. na mashua ndogo tulitaka tuwavushe matájiri wetu kwanza, lakini ile mashua haikuweza kwa mawimbi. ʻaskari wanaojua kogelea, wakajitupa baḥarini, na Wasango wote wakajitupa baḥarini, mashua iwe nyepesi. wakaogelea ḥatta pwani, wakavuta mashua kwa kamba. wakafa Wasango wawili.

tulipofika pwani, hapana mji illa mwitu mtupu. tukajenga kambi, na kupakua vitu katika tishali, tupate kulitengeneza. tukakaa hapo siku mbili, tukafunga lile tishali. na msafara ukapita barrani, ili kwenda Karonga. tishali akachukua bana Fuchs na watu sitta kulipeleka Karonga, kwani hapo Karonga ndipo tunapoondoshea safari yetu ya kwendea Tanganyika. tukenda mwendo wa siku mbili ḥatta tukafika Karonga. na katika siku ya pili hiyo, tulivoqurubia Karonga, katika kambi tuliyoijenga, palikuwa nyumba za Wakonde katika migomba. hawa Wakonde walivotuona, wataka kukimbia. bana Bumiller akamtuma mkalimani kuwarudisha na kuwambia, kama sisi si watu wa vita. wakarudi wakaja katika nyumba zao.

siku hiyo niliyogombana na bana Bumiller sababu ya ṣanduqu. ṣanduqu ilikuwa na vitu vingi vyake, akanita usiku kanambia, nitafute dawa ya ḥoma. na katika gházia iliyokuwa katika ṣanduqu sikuweza kuiona. akauzika, akanambia: „nenda zako“. nikataka

kwenda zangu, walakini sijui paḥali nnapokwenda, sababu kule barrani na miye sina kitu, wala sina silaḥa, na usiku -wa jiza. nilivokwenda nikawambia jama'a zangu Wangazija, wakachanga, kulla mtu katoa rupia sitta ḥatta kumi, ikapata qádiri ya rupia miá. na nguo wakanipa, lakini bana Bumiller hakunifukuza kwa nia yake, alifanya kunitisha na kuniadabisha tu. alivojua, kama nalitaka kwenda zangu, akamtuma 'Othmani bin Sa'id, kamwambia: „nenda kamwite“. 'Othmani akamwambiá: „amekwisha ondoka“. akaondosha 'askari sitta usiku kunitafuta. na wale jama'a zangu walinificha ḥattá aṣ-ṣubuḥi wapate kunitafútia njia ya kunipeleka Karonga. walivosikia, kama ananita, wakanichukua wakanipeleka kwake, ili kusikiliza khabari, alitaka kunifanza. akaámrisha mimi kukaá ndani ya karokoni mpaka aṣ-ṣubuḥi, naye akaweleza wale Wangazija: „sikumfukuza, lakini nalitaka kumwadabisha tu“. ḥatta aṣ-ṣubuḥi akaja, akanichukua katika karokoni, akanipa kazi yangu.

tukafunga mizigo, tukáondoka tukenda zetu Karonga. nasi tulivofika Karonga, tukakuta bana Oehm hawezi na ḥoma, iliyomshika, ḥoma ya ndui. akachukuliwa akapelekwa maḥali pengine katika shamba, ili kuuguza. tukakaa pale — mudda wa siku tatu, ili kungoja, labda atakuwa hajambo. ḥatta siku ya tatu akafa. na 'askari moja wetu akashikwa na ndui vilevile, tukamwacha Karonga.

tukasafiri kwenda zetu Tanganyika. tukenda mwendo wa siku mbili, tukafika nyika. siku tulipofika nyika, Wasango wetu wakatukimbia. bana Wissmann akamwamrisha bana Bumiller kwenda kupeleka khabari hii kwa Merere, ya kuwa watu wake, aliotupa, wametupa mizigo yetu wamekimbia. bassi tunataka watu wengine.

siku hiyo tukaachana msafara wetu, bana Bumiller

akachukua 'askari 'asherīn na sitta, Sudani kumi na moja na Wasuaḥeli kumi na watano. mwendo wȧ siku tatu tukafika Usango. tulipofika — Merere akashtuka. akatuuliza: „kuna khabari gani?“ akamwelezea khabari, ya kuwa watu wake wamekimbia, bassi na atupe watu wengine. na wale waliotukimbia, wamekwisha, fika kule mjini. akawakamata akawafunga. akatwambia: „vema, ntakupa watu“.

tukakaa pale qádiri ya siku nne kutafuta watu. naye akatwambia, kama anataka kukusanya watu wake, ili watupeleke njia ya kupitia kwa Zunda na Kimaraunga. ma'ana Zunda na Kimaraunga ni watu wake, nao wamemw'aṣi. nao wanapiga misafara, inayopita katika inchi yao. akatwambia: „bassi twende tukafanye mashauri nao. [tupatane, kama wamekataa tupigane nao“. bana Bumiller akamjibu: „vema, lete watu, lakini sitaki vita. kama nikenda kuonana nao, takwenda kufanya ṣuluḥu na kuweka bendera yetu ya kideutschi. kama wakikataa bendera kuchukua — waqati huu lázima nitapigana nao.

Merere akamwamru mtoto wake Mgándire na waziri wake, akaondosha na watu elfu nne, ili kutupeleka katika njia hizi, lakini sisi hatukujua, ya kama atachukua watu wengi. siye kuondoka Uténgure tuliondoka na watu kidogo, ḥatta tulipokwenda mwendo wa sa'a sitta tukafika kambini, tukakuta kambi imejengwa, wamezungusha boma Wasango arba't alāf, tukashtuka. bana Bumiller akamwuliza yule Mgándire — kama: „watu hawa wote wanakwenda kufanya nini?“ kamwambia: „watu hawa wanakupeleka kwa Kimaraunga na Zunda, kwani watu wabaya hao. siye tunajua, kaṃa lázima watafanya vita“.

siku ya pili tukaondoka, tukenda ḥatta sa'a sitta, tukatelekeza, wakatwambia: „mwendo wa sa'a mbili

ḥatta kufika kwa Zunda". sa'a saba' u nuṣṣu tukaondoka, tukenda kwa Zunda. na qaribu ya mji pana mwitu kilimani. na mtu akisimama hapo kilimani, huona huo mji wa Zunda. tulivokuwa tunakwenda qurubia mji, wakatuona. marra wakaji, ḥāżari, wakajua Wasango wanakuja. wakatoka nje na bendera yao, wakaanza kucheza na bendera na kuipepea bendera, ili kuonyesha kama ni vita. Wasango wakatwambia: „wale wanataka vita, sababu wanatuonyesha bendera yào na kupiga bunduqi kwa furaḥa ya vita". ḥatta tuliposogea qaribu na mji, tukatuma mkalimani wetu kwenda kuwambia, kama anakuja Mzungu, wasifanye vita. wakamjibu: „mbona tunaona Wasango wengi? haiyumkini, kama Wasango hawa watakuja huku burre, billa kuja kufanya vita". akarudisha kuja kutwambia, kama hapana rukhṣa kwenda mjini. akarudishwa yule Belushi Jemadari, aliyokaa miake saba't'ashara kwa Merere, kwenda kuwambia: „huyu Mzungu hataki vita, ataka kusema na mfalme wenu na kumpa bendera ya kideutschi, ma'ana nyie ni ra'ia za Madeutschi". akenda akawambia. akamwambia — kama: „vema, Mzungu na aje pekeyake, lakini asije Msango wala mtu mwingine".

alivorudi akaja akatwambia bana Bumiller akawarudisha Wasango kuweka mbali, wasije mjini. akachukua na 'askari kumi na wawili na yule Belushi na wakalimani watatu, wawili Wasango na mmoja Mnyika. tulipofika langoni, tukakuta ule mwango umefungwa. wakatokea watu wawili nje kusema nasi. wakatwambia — kama: „hàpana rukhṣa kuja na watu wengi. kama mnataka shauri — huyu Mzungu pekeyake na mkalimani moja, lakini hapana rukhṣa kuchukua silaḥa, waingie mikono mitupu".

tukafikiri, tukaona kạtika 'aqili yao wataka kumtia

bana Bumiller kule bomani, wende wakamfunge, amma wamwue. bana Bumiller akataka kuingia. tukamwambia — kama: „usiende pekeyako, lázima ukiingia huko bomani — ufuatane na watu wako qádiri ya bunduqi sitta bassi". bana Bumiller maneno yale yakamtua, asiingie. akawambia: mwiteni mfalme wenu, aje, tufanye shauri, kama nyie hamṣadiqi, kama siye maqṣudi yetu kuja hapa kufanya ṣuluḥu". bassi wakamwita yule mfalme, akafuatana na waziri wake, wakaja. bana Bumiller akamwambia: „tunataka paḥali tujenge kambi, khalafu tufanye shauri". yule mshenzi akatuonyesha paḥali pasipo maji, na bado mbali ya mjini, tujenge. tulipoona vile alivotuonyesha paḥali pabaya kujenga kambi, tukakataa kujenga pale. tukenda paḥali pengine pazuri katika mashamba yao, palipoelekea na mjini, tukajenga kambi. tukawambia — kama: „huyu bana anataka, ya kama mlete chakula cha ʻaskari na n̄gombe tununue". wakatwambia: „hapana n̄gombe na vyakula hapana, taʻabu sana, pana njaa katika mji". lakini khabari ile pia ni uwongo, vyakula viko na n̄gombe, lakini hawataki kutoa billa kufanziwa nguvu. akaambiwa: „kama huleti vyakula na kutuuzia na n̄gombe — tutachukua kwa nguvu. na siye kunyanganya hatutaki, afaḍali ulete tununue". akatwambia, kama anataka rukhṣa, akafanye shauri na watu wake. bana Bumiller akamwambia: „kama unakwenda, kwanza chukua hii bendera ya kideutschi, ukatweke katika boma lako. na kama ukiona msafara wa Wazungu amma Waʻarabu, tungika bendera hii, khalafu hawakuḍuru. ḥatta Merere akiona bendera hii — hakupigi". yule Zunda asisikie, akamwambia: „kwanza niwashauri watu wangu". akamwambia: „vema, nenda kawashauri".

akenda akakaa mudda wa saʻa. tukatuma mtu ende akamwite, upesi alete majibu, kama anatuletea chakula

na tenna majibu ya khabari ya bendera. yule mkalimani akenda, akamleta yule Zunda. akatwambia — ya kama: „bendera hatuijui". bana Bumiller akamwambia: „lázima uijue, sababu weye uko chini ya bendera hii". yeye akasema: „la, miye chini ya bendera yangu mimi, sijui bendera ya kizungu wala ki'arabu". bassi bana Bumiller alivosikia vile, akaamrisha 'askari kumkamata yeye na waziri wake wafungwe. wakawafunga, na huyo moja mtu wa Zunda akatumwa: „nenda mjini upesi kawambie, kama hawakuleta vyakula upesi — tutamwua huyu mfalme wao na waziri". akarudi mjini kwenda kuwapasha khabari.

akarudi akaleta ñgombe wawili na unga na mbuzi na mayayi. wakat͟hanni tutawafungulia, walakini tukawambia — kama: „hawa hawakufungwa min ájili ya vyakula, lakini ni kilichowafunga ni msemo wao wenyewe, ma'ana wameitukana bendera ya kideutschi, kama hawaijui. bassi mkawambie hao, walioko mjini, kama waje wachukue bendera ya kideutschi, nao wafungue mlango". alipokwenda akawambia, wakaleta majibu — ya kuwa: „hatutaki bendera, na wachukue huyu mfalme na waziri wake, wafanyize watakavo. wakifa — wako wengine, lakini hatutaki kupatana na Wasango, na bendera hatuitaki". wakapewa mudda — ya kuwa: „siku ya pili sa'a nne, kama hawakuja kuichukua bendera na ṣuluḥu, tutakuja kupiga mji wenu, tutie moto".

tukalala pale, ḥatta siku ya pili aṣ-subuḥi tukatuma mtu kwenda kuwauliza, kama wanataka amma hawataki. akarudi akatwambia, kama hawataki ṣuluḥu wala bendera, tufanyize tutakavo.

bana Bumiller aliposikia vile, marra akaamrisha 'askari na Wasango kwenda kupiga lile boma. tukenda kupigana mudda wa sa'a nne, lakini hatukuweza kuin-

gia bomani. tukachukua mashoka kwenda kupiga mlango tuuvunje. lakini alikuwa Sudani, ndiye mchukua bendera, akachukua shoka kupiga lango, alipoinua mkono marra ya pili — alikuwa mtu bomani, alimpiga riṣaṣi akaanguka. akatokea kijana mwingine, akachukua shoka lile kupiga langoni, akaanguka vilevile juu ya Sa'id Harubu, wakatokea 'askari katika ḥandaqi ya maji kuelemea juu ya boma. na waanawake, waliomo ndani, wakachukua maji ya moto wakatumwagia. bana Bumiller akaniamrisha kumtafuta mwenyi tarumbeta, ili kupiga tarumbeta kuwarudisha 'askari. nilipofika mwangoni, nikamkuta 'askari moja, rafiqi yangu, akanambia: „usiende mbele, sababu yuko mtu hapo anatuandamia, na siye hatumwoni, naye amekwisha piga watu watatu". nikaambia: „natafuta mwenyi tarumbeta, awarudishe 'askari". akanambia: „yuko hapa, namwita". akamwita, akaamrishwa kupiga tarumbeta, 'askari wakarudi wote kambini kwenda kupumzika. nao wameumia 'askari wanne na watatu wamekufa.

bana Bumiller akatuma ṭarishi katika mji wa Wengereza, Mwenzo, ili kumkhubiri bana mkubwa kutuzidishia 'askari na mzinga. na kutoka hapo ḥatta kufika Mwenzo mwendo wa siku tatu. kulla siku tulijaribu kupandia boma, lakini hatuwezi kuingia, limezungushia kwa ḥandaqi ya maji. tumefanya buṣara zote — hatukuweza kabisa. na katika siku tatu hizo, tulizokaa pekeetu, kulla tukipigana nao tukichoka tukirudi kambini — hupeleka mtu kule mjini, ili kwenda kuwaamrisha kuleta vyakula vya mfalme wao na hongo letu. hawakuqaṣiri wakileta, lakini kufungua mlango na kuchukua bendera — hawataki.

na Wasango wakaleta buṣara yao ya kupigana — ya kuwa wafunge mizigo ya majani, ndio wafanzie nguo, kwani riṣaṣi ikipiga katika majani haina nguvu.

ḥatta siku ya nne hatukupata majibu ya bana mkubwa, ikalázima kupandia boma tenna. tulipofika katika boma, tukachoma moto, lakini haikufa'a kitu. wakaumia Wasango wanane na waziri wao akafa. alivoona vile mtoto wa Merere, ya kama waziri wake amepigwa riṣaṣi, amekufa, tulivorudi kambini, akachukua watu wake wapata mia, akenda upande wake, ataka kulipandia boma pekeyake. lakini kupigana kwao si kuzuri, hupigia mbali bunduqi zao, na wakifika bomani hawana nguvu. nao waoga riṣaṣi, ma'ana katika kambi yetu walichimba katika arḍi, wakilala chini ya arḍi, kwani wakipiga katika boma, riṣaṣi kufika ḥatta kambini mwetu. nao wameumia watu watatu usiku.

ḥatta siku ya tano, watu walioshika zamu ya Zunda hapo alipofungwa, kattikatti ya usiku wakapiga makelele: „huyo Zunda anakimbia". wakamfuata mbio ḥatta qaribu ya boma lake wakamkamata, lakini huyu waziri hakupatikana. alivoulizwa, nani aliyemfungulia kamba, akasema: „mchawi amefungua kwa uchawi". akázidisha kufungwa.

ḥatta as-ṣubuḥi yake akatokea bana Fuchs, akaja na mzinga mmoja na 'askari 'asherīn. marra alipokuja, akaamrisha bana Bumiller kwenda kupiga boma. wakaurekebisha mzinga, wakapiga ḥatta mudda wa sa'a sitta. haikufa'a kitu, wala hapana ḥila nyingine za kufanza. ikabidi kuondosha ṭarishi mwingine kumwita bana mkubwa.

tukakaa pale kumngojea bana mkubwa mudda wa siku nne. ḥatta alipokuja bana mkubwa, akaleta bombom [1]), tukapiga — vilevile haikufa'a. ḥatta usiku akaleta buṣara ya kukusanya mawe na mishare na mikuki, akatwaa makumbi na majani na vitambaa vibovu ku-

1) Maximgeschütz.

fungia mikuki na mishale na mawe, na kutia mafuta Ulaya, tuwashe moto, tutupe juu ya nyumba zao ndani ya boma, na kurusha moto wa Ulaya. ḥatta usiku wakagawa 'askari kulla mtu paḥali yake kuzungusha boma. na katika sa'a sitta usiku wakisikia tarumbeta, kulla mtu atupe moto ndani ya boma. ilipofika sa'a sitta, wakafanya hivyo. wale Washenzi wakawacha mji wakakimbia, lakini hapana mtu aliwaona paḥali walipotoka. al-fajiri tukaingia kule bomani, hatukukuta mtu ḥatta moja, illa moto na ng̃ombe na mbuzi. nao wamechimba vilevile katika arḍi wakilala, ndio ma'ana riṣaṣi zisiwapate.

tukakaa kule mjini ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaondoka, tukautia moto kabisa. tukenda zetu Mwenzo. tulipokwenda mwendo wa sa'a nne, tukafika mwituni, tukawakuta watu wa Zunda, wanatungojea na kucheza mchezo wa vita na kupigana bunduqi. lakini hatukuwatazama, wala hatukusema nao. tumekwenda zetu. na kulla mji tunaopita, wamefunga lango lake.

siku ya tatu tukafika Mwenzo. na Washenzi wa papo wamesta'arabika kidogo, sababu kuwa Wazungu Wengereza, nao wamewafundisha kidogo ṭabi'a za pwani. na Mungereza, aliyokuwa hapo, alitufanzia ḥéshima sana. naye amemwoa Mshenzi, hataki kabisa kurudi tenna Ulaya.

tulivoondoka hapo, tukenda kwa Mwenyi Fipa. tukenda mwendo wa siku mbili, siku ya tatu tukafika kwake. aliposikia, kama tunakuja, akapeleka watu kuja kutuchukua njiani. tulipofika mjini kwake, akafuraḥi, akaleta vitu vingi katika kambi yetu kwa ḥéshima. nao Washenzi wa kule wameeta'arabika kidogo, kwani huja misafara mingi kule. nao hodari kulima. na inchi yao nzuri. na kazi yao sana hupiga tembo. kuamkia kwao, wakiamkia mtu mkubwa, hupigia kidevu chini, [1]halafu hupiga makofi.

tukaondoka kwa Mwenyi Fipa, tukenda kwa mfalme mwingine, wakatufuatia watu wa Mwenyi Fipa, wakathannia tunakwenda kumpiga Kimaraunga. ḥatta tulipofika kwa yule mfalme mwingine, vilevile akatufanzia ḥéshima njema sana na kucheza ngoma. akaleta vitu vingi sana, na kumtafaḍḍali bana mkubwa akampige Kimaraunga, kwani huwaużi sana, naye kawazuilia kwenda kupiga tembo kule Rikwa. bana mkubwa akakataa, akasema: „sitaki vita". na pale na Rikwa siku moja. tukapanda vilima vya Ufipa, tukenda zetu Tanganyika. na juu ya vilima kuna bardi sana, usiku huganda barafu. katika kambi tulipolala, jissi ilivokuwa bardi, bana Bumiller hakustaḥamili ile bardi, akatwambia, tumfanzie moto chini ya kitanda. na usiku kitanda kimeungua kidogo, naye hana khabari. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukakuta barafu juu ya meza imeganda.

aṣ-ṣubuḥi yake tukaingilia katika inchi ya Warungu. na watu wa kule hupiga nyama vilevile. na kulima kwao si sana. ḥatta siku moja tukagawa kwenda piga nyama. bana mkubwa amekwenda kupiga nyama yapata sitta siku hiyo — mbogo, punda milia na swara. na siye tukakuta simba mwituni. bana Bumiller akaifuatia kuipiga, lakini imetukimbia, hatukipata.

usiku wake tumelala porini, akaanza kulia fungo, washenzi wakatwambia, kama kesho amma kesho kutwa itakuwa vita, kwani nyama hiyo hailii burre.

siku ya tatu yake tukafika Karambo katika mpaka wa Wengereza na Wadeutschi. hapo tukakuta huyu mfalme wa mji huo Karambo, akatwambia — kama: „njooni huko mkae bomani, ma'ana Wawemba wanakuja". tukaingia bomani tukakaa. ḥatta usiku magharibi tukasikia bunduqi zapata tisa', wakapigia katika boma. wale wenyeji wakatwambia: „hawa ni Wawemba". tulipoondaka nje, wakakimbia. na siye tukaona moto

mwingi sana mwendo wa nuṣṣu saʿa, ndipo walipojenga kambi yao, lakini tukawacha. tulikuwa na bunduqi khamso u ʿasherīn na mzinga moja na bombom moja.

aṣ-ṣubuḥi yake katika saʿa thenʿáshara, jua linavotoka, tunaona msafara unaokuja, msafara mkubwa. nao wana kulla ʿaina ya bendera, bendera ya bun Saʿid, na ya kingereza, na ya kifranza, na ya kibeljik, na ya kideutschi. khalafu tukat͟hanni msafara wa Waʿarabu. tulipouliza wale wenyeji, wakatwambia: „sulṭani Kitimkuru, anataka kupiga miji yetu“. lakini sisi hatukuṣadiqi min ájili ya zile bendera. haikupata nuṣṣu saʿa wamefika pale mjini. nao hawa watu wakubwa wa vita kulla mtu na bunduqi yake na mkuki na mwavuli kama msafara wa kinyamuesi. walipofika bomani, bana mkubwa akawauliza, kasimama juu ya boma: „msafara wa nani?“ hawakusikia kile kiunguja. akamwita mkalimani wetu Slemani, aliyejua maneno ya kiwemba, akamwamru kuuliza, „msafara wa nani?“ wakajibu: „sisi watu wa Kitimkuru na mwenyewe yuko kattikatti ya msafara, anakuja“. akauliza: „mnataka nini?“ wakasema: „tunataka mji huo, kwani ni watumwa wetu“. akawambia: „bassi ngojeni ḥatta tutoke, ndipo mje hapo mjini“. wakatwambia: „hatutaki kungoja, tunataka mji huo leo, kama hamkuondoka, tutapiga pamoja na watu wenu“. bana mkubwa akawambia: „mimi sitaki vita, wacheni tufanye ṣuluḥu, mpatane“. lakini Wawemba hawakusikia, wanataka lázima wavunje lile boma. na kule kusema nao wanazidi kuzungusha boma. bana Fuchsi na bana Bumiller wanamwambia bana mkubwa, kama haifai kusema sana, kwani hawa watu wengi sana kuliko sisi, yapata themánia elfu. na katika boma hili hatupati wote pamoja watu mitēni. wakamwambia: „bassi wacha kusema nao, piga mzinga na bombom, maʿana wanaweza killa mtu kuvunja mti

mmoja, na wakiingia hapa, tumepotea zote". hasikii bana mkubwa, akazidi kusema nao. na mshenzi mmoja, waziri wa mfalme wa Karambo, akatwambia: „kama ninyi hamtaki kupigana, miye ntaanza kupiga". marra akapiga bunduqi yake. alivoipiga, ndivo bana mkubwa alipiga bombom na mzinga. akawambia ʿaskari: „fungueni boma, tutoke nje". likafunguliwa boma, haikupata mudda wa daqiqa nane, Wawemba wamekimbia wote.

nao palikuwa waanawake wawili, walitekwa na Wawemba, ili kuwafanya watumwa. walivoona vile tunavopigana na Wawemba, wale waanawake wakakhiyari kuqábili riṣaṣi zetu, ili kuja kututafuta. na wote wawili walipigwa riṣaṣi, lakini hawakufa. tukawachukua kuwafanzia dawa. tukauliza: „nini maʿana kuqábili riṣaṣi zetu?" wasema: „afaḍali kufa kuliko taʿabu ya Wawemba".

ḥatta mudda wa nuṣṣu saʿa tulivofuatia nyuma ya Wawemba, ikatokea jeshi moja ya Wawemba, yapata watu thalatha mia, kutokea nyuma yetu kutupiga, lakini mwʿezimgu hutujaʿalia, tukaona qabla yao, tukaanza kuwapiga. wakapiga bunduqi marra mbili, wakakimbia. na kulla paḥali tunapoingia mwituni, hukuta maiti ya Wawemba. na upande wetu hapana aliyoumia. wale washenzi wa mji walikuwa na furaḥa kubwa. walichukua vichwa vya watu waliouawa, wakaviweka pamoja, wakapiga ngoma, wakazungusha na kucheza wakipiga ngoma. na katika miji ya qaribu ya Karambo wote walikuja katika mji huo wa Karambo kucheza ngoma, sababu walifuraḥi walivopigwa Wawemba.

ḥatta siku ya pili tukaondoka, tukenda zetu Tanganyika. na hapo mwendo wa siku moja u nuṣṣu ḥatta kufika Tanganyika. tukakuta watu njiani, wakatwambia: „Wawemba wamekwenda mwendo wa siku nne kwa

siku moja, jissi walivokuwa wakiogopa". siku ya pili tukafika baḥari ya Tanganyika. na hapo tulipofika, bana mkubwa akachukua mitumbwi na watu wake kupitia baḥarini, ili kutaka kwenda Kituta, mji wa Wengereza. na siye tukapita barrani. hapo tulipojenga kambi ya kwanza, tukamngojea — siku ya pili hakuja. bana Bumiller akachukua watu na vyakula kwenda kumtafuta, ma'ana hakuwa na vyakula. wakenda mwendo wa sa'a tano, wakakutana naye, wakakuta ile mitumbwi imepigwa na wawimbi imevunjika, wakaja nao kambini.

na katika watu wa kule Tanganyika nyumba zao kama nyumba za Wakonde, lakini si naḍifu kama za Wakonde. nao huvaa nguo kama Wanyamuesi. na vyakula vya kule mtama na mahindi na ngano na samaki wengi sana. na baḥari ikichafuka, huwa mbaya kuliko baḥari kubwa. nayo khaṭari sana koga baḥarini min ájili ya mamba na viboko.

na kambi ya mwisho ya kufikia Kituta, msafara ulivoondoka aṣ-ṣubuḥi, tulivokwenda mwendo wa nuṣṣu sa'a, tukakuta kiboko mwituni. bana Bumiller na bana Fuchsi wakakifuatia kutaka kukipiga, lakini hawakuwaḥi kupiga, kilikimbia mbio, kikapita kattikatti ya msafara wetu kutafuta baḥari. na watu waliokuwa qaribu, wote wakashtuka kwa kishindo kwa jissi kinavokwenda upesi na gházia yake. ma'ana hawakuweza kupiga kwa hivo kilivopita katika jeshi ya watu. wakakifuatia ḥatta kikaingia baḥarini. na mtu akiona kiboko, hut̲h̲anni hakiwezi kukimbia, lakini huenda upesi kuliko frasi.

tulivoondoka hapo, tukenda mwendo wa sa'a sitta, tukafika Kituta. na ule mji wa Wengereza, wana duka lao la bi'ashara ya pembe. na wale washenzi wa hapo welevu kidogo, wanaelewa na khabari ya pwani, ma'ana

huja Wazungu wengi na Wa'arabu, khaṣṣa Rumaliza [1]). na washenzi wa hapo walifuraḥi sana tulipofika. killa siku walicheza ngoma. ḥatta wakicheza ngoma, huwita 'askari kucheza nao. na 'askari hawajui, lakini walikuwa wakiwafundisha. na mchezo wao hutia ngoma kattikatti, hupangiana katika mṣafa mwanamke na mwanamme, huingia kattikatti ya wanja hucheza, wakarudi wakaingia katika mṣafa, hubadilisha kwa zamu. ḥatta mwisho wao hupiga makofi, ndio wanapumzika.

nao naḍifu, huoga sana, na nguo zao hufua, wameshika kama ṭabi'a za pwani. na waanawake mardadi sana. na kupika kwao máthal kidogo kama mapishi yetu, lakini si sana — kidogo. na baḥari ya Tanganyika inawapa samaki wengi na wakubwa, nao wana mafuta wengi.

tukakaa Kituta siku saba'. wale Wengereza wakatwambia, kama pana Mshenzi, anakaa pande za Urungu, yeye huważarau sana, akafanya vita nao, bana mkubwa awasa'idie, amwondoshe huyu mshenzi, jina lake Kabunda. bana mkubwa akaondoka na 'askari, wale Wengereza wakafuatana nao kwenda kumpiga yule mshenzi. na kutoka Kituta ḥatta kufika kwa Kabunda yapata siku sitta. wakenda kule, wakapiga, wakachukua na mateka watu, waliofanywa watumwa kule, wakawaleta Kituta.

tukafanya safari ya kurudi Nyassa, lakini tukarudi njia nyingine, inayotokea Karonga. siku tuliyoondoka Kituta, tumekwenda katika mji moja wa mapadri ya Wafranza. tukalala hapo. kuondoka tukenda siku mbili porini, hapana maji wala mji. na paḥali tulipolala, tumekuta matope. hatujui kama maji

---

1) Muḥammed bin Khalfan.

amma mkojo wa tembo, lakini hapana mtu aliyowacha — wote wamekunywa yale matope.

ḥatta siku ya nne tukafika mji katika Unyika. hapo tulipata vyakula na maji. tukenda tenna kupiga nyama. siku ya tano tukafika Mwenzo. na Mwenzo walivopata khabari, ya kuwa sisi tunakuja, wakaja kutuchukua njiani kupiga ngoma na bunduqi kwa furaḥa, maʿana wanatujua. tumekaa pale, sababu wametuzoea.

ba'ada ya siku nne tukaletewa ṭarishi kutwambia, kama bana Sakrani [1]) wamefuata Wazungu wawili, wanakuja kumtafuta bana mkubwa. tukaondoka Mwenzo, siku ya pili tukakutana naye njiani. akamwelezea bana mkubwa, amekuja kumwita. tukarejeʿa tukenda mwendo wa siku tatu, tukafika Konde. na tulipofika kwa Mlozi tukalala. siku ya pili tukenda Katunga. ilikuwa jua kali sana, na majani yamekauka. katika saʿa sitta ya mchana tukaona moto mbele yetu. ḥatta yapata roboʿ saʿa kufika penyi moto — wengine waliwaḥi kupita na wengine hawakuwaḥi. na majani mengi pale. bana Fuchsi akataka kwenda mbele upesi kukimbia mbio ule moto — ukamwunguza nywele zote na ndevu zake. msafara mwingine ukakaa nyuma ḥatta ule moto ukazimika. jioni tukafika Karonga. tukakaa siku tatu. bana mkubwa akatuma mtu kuleta mashua, na msafara upitie Konde ḥatta kwa Mwakaringa, hapo tutaletewa mashua. tukenda mwendo wa siku mbili, tukafika katika inchi ya Mwakaringa. yakaja matishali yetu kutuchukua, ili kwenda Rumbira.

tulivoingia katika mashua, ʿaskari furaḥa yao kubwa mno, kama walivosikia, meli imekwisha jengwa,

---

1) Hauptmann Prince.

inakwenda tenna. wakemba wimbo katika kuvuta makasia, wimbo huo:

„bassi wē!
mgogoro bassi wē!
meli imekuja,
mgogoro bassi wē!“

na bana mkubwa na bana Bumiller wakawasa'idia kwimba wimbo huo.

tukafika Rumbira, lakini hatukukaa sana. bana mkubwa akenda kupiga nyama Konde, yeye na bana Bumiller na bana Sakrani. huyu akachukua 'askari yake kabisa kwenda zake kwa Merere, mudda wa mwezi arejee Rumbira.

bado kidogo bana mkubwa akarudi. alipokuja, meli siku hiyo ikaja na bana Eltz. ikabidi yeye kukaa Rumbira, na siye kurudi pwani. wakafanya mashauri, ya kuwa bana mkubwa aingie katika stima kwenda Fort Johnston, warudi waje khalafu, ndio turejee pwani.

aliporudi akauliza 'askari, anayetaka kurudi, na anayetaka kukaa Rumbira. wengine wakasema „tunataka“, wengine wakasema „twataka kurudi pwani“.

tukafanya safari kurudi, tukaingia katika meli, na jina lake „Hermann von Wissmann“, tukenda Fort Johnston. kule tukashuka, tukaingia katika matishali ya Wengereza ḥatta kufika Mpimbi. na kufika pale tumekaa katika kambi yetu ya zamani siku moja, tukasafiri kwenda Matope. mashua yetu, iliyo mwisho, waliingia bana Fuchs na bana Frank. siye tulivotangulia mbele, tukenda paḥali, tukashuka kutelekeza. tukaona mtumbwi unakuja kutwambia — ya kama: „ile mashua imekaa nyuma, sababu bana Fuchs hawezi“. bana mkubwa akarudi mwenyewe nyuma,

akenda kamchukua, akaja naye Matope. tukakaa Matope siku tatu kumwuguza, lakini ugonywa umemzidi. na siye tukalala kwa zamu kumtazama. ḥatta siku ya nne bana mkubwa akamwamrisha bana Bumiller kuchukua msafara atangulie Blantyre. bana mkubwa akamtazama bana Fuchs. tulivoondoka usiku tukafika Blantyre. ḥatta aṣ-ṣubuḥi akaja ṭarishi, akatwambia, kama amekufa. bana mkubwa akamzika kule, akaondoka, akatufuatia Blantyre.

alivokuja Blantyre, tukaondoka kwenda Katunga. ḥatta siku ya pili tukafika Katunga. tulipojenga kambi yetu, walikwenda Ḥabashi wawili mtoni kuteka maji. moja akapigwa kofi na mkia wa mamba, akamwangusha majini, akamchukua. mwenzi wake akapiga makelele, ḥatta watu walivoshuka mtoni — hawakumwona.

tukakaa ḥatta siku ya pili, tukachukua mashua, ili kuingia mtoni kwenda Tshiromo. kule Tshiromo tukakaa siku mbili, ili kupiga nyama. bana mkubwa akapiga mbogo, na bana Bumiller vilevile mbogo moja. kuondoka hapo tukafika Msange. na hapo bana Bumiller alishikwa na ḥoma sana, tukathanni atakufa. tukapàta makapakapa [1]) ya Wengereza, tukaingia, tukafika Msongwe. tulipofika Msongwe, ugonywa ukamzidi. ikabidi kushuka pale na kutazama ḥali yake. tukakaa siku tatu. lázima kullă saʿa mbili kushika zamu kumtazama. na bana mkubwa vilevile akashika zamu yake. siku mbili hakuweza kusema, siku ya tatu hajambo kidogo. tukampakia katika stima, akawa hawezi ḥatta tulipofika Shinde, khalafu akapata hajambo kidogo.

na katika njia ile tuliyopita waqati wa kwenda

1) Flussdampfer.

Nyassa, tumekuta vingine waqati wa kurudi, ma'ana kulijengwa sana, wamekuja Wazungu na Wahindi na Mabanyani. khaṣṣa kule Shinde tumekuta zimejengwa nyumba nyingi na maduka mengi. tukakaa siku nne ikaja stima „Wissmann“, ikatuchukua ḥatta Mzumbidji. na kule tukaingia katika meli kubwa „Kanzler“, kwenda Daressalama na Unguja. hio ndio mwisho wa safari yangu ya Nyassa.

# Safari yangu ya Ulaya toka Daressalama ḥatta Berlin

ya

**Selim bin Abakari.**

katika mwaka elfu themānie mia arbaʿ u tisaʿin niliondoka Daressalama katika meli[1]) ya Ostafrika-Linie, ʿázima yangu kwenda Ulaya. nilipoingia katika meli, nikaona anasa kubwa katika mabaḥaria, wanaopandisha Wazungu, wanaosafiri kurudi Ulaya. na dasturi kule Daressalama, ikiingia meli katika bandari, huja Wazungu wengi katika meli. wengine wanakuja kutazama meli, na wengine wanakuja kunywa bier, na wengine wanakuja kuaga rafiqi zao na ndugu zao. huja katika meli kwa furaḥa na buriani kuwapa ndugu zao. na wengine unaona ḥali zao mbaya, hawawezi kwa ḥoma, wanavopata rukhṣa kwenda kubadili hawa kwao Ulaya. wakiingia katika meli, ṣura zao hubadilika, huonekana wazima kidogo kwa furaḥa wanavokwenda kwao kuugua, bassi roḥo zao hurutubika kidogo.

na hawa, wanaokuja kuwapa rafiqi zao buriani, huamrisha mvinyo kugongeana pamoja na ndugu zao na rafiqi zao kwa furaḥa na masikitiko wanavoachana.

---

1) engl. mail.

na waqati meli inavoondoka, mashua zote huzungusha meli pande zote mbili na nyuma, ili kungoja meli ikiondosha nanga. sa'a mbili tatu qabla ya kuondoka, meli inapiga selo [1]) ya kuondokea. na ikitoka bendarini, watu hupepea vitambaa na kupigia hipp hipp hurrah! mashua haziondoki mpaka meli iondoke milangoni. na zile mashua nyingi hupendeza sana kwa uzuri wao. mtu akiwa katika meli — anatazama, kwani kulla mashua hutundika bendera yake, na mavazi ya baḥaria kama mavazi ya mabaḥaria ya manowari. kulla mashua mavazi mengine, nayo naḍifu sana.

na meli ikifika milangoni ya bandari, unaona kisiwa chenyi mnara wa taa. hupitia upande wa mkono mshoto ikitoka. mwendo wa nuṣṣu sa'a meli hufika visiwa vya Kondutshi. ḥatta ikifika sa'a, meli iko kattikatti ya kisiwa cha Unguja na mrima, tenna mtu anaona barra muli na barra kisiwa. bado kidogo kinatokea kisiwa cha Tshumbe. na toka hapa mwendo wa nuṣṣu sa'a inatokea nyumba ya Tshukwani. na nyumba hiyo ya sulṭani wa Unguja ya kubadili hawa. nayo iko katika rasi ya Tshukwani.

na sulṭani akitoka mjini, akienda badili hawa kule Tshukwani, hupendeza mno, kwani huenda kwa gházia, kwa magari ya frasi mnamo waanawake, masuria wake. lakini qabla yeye kuondoka mjini, hutanguliza 'askari na matarumbeta na watu wa kumkhodumu. na siku anayokwenda yeye hufuatana na magari na wapanda wa frasi, na Wa'arabu huvaa ya kibedui [2]), hupanda ngamia, hutangulia mbele, wengine huwa nyuma. na njiani husimama 'askari. hapana rukhṣa mtu kupita mpaka sulṭani apite. na akipita, mtu akimwona, salamu yake „ṣubalkheri seyyidna“. na gari ḷake frasi wanne ḥatta

1) engl. sail ho! Schiff in Sicht! — 2) nach Beduinen-Art.

sitta, nao huwa namna moja, mno huwa weupe. na gari kitambaa chake kimesukwa kwa zari ya żahabu. nao wanaopanda frasi shurṭi wafute panga zao, ziwe mikononi. na Wa'arabu huchukua mikuki ya ki'arabu, hushika mkono mume na upanga hutia begani.

na meli ikiwacha Tshukwani, ikiqurubia mji, unaona jumba la sulṭani bēt el-'ajāib, na mnara wa taa, na nyumba za mabalozi [1]), na nyumba ya sim [2]). tenna waqati ule selo imepanda mnarani. na watu wa pwani wakisikia „selo", hufuraḥi sana, kulla mtu huita „selo" kwa marra moja. ijapokuwa wanakula chakula amma wanaṣali, na watu waliozoea kuita „selo" — huwacha kazi waliyo nayo, huita „selo" kwa furaḥa, ma'ana ndipo wanapopata fáyida yao. tenna kulla paḥali wanapokaa hushukia pwani kutengeneza mashua zao kungojea meli. na ikifika bendarini huja na mashua nyingi, wanavuta wanaijia meli qabla haikutia nanga. sasa huja robani [3]) na bendera yake kuja kuwaonyesha paḥali pa kutia nanga. na robani mwenyi rukhṣa ya kupanda wa kwanza katika meli. waqati wa kutia nanga hupiga mzinga mmoja, ndio desturi.

na mashua zimezunguka meli hungojea ngazi [4]) kurekebishwa. hapo ndipo penyi uzuri, hupendeza sana wale watoto wa pwani. hupigana kwa kugombea ngazi, kulla mtu ataka mashua yake ndiyo iwe ya kwanza kuegesha ngazini, hupigana kwa makonde na vigongo, na kutukana, kwa makasia kugongana na kusukuma mashua ya mwenzi wake. kulla mwenyi nguvu husukuma asiyo na nguvu, sababu apate yeye ngazi kwanza.

na ngazi ikisha rekebishwa, wakiegesha mashua zao, bassi wakipanda ngazini kama nzige kwa wingi

---

1) balozi Konsul. — 2) Post- und Telegrafen-Amt. — 3) Lootse. — 4) Fallreep.

na kusukumana. na kama wakiingia katika meli huwa kama wazimu macho yao. huingia kwa vishindo na gházia kuuliza watu, waliomo katika meli, anayetaka kushuka.

waqati ule ma'abiria hutengeneza kushuka kutazama mji. bassi wakifika pwani, husimama wachukuzi ṭayyari, huja kumchukua 'abiria mabegani katika mashua, humpeleka inchi kavu. na iwapo yuko mwenyi mizigo — hupigania, kulla mzigo hupigania watu wawili amma watatu, kulla mtu ataka kuchukua, min ájili kupata rizqi.

na ba'ada ya hivo wako mabichboi[1]), kazi yao hungojea wageni, wanaokuja, ili kuwapeleka mjini kuonyesha njia. nao vilevile hupigania wageni. huja qádiri ya wanne, husukumana huambiana: „ondoka, huyu mgeni wangu, namjua". mwisho hupigana, na mgeni akiona wanapigana — huchagua mwingine, asiyoingia katika ugomvi wao. ndivo wanavopeleka wageni mjini kuwaonyesha katika hoteli na miqahawa na madukani. wengine wanakwenda Mnazimoja, panapo nyumba za Wazungu, zinazokwitwa club. na wengine wanakwenda N̈gambo[2]) kutazama nyumba za wenyeji, na wengine wanapanda punda kwenda mashamba, wengine wanachukua magari, lakini kulla mtu huwa na bichboi wake.

na wanaokwenda madukani kununua vitu, huenda hupunjwa na Wahindi na Mabanyani. kitu rakhiṣi hununua ghali, kitu ghali hununua rakhiṣi, kwani be'i wanaishika Wahindi: iwapo mtu ananunua kitu cha rupia — hushika be'i ya rupia kumi. nao hushindana sana katika be'i, hupunguza ḥatta mwisho hufika rupia. katika mashindano ya bi'ashara yao mtu akisema „sitaki", akitaka kwenda zake — humrudisha „njoo, haya nunua, sema bana, ngapi utanipa?" ukimwambia „nta-

---

1) engl. beach-boy. — 2) Negerviertel Zanzibar's.

kupa hivi" — hukataa. ukiondoka anakwita vilevile „njoo, njoo, patana bana, hapana kosana, nunua bana". itakuwa hivo mpaka mudda wa sa'a mbili tatu. akiona kama kweli hununui, unataka kwenda zako — hukufuatia njiani hukuita „haya njoo, chukua bana, bakhti yako".

na wengine huenda sokoni, huenda kutazama vitu vinavyonadiwa. wengine hununua, wengine wanatazama namna wenyewe wanavonadi kwa makelele. na mtu akiwa katika soko, ukisema na mwenzio, hasikii kwa makelele, ma'ana watu wengi kule, na madalali wakifanya kelele zao wakinadi — watu hawasikilizani. na kunadi kwao: husimama wanunuzi, huzungusha mṣafa, na dalali huingia katti, hushika kitu kinanadiwa, huanza katika pesa moja kushauri watu, na wanunuzi humjibu majibu ya kupandisha be'i. mwingine husema pesa mbili, mwingine pesa tatu, naye huwa akisema „fels" [1]). iwapo akiqubali husema „alláhu bārek" [2]) — humpa.

na katika soko kulla aina ya vitu vinavyotoka shamba kama ndizi, nazi, machungwa, embe, mastafeli, kangaja, madafu, malimao, mafenesi, ndimu, mananasi, mapera, madanzi, machenza, zambarao, matunda manga, mapapaye, matoffaha, shōkshōki, mabibo, mabalungi, kwaju, duriyani, topetope, muhogo, mahindi, viazi vidogo, viazi vikubwa na kulla namna ya mboga.

na vitu vya mjini, vinavyoletwa sokoni, ni silaḥa kama panga na bunduqi, na fimbo, na miavuli, na nguo kama kikoi, na kanzu, na kofia, na visibao, na suruali. na tenna vyombo vya waanawake kama kanga, na kanzu za kike, na suruali za kike, na madisimali, na kaya nyeusi, na binägir, na mikufu, na mitali, na vikuku, na vikoa, na mapete, na vipini, na hazama, na

1) fels = pandisha. — 2) Gott segne dich.

useja. huleta na sinia, na ṣaḥani, na mabaquli, na maṣanduqu, na vitanda, na magodoro, nà mito, na vyoo, na mazulia, na visu. killa kitu huweza kununua sokoni, na mtu hupata rakhiṣi kuliko madukani sababu ya kuwa mnadà.

na wengine wanakwenda mashamba kutazama miqarafuu na minazi. na mtu akenda njiani, akiqurubia mashamba yà miqàrafuu waqati inapozaa, ʿarufu yao huenda mbali sana. qádiri ya mwendo wa nuṣṣu saʿa husikia ʿarufu yake. na ukiwa mbali, ukàtazama miti yake, hupendeza sana, jissi ilivosimama uzuri, imenyoka, matawi yao yameinukia juu. na ukiingia katika shamba yenyi miqarafuu mingi — hupendeza mno, jissi ilivokwenda miṣafa miṣafa sawasawa, kulla upande hukuta miti yote sawasawa, sababu imepandwa mwakà mmoja.

na katika mavuno yào hualikwa wàtu kwa siku moja, huja kuichukua kwa ngoma na machezo na kwimba kuipeleka forḍani, iende ikatozwe ʿushuru. ikisha hupelekwa nyumbani kwa mwenyewe, amma hupatana na tájiri kule forḍani hununua. na katika mji mzima wa Unguja ni ʿarufu tupu ya qarafuu, killa paḥali mtu anapokwenda.

turejee sasa katika meli yetu, inayotuleta Ulaya. tulipoondoka Unguja, tukenda Tanga. safari ya saʿa sitta. na ukiondoka bandarini Unguja, meli hutambaa qaribu ya pwani, hufanza kama inakwenda kupiga rasi ya Marukhūbi. na ukipita hapo Marukhūbi unaona nyumbà nzuri ya sulṭani ya kubadili hawa pamoja na bustàni nzuri. nyumba ile ilikuwa mali yà Mwʿarabu, jina lake Marukhūbi, àkanyanganywa na Seyyid Barghashi.

na meli ikifika mbele kidogo, huona nyumba ya Mangapwàni, ni vilevile mali ya sulṭani. na kwa juu vilimàni huona mashamba mazuri ya miqarafuu na

miembe na michungwa na minazi tele. ḥatta ukiwa baḥarini, ukitazama — hupendeza mno.

ba'ada ya kupita nyumba hiyo tenna kinatokea kisiwà cha Tumbatu. na hawa Watumbatu wanajua kazi ya baḥari sàna. na kusafiri kwao husafiri kwà nyota. wào mno huwa mànokhoża, kwani katika baḥari ya sawaḥeli hujua kulla paḥali pazuri na pàbaya pa kupita na chombo. ijapokuwa usiku wà kiza, naye hàna dira, lakini huwezà kupita ile miambà ya khaṭari na fungu za khaṭari, naye asiḍurike na chombo chake.

na hàpo Tumbatu meli ikipita, unaona kisiwa cha Unguja nà barra qaribu na Pangani, ya'ani kisiwa cha Maziwe, ndio milango ya Pangani. nà baḥari ya hàpo mbaya kidogo, haikutulizana. ba'ada ya kupitá barra ya Pangani mwendo wa sa'a mbili huona Tanga. na ukiingia milangoni, ukatazama mjini, hupendeza sana lile komo[1]) la minazi na miembe na michungwa, na kattikatti nyumbà nyeupe za kizungu. na nyuma kwa juu huona mṣafa wa vilima vya Usambara, vimefungàna kama kilima kimoja kwa kimoja.

na bandari yake ya Tanga nzuri sanà, maji yake yametulizana. bandari hii imejificha kwa upepo mbaya. ijapokuwa kusi amma kaskazi, maghribu amma maṭla'i, haiwezi kuḍuru chombo, mtu akiwa katika bandari ya Tanga. nayo ndiyo bandari ya pili katika inchi ya Madeutschi Afrika kwa uzuri, kwani iko ghobani[2]) njema. na tenna samaki wengi sana. meli ikisha egeshà, huwa na mitumbwi mingi, inayoleta samaki kuuza.

Wazungu, walioko pwani, wakisha iona meli, huchukua mashua zao, na kulla mtu hutundika bendera yake màshuani, wanakuja kuipandia meli kuwatazama

1) kiangazija = Hain. Die Suaheli sagen kiza cha minazi. — 2) Bucht.

jàmaʿá yáo na rafiqi zào, na kuletà maʿabiria, wanaotaka kusafiri kwenda Ulaya. na zile mashua, mabaharia wanaovuta makasia — huvuta kwa amri. na màvazi yao ni mamoja, mavazi meupe, desturi vilevile kàma kule Daressalama.

na mtu akishuka pwàni, hufika kwànza fordani, khalafu anakwendea bomani. mtu àkiingia sasa mjini, hustaʿajjabu sanà jissi ulivotengenea mji, kwani zamani ulikuwa mji mdogo na nyumba ndogo na mbaya za makuti, lakini sasa, walipoingia Madeutschi, wameuvunja mji, wamejenga vingine, nyumba za misafa. tokà nyumba za mawe hatta za udongo shurti zifuatane msafa mmoja, na njia ziwe pana na kulimiwà. na mtu akiingia sasa mjini ànatembea, anapoona zile nyumba na zile njia na bustàni jissi zilivolimiwa — hujua, kama kweli inchi hii imeingia wàtu hodari, wenyi hékimà na maʿarifa.

na miye nimeonà Tanga na Daressalama qàbla ya Wadeutschi kuingia Dàressalama ilikuwa mathal ya shamba qádiri ya watu thalatha mia, hapana záyidi, na nyumba mbovumbovu. na sasa mtu akiona Dàressalama hushituka kwa jissi ilivo kubwa na jissi ilivotengenea kwà nyumba nzuri, na njia nzuri, kwa bustani njema. na watu wengi wamo sasa, watu wa sirkali, na watu wa kazi, na mabazazi kàma Wahindi na Waʿarabu na Wazungu wenyewe, waliofanya madukà. na upànde wà pwani qaribu na bandari imezunguka majumba ya mawe ya Wazungu, na foroda kubwa, na nyuma yake ya majumba haya ya mawe pana majumba ya mawe madogo kuliko ya Wazungu, nyumbà hizo ndizo za Wahindi na za Waʿarabu. na nyuma ya nyumba hizo za Wahindi na zà Waʿarabu pana nyumba za udongo katika njia nzuri na nadifu. nyumba hizo zote zimepakwa chokaa nyeupe, unavozitazàma huwa kamà bafta. na kulla nyumba ina baraza yake, wenyewe wanàikaa

wakizungumza wakicheza mabao na damá ná kàrata. ná wenyewe ndio Wasuaheli, ndio wanaokaa katika majumba hayo.

sasa na turudi katika khabari zetu za Tanga. Wazungu wamejenga sasa gari la moshi [1]) kule Tanga. wálipoanza kujengá, wamechimba katika ardi chini, wakáfanya hàndaqi, ili kujengea uzuri, liwe na nguvu. gari hilo sasa linakwenda hatta kufika Korogwe. ukienda kwa miguu toka Tanga hatta Korogwe hupata qádiri ya siku nane — gari linakwenda mchana kutwa.

na kuondoka Tanga hatta Mombasa mwendo wa sa'a tano. mtu akifika qaribu ya inchi, akiingia milangoni, kwanza huona gereza ya zamani ya masultani wa Mvita [2]), huiona kwa juu. khatari sana kwa chombo, ikiwa pana vita. bandari ya Mombasa nzuri, iko ghobani.

na hapo Mvita wenyeji wa hapo watu mahushumu, nao watu wa 'elim. na msemo wao kisuaheli, lakini namna nyingine kuliko kiunguja. vitu vingine huita namna nyingine kama kule Unguja, lakini watu husikilizana na watu wa Unguja. na maduka ya hapo ya Wahindi na Wazungu na Wa'arabu na watu wa Mvita wenyewe, lakini si mengi.

na vyakula vya hapo záyidi mtama. mpunga upo, lakini si mwingi. na tenna mahindi yapo na muhogo na viazi. ndizi zipo, lakini si nyingi. na matunda si mengi sana kule.

na hapo Mombasa ndipo linapoanza gari la moshi la Wengereza, linakwenda hatta kufika Uganda.

meli ikiondoka Mombasa, inakwenda kutwa, siku ya pili iko Amu. bandari yake mbali sana, na milango mibaya ya kushukia pwani. kutoka bandarini hatta kufika pwani robo' sa'a. na mtu akiwa bandarini,

---

1) Eisenbahn. — 2) Mombasa.

huoná nyumba nzuri sana na minazi mingi. na akishuka pwani, katika mji njia zake nyembambá sana, majumba yamesongana. na mji si naḍifu, lakini katika nyumba yao, mtu akiingia, huona naḍifu sana. majumba ya mawe mengi sana hapo. na kulla paḥali unapokwenda, ukifika barazani, wenyewe hukuqurubisha, hukupa kiko cha kuvuta, ndio neno la kwanza. na wenyewe ḥatta waanawake huvuta viko. nao hunywa tembo sana, lakini tembo tamu, ndio maji yao wanayokunywa. kulla paḥali, mtu anapokwenda, huqáribisha „qaribu njugu" [1]), huuliza kama watáka chembo [2]) amma kuvuta kiko. wana ḥéshima sana.

watu wa Amu ndio watu zamàni máqabaila wásta-ʿarabu [3]), walioko sasa katika barra ya suaḥeli. nao wanajua ʿelim sána, na kutunga mashaʿiri hujua sana. ndio paḥali katika barra ya suaḥeli, panapopatikana watu, wanaojua kutunga vyuo vya ḥadithi na kufasiri vyuo vya kiʿarabu katika lugha yao. khabari yao kama ṭabiʿa yà kiʿarabu, killà kitu wanayotumia shurṭi waandike kwa kalamu. nao wana khabari nyingi za zamani, wanazozijua katika barra ya suaḥeli. watu wengi husafiri kwenda Amu min ájili ya kwenda kusoma ʿelim. katika ʿelim yoyote unayoitaka katika islamu, ukenda Amu, utaweza kuʿallim.

na katika vyombo vyao vya kusafiria madau na mitepe na betela. mitepe misumari yake ni kamba, hapana misumari ya chuma, na tanga ni jamvi. na watu, wanaosafiri katika mitepe, wana ṭabiʿa moja mbaya. kulla mtu huchukua chakula chake mbali katika kikapu chake. iwapo mmoja amekwishiwa nà chakula, akimwambia mwenziwe „nipe chakula, maʿana changu

---

1) ndugu. — 2) tembo. — 3) arabisierte Stämme.

kimekwisha" — humwambia „hakuna njugu [1]), mchepe [2]) ni mmoja, lakini kulla mtu na kitumbache" [3]).

kule Amu kuna ufuta mwingi, na mtama mwingi, na pamba jingi, na njugu nyingi, na matunda mengi, lakini mpunga si mwingi sana.

na meli ikiondoka Amu kwenda Aden, imemlázima mwendo wa siku sitta. watu wakiqurubia katika barrȧ ya Somali wanaona vilima, vilivyoko katika rasi ya Gardafui. na rasi hiyo khaṭari sana kwa kuḍuru vyombo, kwȧni rasi hiyo inakwenda mbali sana baḥarini. tenna baḥari ya hapo mbaya, sabȧbu maji yana mikondo [4]) miwili, inȧyopigana pamoja. na ile mikondo ya maji huvuta jahazi sana kuipeleka upande kwenyi rasi. ndio maʿana watu, wakipita hapo, lázima watazame sana. katika meli yetu wote walilewa kwa baḥari [5]), watu kidogo waliokuwa wazima, na waliokuwa mezani kidogo sana.

kuondoka hapo ḥatta kufika Aden saʿȧ arbaʿ u ʿesherīn. na mtu ȧkifika qaribu ya Aden, huonȧ jebali la Aden, lakini ḥatta kutia nanga inachukua saʿa mbili u nuṣṣu. juu ya jebali hilo pana mlingote wȧ bendera, huona kulla upande unaotokea jahazi amma meli. na ule mlingote hupandishwa selo, wapashe khabari walio mjini.

tenna pana buruji, iliyojengwa min ájili ya mizinga kuiweka juu. kwȧni Wengereza wameijenga buruji hiyo, kama pana vita wao na qabila nyingine wakapigana, ikipita merikebu ao manowari wȧizamishe na ile mizinga iliyopo katika buruji. maʿana hiyo ndio

---

1) ndugu. — 2) mtepe. — 3) kitumba chake = kikapu chake. 4) Strömung. — 5) für „seekrank sein" hat der Suaheli folgende Ausdrücke: kulewa kwa baḥari, kulewa baḥarini, kuona kizungu cha baḥari, kuona msukosuko wa baḥari, kuona mrama wa baḥari, kuona taʿabu ya baḥari.

njia kubwa ináyofungana na Ulaya na Afrika na barra Hindi na Ṣini [1]), lázima meli zipite Aden, hapana njia nyingine.

tulipokwisha zunguka jebali, marra tukaona majumba na bandari. haikupata nuṣṣu saʿa tukatia nanga. na mbele ya bandari huona kama majumba meupe, lakini si majumba — ni chumvi [2]). na anayefanya chumvi hiyo ni Italiani. meli ilipokwisha egesha bandarini, tukaona gházia ya mashua na meli zinazokuja. mashua hizo za Wasomali. nao hupakia pembe za nyama za mwitu, na ngozi za chui na za simba, na vitunga, huchukua na vitambaa na miswaki, hupakia na Mayahudi [3]), wanaouza nguo za ḥariri na vitambaa vya ḥariri na manyoa ya mbuni.

wakifika katika meli, huwa makelele sana, watu hawasikilizani kabisa kwa makelele yao. wanainua vitu vyao, huonyesha maʿabiria, nao huanza beʿi kubwa sana, huuliza kwanza pauni [5]) mbili amma tatu, ḥatta kushuka rupia mbili tatu. nao hawapati siku zote rukhṣa, kupanda katika meli, lakini wakipata rukhsa, wakija katika meli, huja huwadanganya maʿabiria kwa kucheka na kucheza. na mchezo wao kama watu wenyi wazimu amma watu wapumbavu. hupiga makofi na kupiga makelele, tenna hukusanya miguu pamoja hurukaruka. vyumba vyote vya meli hufungwa na madirisha hufungwa kwa kuogopa wevi, maʿana Wasomali wanakwiba sana. kama hawawezi kupita milangoni, hupita katika madirisha kwiba vitu. nao hawa Wasomali huwasumbua sana hao Mayahudi, huwapiga na kuwatoza mapesa kwa kuwatisha, kwani Mayahudi wa hapo kama popote waoga sana.

watoto wadogo wa Wasomali wana mitumbwi yao

1) China. — 2) Saline. — 3) Juden. — 4) engl. pound.

midogo. huweta Wazungu, huwambia watupe feḍḍa baḥarini, waizamie wachukue. nào huita kwa makelele „hev e daiv“ [1]), hev e daiv“, wakitupiwa nao huzamia, ʿajabu haipotei kabisa. lázima kuipata katika maji, ijapokuwa maji marefu sana. wao hodari sana kwa kwenda mbizi [2]).

na mtu akishuka pwáni, akifika forḍani, vilevile hufanya gházia kwa kupigania màʿabiria wawafuate. wengine huleta magàri ya fràsi, wengine wànaleta punda, wengine wänaletá frasi na ngàmia kuwapangisha maʿabiria. na hao mabichboi wa Aden khaṭari sana, haifai kusikia maneno yao, maʿana watu wabaya na wevi, wanaḍuru watu. wakipata mtu faragha — pekeyake, naye mgeni, humpiga humnyanganya feḍḍa yake. ndio maʿana haifai kwenda mbali pekeyake.

wengine wa maʿabiria walikwenda nà magari kutembea Tawaḥi na Aden, wengine walichukua ngamia amma punda na frasi. wengine walikwenda hoteli na miqahawani, ná wengine katika maduka kununua pembe, na ngozi, na vitambaa vya ḥariri, na manyoa ya mbuni.

nao wanaopangisha watu frasi na gari hawana qawaʿida, hupangisha kama watu wanaofanya biʿashara. ʿaqili yao huwacha mtu akapánda, ḥatta waqati wa mwisho wanamwambia beʿi. na beʿi yao hushika ghali sana. iwapo mtu mwenyi ʿaqili, haqubali kutoa beʿi anayoitaka. akiuliza rupia nne — mpe rupia u nuṣṣu, akitaka asitake, mwachie ende zake.

ukiingia katika mji wa Aden, utaona nyumba za mäwe tu, za mawe meusi. na kulla paḥali unäpokwenda hukutà mqahawa, lakini michafu sana miqahawa ya Aden. na watu wenyewe wachafu sana. ḥatta midele, wanayopikia qahawa na vikombe, wanavyonywea, vi-

---

1) engl. have a dive. — 2) tauchen.

chafu sana. na kule Aden hapana maji ya mto wala maji ya arḍi. maji yao maji ya mvua, amma maji yanayotoka barrani. huletwa katika viriba, hupakia katika ngamiä na punda na frasi, huuza bilauri ya maji pesa. na ukinunua mtungi wa maji ya kogea hutoa rupia.

napo pana inchinia [1], inayopika maji ya chumvi kuyazima maji ya chumvi yawe ya bäridi. na watu wanayotumia maji hayo ni ʿaskari wa Wengereza.

nao watu wa Aden wamechimba chini ya jabali, wamefänya shimo kubwa sana, wakajenga kwa udongo wa Ulaya, ili ikinya mvuä yaingie maji. namo huingia maji mengi sana, lakini Aden hupita mwaka àmma miaka miwili isinye mvua, na ikinya — hunya siku chache tu.

ḥari sana kule Aden. sijaona paḥali penyi jasho kama Aden. na katika inchi hiyo mtu hawezi kuona áṣili ya jani bichi amma mti, hakioti kitu, kumekauka kama jiwe.

na Adeni vyakula vya hapo záyidi nyama ya kondoo na ya ngämia. nyama ya n̄gombe hawali sana, labda Wazungu na Wasomali wanakula, lakini hawa Waʿarabu wa Aden hawali. na vyakula vyote vya Aden vinatoka katika barra ya Yaman. mpunga na mchele unatoka barra hindi, na matunda hutoka Miṣri [2]) na Ulaya. lakini áṣili ya chakula, wanachopanda wenyewe, illa chakula cha hapo — samaki.

kule Aden pana ziyāra [3]) za mawalii [4]), mmoja jina lake ʿEidarusi. na ṣifa yake ʿEidarusi sākin el-Aden. naye alionyesha ʿàjabu nyingi za walii. na kulla mwaka huenda wakizuru ziyara yake na kuweka náḍiri. nayo

1) engl. engine. — 2) Egypten. — 3) Wallfahrtsort. — 4) Heiliger.

ziyara ina karama sana. na ya pili ziyara ya Shekh ʻOthmani. nayo vilevile ina karama. nayo tenna kulla mwaka hufanziwa desturi yake kuizuru kwa machezo na karama, huwa kama siku kuu, ikiwa ziyara. na ziyara hizo, ikipita mwaka, nao hawakufanza qawaʻida ya ziyara, wanasema huḍuru watu, huonyesha ʻajabu.

na kitu kinachotoka Aden, kinachopelekwa katika inchi nyingine kufanza biʻashara ni buni na ubani. na buni, inayotoka Aden, ni buni ghali kuliko buni ya dunya yote. nayo hupendwa sana. na paḥali panapolimwa huitwa Mokha. áṣili ya Mokha ulikuwa mji mkubwa zamani katika inchi ya Yaman, lakini sasa umekufa, umekuwa ghurabu. hapana mtu ḥatta mmoja sasa, lakini majumba ya mawe yako.

na wenyewe watu wa Aden hawanywi qahawa ṣafi. qahawa wanayokunywa maganda ya buni. nao wanasema ʻafya kuliko buni yenyewe.

meli ikiondoka Aden kwenda Suezi mwendo wa siku nne. tulipoondoka bandarini, tukatokea nje, tukaona visiwa vingi viko baḥarini. na kutoka bandarini ḥatta kwisha visiwa hivo huchukua saʻa arbaʻ u ʻesherīn. na hapo ndipo penyi khaṭari ya ḥari, huḍuru watu. watu hufa kwa jasho, khaṣṣa Wazungu hawastaḥamili kabisa. meli ikiondoka Aden amma Suezi, ikipita katika baḥari hiyo, hutia Waʻarabu amma watu wengine wa barra hiyo kutia moto kule katika inchini [1]), kwani Wazungu hawastaḥamili kule chini. na miye, nimeona' marra tatu katika safari tatu wamekufa watu. baḥari hiyo inakwitwa baḥari nyekundu kwa kisuaḥeli, amma baḥari akhmar kwa kiʻarabu, ao baḥari ya Musa. mtu huona kama mawingu ya mvua, lakini ile ni ḥari pia, inayotoka

---

1) engl. engine.

katika maji, yalivoshika moto kwa juu. na maji hayatulizani kabisa, na tenna hapana upepo.

na mkiwacha visiwa vile vya Farsan, moto hupungua kidogo. na mtu akiqurubia Suezi, huona barra zote mbili, barra ya Afrika na barra ya Sham. hapo baḥari inakwitwa juto la Suezi. na hapo katika upande huu pana kilima huitwa Seina, ndipo alipokuja nabbi ʿIsa, akaomba duʿa yake, akapiga fimbo baḥarini, maji yakakauka, akapita kwenda barra ya Sham. na hao makháṣimu wake, watu wa Firaun, waliomfuatia nyuma, kutaka kumpiga, walipoingia kufuata njia yake ya baḥarini, wakafika kattikatti — na yeye amekwisha vukia barra ya Sham — maji yalichanganyika, yakawazamisha. hapo pameelekea sawasawa na Miṣri.

tulipondoka hapo, saʿa thenáʿshara tukafika Suezi, lakini meli haikusimama sana. na mashua za hapo, zinazopandia meli, mashua za matanga na sitima [1]), lakini hapana mashua ndogo. hapo ndipo watu huchukua taa ya sim [2]) na rubani, anayepeleka meli mtoni. tulipotoka bandari ya Suezi, haikupata daqiqa sitta, tukaingia katika juto lililochimbwa. mto huo, waliouchimba Wafranza, zamani hapakuwa mto, ilikuwa inchi kavu. na meli zilipokuwa zikitoka Ulaya zamani, zikenda barra Hindi na barra Afrika na barra ʿArab — lázima kuzunguka Capetown kulla paḥali zinapotoka. lakini alipata mtu mmoja ḥékima kuchimba ule mto, achanganye hizi baḥari mbili, baḥari ya Ulaya na hii baḥari ya Musa, maʿana si mbali. kutoka Suezi ḥatta kufika Port Said qádiri ya mwendo wa siku tatu u nuṣṣ kwa miguu, na kwenda katika meli saʿa arbaʿ u ʿesherīn, kwani meli haiwezi kwenda upesi, kwa ájili mto mwembamba. lázima, ikija meli, inayotokea mbẹle, bassi zi-

1) engl. steamer. — 2) Scheinwerfer.

kikutana, lázima moja ifungiwe kando na moja ipite, ndipo ifunguliwe.

kulla chombo, kinachopita mto wa Suezi, hupimwa ukubwa wake na shehena yake, hutiwa beʿi, hutozwa ʿushuru. na ʿushuru huu ghali sana. katika hizi meli kubwa za sasa, ikipita marra moja, hulipa qádiri ya mark khamsīn elf na záyidi qádiri ya shehena yake. wenyi mto huo wanapata mali sana, kwani zinapita meli nyingi na manowari nyingi, sababu sasa njia imekuwa qaribu ya barra zote kuliko zamani.

na mkifika katika mto, marra nyingi hufuata watoto wadogo na wazee, hufuata meli, wakiomba vyakula na mapesa. kulla upande huweza kuwatupia vitu. na mtu akiwa mbali, huṯhanni meli iko katika inchi kavu. na mtu akilala katika chumba chake cha meli, huṯhanni vilevile yumo katika inchi kavu. mto huo unagawa sasa barra ya Afrika na barra ya Sham, lakini zamani ilikuwa mpaka mmoja, watu wakenda kwa miguu.

kattikatti ya mto iko baḥari ndogo. na zamani ni ziwa la maji, huitwa Bittersee. hapo meli hupata kwenda upesi na rukhṣa kupishana meli. upande wa Miṣri pana mji, unakwitwa Ismailia, zamani alijenga Ismaili Pasha. ni mji wa kubadili hawa, nao ni mji mzuri na bustani zake nzuri sana.

tukiondoka hapo, tukaingia vilevile katika mto mwembamba ḥatta tukafika Port Said. mtu akiingia katika Port Said, huwa gházia sana na vumbi la makaa, maʿana lázima kulla meli, inayokuja hapo, hupakia makaa. waanawake na waanaume wa hapa huchukua makaa. na watu wanaofanya kazi Wanubi na Sudani, nao hodari sana kwa kulla kazi, hufanya upesi sana.

nazo huja mashua nyingi kuchukua maʿabiria na kuuza vitu — nguo, na vitu vitamu, na picha [1]) mbaya

1) engl. picture.

za ʿaibu, na machungwa, na mapera, na kofia nyekundu, na kulla aina ya matunda huleta, na vitu vingine vingi. na watu wa hapa wevi sana. mtu hujiḥáḍari sana katika meli, huibia mtu feḍḍa na saʿa, kulla kitu cha mali hutaka kuchukua.

na mtu akishuka pwani, vilevile hupigania watu katika mashua. pana vilevile mabichboi wa kupeleka watu na kuwaonyesha mji na maduka. lakini khaṭari sana, haifai kuwafuata popote.

tulipoondoka Port Said, tukaingia katika baḥari, inayokwitwa baḥari ya kattikatti, maʿana inayokwitwa kattikatti — imekaa katti ya barra ya Ulaya na barra ya Afrika na barra ya Sham. baḥari hiyo ina ghoba nyingi na nzuri. nayo ina mawimbi sana, na rangi yake kana rangi ya nili.

siku ya pili tulipoondoka, tukaona kisiwa kimoja kikubwa, kinachokwitwa Kreta. na siku ya tatu tukaona inchi ya Italien na kilima kimoja kikubwa, kinachoitwa Aetna, kilima cha moto, unaotoka katika arḍi. kilima hicho kiko katika kisiwa cha Sizilien. zamani kisiwa hicho, watu wanasema, kilikuwa pamoja na barra Italien. na sasa kimekatika, kimo mbali, meli inapita kattikatti. milango hiyo khaṭari, kwani pembamba sana, pana fungu, na maji yanavuta sana. na zamani merkebu za matanga, wanasema zimezama nyingi sana hapa kwa maji yalivo mabaya, kwani maji yake yanavuruka kama mtu anavuruka uji. na mji unauona hapo ni Messina. mtu akipita usiku, hupendeza sana taa zake. n̄gambo ya pili huitwa Reggio.

tulipoacha kisiwa cha Sizilien, mwendo wa saʿa themintaʿshara tukafika Neapoli. na hapo Neapoli bendari kubwa ya Italien, nao ndio mji wa ʿezi. iwapo mtu akiqurubia Neapoli, huona visiwa vidogovidogo baḥarini. na katika visiwa hivo pana kimoja kidogo sana,

ndio maʿarufu, na jina lake Capri. watu wengi huenda wakitazama kisiwa hicho, sababu pana pango. na pango hilo inaweza kupita mashua kwenda upande wa pili. nalo hutisha. huitwa pango nili, sababu maji ya hapo kama nili, na pango lenyewe nuru lake kama nili sababu ya maji yake.

qaribu ya Neapoli, saʿa mbili kwenda pale, kiko kilima cha moto, kinachokwitwa Vesuv. na moto huo umetokea katika arḍi yapata miaka themintaʿshara mia u ʿasherīn, kama watu walinambia, na ḥatta sasa kulla siku unawaka. nao umezamisha miji miwili, iliyokuwa hapo qaribu ya kilima hicho, miji hiyo inakwitwa Pompei na Herkulanum. na sasa sulṭani wa Italien anafanza kazi kuichimbua miji hiyo, ili kutafuta buṣara ya jissi ya moto unavoḥaribu mji. nao wamekwisha pata vitu vingi katika miji hiyo waliyoichimbua. ʿajabu katika watu, waliokuwa katika miji hiyo, wanaochimbuliwa sasa — mtu akiwaona — huwakuta vilevile walivokaa kitako zamani siku, ilivoshuka huo moto, unaokwitwa zaha kwa kiangazija.

tulipoingia bandarini, akaja robani kutīa meli ndani. mtu akiingia ndani ya bandari, hupendeza sana mji, kwani mji huo uko katika ghoba, umezungusha bandari kama boma, na tenna uko kilimani. na mtu akitazama yale majumba yalivo mengi na makubwa na meupe — hupendeza mno. na mawingu ya hapo hupendeza mno katika namna yake, na usiku, taa zinapowashwa, vilevile hupendeza mno.

tulipotia nanga, zimekuja mashua nyingi sana. nyingine huleta maʿabiria, nyingine walipakia watu wenyi matarumbeta na vinanda na matari. watoto wadogo na waanawake na waanaume huja wakipiga vinanda na kucheza na kwimba na kukinga miavuli kuombea mapesa. na wengine walileta matunda, na mboga,

na picha, na fimbo, na sa'a, na miavuli, na nguo, na lozi, kulla aina ya matunda, na kulla aina ya kitu kinachouzwa. watu hao vilevile wabaya — huiba. nao wanajua kuḍiḥaki watu kuwanyanganya.

ba'ada ya kutazama machezo yale, tukashuka mjini kwenda hoteli. na mtu akisha fika pwani, vitu hufunguliwa kutoza 'ushuru. na khaṣṣa kitu, wanachotafuta — tumbako, ndio khaṭari, na kitu kipya vilevile. na mtu hukuta wachukuzi wengi hapa, na mabichboi hupigania mizigo, kama mtu hakutazama sana huibiwa vitu vyake.

tukakaa siku moja katika hoteli, nikenda kutazama mji. na katika mji wake si naḍifu sana — mchafu, na wenyewe wachafu. nao hupita, wakitembeza vitu, kama kule kwetu Unguja. vyakula vyao mno tambi zinazokwitwa makaroni. nao husimama njiani wakichukua mikononi wakila. na hapa pana ḥari sana waqati wa jasho kama kule barra yetu. nayo ndiyo inchi inayofaa kupanda matunda ya kwetu.

tulipoondoka Neapoli, tukaingia katika gari la moshi, tukenda Rom — Mailand — Luzern — München ḥatta tukafika Berlin. tukakaa siku mbili u nuṣṣ katika gari la moshi. na mtu akisha shuka katika gari la moshi, hujiona khafifu sana, kama mtu aliyovunjika mafupa.

# Safari yangu ya Udoe ḥatta Uzigua

## na khabari za Wadoe na mila yao

inatoka kwa

**Mtoro bin Mwenyi Bakari.**

bismillahi er-raḥmani er-raḥim!

hiki qiṣṣa cha safari yangu zamani nilipokwenda Udoe na Uzigua. siku moja nimefikiri moyo wangu, mimi kijana mzima sasa, wala sijui safari iliyo yote. bassi marra nalikwenda kwa Muhindi kubadili biḍaʿa pekeyangu, hapana mtu ḥatta mmoja aliyejua. nilipokwisha kubadili biḍaʿa, kwa siku ya nne nikampa khabari mama yangu, nikamwambia: „mimi nataka kusafiri". akaniuliza: „unakwenda wapi?" nikamjibu — ya kama: „nakwenda Zigua kutembea na kufanya biʿashara kidogo". mama yangu akaniuliza: „utakwenda na nani Uzigua, na wewe mgeni katika barra?" nikamjibu: „nakwenda mimi pekeyangu, wa pili muungu, atakáyenisaʿidia kulla maafa katika njia". akanambia: „nenda", lakini moyo wake hauna furaḥa.

bassi tulipokwisha kuagana mimi na mama yangu, ikawa kutafuta wapagazi wa kidoe na kizigua ḥatta nikawapata. tukapatana mimi nao ḥatta tukaelekezana. tulipokwisha kupatana, tukaondoka, tukenda ḥatta

tukafika shamba, jina lake Nsole, tukapumzika katika shamba la Mwinyi Maulidi. akaja Mwinyi Maulidi, akaniuliza: „Mtoro, unakwenda wapi na biḍa'a?" nikamjibu: „nakwenda kutembea Uzigua". akanambia: „salama inshaallah!" bassi marra Mwinyi Maulidi akamwita kitwana chake, akamwambia: „nenda ukamwangulie madafu bana wako, aje anywe maji". na yeye mwenyewe akenda akakata miwa mitatu mikubwa sana, akawapa wale wapagazi wangu wakatafune. na yule kijana akashuka juu ya mnazi, akatafuta kifuo, akafua madafu, akaniletea nikanywa. khalafu Mwinyi Maulidi akanambia: „tafaḍḍali nataka ushinde hapa pangu". nikamjibu: „ashanta maneno yako, walakin siku ya leo nataka unisámehe, ma'ana nataka nikalale Dunda leo". bassi wapagazi walipokwisha kutafuna miwa na mingine wakachukua, na mimi nilipokwisha kunywa madafu, marra nikataka rukhṣa kwa Mwinyi Maulidi, akanishindikiza ḥatta mwisho wa mashamba ya Nsole, khalafu akarudi, nasi tukenda zetu.

tukenda ḥatta tulipofika qaribu ya Mkwaju wa Mvuani, tukaona embe zimezaa sana. wale wapagazi, walivoona embe, roḥo zao hawakuweza kujizuia, wakanambia: „hapa tutue, tupumzike". na mimi nikawajibu: „vema"; wakatua mizigo. walipokwisha kutua, marra nikawaona wanapanda juu ya miembe, wakatingisha embe. na nyingine wanakula juu ya mti kama mfano wa popo. kisha wakashuka juu ya miembe, wakakusanya embe zao, wakatia katika vikanda.

khalafu tukaondoka tukenda zetu ḥatta tukafika mto wa Chatota qaribu ya Dunda. tukakutana na pazi, anatoka shambani kwake, nikamwamkia, akaniuliza: „unakwenda wapi na biḍa'a?" nami nikamjibu: „nakwenda Zigua kutembea". bassi akanambia: „twende nyumbani kwangu, ukapumzike kidogo". tukenda mimi

naye na wapagazi wangu ḥatta tukafika kwake. akamwita suria yake, jina lake Vumilia: „nenda katika shamba la muhindi, ukamvunjie mahindi Mtoro". bassi na yule suria yake akenda akavunja mahindi, akaja akachoma, tukatafuna mimi na wapagazi wangu. ḥatta tulipokwisha, nikamwaga, nikamwambia: mwenemzi [1]), sasa nataka kwenda Dunda, sababu nimechoka sana". akanambia: „vema, walakin lini safari yako?" nikamjibu: „kesho aṣ-ṣubuḥi". akanambia: „na mimi kesho ntakuja huko kwa ndugu yako". tuzidi kuagana.

tukaondoka, tukenda ḥatta Dunda. tulipowáṣili, wapagazi wakatia ndani mizigo. nami nikaingia ndani, nikamwamkia mke wa ndugu yangu, ma'ana ndugu yangu alikuwa hayupo barazani, amekwenda kutembea. marra akapata khabari, ya kama nimekuja, naye marra akarudi nyumbani. tukaamkiana na kupeana khabari kama niliyo nayo.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi akaja pazi, tukamwamkia, akaniuliza: „utasafiri min gheri ya kwenda katika maqaburi ya wazee wako?" Abdallah, ndugu yangu, akasema: „kweli pazi maneno yako". marra tukaondoka, tukenda maqaburini tukazuru. tulipokwisha tukaja nyumbani, wakanihimizia chakula nikala. nilipokwisha wakanambia: „mbona unakwenda pekeyako Uzigua? nawe mgeni, hujasafiri!" nikamjibu: „ntafanyaje? nataka kufanya safari moja ya barra". wakasema: „haifai". wakanipa mtu moja kufuatana naye. na ndugu yangu mdogo Slemani akasema: „nami ntampeleka ḥatta Zigua".

bassi nikawaaga, tukaondoka tukaenda ḥatta tukafika Sanganzeru mbele ya Dunda. nikaonana na Mkwelengala, mkubwa wa Sanganzeru, naye akataka kuni-

1) mwenye mji.

chukua kwake. nikamwambia: „sipati kwenda kwako, kunraḍi sana, sababu wingu la mvua linakuja, nami nataka kwenda kulala Usako“. bassi tukenda zetu mudda wa sa'a moja ikanya mvua kubwa sana, ikawa nimeużika sana, nikajuta kusafiri kwa ta'abu ya tope katika njia na mashimo yamejaa maji. nikaona 'ażabu kubwa sana, wala hapana paḥali pa kupumzika. bassi tukenda — marra nimeingia katika shimo la maji, marra nimeteleza kwa tope zilivo nyingi — ḥatta tukawáṣili Usako imekuwa usiku auwali ya 'isha. nimechoka sana, sina nguvu.

tulipofika Usako, marra nikamwona Mwinyi Sheḥe, ndugu yake pazi. tukaulizana khabari yeye na mimi. akaamru mkewe kufanyiza chakula upesi. marra akaja ndugu yake, pazi Tandukizi jina lake. nikamwamkia, na khalafu tukazungumza, akanambia: „unakwenda wapi?“ nikamwambia: „nakwenda Uzigua kufanya bi'ashara kidogo“. akanambia: „utaiweza pekeyako bi'ashara ya Uzigua?“ nikamjibu: „sababu nini?“ akasema: „mbuzi wao ao ñgombe wanauza ghali sana, na wewe mgeni“. nikasema: „haiḍuru, ntatazama, nikaona mna makhlaṣa katika bia'shara — ntanunua, na kama hamna — ntawacha“. bassi marra akaja kijakazi, akasema: „chakula kimekwisha“. Mwinyi Sheḥe akajibu: „mwambie apakue“. kikapakuliwa chakula, akaleta kijakazi, tukala pazi na Mwinyi Sheḥe na mimi. tulipokwisha kula, pazi alitaka kuweka maongezi. nikamjibu: „nisámehe mvele wangu, nataka kulala, sababu nimechoka sana kwa mvua na matope“. tukaagana mimi naye na kupeana buriani.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi na mapema tukaondoka, tukaingia katika pori la Mwidu. pori hilo ḍa'ifu sana, simba hutembea usiku na mchana. siku chache qabla ya kupita sisi katika safari, mwenyi safari amefuatana na

kirongozi wake, akatokea simba njiani, akamkamata mwenyi safari, alikuwa juu ya punda, hakupata kumshika sana, lakini alianguka chini. marra simba akamrukia kirongozi, akenda naye. mwenyi safari alipoondoka, akatazama mbele yake, kirongozi wake hayupo — simba amemchukua, sababu safari yalikuwa nyuma, na wao walikuwa mbele pekeyao, na simba amekuja kama mfano wa radi.

ḥatta tulipotoka katika pori la Mwidu, tukaingia Shakini, tukenda kwa Mdoe mmoja, jina lake Mtengwa Kidedede. tukapumzika, sababu jua lalikuwa kali sana, na kiu imetushika.

na katika inchi ya Wadoe na khabari zao na dasturi zao nitawaelezea mambo yote baʿada ya kwisha safari yangu.

ḥatta siku moja tukaondoka, tukenda kulala Wame kwa Mzigua mmoja, mji wake mbaya sana. kuna taka nyingi na mavi ya n̄gombe mengi sana na vidudu katika kitanda — mtu hawezi kulala. bassi tukalala, nami moyo wangu unawaza usiku na uche hima, tuondoke katika mji huo.

bassi usiku ulipokucha, tukaondoka, tukenda kuvuka mto wa Wame. na mto huo mbaya sana, una mamba wengi na viboko. na mtumbwi wao mdogo sana. lakini tukavuka salama ḥatta n̄gambo ya pili.

kama safari kubwa inataka kuvuka hapa, kwanza hupiga bunduqi katika maji kufukuza mamba katika maji, ʿaskari na wapagazi wapate kuvuka kwa miguu, sababu mitumbwi haba.

na kule n̄gambo tukaona Wazigua, wamejifunga vita, wanataka kwenda kupigana wenyewe kwa wenyewe. nikamwauliza Mzigua moja: „wanagombea nini?“ akanambia: „wanagombea mipaka ya inchi, huyu anasema »upande huu wangu«, na mwingine anasema »upande huu wangu«, ndio sababu yao“.

nikenda zangu ḥatta nikafika katika mji wa yule jumbe Kingaru. mji wake mzuri sana, ana mbuzi wengi sana na n̄gombe. akaniqaribisha, akanipa kiti, nikakaa kitako, akaniuliza: „wewe kijana wa wapi?“ nikamjibu: „kwetu Bagamoyo“. akasema: „wazee wako wote wazima?“ nikamwambia: „baba yangu amekufa“. bassi akamwita mke wake akamwambia: „fanyiza chakula hima“. tenna tukazungumza mimi naye, wakaja Wazigua wengi sana kunitazama, moyo wangu ukafanya khofu kidogo. marra chakula kimekwisha tukala. akaniuliza: „umekuja kufanyiza nini huku Zigua?“ nikamwambia: „mimi mgeni katika barra, nasikia kwa watu killa siku Zigua nzuri sana, bassi moyo wangu umeṭam'ani kuja kuiona Zigua“. akaniuliza: „hii biḍa'a unataka kununua nini?“ nikamwambia — kama: „kinachofa'a pwani nitanunua tangu mbuzi ḥatta n̄gombe, tangu n̄gombe ḥatta mpira“. akasema: „vema, kwanza nakutaka usare — wewe uwe ndugu yangu, sababu mimi sina ndugu“. nikamjibu: „vema“.

akamwamru mtumwa wake kwenda kuleta mbuzi. akaja mbuzi akachinshwa, likatolewa ini. akaja mdumilizi na kinoo na wembe, akaniweka juu ya kichwa na huku anasema: „wewe mungwana, umetoka pwani, Kingaru amekutaka urafiqi. nawe umekuja na biḍa'a. Kingaru akatwae doti moja ao mke wa Kingaru akatwae doti moja, na weye ukaqaṣirika, ukenda pwani kumshitaki, kwa sababu ya doti yako, Kingaru akafungwa na sirkali — weye ufe. ao umeona 'adui ya Kingaru, anamteta Kingaru, na weye ukamsa'idia 'adwi, ukasema „kweli Kingaru mbaya“ — ufe. ao umemwona Kingaru ao ndugu ya Kingaru katika mji wako na weye usimtazame kwa chakula ao kwa maji — ufe weye na wa kwenu“. ba'ada ya maneno hayo, aliyonambia mimi, na Kingaru huambiwa kama haya. ba'ada

ya kudumiliza akachanja uchale, akatwaa ini la nyama, akachanganya kidogo cha damu yetu, akatupa, tukala kipande Kingaru na kipande mimi. tulipokwisha, akaja mkewe, nikampa jora ya kaniki na kitambi na ushanga. na yeye nikampa kanzu na kofia, akawa rafiqi yangu sana.

khalafu nikamwambia: „sasa nataka kufanyiza bi'ashara". akanambia: „kunako mbuzi wazuri na ñgombe wazuri mbali sana, wewe huna ḥaja na kwenda, kaa hapa, walakini toa mtu wako mmoja, na mimi ntatoa mtu wangu, tuwapeleke kunako mbuzi wazuri, wakanunue". nikamjibu: „vizuri sana". ḥatta aṣ-ṣubuḥi wakaondoka, wakenda na wale wapagazi wangu kununua mbuzi na ñgombe. wakashinda kule walikokwenda. ḥatta siku ya pili wakarudi na mbuzi na ñgombe wazuri, nikafuraḥi sana.

ba'ada ya siku sitta nikamwaga, akanambia: „nataka nikupe watumwa wangu na mbuzi wangu na ñgombe wangu, uende nao Bagamoyo ukauze, sababu hawa watumwa wajinga". nikamwambia: „vema".

nikaondoka mimi na wapagazi wangu, tukenda ḥatta tukafika Wame. jua limekuchwa, na mtumbwi hapana. mashauri yakatupotea. na paḥali hapo ni njia ya simba, na katika mto mamba anakamata samaki. khalafu nikawambia: „hapana mashauri illa tujitose — mwokozi muungu". wapagazi wakasema: „ndio mashauri yako, walakini mamba anakamata samaki". nikawambia: „yuko mbali kidogo". wakasema: „haya". bassi nikasema: „ēwe rabbi tunuṣuru watumwa wako kwa siku ya leo". tukajitosa na maji yanavuta sana. muungu akatuvua, na yule mamba asituone ḥatta tukavuka ote salama.

tulipofika ñgambo ya pili, tukapanga nyumba kwa Mdoe mmoja, jina lake Luaga. na paḥali hapo pana baridi nyingi sana. wale wapagazi wakahimiza chakula

tukalala. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukenda mchana kutwa, ḥatta mshuko wa al-ʿaṣiri tukafika Usako kwa pazi Pandukizi. akaja pazi na ndugu yake tukaamkiana. akaamru tenna mke wake kufanyiza chakula. ḥatta tulipokwisha, akaniuliza: „safari yako nzuri?“ nikamjibu: „al-ḥamdu lillahi“. bassi akanambia khabari, iliyopita Usako, ya kama mama yake amekufa. nikawapa mkono wa taʿazia.

ḥatta usiku tukalala, aṣ-ṣubuḥi nikamwaga pazi na Mwinyi Sheḥe, tukaingia katika nyika ya Usako kwenda Mwidu. na hiyo njia tuliyoipita yalikuwa ya zamani — yalikufa. tukaifuata tukakuta siafu wengi, wote wamechanganyika — wanapigana vita. na vita vyao ʿajabu kubwa. áṣili yake mdudu mmoja katika wale siafu aliuawa na wenziwe, tenna wale siafu wakafanya vita, lakini kwanza walikwenda siafu watatu kuuliza khabari. walipofika wale siafu, nao wakauawa, tenna wale wengine wakajua, ya kama kuna vita kweli. nao wakaondoka wakenda katika vile vita wakapigana. na kupigana kwao hawapigani wote, wengine wanapigana, wengine wanachukua walio na madonda, na wengine huwachukua wale waliokufa, hawaqubali kuwawacha. na mapigano yao huumana na meno juu ya kichwa ḥatta afe. akisha akenda kwa mwingine. nao waqaidi sana, hawa wakifa — wanakuja wengine, na nyuma hawarudi, wajapokwisha wote. każálika wale wanaowapata katika vita wenyi madonda huwapeleka katika mashimo yao, wakawaweka, wanaopona watapona na watakáokufa watakufa.

każálika vita vya sangarà. hawataki kuona moto katika njia. wakiuona moto, watajikusanya wote sangara, wakauzime moto. na kuuzima kwao huuzima na mate. nao watakufa wengi. hawa wanakwenda na hawa wanarudi, na wengine wanachukua jamaʿa zao

aliyekamatwa na simba. kumpuni [1]) alitaka mtu kerani Mtoni kungojea safari zinazopita kutoka barra. amepatana na Mw'arabu mmoja, naye akaqirri akendá kukaa pale kivukoni. na paḥali hapo desturi yake killa mwaka waqti wa masika mamba hukamata mtu na simba kaẓálika, panakwitwa Kiyembayemba. siku hizi yule Mw'arabu amelala usiku, akasikia mlangoni kama mfano panapo mtu, akastuka katika usingizi, akenda pale mlangoni. alipoushika mlango — akakutana na simba. simba alipomwona Mw'arabu, alimpiga makucha ya kichwa. Mw'arabu akapiga makelele. simba áliposikia kelele yake, alimkamata kichwa alimtoa nje. na wale watu, waliokuwa ndani ya nyumba, wote roḥo zao zalikuwa na khofu. simba akamla yule Mw'arabu.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi wale watu wakapeleka khabari kwa kúmpun. kúmpun alipopata khabari, ya kama mtu wao ameliwa, akenda nyumba ya serkali kupeleka khabari. serkali aliposikia maneno ya kúmpun, alimwamru bana wa 'askari kupeleka mtego Mtoni na mbuzi mmoja. akatega mudda wa siku mbili, siku ya tatu akanasa yule simba. wakaja watu kuleta khabari, ya kama simba amenasa, akaondoka bwana wa 'askari pamoja na 'askari, wakenda ḥatta panapo mtego. walipofika kutaka kumqaribia, simba akanguruma kwa ukali, hawakuweza kufika panapo mtego. akaamru kumpiga. riṣaṣi wakamleta mjini, wakamtembeza mji mzima, watu wote wakamwona. wakatega marra ya pili mtego, akanasa simba mwanamke. ḥatta siku ya saba' akanasa simba mwingine mwanamume, jumla yao walikuwa simba watatu wamenasá kwa siku saba'.

nimesikia khalafu khabari nyingine ya simba aliyenasa, lákini hawakumpiga. zamani moja katika mrima

1) Verstümmelt aus Kompagnie. Gemeint ist die Deutsch-Ostafrikanische Gesellschaft.

kule Lindi palikuwa na simba hukámata watu killa siku. wakamfanyia mtego kumtega. ḥatta siku moja akanasa. siku ileile palikuwa na mwanamke wa kizungu anapita kutembea. yule mwanamke alipomwona simba, roḥo yake ikaingiwa na oga sana, sababu hakumjua ya kama amenasa. mbele hakuweza kwenda, wala nyuma hakuweza kurudi. khalafu moyo wake ukarudi, fahamu zikamrejeʿa, akarejeʿa mbio mjini, akatoa khabari mjini, ya kama simba amenasa. yule mwenyi mtego aliposikia, akajifunga na bunduqi yake, akenda ḥatta alipo simba na Wazungu wengine naye pamoja. alipotaka kumpiga yule simba — riṣaṣi yake yalikuwa mbovu — mshindo haukutoka. simba alipoona mshindo wa bunduqi haukutoka, akamrukia akamkamata. wale wenziwe aliwofuatana naye, walipomwona mwenzao amekamatwa, na wao wakakimbia. katika mbio zao walizokwenda mmoja khofu ilimshika, akaanguka chini, naÿe alifuatana na boi wake, akamwangukia juu yake, moyo wake uliṯhanni ndio simba ananikamata sasa. marra akapiga kelele nyingi sana akaondoka akazidi kwenda mbio, fahamu hana, akenda kujitosa katika mto, na huo mto ulikuwa na khaṭari ya mamba, lakini amenuṣurika. na mwenyi mtego, aliyekamatwa na simba, alipiga makelele mengi sana, simba akaona uchungu — akamwacha. lakini amemtia kidonda mwanzo wa kifuani ḥatta miguuni.

nikashinda Dunda, ḥatta aṣ-ṣubuḥi nikenda mjini, walákin niliporudi nimepitia njia nyingine. nimepita njia ya Yombo. kwanza nalivuka Chatota, khalafu nikenda mto wa Mtakashari. nilipotoka mto wa Mtakashari, nikaingia mto wa Chasimba. khalafu nikenda zangu, nikavuka mto wa Chombe, lakini ulikuwa umekauka hauna maji. lakini waqti wa masika mto huo huwa na mamba.

nilipotoka Chombe, nikaingia Vikukuni. mashamba

haya wanalima Wandengereko, lakini inchi wenyewe Wazaramu. nilipotoka Vikukuni, nikenda Matimbwa. na hayo mashamba ya Matimbwa mazuri sana, mabonde yake na inchi yake ruṭba sana. hustawi kulla mbegu — mtama, mpunga, mahindi, ḥatta miwa na ndizi, wa każālika minazi. na āṣili ya mashamba hayo wenyewe Wazaramu, qabila yao Wanzerekera na Wavyuma na Wapandeni — ndio wenyewe. bassi tulipofika pale Matimbwa, nikenda kwa babu yangu, jina lake Mwenyi Makubi bin Chuma, naye ndiye mkubwa wa katika inchi hiyo. aliponiona, akanihimizia chakula, nikala. ḥatta waqti wa al-ʿaṣiri nikenda mashamba ya Nsole. nilipotoka Nsole, nikaingia Bako. nilipotoka Bako, nikenda Ugeni. na pale Ugeni pana shamba la Tshanzi Mdumi. nikenda nikaonana naye. akataka kuniangulia madafu, nikamwambia: „jua limekuchwa, sasa nataka kwenda mjini". bassi akanishindikiza ḥatta Boñgwa, khalafu akarudi.

nilipotoka Boñgwa, sikusimama illa nimewāṣili mjini Bagamoyo. nilipofika Bagamoyo, akaja mama yangu na ndugu yangu mwanamke na jamaʿa wengine wamekuja kunihongeza, maʿana — mtu akisafiri akirudi, huja watu kumhongeza, humpa mkono wakamwambia: „hongera"; naye hujibu: „al-ḥamdu lillah". marra nikafanyiziwa uji nikanywa, khalafu nikoga, nikavaa nguo nyingine, khalafu nikenda mskitini kuṣali, magharibi nikarudi nyumbani, nikalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi.

nikamwita dalali, akaja nyumbani, nikampa vile vitu, nilivyonunua Udoe na Uzigua. akapeleka sokoni, akauza jumla. nikampa mbuzi na ñgombe wa yule rafiqi yangu Kingaru. akauza jumla, akaniletea feḍḍa, nikawaqābiḍi wale watumwa wake. wakalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi wakenda zao. nikawambia: „salamu kwa bana —ᵃuu sana, nami, muungu akinijaʿali, ntakuja marra

nyingine kumtezama". wakasema: „vema". bassi tangu safari hiyo ḥatta sasa bado kwenda upande huo, simjui yule rafiqi yangu mzima ao amekufa.

---

## khabari za Wadoe.

### mwanzo wa maneno.

maneno haya yanayokuja ba'ada ya kuandika safari ya Udoe ni khabari za Wadoe na dasturi zao. nimezipata kidogo kwao, zamani niliposafiri, na nyingine nimezipata katika mji waqti wanapokuja na bi'ashara zao kuuza. mna wengi wanajua maneno ya kisuaḥeli, hao ndio nilivokuwa nikiwauliza dasturi zao. nami wakanambia, nikazikusanya katika kichwa, na sasa nataka kuziandika zote. na dasturi za bin Adam nyingi sana. mtu huzaliwa na wazee wake, katika udogo wake hushika dasturi za wazee wake. akikua nyingine huzishika, nyingine akaziwacha. na katika qabila za mrima na za barra mila yao mingi inafanana, na mingi inakuwa mbalimbali. nami sasa nitaandika mila ya Wadoe qadri nitakápojua.

### khabari za Wakamba na Wadoe na mapigano yao.

zamani za kwanza katika mirima katika inchi, inayokwitwa sasa Udoe, mlikuwa na watu huitwa Wakamba. walikuwa watu wabaya sana na jeuri nyingi sana. watu, waliokuwa katika mirima, mashauri ya kufanya yakawapotea. khalafu pakaondoka mtu, akenda Kutu, akamkuta pazi, akakaa katika mulki wake, akamwambia: „mwenemzi pazi, nimekuja kwako, nataka vita uende ukaipige pwani, na hiyo pwani inchi nzuri sana". pazi akamwuliza: „'alama yake nini inchi hiyo?" yule mtu akatoa chumvi, akampa pazi. pazi akaonja

chumvi, ikampendeza sana, sababu yeye haijui chumvi. khalafu akamjibu: „vema, nimesikia maneno yako“. pazi akapeleka khabari kwa watu wake wote, wakakusanyika kwa pazi kusikiliza amri. bassi khabâri ya pazi ikawa killa siku anasema: „kesho tutakwenda pwani“; siku nyingi zikapita, wala asende.

na yule pazi ana ndugu yake mwanamke, jina lake Mlalukali. alivomwona ndugu yake Lukali[1]), killa siku amekaa tu, wala hana hamu ya vita, akaqaṣirika sana, akamwambia: „sababu nini amekuja mtu kutoka pwani, amekualika vita, na wewe sultani na hamu ya vita huna? kama wewe unaogopa, mimi ntakwenda pwani nikapigane“. Lukali aliyosikia maneno ya ndugu yake, ghaḍabu zikamshika. pazi akapeleka khabari tenna kule Usukuma, akawaita Wavira na Wanyamwendo, waje wafuatane pamoja kwenda pwani. marra akafunga safari ya vita. wakazidi watu kukutanika, wakawa wengi sana. vikatoka vita. ḥatta walipofika kattikatti ya njia, wakakuta jeshi myingine ya vita. pazi akata'ajjabu sana — ya kama: „nani yule mwenyi watu wengi kama mimi?“ akashinda pale pazi, safari haikwenda, akatuma mtu kwenda kuiuliza ile jeshi, inatoka wapi inakwenda wapi. marra mjumbe akarudi, akamjibu pazi — ya kama: „ile jeshi ya Tshanzira[2]) haina pahali ma'alumu pa kwenda illá wanatembea bassi“. pazi akafanya urafiqi na Tshanzira. ba'ada walipokwisha urafiqi wao pazi na Tshanzira ikawa safari moja kwenda pwani.

### khabari ya yule mwanamke Mlalukali.

siku moja tumbo limemshika sana, akaugua siku tatu, ḥatta ya nne akafa. Wadoe[3]) wakapata khabari, ya

1) Der frühere Name des pazi. — 2) cha nzira = cha njia. — 3) Nach Vertreibung der Wakamba wurden die an der Küste niederlassenden Wavira, Wanyamwendo, sowie ein Theil der

kama Mlalukali amekufa, wakaja wakamtaka kwenda kumzika. walipompata wakafanyiza mashauri ya kumla. khalafu wakamkatakata wakamla. ikawapendeza nyama ya mtu, ndio mwanzo wa kula watu Wadoe. khalafu wakaondoka, wakenda ḥatta wakawáṣili pwani. wakamkuta Mkamba katika mji amestareḥe.

maneno ya vita.

pazi alipowáṣili pwani, marra aliʿazimu vita kumpiga Mkamba. khabari ya Wadoe kupigana kwao na Mkamba: Mdoe, killa akimwua Mkamba, humkata nyama yake kama mfano nyama ya mbuzi, na khalafu huitia katika majungu, wakaipika, wakisha wanakula. każálika nyingine wanachoma wakala. vikawa vita vikubwa sana. Wakamba walipoona mambo ya Wadoe wanakula watu, roḥo zao zikaingia khofu, wakakimbia, wakauacha mrima. na pazi akapata inchi, na khabari ya Wakamba imekwisha.

majumbe, walio qaribu, walipomwona pazi hodari sana, ameweza kumpiga Mkamba, ḥatta akamwondosha, wakamwambia pazi: „sasa wewe mume, sisi waanawake". na maʿana hiyo wameiweka mila, tangu zamani hizo pazi haonani na jumbe. na katika baʿaḍi ya Winde na Saʿadani mwene haonani na mwekambi [1]). katika daraja hizo, tulizozitaja, pazi kuonana na jumbe, ao mwene kuonana na mwekambi, katika watu wawili — mmoja wapo — atakufa. dasturi hiyo ḥatta sasa katika mrima. na mwanzo wake ni hivo vita.

tureje'e tenna kwa pazi. baʿada alipopata inchi,

---

eigenen Leute Lukali's von den übrigen Küstenbewohnern Wadoe genannt und zwar weil in ihrer Unterhaltung fortwährend das Wort doe als Bejahung, Betheuerung etc. vorkommen soll.

1) Alle jumben von Gama bis Uvinje heissen jumbe mwekambi oder diwani mwekambi z. B. jumbe mwekambi Ismail, Bana Kheri bin mwekambi Jumaʿ. Der jumbe mwekambi steht seinem Range nach über den jumben z. B. von Bagamoyo, er steht direct unter dem mwene, hat also denselben Rang wie der shaha bei den Suaheli.

pazi akawambia majumbe: „mimi mtu wa barra, siwezi kukaa pwani, nami nataka kwenda zangu, hapana vita tenna, mna mashauri gani?“ majumbe wakasema: „sisi hatuna mashauri, kama utakálosema wewe — kwetu sisi bassi“. pazi akawambia: „inchi nnawapa mkae, walakini mjue sana, ya kama mimi ndio mwenyewe. wa każálika killa mwaka mnipe kanda langu la inchi, maʿana ʿushuru“. majumbe wakauliza: „nini kanda lako unalotaka? twambie tujue“. pazi akaweka dasturi: kulla mwaka kuja katika mji kutwaa biḍaʿa. naye aliwaonyesha mvinje [1]), akawambia: „killa mwaka mweke biḍaʿa na visua mwanzo wa chini ya mvinje ḥatta juu, hilo ndilo kanda langu“. wakaqubali majumbe.

bassi pazi akenda zake Kutu, walakini zamani anapokuja katika mji kutaka kanda lake, huwa kishindo kikubwa kama mfano wa vita. Waʿarabu na Wahindi na Wasuaḥeli wote hufunga milango na maduka, wala watu hawatembei sana siku hiyo, maʿana huja na watu wengi sana, bassi kama kitu watakáchokiona — watachukua, wajapomwona mtoto wa Mwʿarabu — humchukua. bassi khalafu majumbe humqaribisha pazi, wakatafuta biḍaʿa, iliyo nzuri, wakaipanga katika mvinje, na khalafu humpa pazi akenda zake.

na dasturi hiyo imekaa siku nyingi katika mrima, ya majumbe kumpa pazi kanda lake, walakini khalafu majumbe waliondoka wakaenda kwa Seyyid Barghash wakamwambia: „Seyyid, tunataka neno hili utuondolee kwa mapazi“ [2]). khalafu Seyyid Barghash akaweta mapazi wote, akawambia: „sasa hakuna kutaka kanda la inchi kwa majumbe, illa kaeni ndugu moja“. na mapazi wasimrudi jawabu Seyyid Barghash, wakasema: „vema, tumesikia“. ikesha khabari ya kanda.

---

1) Baum. — 2) Die übrigen pazi im Küstengebiete hatten es unterdessen dem pazi aus Kutu nachgemacht.

khabari ya Wadoe na Wazaramu.

ba'ada ya kupata ile inchi ya mrima, wakagawana pazi upande wake Zaramu yote na Mdoe upande wake ba'ada ya kuvuka mto wa Ruvu mkuranga wote — mwenyewe mwene. ḥokumu ya Winde ḥatta Shakini na Kwere — mwenyewe mwene, hupatana na majumbe wa Winde Makame ya Shani[1]) na Mwekambi[2]). na ḥokumu ya Bagamoyo ḥatta Benderessalama na Zaramu yake — mwenyewe pazi, hupatana na majumbe wa Bagamoyo ḥatta Benderessalama. huo ndio mwisho wa áṣili ya mrima zamani.

## mila yao ya Wadoe.

### dasturi ya mtoto kuzaliwa.

ba'ada ya siku saba' mtoto hupewa jina. akizaliwa mtoto mwanamume, hupewa jina la babu yake, aliyezaa baba yake, na akiwa mtoto mwanamke, hupewa jina la bibi yake, aliyozaa mama yake. ao yule mtoto majina yake humwuguza — hutafutiwa jina jingine katika ndugu[3]) wa kwa baba ao ndugu wa kwa mama. na jina hilo humpa babu yake ao bibi yake. na kama watu hao wamekufa, jina atampa baba yake ao mama yake.

na yule mtoto humtazama sana katika kulala kwake, asilale kifudifudi[4]). iwapo atalala kifudifudi — bassi mtoto huyu hawamlei, husema mtoto huyu mbaya.

na iwapo ametoa meno ya kwanza[5]), humtia katika ungo, wakampeleka kulla nyumba zilizomkhuṣṣi. siku hiyo hufurahi sana. na yule mtoto humtunza, killa mtu humpa kitu alicho nacho, killa nyumba, atakáyopelekwa, harudi billa ya kupata kitu.

---

1) Die jumben von Winde heissen alle Makame ya Shani. — 2) Die jumben von Gama bis Uvinje heissen alle Mwekambi. — 3) Verwandtschaft. — 4) auf dem Gesicht. — 5) unteren Schneidezähne.

na mtoto anapoota meno ya juu kwanza — hawamlei, wanasema mtoto mbaya, humwita kibi. humtupa amma huwapa watu wengine wanaopita kumlea, ma'ana watu wa qabila nyingine, wasio na mila hii. na wazee wake wakimlea — hupatwa na maraḍi, sababu wana khofu nyingi sana.

na hiyo siku ya saba', anayopewa jina yule mtoto, humlaza kattikatti ya mlango, akaja kungwi, akamtia katika ungo, akisha humweka chini kungwi. akashika mchi, na ule mchi huweka juu ya kifua cha mtoto, walakini si sana — kidogokidogo. huweka ule mchi marra saba' juu ya kifua cha mtoto. marra ya kwanza humwambia: „shindia moyo wako, ukipewa kitu na watu wengine — ukitapike". ma'ana yake watu wengine ma'adwi, humpa kitu yule mtoto, akachanganya na uchawi, akala — huḍurika. marra ya pili humwambia: „shindia moyo wako, ukipewa maji na watu wengine kuyanywa — yasikae tumboni, marra uyatapike". na marra ya tatu humwambia: „shindia moyo wako, ukisikia maneno ya watu ya siri, usiwe mwongo — ukayatoe". na marra ya nne humwambia: „shindia moyo wako mtoto, huwi mwenyi fitna kugombanisha watu". marra ya tano humwambia maneno yaliyofanana na haya ḥatta kutimu marra saba'. huḥasibu marra saba', ma'ana yake zindiko [1]), wanamzindika mtoto, anashikwa na watu wengi.

na dasturi yao katika kulea [2]) mtoto kama Wasuaḥeli na Wazaramu, ma'ana mwanamke akiwa analea — hatwaliwi na mwanamume mudda wa mwaka. na kama atatwaliwa na mwanamume — mtoto ataḥaribika, atakuwa na nyogea. na hiyo nyogea mtoto kulla siku huhara, wala hawi mnene, huwa mwembamba sana.

1) **Zaubermittel, dass das Kind bewahrt bleibe. — 2) Brust geben.**

hiyo ndiyo nyogea. bassi yataka wapatikane watu, wanaojua dawa ya nyogea, wamfanyie yule mtoto. na kama hapana mtu — atakufa mtoto.

Wasuaḥeli wote wameshika ṭabiaʿ hiyo, illa mwanamume akiwa na wake wawili anaweza kulala na mkewe wa pili na mtoto haḑuriki. na mwanamke akiwa analea, huwa na wivu sana, naye huwa mkali kama mumewe anatembea.

### dasturi ya Wadoe tangu kuwa wadogo ḥatta ukubwa wao.

Wadoe hawana dasturi ya kupeleka watoto wao katika jando. tangu áṣili mila hiyo hawakuiweka Wadoe, illa sasa, sababu wanakwenda killa marra katika miji, nao wanalala na waanawake, walio katika miji, bassi waanawake wanawambia: „sababu nini ninyi waanaume wazuri hamwingii jandoni?" bassi wale Wadoe wakirejeʿa kwao, hutafuta mangariba, wakawaṭáhiri. ao mle katika mji hutafuta paḥali, akamwita ngariba akamṭáhiri. na akenda kwao, huwapa khabari kama alivofanyiza. pakitokea mwingine yamempendeza mambo yale, naye hufanyiza. lakin sasa wengi wanaṭahiriwa, wakesha wanakwenda katika mji, wakatafuta waʿallim, wakawafundisha kuṣali na kulla mambo ya ḥaramu na ḥalali. na wengine wanajua kusoma, lakini si wengi, wanaojua kusoma. na wakesha kujua mambo kama hayo, si mno kupenda kurejeʿa kwao, hushika sana dini. kwao wanakwenda kutezama jamaʿa zao, wakesha hurejeʿa pwani. na akiwa katika mji, jina, alilokuwa nalo kwao, huliwacha, hupewa jina la kiislamu. na akitaka kuoa anaoa kwa mażehebi ya islamu.

### mambo ya mtoto mwanamke aliyevunja ungo.

maʿana yake baʿada ya kupata miaka kumi na minne

ao kumi na mitano bassi huwa mwari [1]), na ma'ana ya kwitwa mwari — yule mtoto hutoka na damu, ndio ma'ana ya kwitwa mwari. bassi yule mtoto akiona ametokwa na damu, asinyamaze kimya, lázima alie sana, ḥatta aje mama yake ao bibi yake wamwulize: „unalilia nini?“ naye awaoneshe damu iliyomtoka. na wale wazee wake wakiona damu, watajua, ya kama amekuwa mwari. bassi tenna hakai katika nyumba ya wazee wake, atakuja kungwi lake, ambebe, ende naye ḥatta nyumbani kwake, amwoshe na kulla siku kumfundisha dasturi ya mambo yote ya kike. ḥatta ukapata mwezi mmoja, wazee wa yule mtoto na kungwi lake watatoa khabari kwa watu wote, ya kama mwari anataka kuchezewa ngoma. bassi wakesha sikia wale jama'a zake wote, ba'ada ya siku saba' hupika pombe nyingi sana za mwari kwenda katika mkole [2]). na huko kunako mkole, ndiko kunako mizungu [3]) mingi sana. na ma'ana ya mkole — mti, jina lake mkole. mwari hukaa chini ya mti huo kimya, hasemi wala hali. na watu wanacheza ngoma mchana kutwa ḥatta jioni, ndipo wanaporudi majumbani. na yule mwari atareje'a kwa kungwi lake. tenna hana jina jingine, killa siku jina lake mwari, ḥatta aolewe azae mtoto, khalafu atakwitwa mamiye mtoto.

na dasturi ya mwari — nguo havai kifuani, maziwa huwacha wazi, nguo yake huvalia kiunoni. ukipata mwaka mmoja, hufanyizwa pombe marra ya pili, wakacheza ngoma, hiyo ndiyo marra ya mwisho. tenna mwari hutoka nje, akatembea na kusema na watu, sababu zamani, alipoanza kuvunja ungo, hana rukhṣa

1) mwari wird jedes junge Mädchen mit Beginn der ersten Menstruation genannt. Sie behält diesen Namen so lange bis sie ein Kind bekommt, dann wird sie meist mamiye Mtoto, mamiye Khamisi etc. genannt. — 2) Baum. — 2) mizungu ya kike.

kusema na mtu, wala kucheka na mtu, illa yeye na watu, walio katika nyumba anayokaa. kama hakutimizá mwaka — nyumbani na nje hatoki.

naye mwari si lázima juu yake kunyoa nywele za kinena pekeyake. afanyapo mambo kama haya, na wazee wake wakamjua, akazaa mtoto — hawamlei, watamwua, ma'ana yake si dasturi mtoto mwanamke mwari kunyoa nywele za kinená pekeyake, illá kwa amri ya kungwi lake. hiyo ndiyo dasturi ya mtoto mwanamke mwari.

### dasturi ya mtoto mwanamke akiwa anataka kuolewa na mume.

yule mume humposa baba yake. na baba yake huambia ndugu zake na jáma'a zake wote, na wao husema: „sisi hatuna maneno, walakini maneno kwa bibi yake na mwenyewe mke". bassi khabari huambiwa bibi yake na yule mtoto mwanamke. bibi yake husema: „mimi nimequbali na mjukuu wangu amequbali, walakini mume tunataka kumwona". bassi yule mume hupelekewa khabari — ya kwamba: „wakwezo na bibi zako na babu zako wote wamekuqubali, wa kázáliká na mchumba wako amekuqubali, walakini mke anataká kuonana nawe kwanzá". bassi yule mwanamme atakuja katika nyumba ya bibi huyu panapo mchumba wake, akakaa naye pekeyake kuzungumza naye. ḥatta jioni atakuja bibi yao kuwatazama. yule mwari akichekacheka, bibi yake atamwuliza: „khabari gani?" yule mwari atasema: „huyu ndio mume wa kunioa mimi". bassi na bibi yake atafuraḥi sana. marra atakwenda kufanyiza ugali wa mtama, ulio mzuri sana, na kuku wa kuchoma amletee. akisha kula, yule mume ataaga kwenda zake. na yule bibi atapeleka khabari kwa baba yake, ya kama mwari ndiye mume anayem-

taka. bassi babiye mtu atasema vitu vya uposa wa mtoto wake.

wa kazálika yule mume iwapo jongoo[1]) — halipandi mtungi, ao hupanda marra moja juu ya mtungi, khalafu likaanguka, bassi yule mwanamke hächekicheki. akija bibi yake kumwuliza „wamwonaje mwanamume huyu“, yule mwari hunyamaza, hasemi wala hacheki. bassi mwanamume khánithi hafai. kama ametoa feḍḍa yake, watamrudishia. na kama bado kutoa, hawaitaki feḍḍa yake, na yule mume haji tenna. na bado mwenyewe mume hamtaki — baba yake wala mama yake wala babu yake hawamwozi kwa nguvu.

na khabari ya uposa wao yalikuwa kuposana kwa nguo doti arbaʿīni, na ushanga, na vitambi sitta ao sabaʿ, na mbuzi tangu wanne ḥatta sitta, walakini sasa wanaposana kwa feḍḍa reale ʿesherīni na mbuzi vilevile kama watakávopatana. walakin ukesha mpata mtoto wa kidoe kwa dasturi ya mrima — umepata mwanamke, maʿana ana adabu nyingi sana na moyo wake unaoga, una khofu ya ugoni, hawi na macho ya nje kama wengine. huo ndio mwisho wa dasturi hizi.

khabari yá kuoa mtoto mwanamume.

kama anataka kuoa mke, shurṭi aonekane hodari sana, anaweza kulima na kujenga nyumba pekeyake. baʿada ya kwisha kubáleghi, atamwambia baba yake — ya kama: „mimi nataka mke“. na baba yake akimwona mtoto wake hodari sana, anaweza kazi zote, atamwuliza: „umemtafuta mchumba ao bado?“ kama amempata, atasema: „nimempata mchumba, amenipendeza“. bassi baba yake atapeleka posa kwa wazee wa mwanamke. wakiqubali wazee wa mwanamke posa, kama

1) impotent.

yule babiye mume anaweza kutoa feḍḍa yote kumposea mwanawe — atatoa. na kama maskini — hana kitu, mwenyewe mtoto atatoa feḍḍa ampe baba yake, na baba yake apeleke kunako uposa. walakin maneno ya uposa: watu walio katika mji wanasema „posa“, Wadoe wanasema kufunga zengere“ [1]).

bassi akesha oa hupata ḥéshima kubwa kwa wakwe wake. na dasturi ya ukwe wa kidoe, mtu hali na mkwewe [2]) pamoja, wala katika nyumba ya mkwewe haingii. akifanya mambo kama hayo amekuwa hana adabu, watu wote watamcheka. na Wadoe mkwe [2]) humpenda sana, killa kitu cha tunu humpa. na wao Wadoe hawana fungate [3]) katika ʿarusi siku sabaʿ kukaa katika nyumba. hiyo si dasturi yao. wala mtoto mwanamke si sherṭi kuweka kizinda ḥatta siku ya ʿarusi.

### qiṣṣa cha kuoana kwao kwa Wadoe.

mtu mwenyi kutaka mwanamke wa kidoe kumwoa, baʿada ya kupatana mwanamume na mwanamke, kwanza aende kwa babu yake na bibi yake, aseme nao sana, tenna awafuraḥishe awape kitambi killa mtu kilicho kizuri. wakesha furaḥi watasema na babiye mtu, ya kama „mume huyu ndiye mume wa kumwoza mwari, maʿana mwari anampenda sana“. bassi babiye mtu hasemi maneno. baʿada wamequbali watu hao, marra ataozwa.

na kuozwa kwao hawaoi kama islamu, sababu wao hawana dini wala hawajui kusoma, wala hawana mwʿallimu wa kuwafundisha dini iliyo yote. wamekuwa kama mfano wa vipofu wasiwo macho. bassi khabari ya kuoa: siku ya kuoa hukutana watu, wakaja kwa babiye mke, na mume na jamaʿa zake vilevile. babiye mke hutamka;

1) Ehe. — 2) Schwiegereltern. — 3) wie bei den Suaheli.

akamwita yule ʿarusi, humwambia: „nnakupa mtoto wangu huyu, ndio mke wako. na kulla paḥali unapotaka kwenda naye rukhṣa, walakin kwa lugha ya kidoe". na yule mume huqubali maneno yale. marra atatoa ushanga na jogoo la kuku, ampe babiye, huo ushanga ndio nikaḥa yao. baʿada ya kwisha pakiwa, pana pombe hutolewa, watu wakanywa. na babiye mke hupika ugali mwingi wa mtama na mhindi, na kitoweo nyama ya kuku ao mbuzi, iwapo wanaweza mambo hayo. na kama hawawezi — maskini, hufanya pombe qádiri ya watu watakaokunywa, maʿana dasturi kubwa kwao.

na baʿada ya kwisha kuoa yule mume, huja watani[1]) zake, wakamtania[2]), humwambia: „mwanamke huyu humpati, illa utupe utani wetu". bassi yule mume atatoa utani awape. na akitaka kuingia katika nyumba, każálika atakuja babu ya mke, atamwambia mume: „nataka poka mke[3]) wangu". na maʿana „poka mke" — „umeninyanganya mke wangu". bassi yule mume hawezi kufanyiza uqáidi, sababu hiyo dasturi, atatoa kitu ampe babu yake. baʿada ya kwisha mambo hayo yote, mke ameṣiḥi kuwa wake. tenna mume ana khiyari kukaa katika mji wa wakwe zake, ao kwenda paḥali atakapo na mkewe.

Wadoe wazuri sana, khaṣṣa waanawake. maʿana watu, walio katika miji, wanapenda kuoa watoto wa kidoe, sababu dasturi yao nzuri. wa każálika mtu, akioa mwanamke wa kidoe, mfano wake kama aliyenunua mtumwa. maʿana mume wake akifa, harudi kwao, atakaa katika nyumba ya mumewe, na kule kwa wazee wake atakwenda kuwatazama tu.

1) Verwandte desselben Stammes. — 2) kutania heisst jemandem von den Stammverwandten das gewohnheitsmässige Geschenk verabreichen. — 3) Hier ist mke scherzweise für mjukuu gebraucht.

khabari ya kuachana.

mwanamke na mwanamume wanapotaka kuachana, katika watu wawili mmoja ataanza ugomvi, mume ao mke. akiwa mume, atalala na mwanamke mwingine, aje aṣ-ṣubuḥi, mwanamke akitaka kusema, humjibu: „unanitakia nini?“ mwanamke hunyamaza. na akapika chakula, humwambia: „chakula hiki kibichi, mimi sikiwezi kukila“. na katika maongezi humtaja yule mwanamke, aliyelala kwake, ya kama mwanamke mzuri sana, anajua mambo mengi, bassi yule mwanamke huqaṣirika sana, hupeleka maneno kwa wazee wake. na yule mume havimḍuru, killa siku hufanyiza mambo ya kumkirihi. tenna mwanamke akimwona anazidi killa siku kufanyiza mambo mabaya, naye mwanamke atafanyiza uzuri wa kikwao. akisha atapika chakula, awache, afunge mlango, atoke, ende kwa mwanamume, anayempenda, akazungumze ḥatta hamu yake imwishe. akarudi nyumbani, mume wake ameqaṣirika, atampiga sana, na khalafu yule mwanamke atakwenda kwa wazee wake. tenna mwanamume atakuja kwa wazee wa mwanamke kumtaka mke wake. mwanamke atamjibu: „mimi kwako siendi, hapo uliponikuta — kwetu, na sasa utakaa papà hapa“. bassi mwanamume, kama anampenda mke wake, atambembeleza, amwangukie miguu, khalafu mwanamke atamfuata. na kama hampendi atamwuliza: „utanifuata ao hunifuati?“ mwanamke atajibu: „sikufuati“. atamwambia: „unataka nini sasa?“ mwanamke atamjibu: „wewe sikutaki, nakuona kama ndugu yangu“. mwanamume akisikia neno hilo, marra huqaṣirika, bassi atamwacha.

na kuwachana kwao si kama islamu kuandika ṭálaqa na kumpa máhari ao kusámehe máhari. hawana dasturi hiyo, illa humwambia baba yake mke — ya

kama: „mtoto wako amefika“. na babiye mtu hujibu: „amefika“. bassi mwanamume atatafuta mwanamke mwingine, na mwanamke atatafuta mwanamme mwingine. hiyo ndiyo khabari ya Wadoe kuachana kwao.

### khabari ya kuzika.

kama mtu amekufa, dasturi ya Wadoe hupeleka khabari kwa watu, walio jamaʿa zake. nao wote huja, na kulla mtu huchukua sānda yake doti ya bafta ao záyidi kuja kuzika. bassi watu wakesha kukutana, huamru sānda kukatwa na kushonwa. ḥatta inapokwisha kushonwa, humtia yule maiti katika sanda, wakisha humweka juu ya kitanda, walakini tenna huja watani wake kumtania, sherṭi wapewe ʿada yao. na kama hawakupewa ʿada yao — maiti hatoki kwenda kuzikwa, maʿana ndio dasturi yao. na baʿada ya kwisha kuzika huenda kwa mganga kutezamia, sababu gani iliyomwua maiti huyu? amekufa kwa amri ya muungu, ao amerogwa? bassi iwapo amerogwa na mchawi, wanamjua, watamkamata wamfunge kamba, kwa dasturi ya zamani na yeye mchawi watamchoma moto, lakin sasa wana khofu.

na kuzika kwao: maiti akifa hawamwoshi kama islamu, humzika vilevile. nao hulala tanga siku tatu ao sabaʿ. illa khítima hawasomi, wala hawana dasturi ya kuvunja fungu[1]) katika qaburi baʿada ya siku arbaʿīni, walakini, kama wanataka kwenda kuzuru katika qaburi, hupika pombe ao togwa. siku ya kwenda katika qaburi, hutia pombe katika kibuyu na unga wa mtama, wakenda ḥatta panapo qaburi, humwaga unga na pombe juu ya qaburi. na kama amekuja mkewe katika qaburi, kama mumewe amekufa, hulia

1) Grabhügel nach 40 Tagen ebenen wie bei den Suaheli.

sana. na kulla mwaka, wakitaka kuzuru, dasturi yao ni kama hiyo.

wa każálika siku ya kuzika, kama ana ndugu yake yuko mbali kidogo, nao wamezika pekeyao, hawakumngoja, akija, ataqaṣirika sana, na kama hawakupatana mashauri — vitakuwa vita. labda atoe amri ya kuzika baba yake ao ndugu yake — juu ya hayo ataqaṣirika. hiyo ndiyo khabari ya kuzikana kwao Wadoe.

### khabari ya mwene anapokufa.

siku ya kufa mwene kwanza hawatoi khabari, ya kama mwene amekufa, illa wanajua watu walio katika nyumba. ḥatta aṣ-ṣubuḥi hupelekwa khabari kwa mwene mwingine, ya kama mwene fulani amekufa. na khalafu wale mamwene [1]) wote watakuja, wakafika katika nyumba ya maiti. huja na ngoma ya mṣiba, nayo hupigwa vizuri sana, haipigwi illa amekufa mwene ao mtu mkubwa katika Wadoe. na khalafu wale kina mwene wakesha kukutana, na sanda zimetimia, na kulla ʿada iko ṭayyari, khalafu mwene atatoa amri ya kunadi sanda ya kulla mtu, aliyoleta, tangu ndugu zake ḥatta jamaʿa zake. na huyo anayenadi sanda jina lake kibirikizi. baʿada ya kwisha kunadi, sanda itaamrishwa kushonwa. watakuja watani kutaka utani wao. watapewa, na khalafu watafuraḥi watasema: „hache kula". watarukaruka kwa furaḥa nyingi, sababu ndio dasturi yao. khalafu watakwenda wakachimbe qaburi wale watani. na yule maiti katika kitanda watamchukua wao ḥatta qaburini. bassi baʿada ya kwisha qaburi kuchimbwa, huletwa pembe, ikawekwa katika qaburi, ikafukiwa pamoja na yule maiti. wakisha zika, atakuja tenna kibirikizi kwa mwene kuuliza khabari ya tanga: „pana tanga ao hapana?" na mwene atajibu: „lipo tanga siku sabaʿ".

1) plur. wene und mamwene.

simami illa katika mji wa mwene. na wengine huingia ndani ya mwitu kuwatazama watu waliokuja na vita. kama pana vita — watapigana, na kama hapana vita — watasikiliza amri, inayotoka kwa mwene. kama kuna vita viko mbali, atawambia — ya kama: „nendeni katika mji wa fulani mkaupige, sababu jeuri, hasikii amri yangu". bassi Wadoe hawairudi amri ya mwene wao. na vita vinapoingia katika mji, mwenyewe mwene naye hupigana. na anapopigana hujifunga bunduqi na uta na mishare na sime yake kiunoni.

na vita kama viko mbali, siku ya kutaka kwenda vitani kwanza hutambika [1]) katika maqaburi, hupeleka pombe na unga, ndipo wanapokwenda kupigana. illa iwapo vita vimewatokea ghafla katika mji, imekuwa lázima kupigana billa ya kutambika. haya ndio maneno ya kilingo cha mwene, yamekwisha.

### khabari ya nyumba zao mfano wanavojenga.

kwanza hukata miti ya kusimamishia nyumba, na khalafu hukata fito za kufungia viwambaza. tenna huenda mwituni, wakachuna kamba, ma'ana kamba zao zinatoka katika magome ya mti. vikesha timia vitu hivyo, hupima kiwanja cha nyumba. na tenna huchimba

---

1) Am Grabe der Verstorbenen mit denselben reden. Die Suaheli sagen auch kufyagia maqaburi d. h. sie liegen auf den Knien, reinigen mit den Händen das Grab und sagen ihren verstorbenen Angehörigen, was sie für die nächste Zeit vorhaben und erbitten sich deren Beistand. Vor einer Reise in's Innere z. B. besucht der Suaheli das Grab seiner Eltern und spricht etwa folgendes: „nimekuja kwenu, wazee wangu, mimi msafiri. muungu anifungulie safari yangu, nuakokwenda niseme na watu vema, nende salama, nirudi salimini. na nitakaporudi nitawakumbuka kwa kijungu ao karamu. bi'ashara yangu itoke, na matájiri yangu niseme nao vema.

mashimo kwa duwara, wakesha hutia miti ya kusimamishia nyumba katika yale mashimo. na tenna huchimba shimo kattikatti, hiyo ndiyo nguzo kubwa. wakesha huvifunga viwambaza na vinapokwisha viwambaza hufunga fito za juu, ndio wanasimamisha msonge [1]). na nyumba zao mfano wake kama mwavuli, zina nguzo moja katti. walakin iwapo imejengwa vizuri, hukaa miaka mingi sana.

mwanamume akijenga nyumba, ḥatta ikesha, hufanyiza pombe ao togwa, akawaalika jamaʿa zake — ya kama: „kesho nnawataka mje kwangu, kuna pombe, nataka msaʿada wa nyasi [2])“. bassi wakesha sikia, killa mtu atakwenda mwituni kunako nyasi, akakate killa mtu mzigo mmoja wa nyasi, walete kwa yule jamaʿa yao; wakesha wanywe pombe. hio ndio karamu yao.

kazi ya mwanamume imekwisha katika nyumba, sasa kazi ya mwanamke. mwanamke akiona mume wake nyumba amekwisha kuijenga, naye atafanyiza pombe, awambie waanawake wenziwe — ya kama: „siku fulani nawataka kwangu, kuna pombe ya kukandikia nyumba“. bassi waanawake wakisikia, ḥatta siku wanayojua, leo tunakwenda katika kandiko, killa mwanamke huchukua mtungi wake wa kutekea maji ya kukandikia nyumba. ḥatta wakafika, marra watakwenda katika shimo la udongo. wengine wanachimba udongo na wengine wanachukua, wengine wanaponda na kukandika na kuteka maji. na huku wanakwimba nyimbo. mudda wa siku mbili nyumba imekwisha yote kukandikwa.

tenna mwanamume atapanda juu kuwezeka, na maʿana ya kuwezeka ni ile nyumba kufunikwa ma-

1) Dach. — 2) Die Wadoe verwenden umotomoto-Gras zum Decken ihrer Hütten.

nyasi juu, wasipate jua wala mvua. wakisha watahamia.

na nyumba zao hazina vyumba wala kumbi, wanajenga behwa [1]), meko, na paḥali pa kulala, na choo kidogo si mbalimbali, illa choo kikubwa wanakwenda mwituni kufanya ḥaja zao. na katika nyumba zao wanaziṣafi sana. ukaingia moyo wako haukirihiki, illa mtu aliye mchafu tangu zamani, huwezi kukaa nyumbani mwake. haya ndiyo majenzi yao Wadoe.

### khabari ya mji wao Wadoe.

Wadoe miji yao wanapotaka kuijenga, sharṭi watafute mwitu ulio mkubwá, mwenyi miti yaliyo na imara. na khaṣṣa ule mwitu ukawa na maji yapo qaribu, huupenda mno. wakesha uona mwitu, umewapendeza, killa mtu atashika munda na shoka, waukate mwitu, na majani kuyapiga moto. ḥatta ukesha husimamisha jengo, wakajenga majumba katti ya mwitu. na katika pembe ya mwitu hufanyiza boma la miba. na miba hiyo khaṭari sana, mtu mwengine hajui kama mna miba illa wao wenyewe. na mfano wa miba hiyo: huchonga miti, ikawa na ncha iliyo kali. wakisha wakaizika killa paḥali, mji mzima, na mbele ya lango lao kaẓálika, maʿaná hilo ndilo boma lao. illa husaza njia moja ya kutokea. huko hawatii miba [2]). ikawatokea khaṭari ya vita, watoto wao na waanawake wao huwapitisha katika njia hiyo isiyo miba. na wenyewe waanaume huziwia mji kusikiliza mwisho wa khaṭari. wakiweza kupiganá — watapigana, na kama hawawezi — watafuata njia, waliyopita watoto wao, wauwache

1) grosser Raum, der alles vereinigt. — 2) Die Spitzen sind so verborgen, dass man sie nicht sehen kann. Nur auf den den Bewohnern bekannten Wegen sind keine.

mji. na huko wanakokwenda kuna mwitu mwingine ulio mkubwa. wakaingia katika mwitu huo, mtu mwingine hajui kama mna watu humu. hukaa kimya, wakasikiliza ḥatta vita vishe. ndipo wanapotoka nje. na lango lao la pili, jina lake kiri, hulifunga marra tatu. hufunga kwa miti, iliyo mikubwa, na kamba. kwa vita vyao wenyewe kwa wenyewe hupigana siku nyingi. illa vita vya mzinga ḥatta sa'a moja haipati.

wa każálika katika mji wao ndani ya mji majani ya vyakula mahindi ao mtama, na kulla matakataka ḥatta majivu ya moto hawamwagi katika mji, illa wanamwaga nje ya mji. mudda wa miaka mitatu pale wanapomwagia majivu na mataka panakuwa chuguu kubwa. na hiyo chuguu hawavunji kabisa, huwacha vilevile ḥatta wakihama.

wa każálika kuni zao za kupikià shàrṭi za kuchagua miti yake, hawapikii ovyo billa ya kuchagua, ma'ana mnà kuni nyingine — mzio [1]), haziingii katika mji kupikiwa. na kama mwanàmke mgeni amevunja ukuni, usioingia katika mji, na wenyeji hawakuuona ule ukuni, ukatiwa jikoni — bassi haipati mudda wa sa'a wataona majoka yanaingia katika mji, ao usiku simba ataingia ndani ya mji. na akiingia simba, hatoki illa apate mtu kumla. bassi wenyewe wakisha ona ule ukuni katika jiko, marra watautoa. wakesha watafanyiza dawa zao za kuondoa majoka, na simba asirudi tenna katika mji ma'ana miji yao wanapojenga huijenga kwa zindiko [2]), kulla nyama asiwaḍuru. na ba'ada jua likatuà, hawapaliani moto, sababu wanachelea mambo kama hayo ya simba nà nyoka.

1) Verbot. — 2) d. h. sie machen dawa, stecken einen Stein oder Holz mit den nöthigen Zaubermitteln an einem Kreuzweg vor dem Ort in die Erde, damit derselbe vor Schlangen und wilden Thieren bewahrt bleibe.

na ṭabia' yao wanapojenga pamoja, mmoja usiku akipiga makelele, mnyama kama amemwingilia katika nyumba ao mwizi — bassi fahamu wote watatoka nje, wajifunge sime, wakamsikilize mwenzao jambo lililompata. huo ndio mwisho wa maneno hayo.

### nguo za Wadoe.

áṣili zamani Wadoe walikuwa hawajui nguo, walikuwa wakivaa magome ya mti. huyaponda, wakesha wakayasuka na nyuzi, wakavaa. na jina lake mavazi hayo yanakwitwa kiyombo. bassi mwanamume husuka viyombo viwili vya mke wake, kimoja hujifunga mbele na kimoja akajifunga nyuma, yamekwisha mavazi yake mwanamke. na mwanamume kaẑálika. na hivo viyombo haviwi virefu, mpaka wake magoti bassi, na mwanzo wake kitovuni, kichwa na mabega vi wazi, hapana kitu cha kujifunika. na wakizaa mtoto, kaẑálika humfanyizia bwende[1]), akavaa kiunoni, wakamfunga mbele, nyuma hana kitu. na wengine wanajua kusuka viyombo, wengine hawajui, wananunua. kuna watu wengine hawana kazi illa hivo viyombo. na kuuza kwao hupatana kwa themani ya mhindi ao mtama, sababu zamani walikuwa hawajui mapesa wala feḍḍa, walakin sasa wamekuwa werevu, wanajua killa kitu, wanavaa nguo kama watu wengine, waanawake wanavaa leso na kaniki, ao huvaa doti ya shuka moja. na waanaume huvaa shuka, walakin huishona pande mbili, jina lake kigwembe. na kama hawezi kuzipata shuka mbili pamoja, huvaa shuka moja mwanzo wa kitovuni ḥatta katika magoti. bassi amekwisha, hana kofia kichwani wala kanzu maungoni.

---

1) Die Wadoe nennen jedes Kinderkleid bwende, die Suaheli sagen shegele pl. mach. Doch ist ihnen auch der Ausdruck bwende bekannt.

na usiku wȧnapotȧkȧ kulala, zile nguo alizovaa mchana, na usiku ȧtajifunika ileile. na kama wáqti wa baridi huweka gogo la mti, wakalichoma moto, wakaliweka qȧribu ya kitanda, bassi ule umotomoto ndio mfano nguo yȧ pili, sababu nguo ya kujifunika hawana usiku. na mwanamke akiwa na mimba — saná huvaa kaniki. hio ndio dasturi ya mavazi yao Wadoe.

khábari ya nguo zao wanavofanyizȧ.

nȧmna wanávofanyiza nguo zao: hawazifui, illa huzivaa tangu kutoka dukȧni kwa Mhindi ḥatta zikawa chakavu. bassi zinapokuwȧ chakavu, huzitia mafuta ya nyonyo, waȧnaume na waanawake hufanyȧ kama hivo. na hayo mafuta ya nyonyo áṣili yake mti wa mbono, huzaa matunda, wakayachuma, wakesha wakayaanika juȧni ḥatta yakakauka. na khalafu huyapika katiká mitungi ḥatta yakawiva. tenna huchuja yale mafuta, huyatia katika vibuyu, wakayaweka. na mafuta yake dawa sana kwa maraḍi ya mshipa [1]), iwapo mtu mgonywa, akichuliwa [2]), hupata uzima.

wa kaẑálika wale walio mardadi wanafua nguo zao, lákin si killa siku. amma mafuta záyidi wanatumia katika nguo, wa kaẑálika na kupakaa mȧungo mazima waanawake na waanaume. na nguo zao huweka chini ya mchago wȧnapolȧla, ao huzitia katika kilindo, ao mtungi, ndio maṣanduqu yao. na nguo ikiwa kukuu hawaitupi, huiweka vema ḥatta waqati wa vyakula, mashamba vinapowiva, humpa mtu ungojezi wa kungojea vyakula mashamba visiliwe na nyama, ndege ao nguruwe. ao hutokea mtu, aliye maskini, kutafuta nguo, iliyo kukuu, kununua kwa themȧni

1) Rheumatismus. — 2) kuchua bei Rheumatismus mit Ricinusoel fest einreiben.

ndogo, sababu nguo mpya hawezi kuipatā. hiyo ndiyo khabari ya nguo zao wanavofanyiza.

## khabari ya waanawake mavazi yao katika kiuno.

waánawake wa kidoe mwanzo wa kupata ʿomri wa miaka kumi hununuliwa ushanga na wazee wake mwingi. ukeshá ule ushanga hutungwa, ukasukwa kama mfano wa mtu, anayesuka mkeka. tenna ukawa na kiwimbo, kilicho kinene, mfano wa mguu wa mtu. na khalafu yule mtoto mwanamke huvaa katika kiuno chake. huo ni uzuri mkubwa kwa Wadoe. na akiwa mwanamke mkubwa, huwa na ushanga mwingi. bassi anapouvaa mwanamke, akiwa mwembamba wa kiuno, akivaa ushanga huo, atakuwa mnene kiuno chákc. nao huvaa wanapotoka nje kwenda kutembea, walákin wanapotaka kulala huuvua. nao hutangulia kuvaa ushanga, na khalafu akavaa nguo. na ushanga huo wote huuvaa vijana na wazee. na akifa hurithi mjukuu wake. na kama hana mjukuu, bassi haurithiwi na mtu mwingine. na wenyewe wamezoea uzito wa ushangâ huo. huchukua mtungi wa maji, na mitungi yao mizito, wakapanda juu ya vilima upesi. na mwanamke akiwa na mume, humnunulia ushanga huo kwa wingi. na kamá hakumpa, hawapatani mashauri nyumbani, killa siku ugomvi, sababu hapana mwanamke wa kidoe asiyekuwa na ushanga huo kiunoni mwake, ajapokuwa maskini, ameqirri kukosa vitu vyote, walakin apate ushanga. na wao Wadoe waanaume, mwanamke akivaa ushanga huu, hufurahi sana.

wa każálika siku, wanayoalika na ngomá, bassi siku hiyo ndipo wanapojipamba. katika miguu huvaa

vitindi [1]), na mikononi kaẑálika huvaa vitindi. na khalafu atavaa kaniki, ajitande kitambi, atie mafuta ya nyonyo katika kichwa. na anapokwenda vile vitindi hulia miguuni. na hivo vitindi shaba kama señgenge, huikunja duwara qiási cha miguu yake na mikono yake, na khalafu hufanya uzuri mkubwa. na kidoleni huvaa pete za riṣaṣi, na shingoni akavaa ushanga, walakin si mwingi. wakesha wakenda ngomani. hayo ndio mavazi ya mwanamke wa kidoe.

### khabari za nywele zao waanaume na waanawake.

waanawaume wengine wanasuka na wengine wananyoa. na kusuka kwao kwanza huosha nywele na majani ya mkunuñgu na maji yaliyo moto kidogo. na majani yake yanateleza sana maji yake. akesha osha kichwa, huleta udongo mwekundu, khalafu huzisuka zile nywele, na kupaka udongo juu yake. akesha suka hutia mafuta ya nyonyo kichwani. huo ndio msuko wa waanaume.

wa kaẑálika waanawake wanafanya kama hivo. mwanamke hanyoi nywele zake, illa anayetoka katika uzazi, baʿada ya kwisha kuzaa kwa siku arbaʿīni, hunyoa nywele zake, amma kama hakuzaa hazinyoi. walakin waanawake namna wanayosuka nyingine na waanaume namna nyingine, bali [2]) wote wanatia udongo mwekundu kichwani na mafuta ya nyonyo. waanawake wanasukwa na waanawake wenzao, na waanaume kaẑálika, walakin khabari ya kusuka waanaume yalikuwa zamani, sasa mno wananyoa. na waanawake misuko

---

1) suah. señgenge Messing- oder Kupferdraht, den sie in Spiralen drehen.. — 2) aber.

ya kizamani wameiwacha, wanasuka namna ya sasa. kaẓálika udongo mwekundu hawautumii sana.

na siku ya kwenda ngomani mwanamke wa kidoe huosha nywele zake, akesha akazisuka kwa msuko wa zamani, akavaa kaniki yake chini, akajitanda kitambi barawaji, na miguuni akavaa vitindi, na mikononi kaẓálika. bassi siku hiyo mwanamke, kama ana mume, hamqubalishi kwenda pekeyake, na akikataa — utakuwa ugomvi. ba'ada ya kwisha kusuka nywele, lazima usoni hutinda sekini[1]) ma'ana hiyo sekini mwanamke huzidi kuwa na háiba uso wake. na jina la kidoe sekini inakwitwa denge. waanaume wengine hutinda sekini, lakini sherṭi awe na nywele nyingi. lakini waanaume wananyoa duwara kichwa kizima, waanawake wananyoa mbele ya uso. lakini kama hajaolewa, si desturi kunyoa denge, kusuka haiḍuru.

### namna ya meno yao.

meno yao ya Wadoe yanaota kámili kama kwa watu wote, lakini ba'ada ya kuwa mkubwa, hutaka kufanya uzuri, huwashauri wazee wake — ya kama: „nnataka kupanya mwanya[2])“. tenna huitwa fundi, akaja na vyombo vyake, wakamwambia: „tunataka umpanye meno huyu kijana“. wakesha patana naye yule fundi, watamleta yule kijana mbele ya fundi ampanye. na kupanya kwake huja na vyuma viwili, kimoja hushika mkono wa kiume, na kimoja mkono wa shoto. tenna humpanya kama mfano wa mtu, anayefanyiza nakshi katika ubao. lakin desturi ya meno

---

1) Die Frauen rasieren Stirn und Schläfen aus, während die Männer einen Kreis rund um den Kopf herum ausrasieren lassen. — 2) sie splittern die beiden obern Vorderzähne ab bis sie spitz werden und so eine Lücke (mwanya) entsteht.

wanayoyapanya — meno ya juu, lakini ya chini hawayapanyi. na hayo ya juu si yote illa meno mawili. nayo hawayapanyi yakiwa na ncha kama meno ya paka, illa qádiri ya kujua mtu huyu amepanya. każálika waanawake vilevile wanapanya, lakini wana qabila wanawopanya, wengine hawapanyi. na yule fundi akisha, humpa mchele wake, sababu si desturi kupanya burre. na ile siku anayopanya, hawezi kula chakula kilicho moto, illa kipoe. wala pale anapokwisha kupanywa, marra hawezi kula chakula, illa upite mudda kidogo. huo ndio uzuri wa meno yao Wadoe.

kazi wanazofanyiza waanaume kwa Wadoe.

waanaume ba'ada ya kurudi mashamba kulima, hutoa kicha[1]) cha muyaa na kisu, wakisha hutandika jamvi, wakakaa kitako, wakachana[2]) muyaa, na huku wanatafuna muhindi mteke[3]) wa kuchoma. wakisha chana ule muyaa, huanza chanzo[4]) cha bambo[5]) kusuka qádiri pima settini. likesha bambo hushona jamvi lililo kubwa. linapokwisha jamvi, hupeleka Winde kuuza. jamvi moja hupata rupia u nuṣṣ. na khalafu hununua chumvi, akanunua mavazi, khalafu akarudi kwake.

na kazi ya pili husuka vikapu vikubwa na vidogo. vikapu vikubwa kazi yake, wanapovuna mashamba, hutilia muhindi ao mtama, wakachukua majumbani. wa każálika vingine hupeleka Winde kuviuza. na vikapu vidogo vilevile.

wa każálika husuka na vitanga. na hivo vitanga msuko wake duwara, lakin vikubwa sana, huvisuka

---

1) Bündel, auch tita la muyaa. — 2) in Streifen schneiden. — 3) weich. — 4) kleiner Anfang. — 5) Mattenstreifen.

kwa wingi, wakiwapelekea Washihiri, wanavipenda. na ṅgongo zinazobaqi katika miyaa huzikusanya qádiri ya mizigo thalathini, wakauza kwa Washihiri, hupata mapesa ya kutumia.

na wengine kazi yao kugonga mpira mwituni na kuchimba sandarusi.

hio ndio kazi ya waanaume.

### kazi ya waanawake.

baʿada ya kurudi mashamba, huchambua chunga na kuhimiza chakula, akala yeye na mume wake. tenna hutwaa jembe lake, akenda panapo shimo la udongo, akauchimba, na khalafu hutia katika kikapu, akarudi nyumbani kwake, akauponda ḥatta ukawa leini. tenna huanza kufinanga vyungu na mitungi, akafinanga na mikungu ya kulia vyakula. baʿada ya kwisha kufinanga vile vyungu, huviweka juani mudda wa siku tatu ḥatta vikakauka. vikesha kukauka hukata kuni, akatwaa vyungu vyake, akavichoma moto ḥatta vikawiva. vinapokwisha wiva, huja waanawake wa kidoe, wakanunua vyungu na mitungi, na vingine hutumia mwenyewe. na kama akiona havitoki, huvichukua Winde akaviuza.

na kazi yake ya pili mwanamke husuka mikeka ya ukindu[1]) na miyaa, walakin haina nakshi kama mikeka, wanayosuka waanawake, walio katika miji. mikeka yao yote meupe. na Wadoe hawajui jina la mkeka, wanasema hinda la kulalia ao la kukalia. na yakiwa mengi huuza. na asiyojua kusuka, wala mapesa hana ya kununua mkeka, wanatandika nguo zao juu ya kitanda, lakini wenzao huwacheka sana wafanyapo mambo hayo. hiyo ndio kazi ya waanawake.

1) Baum, aus dessen Blättern Mattenstreifen geschnitten werden.

### khabari ya ukulima.

inchi yao Wadoe ina ta'abu kubwa ya maji, sababu mkuranga. watu wakiondoka aṣ-ṣubuḥi kwenda kuteka maji — majira ya kaskazi hurudi sa'a nne. walakini vyakula katika mashamba vinastawi.

wote wanalima mume na mke. kwanza mume hulima shamba yake, akapanda killa mbegu muhindi, mtama, mhogo, viazi, karanga na kulla kitu. na mwanamke shamba lake mbali pekeyake, walakin mbegu lázima mume anatoa. na katika ba'aḍi ya siku mume huenda katika shamba la mke wake kumsa'idia, iwapo ile shamba ina majani mengi, mwanamke hayawezi pekeyake. każálika siku ya kupanda hendi mwanamke pekeyake, huenda na mumewe kumsa'idia mpando. na siku, anayopanda mume, huenda mwanamke kumsa'idia mumewe. iwapo mpando umekuwa qaribu, na shamba zao bado kwisha, wote wawili husa'idiana kuwaḥi huo mpando pamoja na watu, sababu watu hupanda kwa miongo [1]). wakiukosa mwongo, ukiwa umetangulia pekeyako kupanda, ao umepanda nyuma, watu wote wamekwisha, wewe hupati vyakula. watu wakivuna áuwali, wewe ukavuna mwisho, vyakula vyako vitaliwa na ndege, ao ukatangulia kuvuna qabla mashamba ya watu wengine hawajavuna — każálika vitaliwa na ndege. ao mimea itakufa kwa maji, sherṭi mpande sawasawa na kuvuna każálika.

aiḍa zamani za nyamizi [2]), vyakula vimewiva, mashamba lázima mume kumsa'idia mkewe kumpa mtu wakaamie pamoja. każálika atafute mtu mwingine amsa'idie shamba yake, ma'ana katika ukulima ta'abu kubwa kuamia ndege. huo mwisho wa makulima yao mke na mume.

---

**1) Jahreszeiten. — 2) kuamia ndege.**

khabari ya mavuno yao.

vyakula vinapowiva mashamba, wakitaka kuvuna, havuni mtu moja pekeyake, illa hualikana jama'a na majirani — ya kama: „siku każa wa każa mimi ntavuna shamba langu, allah allah mje!“ ḥatta ile siku waliyoagana — ikatimia, killa mtu huja na kapu yake, wakenda shamba kuvuna. na wakesha vuna, killa mtu humpa qádiri yake. nao hawavuni illa kwa tambiko[1]) zao.

wa każálika khabari ya tambiko ya mavuno: ba'ada ya kwisha kuvuna, ukiwa mpunga, hutwaa mchele qádiri ya magao[2]) mawili, wakapika katika kijungu kipya, na khalafu hupeleka panapo njia panda. wakesha wakajenga kibanda kidogo, wakakiweka kile kijungu pamoja na ule wali walioupika. na ma'ana yake wanasema sehemu ya kinyamkera[3]). na vyakula vipya hawavili kwanza illa kwa mkumbi. na huo mkumbi unga wa mti, rangi yake majani, huchanganya pamoja katika chakula, wakesha wakala. bassi wakesha kufanyiza mambo hayo, ndipo nao wanapokula vyakula vipya.

wa każálika iwapo wamevuna mtama ao mpunga, lázima hufunga kicha cha mpunga ao shuke la mtama, wakalipeleka njia kuu kuliweka. bassi vitu hivo katika wao Wadoe, wakiviona katika njia kuu, hawachukui, sababu si mila yao, illa apite mtu, atokaye Winde ao Bagamoyo, akiona atachukua.

aiḍa ba'ada ya kwisha kuvuna, hutenga vyakula, ambavo watakula, wakiviweka mbali, na watakávyotumia huviweka mbali. na mahindi ya kutumia hawayamenyi majani, wanawacha vilevile mudda wa mwaka. illa wanapotaka kufanyiza chakula hutwaa qádiri. hii khabari ya mavuno yao.

---

1) Erklärung folgt. — 2) Handvoll. — 3) kinyamkera — Geist.

### maneno ya vyakula vyao.

vyakula vyao wanavyovipenda muhindi ao mtama. na huo muhindi jinsi wanavofanyiza: kwanza wanautwanga, na khalafu wanautia katiká jungu la maji ukaroana [1]. wakesha wakautwanga marra ya pili. bassi pumba [2] yake huibambika [3] katika maji mudda wa siku mbili ao tatu, wakesha huitoa katika maji, wakaipika uji. wanauita uji wa bambiko, wanaupenda sana uji huo. każálika na ule muhindi baʿada ya kuutwanga hutokea unga mweupe mno na ugali wake każálika mweupe.

aiḍa mtama każálika wanàufanya kama wanavofanya muhindi, lakini ugali wa mtama hawaupendi, sababu mzito katika tumbo, hautoki hima.

muhogo na mpunga wanalima sababu ya kuuza kupata mavazi, walakini hawakujaʿali, ya kuwa ni chakula. náo aṣ-ṣubuḥi wanakula ugali, ao ni huo uji wa bambiko. na mchana każálika ugali. na usiku hawali, illa wanakula jioni jua linapotua. na chakula cha aṣ-ṣubuḥi na mchana wanakula katika nyumba zao, illa chakula cha jioni hukutana wote, wakala pamoja. waanaume wanakula pekeyao na waanawake pekeyao.

na ṭabiaʿ yao wanapokula, tonge zao wote wanamega upande mmoja, tenna paḥali pamoja, maʿana yake wanásema , ugali kumega upande mmoja vizuri sana, maʿana unaobaqi hauḥaribiki, mwanamke anaweza kufanyiza togwa. maʿana ule ugali unaobaqi waanawake huutia katika mitungi, wakaupika togwa, wenyewe wanasema mvato. wanalipenda mno togwa hilo. wanakunywa wanapokuwa shamba wanalima ao wanaporudi, maʿana li baridi sana.

na ṭabiaʿ yao katika vitoweo hutowea chunga. na

---

1) weich werden. — 2) Spreu. — 3) in Wasser stecken, zudecken und stehen lassen.

hiyo chunga ni mboga, walakini chungu sana. huipika na khalafu wakachuja, ule uchungu ukaondoka kidogo. ná khalafu huipika marra ya pili, wakeshá wakatia chumvi na ufuta ao pato[1]) nyingine. na hiyo pato nyingine ni kokwa za matango, yaliyo mapevu, ao kokwa za mbede. na mbede ni kama matikiti. bassi kokwá zake ndizo wanazozikaanga ḥatta zikaungua, khalafu huzitwanga katika kinu, unga wake wakatia katika chunga, wakatowelea na ugali wa mahindi ao wa mtama. wenyewe wanapenda mno Wadoe.

wa każálika Wadoe panya na nyani na kima wanakula. lakini zamani walikuwa wengi wanaokula, sasa haba wanaokula.

namna ya silaḥa zao Wadoe.

silaḥa zao tangu zamani walikuwa hawana bunduqi, illa silaḥa zao nyuta na mishare na sime. sime hujifunga kiunoni, mishare hushika mkononi, na upindi begani. na hiyo mishare hutia katika bode, ndani ya bode huwa na mishare khamsini. na watoto wao huwafundisha kurasha[2]), huweka kitu mbali, akisha humwambia „piga". akiweza, tenna huenda naye mashamba kumfundisha kurasha ndege ḥatta ajue. każálika sime vilevile humfundisha jinsi inavotumiwa. humwonyesha kitu kilicho kiteke, akamwambia „piga". na yule mtoto hupiga, lakini marra moja hawezi, illa kwa kufundishwa marra nyingi, sababu silaḥa ya sime mapigano yake yanataka maʿarifa. każálika uta na mshare unataka maʿarifa, kama hujui maʿarifa yake hupigi kitu.

wa każálika mundu wanachukua Wadoe, lakini silaḥa hiyo hawaichukui katika vita, hiyo silaḥa ya mjini ya kujengea majumba ao kukatia mwitu mashamba, na

1) Fett. — 2) schiessen.

kuulia nyoka. wakiwa katika mji silaḥa zote huzivua, hubaqi na huo mundu. lakini kama wanagomba wenyewe kwa wenyewe hupigana kwa hiyo miundu. amma silaḥa yà shoka wao hawana.

na tángu zilipoingia silaḥa za bunduqi, nyuta na mishare wameiwacha wote, wanashika bunduqi, lakini sime hawakuiwacha.

na silaḥa ya mwisho ni kisu, wanachukua ya kuwa kukatia nyama, ao amejichoma mwiba kutolea. hawakukifanya kuwa silaḥa. imekwisha khabari ya silaḥa zao.

### namma ya sumu[1]) yao wanayotia katika silaḥa zao.

namna ya kwanza jina lake msunguti. na huo msunguti ni mti wa mwituni, mbaya sana. bassi wale wawinda, ndivo wanavoqaribia mti huo, huupika uchungu. na kupika kwao kwanza huuchuna magome yake, akaupika katika chungu, kilicho kipya, ḥatta yakawiva. na mudda wake siku saba'. yale mafuta, yanayotoka katika yale magome, ndio msunguti. bali msunguti jina la mti, amma yale mafuta jina lake uchungu. bassi unapokwisha kupikwa, yale majungo huyavunja, sababu khaṭari kubwa mno. kama mtu hajui, kama jungu hilo limepikiwa uchungu, akaliramba — marra atakufa, hapana ṣúbira.

kaẓálika ḥokumu ya ule uchungu huutia katika mishare yote na mikuki, sababu anapokwenda kuwinda, akimpiga mnyama mshare mmoja — haondoki. ujapokuwa ule mshare haukumpata sana, muradi atakufa, sababu sumu mbaya. na bin Adam kabisa hawezi kuuchukua.

na áṣili walivovumbua sumu hiyo, Wakamba ndivo

---

1) suah. liga pl. mal. oder uchungu.

walivokuwa wakitia katika mishare yao. każālika nyingine, jina lake kulēga, mti huupika kama msunguti, lakini hiyo sumu ya kulega haiui upesi kuliko msunguti. na wakitaka kupaka katika mishale zao ao mikuki, hawashiki na mikono, wanapaka kwa ujiti. washikapo kwa mkono, khalafu wakila chakula, mwenyi ʿomri, ulivo mchache, atakufa. na wanapoweka, hawamwonyeshi mwanamke, wanachalea kuwaua. na mwanamke akiwa na ḥeḍi, haishiki sumu hiyo — vibaya, hukatika ile ḥeḍi. hiyo ndiyo khabari ya sumu.

namna ya kuvinda kwao.

kwanza wanawinda kwa wavu. na huo wavu ni kamba, zilizo nyembamba, wanazisuka zikawa na tundu nyingi. na khalafu huchukua wavu, wakenda nao mwituni wakatega. na kutega kwao hunyosha ule wavu mwanzo wa pembe ḥatta mwisho wa pembe, tenna wakafunga na miti. wanapokwisha, wote huondoka, wakenda wakatafuta nyama mwitu paḥali walipolala. wakiwaona huwasituza, wakapiga ukelele. na wale nyama mwitu, wakaposikia ukelele wa wana Adamu — husituka. tenna wale wawinda huwafukuza wale nyama upande ulivo na nyavu zao. na huku wanapiga makelele. bassi wale nyama watakwenda mbio ḥatta wakaingie katika nyavu. wakesha waje wawakamate. ḥila zimeweshea wale nyama.

każālika namna ya pili hutega nguruwe ao nyama wengine kwa namna nyingine. kwanza huchimba mashimo, yaliyo makubwa, huku na huku, tenna wakenda kuwatafuta nyama mwitu, wakawasituza vilevile, wakenda mbio ḥatta katika mashimo. wakiwa ndani ya mashimo, hawawezi kuruka. huja na mikuki na mashoka, wakawapiga ndani ya yale mashimo, wakapata nyama.

illa ndege, wàliwo wakubwa, huwatega kwa tanzi. hufunga kamba katika mti, wakesha hufanya kitanzi, wakaweka chini ya kitanzi ndege aliyo mdogo. bassi dege, lililo kubwa, likaona kidege, huṭamʿani kwenda kukimata — marra litanasa.

ao wanagonga urimbo, wakapaka katikā mti. wakesha wakaufunga, wakabandika juu ya urimbo nyenze[1]. ndege akiona nyenze, huṭamʿani kwenda kumla, akakaa juu ya urimbo — amenasa. hizi ndizo ḥila za matego yao ya kuwinda.

### mambo ya watu wenyi marắḍi.

mtu mwenyi ukoma Wadoe hawali naye, wala hawakai naye qaribu. lakini humtafutia waganga wa kumṭibu ḥatta apate náfuʿu. na kama waganga wamemṭibu, naye killa siku vidole vinakatika, na kupona haponi, bassi humwambia: „wewe tenna si mwenzetu, mtu mwingine, na katika mji huu toka". bassi akiwa na jamaʿa zake, huenda nje ya mwitu, wakamjengea kibanda pekeyake, vyakula hupika mwenyewe. na kisima chake cha maji pekeyake, maʿisha yake hukohuko mwituni. ao akiwa bakhti yake ḍaʿifu, usiku atakuja simba ao fisi wamtafune.

każālika mwenyi wazimu, akiwa hakuṭibika, killa siku anapiga watu, na kuvua nguo, akenda uchi, ao hutaka kuunguza majumba katika mji, naye vilevile humtoa katika mji, wakamjengea kibanda katika mwitu pekeyake.

aiḍa każālika ugonywa wa buba huogopa kukaa naye pamoja, sababu wanasema, ugonywa mbaya wa buba, marra hutoka kwa huyu ukaingia kwā huyu, naye humtoa katika mji.

---

1) Wurm.

maraḍi matatu hayo Wadoe wanayokhofu sana, illa maraḍi ya ndui — mgonywa wa ndui hawamtoi katika mji, watamwuguza ḥatta apone ao afe.

kinyume cha Wazigua — mgonywa wa ndui na wa buba humtoa katika mji, walakini mgonywa wa ukoma rafiqi yao, wanakula naye, wanakaa naye pamoja.

na ṭabia' ya Wadoe mwanamke mwenyi mume, na mume huyo amekufa kwa maraḍi ya ukoma ao ya buba — hapana amtakaye. hiyo ndiyo khabari za maraḍi.

haya maneno ya vyapo.

iwapo mtu mwizi, ämekwiba, lakini hawakumwona, wanatuhumiana, bassi kwanza hupika maji ya moto, wakesha wakajikusanya wote kama wanavojituhumu. wakesha wakaombokeza[1]: „mimi fulani, kama ndio niliyokwiba kitu cha fulani, kiapo kinigwie, na kama sikwiba, kiapo nihongeze“. bassi tenna mtu hutia mkono wake katika jungu la maji ya moto, kama hakwiba — mkono utatoka salama, na kama mwizi — mkono utaungua, hawezi kuyashika maji ya moto.

namna ya pili: humwita mganga akaja, wakamwambia — ya kama: „sisi tunataka kiapo kwako cha sanga“. bassi hupatana naye yule mganga fungu lake watakalompa. wakesha patana, mganga hutoa kibuyu chake, na ndani ya kibuyu mna shindano, jina lake sanga. watakuja, wanaotoka kuapana, mganga atasema maneno yake — ya kama: „sanga unakwenda katika jicho kutafuta mwizi, iwapo ni mwizi — usitoke sanga, na kama si mwizi — si nyumba yako sanga, toka nje“. atamtia shindano katika jicho, na huko anakwimba: „sanga ndekera[2]) mwanangu[3])“. na watu wanaitikia. kama si mwizi, shindano haiingii katika jicho. na kama

---

1) = dumiliza. — 2) = niwachie. — 3) gemeint ist das Auge.

ni mwizi, shindano inaingia na khalafu hutoka tenna, lakini jicho hugeuka likawa jekundu. na watu wote watajua, ya kama huyu mwizi. na yule mwizi hana ḥila ya kukataa, kama „mimi si mwizi“, atalipa vitu vilivokwibiwa. na akikataa, watampeleka kwa mwene, naye mwene atamlazimisha kulipa.

iwapo wote wamehongera, hapana mtu kiapo kilichomshika, itakuwa daʿawa kubwa, ao awalipe feḍḍa ao mbuzi awape watu, aliwowasingizia wizi. na kama hakutoa watapigana. hii ndio khabari ya vyapo vyao Wadoe.

## khabari ya udugu wao jinsi wanavotakana.

huondoka mtu mmoja, akamwambia mwenziwe: „somo, mimi nakutaka udugu“. na yule wa pili humjibu: „vema, nakutaka“. bassi humwuliza: „kwenu wapi?“ naye humwambia: „kwetu paḥali każa wa każa, na wazee wangu kina fulani. na mkutano wao sana katika pombe, ndipo wanapojuana watu wengi. bassi wakesha patana, yule mmoja humpeleka kwa wazee wake, akawambia — ya kama: „huyu nnamtaka urafiqi“. na wazee wake humjibu: „vema“. bassi tenna, akiwa anajiweza, atatoa mbuzi, wamchinshe wafanye udugu wao. na kama si mweza wa mbuzi, atatoa kuku, muradi wapate ini la usare [1]), khalafu atakuja mdumilizi [2]), awadumilize, awambie: „wewe umemtaka Mtengwa udugu, na Mtengwa ana ndugu wadogo waanaume, na wewe una mke, ndugu za Mtengwa wakilala na mke wako usiqaṣirike. ukiqaṣirika, ukenda pwani kumletea ʿaskari, ao ukenda kwa mwene kumshitaki, nawe ukataka kulipwa ugoni — — ufe“. na yule wa pili huambiwa kama hayo. kha-

1) Blutsbrüderschaft = udugu, und sare yangu = ndugu yangu mein Blutsbruder. — 2) Leiter der Ceremonie.

lafu wakachanshwa wote wawili, wakapewa nyama ya ini killa mtu kipande, kikapakwa damu ya huyu na huyu, wakala pamoja.

namna nyingine hufanyiza udugu kwa mchanga wa Mzia [1]). nao mchanga huo mweupe kama sukari, lakini mwembamba kama unga wa ngano. wanapotakana udugu, killa mtu huramba mchanga huo, lakini manuwiyo [2]) kama tuliyotangulia kuyasema katika ini la kuku.

wakesha fanyiza udugu huo, hupendana kama ndugu wa kuzaliwa. hawatetani, wala, wakiombana kitu, hawafichani. na zamani za kwanza udugu huo walikuwa wakirithiana, mmoja wapo iwapo amekufa, lakini sasa hayako mambo hayo. yamekwisha maneno ya usare na udugu.

## khabari ya kuomba mvua.

iwapo wameikosa mvua, hufanyiza mashauri kina mwene wote — ya kama: „mwaka huu jua, vyakula haviji juu tukipanda, lázima twendeni mzimni“ [3]). bassi hutafuta doti ya kaniki na doti ya bendera, wakaondoka mamwene, wakenda Nguu, kunako mzimu, kutambika. na huo mzimu umo katika pango ya jiwe, walakini nafasi sana. wanapofika huamkia mzimu wale mamwene. na mzimu nao hunguruma kama mfano wa mvua. na kama wamefuatana na mtu mbaya, mzimu wao huambia: „katika safari yenu mmefuatana na mtu mbaya, amevaa nguo namna każa wa każa“. bassi akiwamo katika safari, watamfukuza. bassi wakiwáşili katika mzimu, watasema maneno yao kama wayatakayo — ya kama: „mwaka umetutupa jua jingi, vyakula

1) Mzia ein Ort in der Nähe von Pangani. — 2) Anwendung = madumilizo. Das Verb nuwiya (ar.) = dumiliza. — 3) mzimuni Ort, wo die Geister der Verstorbenen hausen.

haviji juu, na maraḍi mengi sana, sasa tunakuombea utupe mvua". khalafu utanguruma marra ya pili mzimu, bassi watafuraḥi wote, ma'ana wamejibiwa. na kama mzimu umeqaṣirika — haujibu, utanyamaza kimya. na iwapo wamepata furaḥa, mvua itakunya nyingi, na kama hapana furaḥa, watarudi na jua.

na áṣili ya mzimu huo — mtu, alikuwa jumbe katika Ukami. naye alikuwa mchawi sana. bassi ḥatta siku moja watu wakafanyiza vita kuja kumpiga — wasimweze, sababu riṣaṣi wala sime wala mshare haviingii vitu hivo katika maungo yake. lakini walikuwa na magomvi yeye na mke wake. na yule mke wake akawambia wale wa vita: „kama ninyi mnamtaka kumwua mume wangu, mimi ntawapa ma'arifa yake". wale wa vita wakamwuliza mke wake: „nini ma'arifa yake?" mwanamke akajibu: „mume wangu mchawi sana, nanyi wote mnajua". wakajibu: „kweli". akawambia: „mkataka kumwua, marra moja afe, tafuteni kikonyo cha mboga, mumpige, huo ndio mzio[1]) wake, marra atakufa". bassi marra wale wa vita wakatafuta kikonyo cha mboga. walipokipata, marra wakampiga yule jumbe palepale hakuvuta mguu wake, marra alikufa. na kufa kwake hakuonekana, illa marra yalivuma ṭufani, na yeye asijulikani alikokwenda. ṭufani ikampeleka ḥatta katika pango hiyo iliyoko sasa. kwa ba'aḍi ya siku wakaona katika ile pango silaḥa zake na nguo zake na kilemba chake, wakapeleka khabari watu katika mji — ya kama: „jumbe tumeona katika pango nguo zake, walakini yeye hatukumwona". wakenda watu

1) Verbot. Jeder Familienstamm hat ein bestimmtes Fleisch oder gewisse Fleischstücke oder Fische, die sämmtliche Familienangehörigen nicht essen dürfen. Der Betr. sagt z. B. mwiko wangu kidali mein Verbot ist ein Bruststück (vom Thiere zn essen). mzio hier ist dasselbe wie mwiko.

kutezama, wakaona kweli, ikasiri kuwa ndio mzimu. na ma'ana ya mzimu wameona 'ajabu ya mambo hayo ya mtu aliyekufa, naye wasimjue pahali alipokwenda. na 'ajabu ya katika mwitu huo: wenyi mzimu katti ya mwitu — walakini ndani mchanga mweupe, kama kunakwenda watu kufyagia.

na ba'adi ya siku hulia ngoma katika huo mwitu na vigelegele kama kunako 'arusi. hio ndio khabari yá mzimu wa Kolelo[1]. na majumbe, waliwo barra wote, huo mzimu wao mkubwa. mamwene na mapazi na kina Kingaru[2] wote hawaudarau mzimu huo.

1) Ort in Nguu wo der mzimu seinen Wohnsitz hat. — 2) jumben von Ukami.

# Safari yangu ya Afrika toka baḥari ya suaḥeli ḥatta baḥari ya pili

## katika safari ya bwana Graf von Götzen

ya

**ʿAbdallah bin Rashid.**

Bismillah er-raḥman er-ráḥim!

auwali ya safari yetu — ya bwana Graf Götzen na bwana Prittwitz — tulitoka na ndovu wawili na watu sitta mia wa settīn, ʿázima yetu kwenda barra. tukapandia kwa Pangani. tulipofika qaribu ya Mauwya, ndovu moja akazama katika matope. akaʿazimu bwana mkubwa Graf Götzen kuwarudisha, akaonelea, ya kama tutapatikana na taʿabu sana njiani ya hawa ndovu. wakarudishwa Tanga, na siye tukenda zetu Mauwya. tukabaqia siku kumi, kutengeza safari yetu ḥatta ikatimia.

khātima tukasafiri, tukenda Uzigua. tukaona watu wake wema sana, na ḥéshima zilizo nyingi sana. na katika biʿashara yao njema sana. mbuzi huuza kwa mikono kumi na sitta ya nguo, mbuzi aliye mwema, na unga wa mahindi chakula cha siku nne kwa upande — hapana záyidi, na kibuyu kidogo cha asali vilevile kwa upande.

khātima tulipotoka Uzigua, tukenda vilima vya Nguu, tukafika Mgera kwa mudda wa siku kumi. tulipofika Mgera, bwana Graf Götzen akasema — kama: „hapa na tufanye kambi qádiri ya siku kumi kutengeza vyakula, kwani mbele yetu kuna pori la siku kumi“. ikawa kutaakhkhari kutengeneza vyakula ndiani [1]) mudda wa siku kumi. ikawa kununua doṭi chakula cha siku kumi, na mbuzi mmoja kwa doti moja, na ñgombe moja kwa gora tatu kwao wenyewe Wanguru na Wamassai.

khātima tulipokwisha nunua vyakula, tukaondoka tukaingia katika pori la Wamassai. mudda wa siku tis'a ndipo tulipotoboa Burungwe. tukataka khabari ya vyakula, wakatujibu — ya kama: hatuna vyakula, lakini iliyo riziqi yenu mtapata, kwa sababu tumeingiliwa na nzige. ikawa kutafuta vyakula, tusipate vyakula kabisa illa unga wa mawele, kitunga kwa upande.

tukalala siku moja katika mji huo, siku ya pili tukaondoka kwenda Irangi. tulipofika Irangi, tukaona mji mkubwa mno. muna matunda mengi mno, muna mitende na mikomamanga na killa namna ya matunda. na mji huo mwenyewe Moḥammed bin 'Omari Nabehani, yeye ndiye luwali wa mji huo. tukapata ḥéshima kubwa sana, ili kumfuraḥisha bwana Graf Götzen. tukauliza sa'ari ya vyakula, wakatujibu — kama: „vyakula humu mwetu siku hizi ni 'adimu“. tukawajibu: „ḥatta kwamba ni 'adimu, twataka mtuuzie kwa uchache wake“. ikawa kutuuzia ungo wa unga wa muhogo kwa upande, na mbuzi mzuri kwa doti mbili, na mbuzi aliye ḥafifu kwa doti moja.

tukakaa mudda wa siku nne, khātima tukaondoka kwenda Uassi, khalafu Ufiome. watu wake wema, lakini ckakula ghali. khalafu tukenda Mangati, tukaona

1) njiani.

mji mkubwa sana na watu wengi sana. lakini miji yao i vilimani, na nguo zao ngozi, na vyakula vyao maharagwe na maziwa na mahindi. na sa'ari ya vyakula kwao ghali: pishi ya maharagwe kwa upande wa satini, na buyu la maziwa kwa upande, na buyu la asali kwa upande, na kuku wanne kwa upande, na mbuzi kwa doti moja.

na waṣifu wa watu wake — ṣura zao kama Wagalla. na wao si mno kuqurubiana na watu, na wakitaka fanya bi'ashara, hawaji kambini, hukaa mbali ya kambi, wakakusanyikana kikundi, watu wakenda kwao kununua vyakula kwao. lakini mtu akifanya nao bi'ashara, ataḥáżari nao sana, kwani ukighafilika kidogo — hukupokonya nguo yako, wakenda mbio.

khātima tukaondoka tukenda zetu Mburu. watu wake wema sana, na ḥéshima nyingi sana kwao, lakini vyakula kwao 'adimu.

tukaondokā kwenda zetu Nyaraza, ziwa la chumvi. twalikuwa na mtu mmoja mgonywa wa ndui, amebaqia nyuma, na mmoja anayemtunza mgonywa. wakaonana na Wandorobbo, wakampiga mgonywa wa ndui ḍarba mbili za mikuki. akapiga kelele — kama: „nauáwa". marra akaja 'askari mmoja, jina lake Ḥamisi, wakakimbia. wakaja zao mpaka kambini, akawauliza bwana mkubwa Graf Götzen khabari, iliyopita kwa watu wake na Wandorobbo. akaużika ghaya, aka'azimu kuondoa safari aṣ-ṣubuḥi ya watu wake. akabaqia yeye mwenyewe na bwana Prittwitz na bwana daktari [1]), ili kuwaotea watu hao, na 'askari wao watatu na maboi wao. wakakaa mudda wa sa'a, marra wakatokea kutafuta vitu katika kambi. marra 'askari Ḥassani Jusuf akawaona. alipowaona akampigia bwana mkubwa uruzi,

1) Doktor.

ili kufahamu bwana mkubwa, ma'ana alikuwa na mi'adi nao, alisema: „kulla awaonao mbele, ana amri kupiga uruzi“. aliposikia ṣauti ya uruzi, akafahamu, akapeleka macho, marra akawaona wakaja zao Wandorobbo ḥatta qaribu ya bwana mkubwa. marra ziliwatoka bunduqi wote Wazungu watatu, wakawapiga, wakenda mbio. wakampiga mmoja, lakini hakufa, alikuwa jeriḥi, khātima wakarudi kuandama safari. ndio khabari, iliyotupata Nyaraza, ziwa la chumvi.

khātima tukaingia katika pori la kwenda Miatu, pori lenyewe lina vilima vidogovidogo. tukatoboa Miatu, tukaona mji wake mkubwa mno, lakini wenyewe walipotuona wakatukimbia katika vilima. tukat͟hanni, kama waogopa — kumbe ni khada'a watufanyia. kwa kulla tukimwita mtu mmoja — hutukimbia.

tukenda zetu ḥatta kwa mkubwa wao, ili kutaka panga. tulipofika paḥali hapo, ikawa bwana mkubwa Graf Götzen akasimamisha safari, akasema — kama: naiṣubiri safari hapa, ma'ana watu hawa labuda wanakhada'a, wataka kutukhada'a, lakini nitatangulia mimi na 'Abdallah na Khērallah na Taufiqi na maboi wangu, tukatezame khabari zao. kama hawana vita, tutakuja itwaa safari“. akenda bwana mkubwa ḥatta mjini kwao, akataka amani. wakasema: „sisi hatuna amani, wewe Mzungu umekuja kwa vita, bassi hatuna amani nawe kabisa“. akawajibu bwana mkubwa — kama: „sisi hatukuja wala hatuna ḥaja ya vita kabisa, nimekuja kutezama miji na kupiga picha[1]) bassi“. wakamjibu: „kama kweli umekuja kwa amani, panga hapa qaribu ya mto“. akariḍia bwana Graf Götzen. kumbe vile ni khada'a wataka tufanyia! na sisi tusielewe kabisa.

khātima tukapeleka mtu mmoja kutuulizia vyakula,

---

1) engl. picture.

ili kununua. wakatujibu — ya kama: „sisi hatuji kambini kwenu, labuda nyie muje mjini kwetu“. bwana mkubwa akawajibu: „kama hamleti vyakula vya kununua, tutakuja mijini mwenu kuwapokonya. bassi tezamani khiyari yenu“. wakasema — kama: „hatuwezi kuja kambini, twaogopa“. tuka'azimu kwenda mijini kwao, tutafute vyakula. wakatoka ba'aḍi ya 'askari na wapagazi billa silaḥa, ili kuwatoa khofu. walipofika mjini kwao, wakawaona hawana silaḥa, waka'azimu washenzi kuwapokonya nguo zao; wasiriḍie. walipofanya nguvu, ikawa kuwapiga mikuki, ikawa kukimbizana wapagazi na 'askari ḥatta qaribu ya kambi. marra ile tukaona wapagazi wawili — mmoja amefumwa, na mmoja amepigwa mkuki. ikiwa wakaulizwa na bwana mkubwa: „mbona munaumia, muna khabari gani?“ wakamjibu — kama: „khabari ni kheri. tuliondoka kambini, 'ázima yetu kwenda kuhemera. tulipofika mjini mwao, wasiqaṣiri, ikawa tukiuza wakinunua. khātima yake wakatugeukia unyama, ili kutaka kutunyanganya; tusiriḍie. ikawa kutupiga, tukakimbia. 'alama yetu waiona tulivofanywa. na wengine wakali kuko, nao allahu a'alam kwa ḥali zao“.

marra bwana Graf Götzen, alipopata khabari ile, akaghaḍibika sa'a ile, akawambia 'askari wake: „antreten“, tupate wapa ażabu, watu wangu wasiqaṣiri“. marra wakajifunga. akatoka bwana Graf Götzen na bwana wa 'askari Prittwitz. bwana mkubwa akenda upande wa yamini, na bwana wa 'askari akenda upande wa shemali, ili kuwatafuta. walipoona Washenzi, kama Mzungu anakuja, wakakimbia juu ya majabali. ikiwa bwana mkubwa kutia moto majumba yao na vyakula vyao, na bwana wa 'askari każálika na katika vyakula vyao na mbuzi wao. khātima ikawa kutezama watu waliopigwa, tukaona watu saba' waliokufa na watatu

majaruḥi. ikawa bwana mkubwa kusikitika sana kwa khabari yao Wamangati waliotufanya.

akawataka mashauri wanyampara wake: „mmeonaje, tuondoe safari hapa ao tushinde?“ wakamjibu — kama: „kheri tushinde, ma'ana hawa wanatupiga, nasi lázima twataka jilipiza“. akawajibu bwana mkubwa: „nimesikia khabari yenu, si mabaya; kesho tutashinda, twendee mijini mwao — hapana buddi“.

tukalala, ḥatta aṣ-ṣubuḥi na mapema bwana mkubwa akapiga 'askari „antreten“, wakajifunga ṭayyari. akaondoka bwana wa 'askari Prittwitz na bwana daktari, Wazungu wawili, na 'askari arba' u 'asherin, ili kwenda kuwatafuta, na ba'aḍi ya wapagazi wachache. walipofika mjini mwao, hawakuona mtu, wote wamekimbia katika miji yao. ikawa kuwatafuta, wasiwaone kabisa. wakateka mbuzi wao na silaḥa zao, wakatia majumba yao moto. khātima wakareje'a kambini.

ḥatta siku ya pili tukan̄goa safari kwenda zetu. tulipofika katti njia, bwana daktari, aliyekuwa nyumä, akaona Washenzi wawili juu ya vilima, akauliza: „wale ni watu gani?“ akaambiwa — kama: „ndio waliotupiga jana“. ikawa kumpiga, ikampata mmoja katika mguu, akaanguka, mwenziwe akakimbia, isiwe mtu kumwendea.

tukenda zetu ḥatta mwanzo wa Usukuma kwa Mwera kwa Nyuma, jina la mji Uduhe. paḥali pazuri sana, na watu wake wazuri sana. ikawa sulṭani wao kumfuraḥia bwana mkubwa, wakamleteá ḥéshima iliyotama. tukataka kwao kujua sa'ari ya vyakula, tukaambiwa sa'ari yao. tukaona kama ni rakhiṣi sana. tukafuraḥiwa sana. ikawa kununua mbuzi mmoja kwa upande, na kuku saba' kwa upande wa kaniki ao satini, na njugu pishi kumi kwa upande, na maziwa buyu kubwa kwa koja tatu, za ushanga, na buyu la asali, lililo kubwa, kwa koja sitta za ushanga. na vyakula vyao ni unga wa

mtama na unga wa mhindi na kunde. na katika inchi yao haina milima, na ikinya mvua huwa na matope mengi sana.

tukakaa mjini mwao Uduhe siku mbili, ili kutengeza mitumba na sababu ya Wassukuma, waliotaka kwenda kwào, mà'ana bwana mkubwa hakutaka pita njia ya Mwanza, alitaka kupita mkono wa kulia, na Mwanza i mkono wa kushoto. khātima wakafanya shauri yeye na bwana 'askari, ili atoe mnyampara na 'askari kidogo, ili kuwapeleka mpaka mjini mwao Mwanza. safari ingine ikenda zake na bwana mkubwa ḥatta tukafika Ukoka. tukaona watu wake każālika wazuri sana, na ḥéshima iliyotama kwao, wasiqaṣiri. wakamletea bwana mkubwa ḥéshima yake, akafuraḥiwa sana. ikawa kuuliza sa'ari ya vyakula, tukaambiwa — kama: „vyakula vimo, lakini vi ghali kidogo". wakenda kwao kutafuta vyakula, tukapata kwa qiasi kitu, lakini ghali. unga wa mtama kitunga kwa mikono miwili ya Mombei[1]), na kuku wanne kwa upande, na mbuzi doti mbili. ndio khabari ya Ukoka.

khātima tukaondoka kwenda Shinyanga. każālika watu wake wema sana, na vyakula 'adimu.

khalafu tukenda Nindo kwa sulṭani jina lake Muhankira. tukaona mji wake mkubwa sana, na mwenyewe mtu mzuri sana. akapendezewa bwana Graf Götzen kushinda siku tatu kufungua mitumba yake, ili aianike, ma'ana ilipata mvua siku nyingi.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi na mapema tukenda mjini kuuliza sa'ari ya vyakula. tukaona hapana vyakula vinavotutosha. ikawa tukitafuta tukapata kidogokidogo, lakini ghali sa'ari yao; kitunga cha unga wa muhogo kwa upande, na kuku watatu kwa upande, na mbuzi doti tatu.

1) Bombey.

na mji huo auwali wa watu, wanaofanya miti nguo[1]) za kuvaa. na desturi hii yatoka kwa Waganda. namna ya watu hao, mfano wa nguo zao, wanavofanyiza, ni hiyo: kwanza hutwaa mti, jina lake muyombo, wakauchuna maganda. na khalafu yale maganda huyaweka katika jua kidogo, tenna wakayaondoa yale maganda, huyaweka mahali panapo mbau kubwa, tenna huja na nyundo wakayagonga na nyundo hatta yakawa leini kama mfano wa uzi. khalafu huleta jungu, lililo kubwa sana, ao mtungi, wakayatia maganda. wakisha huyapika sana hatta yakawiva, tenna huyawacha yakapoa moto qádiri ya siku sába' ao záyidi. na khalafu huyatwaa mle katika mtungi, huyapiga tenna kwa nyundo kubwa hatta yakawa leini. tenna hutwaa vipande wakashona, nguo imekwisha.

bassi pahali hapo tulibaqia siku tatu. tulikuwa na punda 'asherīn na watano, waliochukua mizigo. tulipofika Nindo, ikawa hawawezi kwenda tenna kwa ájili ya matope. bwana mkubwa akaonelea „ni kheri kumpa sultani wa Nindo, labuda atanipa wapagazi". akampa punda hao sultani wa Nindo, naye asiqasiri, akampa wapagazi thelathīn kumpelekea mizigo yake hattaMsalala.

khātima tukaondoka Nindo kwenda zetu Msalala. tukafika Msalala, tukaona mji wake mzuri sana. nao wakaa mapádiri ya Wafranza[2]), wasomesha watoto wa Wanyamŭesi. nao hao Wafranza wanautengeza mji wa Msalala vizuri sana billa qiasi; na majumba yao mazuri sana.

na katika mji huo sultani wao jina lake Himo, qabila yake Munyamŭesi. aliposikia huyu sultani, kama amekuja Mzungu, atoka pwani, akafurahiwa sana, akatupa héshima nyingi sana, akamwambia bwána mkubwa

1) Rindenstoffe. — 2) französische Missionare.

— kama: „mudda wa siku tatu watu wako wasinunue vyakula kabisa“. siku ya áuwali alileta malindo ya vyakula, mizigo ya watu khamsini. na siku ya pili akatuletea mizigo khamsini ya vyakula, na siku ya tatu mizigo khamso u arbaʿin. khātimá akamwambia bwana Graf Götzen: „ḥéshima yako kwangu mimi imefika, aḥsante, sasa nataka uwambie watu wako, waletee watu wangu vyakula vya kuuza, ili wanunue, maʿana wamepata posho kwangu“. akamjibu: „inshallah, vitakuja“. akamwuliza: „na vyakula vya hapa vyauzwaje?“ akamjibu — kama: „lindo la unga kwa upânde, na kunde lindo kwa upande, na mbuzi doti, mbuzi aliye mwema sana, na buyu kubwa la asali kwa upande wa kaniki, na buyu kubwa la maziwa kwa upande. ndio ṣarifa ya hapa petu, maʿana mwaka huu wametujia nzige, maʿana chakula kuwa ghali“. akamwambia: „aḥsanta sana, nimesikia maneno yako, nimefuraḥiwa sana“.

tukalala siku ya kwanza na siku ya pili na siku ya tatu, sababu bwana mkubwa Graf Götzen akashikwa na ugonywa. ikawa kutaakhkhari, ili kumngojea bwana mkubwa. tukakaa siku tisʿa katika Msalala. siku ya kumi bwana mkubwa akataka wapagazi kwa sulṭani Himu, akapata watu thalathīn, ili kumchukulia mizigo yake ḥatta Kirimbogo. wakapatana kulla mtu doti na upande ḥatta Kirimbogo.

tulipofika Kirimbogo, tukaona watu wake wema sana, lakini hawana vitu, wameshikwa na njaa. ndio khabari yake ya Kirimbogo.

hkātima tukenda Ushirombo. nao każálika ni mji wa Wafranza, mapádiri. na sulṭani ni Mnyamuesi, jina lake Mwana Ndege, mtu mmoja — ana watu wengi na mali mengi. naye ni rafiqi yao mno na Wafranza. Wafranza wameutengezā mji wake vizuri sana.

khātima tukataka khabari ya sa'ari ya vyakula, ma'ana tulisikia, kama Ushirombo kuna njaa. wakasema — kama: „ni kweli khabari muliyosikia; hapa chakula kwetu ni kunde na viazi, hapana záyidi. na sa'ari ya kunde doti, chakula cha siku kumi, na viazi upande, chakula cha siku sitta. na katika vitoweo ni ghali sana: kuku watatu kwa upande, na mbuzi mzuri kwa doti tatu, na ñgombe doti thalathīn, na chooko pishi tatu kwa doti. na ukitaka mpunga — wakutafuta pishi tatu kwa doti, labuda wapatikána; na samli kibaba kwa upande". ikawa lázima tukanunua kwa sa'ari hii kama walivotwambia.

na ṭabia' zao za watu — hawali waanawake wao kuku wala mbuzi kabisa, kwao ni mwiko, illa waanaume wao hula nyama hizo.

tukakaa kwao mudda wa siku 'asherīn, ili kungojea safari, iliyokwenda Mwanza. iliporeje'a safari yetu, tuka'azimu kusafiri. akataka bwana mkubwa wapagazi kwa sulṭani Mwana Ndege. akapata khamst'ashara, ili kumchukulia mizigo yake mpaka Ulangwa kwa sulṭani, jina lake Pembe.

tulipofika kwa sulṭani wa Ulangwa, alitufanyia ḥéshima, iliyo kubwa sana. naye ana mji mkubwa sana, na tenna mji wake maḍubūṭ sana. naye huyo sulṭani qabila yake Mnyamŭesi. akamwambia bwana mkubwa: „leo tafaḍḍali shinda hapa pangu". akamjibu — kama: „siwezi shinda kwako, ma'ana sina wapagazi". akamjibu — kama: „tafaḍḍali shinda hapa, kesho kutwa nitakupa watu". akariḍia bwana mkubwa ili kushinda, akamfanzia ḥéshima kubwa sana, tukafuraḥiwa sote pia.

na katika khabari ya vyakula katika mji wake: lindo la unga wa mawele kwa upande, na kunde pishi tatu kwa upande, na mpunga pishi tatu kwa doti. na katika vitoweo ghali sana: kuku watatu kwa upande,

na mbuzi kwa doti mbili, na n̄gombe doti thalathīn, na ndizi mikungu miwili kwa upande, na mayayi kumi kwa upande, na asali kibuyu kikubwa kwa doti moja, na maziwa kibuyu kikubwa kwa upande.

na wao watu wa mji huo watu wamoja naḍifu sana, wana qaʿida nyingi sana za pwani, na adabu nyingi sana.

khātima tukaondoka kwenda zetu Usambiro. tulipofika Usambiro, tukaona mji wake mkubwa mno, na watu wake wazuri mno. tulipokwisha fika katika mji wa Usambiro, marra sulṭani wake akatuletea ḥéshima nzuri sana, tukafuraḥiwa sana kwa ḥéshima aliyotufanyia, walakini mji wake hauna vyakula kabisa illa mhogo na kunde bassi. hapana záyidi kabisa illa ulevi wa nsoga, uko mwingi sana billa ʿidadi, si wa kuuliza.

khātima tukaondoka kwenda zetu Usuwi. tulipofika qaribu ya mji wake, tukaona kirongozi wake amekuja kutulaqi. tukaandamana ḥatta mji wake wa kwanza, una mtongi wake sulṭani wa Usuwi. tulipofika akatufanyia héshima kubwa mno. akamletea bwana mkubwa mbuzi tisʿaīn kitoweo chake na mitungi kumi ya asali. hio ndio ḥabari ya mtongi wake wa Kassusura.

tukaondoka hapa kwenda kwa mwenyewe sulṭani wake. tulipofika qaribu ya mji wake, tukaona mto wa kuvuka maji ya kiuno. tukavuka, tukenda mudda wa nuṣṣu saʿa, tukafika mjini mwake, tukaona mji wake mzuri sana. na ṣifa za mji huo una ndizi nyingi sana billa ʿidadi, ndicho chakula chao, na viazi, hawana chakula kingine. na nyama kwao nyingi mno. na kuni katika mji huo ʿadimu sana.

tukataka saʿari ya vyakula, akasema — kama: „usinunue vyakula, nitakuletea vyakula vinavyokutosha". marra ile vikaja vyakula vinavotutosha. aka-

mwambia — kama: „leo umekuja waqati ḍaʿifu, lakini kesho itakuja ḥéshima yako". tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, marra tukaona jeshi ya tujia, tukasitaʿajjabu. walipofika kambini, tukaona wanachukua vyakula vingi mno. tukaḥesabu ʿidadi ya watu, waliochukua vyakula, tukawaona watu mia u khamsīn, na waliochukua mbuzi watu mia, na waliochukua nsoga watu ʿasherini, na waliochukua mitungi ya asali watu kumi. hio ndio ḥéshima ya siku ya kwanza.

na siku ya pili akaleta mbuzi thalathīn, na mizigo settīn ya vyakula, ndizi na viazi, na mitungi mitatu ya asali. siku ya tatu akaleta mtu wake — ya kama: „kesho nitakuja kukutezama aṣ-ṣubuḥi". akamjibu — kama: „vema", kamwambia — kama: „nitafuraḥiwa, kama utakuja kunitezama".

ḥatta siku ya tatu aṣ-ṣubuḥi katika saʿa mbili tukasikia ngoma kubwa sana, tukauliza — kama: „kuna khabari gani?" wakatwambia — kama: „sulṭani anakuja hivi sasa, ili kukutezama". marra tukaona jeshi kubwa sana mbele na nyuma, na yeye mwenyewe amechukuliwa katika kiti, kinafunikwa kitambi cha zari. naye mwenyewe amevaa juba na suruali na kofia ya tunusi [1]. akaja mpaka kambini kwa bwana mkubwa, wakapana mikono, wakaulizana khabari ya pwani. akampa khabari za pwani, naye akampa khabari za barra.

akasitaʿajjabu bwana mkubwa kwa yale magoma wanayopiga, akamwuliza: „haya magoma mbona hayanyamazi? sababu yake nini?" akamjibu — kama: „hii desturi ya ufalme wetu, maʿana sulṭani akisema, asipate sikilikana na mtu, illa mwenyi ḥaja naye, mwingine asisikie ṣauti yake". tukasitaʿajjabu sana.

---

1) **Tunesischer Fez.**

na ṣifa zake sulṭani huyo: akisema na mtu — hamtezami kabisa, na akiteka [1]) — watu wote wake, waliomwandama, wanalazimiwa na kucheka na kupiga makofi [2]).

akamwambia bwana mkubwa — kama: „miye kesho naṭamaʿani kuja kutezama mji wako". akamjibu — kama: „nimesikia bwana mkubwa, nitafuraḥiwa sana utakápokuja kwangu". tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, bwana mkubwa akaʿazimu kwenda mjini kwake. akenda na ʿaskari kumi na moja. alipofika katika mji wake, wakamwambia: „kama wataka onana na sulṭani — rukhuṣa". akapita bwana mkubwa na ʿaskari wake. wakapana mikono, wakaulizana ḥali. akataka bwana mkubwa kumpiga picha, akakataa kabisa kwa khofu aliyo nayo. akisha kumṣiḥi — asiqubali kabisa.

khātima tukarudi kambini. alipofika kambini, bwana mkubwa akapeleka mtu, ili kumpa khabari — kama: „mimi, bwana mkubwa, kesho nenda zangu, nataka unipatie wapagazi ʿasherin na watano, wanichukulie mitumba yangu ḥatta mto wa Kissaki, maʿana wapagazi wangu wengi wamekimbia. bassi fanya eḥsani unipe hao watu". ilipofika khabari kwa sulṭani, marra wakaja wapagazi ʿasherin na watano, wakachukua mitumba ya bwana mkubwa ḥatta mtoni.

tukavuka mto huo, ikawa kuingia katika miji ya Kissaki, walakini miji yao midogomidogo. na vyakula vyao ndizi, na mavazi yao ngozi, wáke na waume, hapana záyidi ya mavazi illa hayo.

na saʿari ya vyakula kwao: mikungu mitatu mikubwa ya ndizi kwa upande, na mbuzi mmoja kwa upande, ndio saʿari yao.

na silaḥa zao mikuki. na ṣura zao kama Wasomali.

---

1) akicheka. — 2) in die Hände klatschen.

na katika miji yao hakuna kuni kabisa. wenyewe hupikia mavi ya ñgombe makavu na majani makavu, hapana záyidi kabisa.

ikawa tukenda katika miji yao, tukiuliza sulṭani wao, wakiwa wakitudanganya siku ḥatta siku. ḥatta ba'ada ya siku wakatupa khabari, kama sulṭani wao amejenga qaribu ya kilima cha moto, jina lake Kirunga; „bassi kama mmemtaka sulṭani wetu, wambieni wakubwa wa miji, munayopita, — kama: „twataka kirongozi wa Kirunga", ndipo mutakápomwona sulṭani wetu".

ikawa bwana wetu Graf Götzen kushika maneno yao aliyoambiwa. tukenda zetu, tukapanda vilima killa siku, ḥatta tukafika kwa mwanangwa [1]) wake. tukamtaka khabari ya sulṭani wake, „yuko wapi?" asitupe khabari kabisa. ikawa kutuficha, sababu wakaona khofu, ma'ana hawajaona mtu namna kama bwana Graf Götzen.

tukasikia khabari, kama kuna mwanangwa, jina lake Kawahehe, ndiye atakayetuonyesha. tukenda ḥatta kwake. tulipofika mjini kwake, tukaona kama sasa tunaqiḍi muradi wetu, asiqaṣiri. akatuletea vyakula mizigo saba'īn ya vyakula, na mbuzi 'asherīn, na mitungi minane ya nsoga ili ḥéshima ya bwana mkubwa. akafuraḥiwa sana.

tukauliza sa'ari ya vyakula, tukaambiwa, kama vyakula vya hapa ndizi na vyazi na nyama — hapana záyidi. na sa'ari ya vyakula tukaambiwa: mikungu sitta kwa upande, na mbuzi mmoja kwa doti. Kawahehe akasema: „na kama wataka sa'ari ya pembe hapa, ziko nyingi sana, frásila kwa doti thalathīn, frásila iliyo nzuri sana, na iliyo ḥafifu — doti khamso u 'asherin. ndio sa'ari ya hapa petu". akamjibu bwana mkubwa — kama: „sisi hatukuja kutaka pembe, tume-

1) Sultans Sohn.

kuja kutaka tezama miji na kupiga picha, ndio safari yangu. na hivi sasa nataka wapagazi, watakao kupagaza, ili kunichukulia mitumba yangu". akamjibu — ya kama: „hawa watu wangu hawawezi kuchukua mitumba, maʿana si mazoea yao Watussi kuchukua mizigo — kabisa; bassi wewe bwana mkubwa uwe raḍi sana, nachelea wasije kuitupa mizigo yako, siyo desturi". aliposikia khabari ile, bwana mkubwa akaʿazimu ili kuifungua mitumba yake, kuwapa watu wake chakula — mmoja gora moja, posho la siku tisʿaīn, maʿana kupunguza mizigo. akawapa.

siku ya tatu tukaʿazimu kuondoka kwenda zetu mto wa Mgesi. tulipofika mto wa Mgesi, tukavuka salama salimīn pia sote. tulipokwisha vuka, tukamwona mtoto wa Kigeri, sulṭani wa Ruanda, jina lake Shirangawe. hapo tulipofika — tokea Pangani ḥatta hapo miezi sitta. tulipomwona akatupa ḥéshima nyingi sana. akamwambia bwana mkubwa — kama: „tumetoka kwetu pwani siku nyingi, hatujaona mji mkubwa kama huo. na tokea tulipoingia Ruanda, twauliza mji wa baba yako, watu hawataki kutwambia; maʿana yake nini?" akasema — kama: „wao waogopa, ili wasipatikane na maḍara, lakini kama wataka uonane naye — nitaandamana nawe ḥatta kwa baba yangu, upate kumwona". akafuraḥiwa bwana mkubwa na watu wake pia kwa matamko ya Shirangawe. ikawa kuandamana naye, kwa kulla mji tukipita huenda Shirangawe na watu wake wakituletee mbuzi na vyakula vingine kwa kulla siku. ḥatta tukafika mto wa Nyavarongo, akatwambia — kama: „hapa sasa qaribu na baba yangu Kigeri".

ikawa killa siku twaqurubia ḥatta tukafika mjini mwake, tukakaa qaribu ya mji wake, tukatuma mwanawe Shirangawe — ya kama: „kamwambie baba yako, kama sisi tumefika chini ya mji wake, twataka onana

naye". akasema — kama: „nimesikia, lakini hamna rukhuṣa kupanga huku juu kwangu, pangeni hukohuko. mimi khātima nitakuja kuwatezama". aliposikia bwana mkubwa maneno yake, akaghaḍibika sana, akaona kama labuda asema, kama mimi namwogopa. marra ile akawambia ʿaskari: „antreten", tutakwenda kwake, lázima hatuna buddi, lakini wapagazi na watuṣubiri na ʿaskari kidogo". akawambia watu wake, wapigao miganda, wa kwanza ʿAbdallah na wa pili Ḥamisi: „pigeni miganda, mpite mbele, msitie khofu, mnaandamana na bwana wenu Graf Götzen, ukalie mganda ḥatta ndani ya mji wake, ndani ya ua wake". akamwingilia ndani, akamwambia waziri wake: „mwambieni sulṭani wenu, nataka onana naye, wala sina buddi kuonana naye katika waqati huo, bassi mpeni khabari".

akatoka waziri wake, ili kumpa khabari — ya kuwa: „bwana mkubwa amewáṣili hapa, ataka mwajaḥa wako hivi sasa". akamjibu — kama: „nitakuja". marra akatokea, wakapana mikono. akauliza khabari za pwani, akampa na yeye khabari za barra.

khalafu akamwuliza khabari ya kilima cha moto, akamwambia — ya kama: „kipo, lakini ki mbali sana". bwana Graf Götzen akamjibu — kama: „sina buddi na kufika, ili kuona moto huo. nataka unipatie watu kunionyesha njia ya huko". akajibu: „nimesikia, kwanza nenda kapumzike, khātima tutaonana, tuseme khabari ya kilima". akatutafutia kambi, tukapanga qaribu na mji wake. akatufanyia ḥéshima nyingi sana, akatuletea mbuzi wengi sana na vyakula vingi sana.

ḥatta siku ya tatu akaleta khabari — kama: „kesho aṣ-ṣubuḥi nitakuja kambini kwako, ili kukutezama ḥali yako". akamjibu bwana mkubwa — kama: „nimesikia, nitafuraḥiwa sana, kama kesho utakuja kwangu". tukálala ḥatta aṣ-ṣubuḥi katika saʿa tatu, tukasikia ma-

goma, tukauliza: „kuna nini?“ tukaambiwa — kama: „sulṭani Kigeri anakuja“. marra bwana mkubwa akatoka kumlaqi. wakapana mikono, wakenda ndani ya ḥema yake bwana mkubwa. wakaulizana khabari, wakapana, killa mtu akampa mwenziwe khabari, wakafuraḥi sana.

kisha bwana mkubwa akataka kwake wapagazi thalathini, ili kuchukua mizigo yake ḥatta kilima cha moto. akasema kama áuwali: „nipe zawadi za pwani, nami nitakupa zawadi za barra, na wapagazi utakao — sina buddi“. akamjibu bwana mkubwa — kama: „si desturi yetu kutoa mbele sisi áuwali, nipe wapagazi thalathini, sitaki kitu kingine kabisa. usiponifanyia hayo, sitapendezewa kabisa“. sulṭani akamjibu — kama: „nipe wewe zawadi za pwani kama wataka“. bwana mkubwa asiqubali. akaqaṣirika sulṭani, akenda zake, akasema: „usiponipa wewe kwanza — nami sikupi; tenna utarudi pwani, hufiki huko ukotakako, nitakupa watu wa kukurudisha pwani“. aliposikia bwana mkubwa, akaghaḍibika sana, akasema — kama: „usiponiletea wapagazi thalathini, nitakwenda mimi mwenyewe na ʿaskari wangu nikawakamate, yeye mwenyewe sulṭani wao apate nijua, kama mimi bwana mkubwa“.

akanyamaza. ḥatta usiku akawasha vitu vya kuwasha [1]), vina baruti, huruka juu sana, ili kuzungumza na watu wake. alipoona sulṭani moto ule, akaogopa, akathanni, kama ataka mtilia mji wake moto. marra akaleta mtu wake, ili kumwambia bwana mkubwa: „usiwashe huo moto, ukatutilie majumba yetu moto. na kama ni hao wapagazi — kesho aṣ-ṣubuḥi watakuwaṣilia, hapana buddi“. aliposikia bwana mkubwa maneno yake, akafuraḥiwa sana, akaona, kama hawa washenzi hawana ʿaqili kabisa.

1) Raketen.

tukalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, tukaona ameleta wapagazi arbaʿīn na mbuzi ʿasherīn. akafuraḥiwa bwana mkubwa, akawambia: „sasa nitawapa zawadi za pwani". akawapa zawadi za pwani. naye sulṭani Kigeri akatoa na kirongozi kutufikisha kilima cha moto.

tulipofika kilima cha moto, bwana mkubwa akasema — kama: „nataka kukipanda kutazama kilima hicho". akaʿazimu kupanda, akaondoka, akapanda tokea saʿa moja ḥatta saʿa kumi na mbili, akafika juu ya kilima. akaona visima viwili, kimoja kikubwa na kimoja kidogo, na moto wake mwingi sana. akaona ʿajabu iliyo kubwa sana. khātima akarejeʿa kuwapa watu wake khabari za kilima na kuona ʿajabu iliyo kubwa sana. na jina lake mlima huo Kirunga kwa jina la washenzi.

khātima tukaondoka kwenda Kivu, kutazama baḥari ya Kivu. tukaiona baḥari kubwa sana. tukafanya kambi mudda wa siku tatu, ili kutazama khabari iliyo hapo. tukaona watu wake waoga sana, walikuwa wakitukimbia. khātima tukawambia — kama: „siye hatuna vita na mtu, tumekuja kutazama baḥari ya Kivu". khātima wakaja katika kambi, wakituuzia vyakula. na vyakula vyao unga, na mtama, na asali, na mbuzi. na themani yake doti, chakula cha siku nane, na mbuzi moja doti. na doti yake żiraʿa nane. na asali mtungi kwa upande, na upande żiraʿa nne.

tukakaa, ḥatta siku ya tatu wakatutokea usiku, wakatupiga mishare. wakapiga mtu mmoja katika wapagazi wetu. marra tulipoona khabari ile, wakaondoka maboi ya bwana mkubwa, Wasomali, wakawapiga wakakimbia. nao ni watu waliokuja wengi mno, lakini wakakimbizwa na watu kidogo sana. tulipozinyamazisha bunduqi, tukenda kutezama, tukaona watu waliokufa watu sitta katika washenzi, na kwetu hapana mtu illa mmoja majuruḥi kwa mshare katika wapagazi.

tukakaa ḥatta aṣ-ṣubuḥi, akaondoka bwana Prittwitz kwenda kwa mkubwa wao kueleza khabari, kama hivi vita vyatoka kwake ao vyatoka kwa nani? alipofika njiani, akamwona mkubwa wao anatokea, ili kujȧ kwa bwanȧ kumwuliza khȧbari, iliyopita usiku — ya kwamba: „khabari hii iliyopita usiku — mimi sina khabari nayo yá vita vyao; illa aṣ-ṣubuḥi ndipo niliposikia. nikasema — kama, labudȧ bwana mkubwa atathanni, kama vita hivi nimevileta mimi, lakini nitakwenda mpa khabari, kwamba mimi sijui khabari hiyo. na kama amekufa mtu — haiḍuru, wao ndivo walivotaka wenyewe.

akareje'a yeye bwȧna Prittwitz na mkubwa wȧo washenzi ḥatta kambini. akampa khabari hiyo bwana mkubwa — kwambȧ: „sina khabari iliyopita jana usiku, bassi nataka uwe raḍi sana, mimi sina khabari". bwana mkubwa akamjibu: „haiḍuru, ma'ana hapana aliyekufa mtu, lakini wao wameumiȧ sana". wakapana khabari za pwani. khātima washenzi wakaondoka, marra wakaleta mbuzi watatu na mbuzi moja kwȧ bwana mkubwa. na wao wakapata bakhshishi kwa bwana mkubwȧ. ba'ada ya hayo wakaagana wakenda zao. akawambia bwana mkubwa — kama: „kesho nenda zangu kutazama mlima mwingine, nataka kirongozi kwako". akampa, tukenda zetu. nȧ hapo ndipo mwisho wa Ruanda.

tukaondoka tukenda zetu katika pori mudda wa sa'a mbili, tukafika katika mji, jina lake Uyungu. na watu wa hapo desturi yao kuchonga meno. na mavazi yao mbinda kama Banyani. na chakula chao ndizi, hapana chakula kabisa illa ndizi.

tukenda zetu, tukatafuta miji, iliyo na vyakula. tukaingia katika pori siku sitta, ndipo tulipoona vijiji vidogovidogo, wala havina watu. watu kidogo walioko, wamekimbia. wamepigwa na Wamassai. wala hamna

vyakula illa ndizi za shiddă sana — vidogovidogo. tukashikwa na hamu sană kukosa vyakula, tukauliza khabari — kama: „hiyo ndio miji gani?“ tukaambiwa: „ndio miji ya Utembe, wenyewe wameuliwa na Wamassai, hapana mtu aliyobaqia kabisa illa mmojammoja“. bwana mkubwa akaona hapana ḥila ya kufanya, illa kukimbilia miji mingine, tutakáyopata vyakulá.

na waṣifu wa inchi hiyo: muna milima mingi sana, haiḥesabiki ilivo mingi.

tukaingiá katika pori la Mwanzi mudda wa siku tatu. khātima tukawaona wenyewe Watembe. tukapata na vyakula vingi sana, lakini vyakula vyao ndizi, hapana zayidi kabisa; wala hawana mbuzi wala kuku wala kitu kingine kabisa. nao hula watu, ni watu wabaya sana. wala hawana silaḥa za chuma, illa silaḥa zao miti kufanyia mishare na mikuki, ndio silaḥa zao. tenna hawana nguo kabisa, illa nguo zao huponda miti, wakafanya nguo. na mavazi yao kama Banyani. na maneno yao kama mbwa. nao ni watu wamoja wanene sana, nao wana chale nyingi sana. mtu akija katika miji yao, haoni waanawake wao kabisa, illa waanaume. ndio khabari yao Watembe.

khātima tukataka kirongozi, kutuonyesha ndia, kulikokaa waungwana[1]). wakatupa watu wawili, walio wema. bwana mkubwa akasema — kama: „hawa watu wawili, virongozi wetu, watatangulia wao na mnyampara ʿAbdallah. na watu watatu wawe wakifanya ndia na ʿalama katika miti, nasi tutafuata ʿalama. maʿana huko mbele nasikia kuna waungwana, bassi napenda ʿAbdallah awe mbele, maʿana ni Mwʿarabu, wakimwona Waʿarabu, wenziwe, watapana khabari, ya kuwa huyu

1) waungwana „freie Leute“ werden im Innern die „Küstenleute“ genannt.

Mzungu amekuja ili kutembea na kutezama miji na kupiga picha".

akamtoa ʿAbdallah na virongozi wawili na ʿaskari watatu, wakaondoka kutangulia, ili kufanya ʿalama. siku ya pili akaondoa safari. tukaingia katika pori mudda wa siku sabaʿ, hapana miji, lakini tulikuwa tukiona ndizi kidogokidogo. ḥatta tukatoboa miji ya waungwana, ikawa furaḥa nyingi sana. wakaonana bwana Graf Götzen na mkubwa wao waungwana, aliyo katika mji huo, jina lake Senga kwa kishenzi, na kiungwana jina lake Kawareware. wakatufanyia ḥéshima nyingi sana, akafuraḥiwa sana bwana mkubwa kwa taʿabu iliyompata — nyingi sana.

na katika mji huo mna bendera ya beljiki[1]). bwana mkubwa akasema — kama: „nataka toa salamu ya hii bendera". wakamwambia — kama: „tutafuraḥiwa sana". marra bwana mkubwa akawambia ʿaskari wake: „antreten", twataka toa salamu ya bendera". wakasimama, wakapiga „feuer" mbili, salamu ya bendera.

kisha wakatuonyesha kambi ya kupanga. bwana mkubwa akasema — kama: „twataka watu wako wafanye soko mbele yako, ili wapagazi wangu wanunue, maʿana watoka katika ḥali mbaya sana". marra akaamrisha watu wa mji kufanya soko, na saʿa ileile wakafanya soko, watu wakanunua vyakula.

na beʿi yao: kuku wanne kwa doti, na wawili kwa upande, na mpunga pishi thalathini kwa doti mbili, ndio saʿari yao. lakini mbuzi ghali sana, themani yake moja doti nane ao sitta. na ndizi mikungu minane kwa doti. na saʿari ya pembe frásila doti kumi ao kumi na moja. na matumizi yao: nguo kwa wao waungwana, na washenzi matumizi yao ushanga mnene

---

1) belgische Flagge.

sana ao nguo, lakini nguo hawapendi sana kama ushanga wao.

tukapumzika katika mji huo siku tano. wakataka kutuuzia pembe. bwana Graf akasema: „sitaki pembe, mimi sikuja fanya bi'ashara, nimekuja fanya picha, na kutazama miji na watu wake, na kujua khabari za miji". tenna akawambia bwana Graf — jinsi kama: „mimi nimekuja fanya ndia, kama mwataka kwenda pwani, nimewafanyia ndia, hapana khofu, nayo ndia nzuri sana". wakajibu — kama: „tutafanya shauri na wenzetu, tutafute pembe, tupite njia hiyo, uliyopita wewe". akifuraḥiwa sana bwana mkubwa kwa maneno yao waliyosema. akawauliza — kama: „twataka fika kwa Wazungu, twasikia huko mbele kuna Wazungu, bassi twataka mtupeleke huko". wakamjibu — kama: „ni kweli, kama kuna Wazungu, lakini si kama wewe, hao qabila yao waitwa Mabeljiki, ndio qabila yao. twasikia khabari, ma'ana hatujaona ṣura zao; hatuwezi waṣifia, lakini tutawapeleka ḥatta Kirondo, ndipo panapo na mto wa Rugarawa; twasikia, kama ndipo panapo Wazungu".

khātima bwana mkubwa akasema — kama: nnataka kirongozi wa kunipeleka ḥatta Kirundu". wakampa virongozi wawili. akaondoka, ili kukimbilia hawa Wazungu, tulioambiwa. tukenda zetu, ikiwa tukapita miji midogomidogo, hamna vyakula illa kidogokidogo, ḥatta tukafika kwa Mwinyi Mzinga, ndipo tulivopata vyakula vinavotutosha. tukashinda siku mbili — chakula cha njiani, khātima tukaondoka katika mji huo.

tukaingia katika pori siku nane, hapana chakula illa mboga ya viazi, na tembere jina lake. ikawa ta'abu inatupatá sana; ikawa wapagazi killa siku wengine wakimbia, wengine hufa kwa ta'abu, iliyotupata kwa kukosa chakula. bwana mkubwa akasema — kama:

„sasa hapana shauri illa kutenda — chinsheni punda wangu, ma'ana wapagazi wangu wana njaa sana; enye wanyampara wangu, fanyeni mashauri, yafaá kwa wapagazi, mnipe khabari kwa upesi". wakaondoka wanyampara kuwataka khabari wapagazi wao. wakajibu wengine kama „twataka", wengine wakasema kama „hatutaki, tutastaḥimili, haiḍuru, ḥatta hapo siku ya pili labuda tutaona mji, ulio na vyakula, tutasitirika pia sote".

ikawa kuondoa safari kwenda zetu upesiupesi kukimbilia vyakula. mudda wa siku tatu ndipo tulipotoboa mto, jina lake Ruvuto, mto mkubwa sana, na maji yake yavuta sana. tulipokwisha vuka katika mto huo, kulla mtu hafai kwa njaa iliyompata. hapo ndipo tulipopata vyakula kidogo. na vyakula vya wenyewe ndizi, hapana vyakula vingine kabisa. tukakaa hapo siku mbili, ili kupumzika.

khalafu kwa siku ya tatu tukaondoka kwenda zetu kwa Sishenyongo. tukenda kambi mbili, tukafika ndipo tulipopata vinavotutosha. watu wote wakafuraḥiwa sana. siku ya pili tukaondoka, tukafika katika mji mwingine kw aMzee Bendera. na siku nyingine tukenda kwa Biro Mzungu. ndio mwisho wa miji ya waungwána.

ndipo tulipotoboa mto wa Rugarawa kwa mudda wa miezi kumi. tukauvuka kwa mitumbwi, tukenda upande wa pili, ndiko kulikojenga Wazungu, Mabeljiki. na jina la mji huo Stanleyfalls. ndio mwisho wa safari ya bwana Graf Götzen kwa miguu.

ikawa kwenda katika mitumbwi siku sitta ḥatta pápo Kisingitini, panapofika sitima[1]). ma'ana sitima ya mto tukakaa siku 'asherini na nne kungojea sitima. khātima ikaja sitima. tukaingia ndani kusafiri, na safari yetu mchana kutwa ḥatta mchana kutwa — tu-

1) engl. steamer.

kashuka katika mji wa Wazungu. tukapanga kambi zetu siku zote katika miji ya Wazungu. mudda wa siku khamstʿashara katika stima ndipo tulipofika katika mji moja, lakini jina lake nimelisahau. ndio mwisho wa mwendo wa sitima, kwa sababu hapo pana jabali, hapapiti sitima. nao ni mji mkubwa sana, na Wazungu wengi sana; lakini pana ʿilla kubwa sana — pana mainzi wadogowadogo huuži watu sana, na tenna maraḍi ya tumbo mengi sana. tukakaa siku tatu kupumžika, wala hapana vyakula kabisa illa muhogo wa kivundi, na muhogo mwingine kufanya vyakula kama mikate, jina lake chikwanga.

tukaondoka kwenda zetu marra ingine mudda wa siku kumi na sitta katika miji ya Wazungu na miji ya washenzi wa Congo, ḥatta tulipofika Kitambe. hapo ndipo mwisho wa mwendo wa miguu. ndipo palipo na mji mkubwa sana na magari ya moshi, na merikebu, na maduka mengi sana na vitu vizuri na rakhiṣi sana.

tukakaa siku sabaʿ, khalafu tukaondoka katika merkebu ndogo kwenda zetu Banana, kuliko na baḥari ya maji ya chumwi. mudda wa saʿa sitta tokea Kitambe ḥatta Banana, palipo na Guverneri wao wa Beljiki na balozi wa Wengereza katika mji huo. lakini mji huo wa Banana una maraḍi tele ya matumbo, na mafunza mengi katika inchi hii. ndio khabari ya mji huo.

khātima ndipo tulipoingia katika merkebu kubwa kuja zetu Unguja, na bwana mkubwa wetu Graf Götzen na bwana Prittwitz wakenda zao Ulaya. ikawa tukabaqia katika baḥari mudda wa siku khamso u ʿasherin ḥatta tukafika Unguja. katika watu sitta mia u settīn, tulioondoka pwani, tukabaqia watu mia u settīn, hapana záyidi. ndio mwisho wa safari ya bwana Graf Götzen.

# Khabari ya inchi ya Wazaramu

na

# dasturi za Wazaramu

kama zilizotungwa

na

**Mtoro bin Mwenyi Bakari.**

## mwanzo wa maneno.

mimi mwenyi kuandika maneno hayo nimezaliwa Dunda Uzaramu qaribu ya Bagamoyo. nami sikukaa sana kule illa zamani za udogo wangu. nilipokuwa mkubwa, nimekaa sana Bagamoyo, lakini marra nyingine hurudi Dunda, nikakaa miezi miwili ao mitatu, nikesha hureje'a tenna Bagamoyo. hivyo nikakaa siku zote pamoja na Wazaramu, nikasikia dasturi zao, ḥatta nikazijua zote, nyingine nimezisikia mjini, wazee wangu wamenambia na nyingine nimezisikia Dunda. na sasa nataka kuziandika zote, bassi wanaosoma maneno haya na wanaosikia, yakiwapendeza, muungu awazidishie furaḥa, awaondolee nyongo ya uchungu wa moyo.

kwanza nataka kuandika khabari za mapazi[1]), na

---

1) pazi wird in Uzaramu der Orts- oder Landes-Aelteste genannt, je nachdem demselben nur einer oder mehrere Orte gehören.

tenna amri za ḥokumu za Wazaramu za zamani na za sasa. baʻada ya hayo nitawaʻarrifu killa namna za dasturi za Wazaramu kama nnazozijua.

khabari ya inchi ya Uzaramu.

tangu zamani inchi yao Wazaramu. tokea walipoanza kuimiliki inchi hiyo katika zamani za kwanza, hakutokea mtu mwingine kuwataʻarraḍi. tangu áṣili mashamba yao hawauzi, illa hukaa wenyewe mapazi na watoto wao. na akitokea mgeni, kutaka shamba kupanga — watampa, lakini watampa shuruṭi zao yule mgeni, watamwambia: „tunakupa shamba, ulime qádiri ya nguvu zako, na kulla náfaqa panda, na matunda jamíʻi panda, illa mnazi usipande, sababu mnazi una daʻawa. wewe ukifa, wakija jamaʻa zako, watatudaʻi, watataka shamba lote, ndio sababu yake“. lakini wenyewe wanapanda minazi mingi.

zamani moja mbele ya miaka khamso u ʻasherini majumbe wa Bagamoyo walitaka kuuza shamba paḥali panakwitwa Kivumo qaribu ya Bagamoyo. wameuza — beʻi imekwisha, baqi kuandika khaṭṭi barazani kwa ḥayati[1]) shekhi Naṣur. mapazi wakapata khabari, ya kama shamba la Kivumo limeuzwa, na kesho wanakwenda kuandika khaṭṭi. mapazi wakapeleka mtu kwa shekhi Naṣur — ya kama: „khaṭṭi usiandike shamba walilouza májumbe“. nao wakajikusanya jamíʻi wote kutaka kuwapiga vita. shekhi Naṣur akasikia, ya kama mapazi wamekuja na vita, wako mashamba. akauliza shekhi Naṣur: „sababu nini?“ watu wakamjibu: „sababu shamba walilouza majumbe Kivumo“. shekhi Naṣur akatuma mtu kuweta. wakaja akawauliza: „khabari yenu nini kutaka kupigana na majumbe?“ wakajibu:

1) verstorbene.

„sisi waanaume na hawa waanawake, kwa nini kuuza mashamba billa ya shauri yetu?“ shekhi Naṣur akawapatanisha, beʿi ikavunjika.

khabari ya mapazi.

zamani sana hawakuwa wengi mapazi. Sungwi alikuwako mmoja, qabila yake Mumtonga. ḥokumu yake yalikuwa Sungwi ḥatta Benderessalama. na Yombo alikuwako mmoja, jina lake pazi Mazongera. na Dunda alikuwako mmoja, alikwitwa pazi Magubika, qabila yake Mzerekera, naye ḥokumu yake yalifika Mbweni. każalika Mbweni alikuwako mmoja, jina lake pazi Gogo la Msiga, naye alikuwa qabila yake Mzerekera, walikuwa ndugu moja[1]. lakini hao ndio mapazi maʿarufu wa zamani, sasa wamekuja wengi.

Kitopeni yuko mmoja, yeye mkubwa wa ʿomri, jina lake pazi Kwembe. na Yombo yuko mmoja jina lake pazi Mazongera. Dunda hapana pazi, amekufa mwaka jana. Usako pazi mmoja, jina lake pazi Pandukizi. Mbwawa na Tondo mapazi mawili, Mbwawa pazi Madenge na Tondo pari Ugoko wa Nyani. każalika Buma alikuwako pazi Mkungwipara, naye amekufa. Mlingotini kuna pazi mmoja jina lake Kumvi la Moto. hawo ndio mapazi, walioko sasa, lakini waliwokuwa maʿarufu — tuliotangulia kuwataja.

khabari ya pazi kutawalla.

pazi akitaka kutawala, kwanza hutaka shauri mjomba wake ao ndugu yake[2]. wakiqubali watamjibu:

---

1) maʿana mama moja baba mbalimbali. — 2) Dem pazi folgt der ältere Bruder desselben. Wenn dieser nicht will, der nächste Bruder oder der Onkel. Sind keine Brüder oder Onkel vorhanden, so wird aus dem pazi-Geschlechte der Nachbarschaft oder einem befreundeten ein pazi gewählt.

„wewe ndiwe mwenyi upazi, lakin kwanza tunataka mnoñgono[1]) wetu". ma'ana wanataka kitu kidogo awape. atatoa kama kitu alicho nacho, ikawa reale kumi ao then'ashara. huo ndio mwanzo.

wakesha watakwenda zao. nao watakuwa wakitoa khabari kwa watu, ya kama fulani anataka tawalla. ba'ada ya mwaka ataweta marra ya pili kuwapa kkabari: „mwakani mimi nataka kutawalla". watamjibu: „kama utakavo, lakin mnoñgono tumeuona, sasa tunataka mkalio[2]) wetu na 'ada zetu, sababu wewe sasa pazi, tutakwamkia, tukuvulie kofia, nawe mdogo wetu". atatoa 'ada awape.

marra watakwenda kwa mapazi, waliwo wakubwa, kupeleka khabari, ya kama fulani mwakani anataka kutawalla. nao mapazi watataka 'ada zao, watasema: „zamani alikuwa mwene viale[3]), akitwamkia sisi, na kofia akivua, sasa havui kofia, illa tutapeana mikono — lázima atupe 'ada zetu". marra watakwenda kumjibu, atatoa feḍḍa awape wapeleke kwa mapazi; na vinyogori[4]), na kina chuma[5]), na kawambwa[6]), na mwene goha[7]), na jamie'i ya mawaziri ya kipazi watapewa feḍḍa. kisha atakuja mshenga[8]), anayetoka kwa watu wa mji, waliwo wakubwa na vijana, nao watataka 'ada yao. każálika watapewa. kama hakuwapa, hawamwamkii kwa ḥéshima.

wakipata 'ada zao wote, na watu wote wamejua, watakaa ḥatta qaribu ya kutawalla, atatoa ta'arifu, ya kama mwezi każa wa każa pazi atatawalla. ḥatta siku zikawa qaribu ya kutawalla, ataanza kupika pombe

---

1) von noñgona leise flüstern, mnoñgono Geheimniss. — 2) ma'ana nataka újira wa kukalia maneno yako. — 3) Jüngling. — 4) mawaziri ya mapazi. — 5) entsprechend shaha im Suaheli. — 6) entsprechend mwenyi mkuu im Suaheli. — 7) entsprechend mwinyi im Suaheli. — 8) Bote.

nyumba zote za watu wake. ḥatta siku ya mkutano ya watu wote, siku ya kutawalla, atatiwa ndani, waje mawaziri wampige kilemba, ao humfunika kofia yenyi makucha ya simba, wamfundishe desturi ya daraja yake. wakisha kazi ile, atatoka nje barazani, panapo watu, awaamkie mapazi, walio wakubwa, na mawaziri wengine waje kumwamkia. marra watakuja watani kutaka ʿada zao, watapewa. marra watamtia katika kitanda na mjakazi mmoja, ameshika mwavuli, lakini mjakazi sherṭi awe mzalia. watamtembeza juu ya kilili killa pahali, wanakwimba kwa furaḥa, wanapiga na bunduqi. mwisho watamrudisha nyumbani kwake, ataingia ndani, hatoki nje mudda wa siku sabaʿ ao mwezi.

baʿada ya kwisha kutawalla kukaa kwake sherṭi juu ya mkeka, na huu mkeka si desturi kukunjuliwa wote, illa hukunjwa nuṣṣ bi nuṣṣ. jina lake kikuto cha pazi. mtu, asiyekuwa pazi, si desturi kukalia kikuto. każālika mtu, asiyekuwa pazi, hakalii barazani ngozi ya simba ao ya chui. mapazi wakimwona huqaṣirika sana. hii ndio khabari ya kutawalla kwake pazi.

### khabari ya pazi na jumbe katika daraja zao.

katika mkutano wa watu hao, akiwapo pazi ao mwene[1]), hukaa juu ya viti, na majumbe hutandikiwa majamvi, wakakaa chini. na katika desturi jumbe haonani kwa pazi macho kwa macho. wakionana — atakufa jumbe ao pazi. wa każālika kule Udoe ao Uzigua mwene haonani na mwekambi[2]). wakionana — atakufa mwekambi ao mwene. watu hao wanapotaka kuonana, ikawa katika barza, hufungwa pazia, pazi akiwa upande huu na jumbe akiwa upande huu. wakiwa

1) In Udoe wird der Orts- oder Landes-Aelteste mwene genannt. — 2) Der unter dem mwene in Udoe steht.

na maneno yao wakasema, walakini kuonana hawaonani. illa pazi na mwene wanaonana, na mwene na majumbe wanaonana, na pazi na mwekambi wanaonana, hao hawaḍuriani. walakini ḥaṯhṯhi[1]) hizo sana zamani walikuwa wakifanyiza. sasa wanafanyiza, walakin kwa żarau, wote wanażarauliana, sababu mambo yamekwisha.

### kuamkia kwake pazi.

kama pazi na mwene wanakaa pamoja, kwanza utamwamkia pazi na khalafu umwamkie mwene. na kumwamkia kwake pazi kwanza uvue kofia, na ukiwa na vyatu — uvue. na ukiwa na fimbo ao kisu ao sime ao bunduqi — vitu hivo vyote ukiwa umechukua, kimoja wapo[2]), lázima kuweka chini, na khalafu uende qaribu ya pazi, upige magoti useme: „simbamwene[3])“. náye ataitikia: „āāāā!“ wa każálika mwene ukataka kumwamkia — vilevile. kama umechukua silaḥa, uziondoe zote, walakini dasturi ya mwene haamkiwi na watu wengine illa na mawaziri wake na mashaha. lakini watu wengine wakenda kwa mwene, hawamwamkii, hukaa kitako bassi.

### kazi ya pazi.

kazi yáke ba'ada ya kwisha kutawalla anashika ḥokumu. mtu aliyeua ao mwizi na watu wenyi da'awa zo zote zamani yote ḥokumu yake mtu aliyeua — naye huḥokumu kuuawa. na ḥokumu ya mwizi, humlazimisha kumlipa. każálika ḥokumu ya ugoni — yule mgoni hulipa.

na kazi ya pili yake ukulima. hulima mashamba yeye na watu wake. ikawa kubwa, anaalika watu wakaja kumsa'idia. naye hupika pombe, akawakirimu na vyakula. każálika mapazi wa zamani shamba lake analo-

---

1) Grad. — 2) kikiwapo. — 3) Herr der Löwen.

lima sirkali. mtu mwenyi njaa akipita, kama kitu atakáchokiona katika shamba — rukhṣa kuchukua, si desturi kumkataza.

kaẓálika nyumba yake ukaliona kome [1]) lake, ukalichukua, ukamwonyesha mtu mwenyi feḍḍa, ya kama hili kome la pazi, nataka feḍḍa kaẓa wa kaẓa — atakupa [2]). mwenyewe akipata khabari, ya kama kome lako liko kwa fulani kwa reale kaẓa wa kaẓa, atapeleka feḍḍa, akatwae kome lake. si desturi kuqaṣirika. lakini desturi hiyo yalikuwa kwa mapazi wa zamani, walikuwa na vitu, hawa wa sasa hawawezi mambo hayo.

kaẓálika akiwa barazani pake, huchana muyaa [3]), akasuka vikapu vidogovidogo vya nyumbani mwake, maʻana kukaa hana kazi katika mikono hujiona amepooza. hiyo ndiyo kazi yake pazi.

## amri za ḥokumu za Wazaramu za zamani na za sasa.

### ḥokumu ya mwizi.

mtu mwizi akionekana kama amekwiba muhogo ao mtama, mwenyi shamba hana rukhṣa kumpiga. yule mwizi humkamata, akamfunga mikono nyuma pamoja na shina lake la muhogo, ndiwo ushá hidi wake, humpeleka kwa pazi. humwuliza: „sababu nini umekwiba?“ mwizi hujibu: „nimekwiba sababu nna njaa“. pazi humlazimisha kumlipa. iwapo anaweza kulipa, atatoa rupia mbili, kama hawezi — atafungwa. na kifungo chake huwekwa barazani mchana kutwa, ḥatta jioni humpa rukhṣa.

na iwapo amekwiba kitu kinachò themani nyingi, kaẓálika humkamata wakamfunga, na kile kitu alichokwiba, ḥatta panapo barza ya pazi. naye humlazimisha

1) langer Stock des pazi. — 2) den Stock lässt er als Pfand da. — 3) Blätter der muyaa-Palme.

ḥatta akamwona ameqirri kuwa mwizi, na dalili zote za wizi zimeonekana, tenna pazi humlazimisha kulipa kama khasara aliyokwiba. na kama hawezi kulipa, hufungwa, hutiwa gogo shingoni. na akiwa na shamba, huuzwa, kuḍaminiwa vitu alivokwiba, kupewa mwenyi kuibiwa. hii ḥokumu ya zamani.

sasa iwapo mqaidi, amelazimishwa kulipa, na kutoa hataki, mwizi na mwenyi kuibiwa na masháhidi wote ḥupelekwa na pazi katika nyumba ya serkali, wakaḥokumiwa na Mzungu. hii ndio ḥokumu ya sasa.

### ḥokumu ya kupigana.

zamani watu wakipigana, pakitokea mmoja amempiga mwenziwe ḍarba, iliyo kubwa, marra hukamatwa mwenyi kupiga, akapelekwa kunako ḥokumu. marra huulizwa: „sababu nini kumpiga mwenzio?“ naye atataja sababu ya kumpigia. na kama akikataa — ya kama „sikumpiga“, huletwa masháhidi, hawezi kusema neno. ndugu za yule aliyopigwa nao hutaka apigwe vilevile — pazi haqubali maneno yao, atamlazimisha kitu ampe yule aliyopigwa. na kama mkiwa, atamfunga katika gogo mudda wa siku saba, tenna atamfungua.

na iwapo amempiga ḍarba, iliyo kubwa, maneno hayo pazi hawezi sasa kuyafanyiza, illa humkamata aliyepiga na walioshuhudia, akawapeleka mjini katika nyumba ya shauri. lakini katika maneno madogo pazi anayo rukhṣa kuyaḥokumu. hii ndio khabari ya ḥokumu ya ugomvi.

### ḥokumu ya kufumaniana.

watu iwapo wamefumaniana mtu na mume mwenziwe katika nyumba ya mkeẉe, yule aliyefumaniwa hutaḥayyari sana yeye na mwanamke, marra watakuja

watu kuwasemea na kuwachekea. yule mume åtawakamata wote, awapeleke kwa pazi, akashitaki atamwambia: „huyu nimemfumania katika nyumba yangu yeye na mke wangu. marra atauliza masháhidi. wakapatikana, walioona mambo hayo, kuwa ḥokumu ya kipazi atalazimishwa kutoa ugoni reale then'ashara. na kama akafanyiza uqaidi kutoa feḍḍa ya ugoni — pazi atawambia: „nendeni mjini kwa bana mkubwa, akawaḥokumu maneno yenu". wakifika mjini kwa khabari ya ugoni, bana mkubwa akaona masháhidi, naye ataḥokumu kama sheri'a.

ḥokumu ya deni.

deni zao wanapokopeshana khaṭṭi zao kijiti ao mafundo. yule aliyokopa humpa yule aliyemkopesha kijiti, naye hukiweka kile kijiti kama siku atakázoagana kulipana. na kama kijiti hicho kikampotea, siku ya mudda kutimia akaṭaka feḍḍa, naye hana kijiti, feḍḍa yake imepotea, wajapokwenda kunako sheri'a, ataulizwa: „unao usháhidi?" atajibu: „umenipotea". atamwambia huyu pazi: „nenda ukatafute".

na iwapo khaṭṭi (kijiti) unayo, deni zao kulipana kwa ta'abu. siku atakáyokuja mda'i kutaka feḍḍa yake, yule anayewiwa marra atakamata jogoo la kuku, alichinshe, atahimiza chakula, atamwambia mkewe: „peleka maji chooni, akoge mgeni". marra atakwenda koga, apakuliwe chakula, wampe, ale, wakesha watazungumza, marrà atauliza: „jē, rafiqi yangu, nataka feḍḍa yangu sasa". atamjibu: „muhogo wangu bado kukauka, lakini nenda, mudda wa mwezi akesha ureje'e". naye ataondoka. na atakápoondoka, atampa vilevile jogoo, atamwambia: „chukua, rafiqi yangu, ukafanyiza kitoweo kwako, salamu shemeji[1]) nyumbani". mudda ukatimia,

---

1) eigentlich Schwager, hier ist aber die Frau des betreffenden

atakuja marra ya pili, atamfanyizia ḥeshma kupita marra ya kwanza. ataqaṣirika mwenyi feḍḍa yake, atampa maneno mazuri. kesha atampa marra nyingine kitoweo na muhogo, atamwambia: „kwa ḥeri, rafiqi yangu". watu wakimwuliza, „umempa rafiqi yako feḍḍa yake", atajibu „bado, gendá ubwere, mburi silemile", ma'ana yake „nenda ukarudi, da'awa sikukataa". Wasuaḥeli wanasema: „kaunde uje, mwamba haukaliliwi [1]". bassi atakwenda zake rafiqi yake. killa mwezi itakuwa anakwenda akirudi, ḥatta wafike kunako mashitaka. akimpa feḍda yake, da'awa imekwisha. kama hakutoa, pazi atawapeleka kunako nyumba ya shauri. hii khabari ya deni zao.

### ḥokumu ya ḍamana [2].

mtu iwapo anawiwa, na feḍḍa ya kulipa hana, mda'i anataka feḍḍa yake, hutokea rafiqi yake ao jama'a wakasema: „mpe mudda huyu, akutafutie feḍḍa yako". na yule anayewia hukataa kumpa mudda, husema: „killa siku ananisumbua, na feḍḍa yangu kunilipa hataki". watatukanana ḥatta khalafu rafiqi moja atasema: „mwache, mimi nimemḍámini, akakimbia ao akifa — feḍḍa juu yangu". yule anayewia ataqubali, atasema: „twende mbele ya pazi, akashuhudie tenna anipe kijiti". atakwenda ḥatta kwa pazi, atampa kijiti, ndio khaṭṭi yake. bassi hutokea wengine, ba'ada ameḍaminiwa, hutimiza 'áhadi, akafanya júhudi kuuza vitu vyake, vilivomo katika shamba, ḥatta apate feḍḍa alipe. lakini

---

gemeint, da man sowohl bei Bestellung von Grüssen wie bei Erkundigung nach dem Befinden derselben das Wort „Frau" vermeidet. Man sagt auch salām watoto wako oder salam nyumba yako.

1) Bessere das Boot aus und komme wieder, über eine Klippe (die das Boot zum Kentern gebracht hat) ärgert man sich nicht. — 2) Bürgschaft.

mwingine, ukamḍámini, atakuachia janga [1]), naye akimbie usimwone ma'isha yake.

kaẓálika kafala [2]) — ḥokumu ya kafala kama ḍamana, lakin ḍamana ni kumḍámini mtu na feḍḍa, akipotea mtu ukalipa, amma ḥokumu ya kafala ni kumḍámini mtu min gheri ya feḍḍa. akapotea mtu, ikawa juu yako kumtafuta, ḥatta umpate. illa iwapo amekufa, deni itakuwa juu ya mwenyi kuḍámini.

desturi ya Wazaramu ukamḍámini, ao ukamkáfili — kwao uẓia. atakufanyizia matata, mwisho wake ḥatta deni ikulázimu wewe. illa wasiwopenda matata, hao wepesi wa kulipa, ma'ana wao kufika barazani kwa mapazi ao mjini katika nyumba ya shauri hawataki, roḥo zao zinakhofu sana. hio ndio khabari ya ḍamana.

### ḥokumu ya rahani.

zamani Wazaramu yalikuwa hawana rahani illa mpwawe [3]). iwapo ametokewa na deni, ao ameua mtu, ao amefanyiza ugoni, hana feḍḍa — atajiweka mwenyewe rahani ao mpwawe, wapeane midda, naye atafute feḍḍa ya watu ḥatta aipate, akamkomboe mpwawe. lakini mtoto wake aliyezaa mwenyewe ao mtumwa wake — hao hawaweki rahani, ijapokuwa ana deni nyingi. na kama hana mpwa, na kujiweka rahani mwenyewe hawezi, akiwa na shamba, atairahanisha.

katika Zaramu zamani za kwanza mtu asiyekuwa na mpwa — huyu maskini. akiwa na ndugu mwanamke, naye ameolewa na mume, ndugu yake atajitáhidi pamoja na mumewe kutafuta dawa za hoto [1]) la uzazi,

---

1) Klage, Prozess. — 2) Bürgschaft. — 3) mpwa Neffe oder Nichte. — 4) hoto ist ein Mittel für Kinderzeugung, das der mganga besorgt. Dasselbe besteht aus Wurzeln eines Baumes, die mit einem

ma'ana yake ndugu yake apate mtoto, naye awe na mpwa. katika Zaramu mtu akiwa na fedda qádiri, akiwa na mashamba, akipata na watoto, lakini kama hakuwa na wapwa, watu hawamja'ali kitu. hokumu hizo za rahani, iwapo imetokea magomvi, moja wapo anataka kumthulumu mwenziwe, pazi huingia katika maneno hayo. na iwapo yamemshinda, huyawacha, akawambia: „nendeni mjini kwa bana mkubwa". na sirkali anakataza kuweka rahani watoto ao watumwa. akiwasikia wamewekeana rahani mtoto ao mtumwa, sirkali huwafunga wote wawili. ao marra ya kwanza humwambia yule mwenyi mtoto — humpa rukhsa ya kupata mtoto wake, lakini humwambia: „siku nyingine usifanyize khabari ya kuweka rahani mtoto". huwasámehe wote wawili. imekwisha khabari ya rahani.

### hokumu ya mwenyi kuua.

zamani za kwanza katika hokumu za mápazi, mtu iwapo ameua, marra atakamatwa, afungwe mikono nyuma, wampeleke kwa pazi. marra atamwuliza sababu ya kuua, naye atajibu, lakini majibu yake hayana njia, iwapo analázima ya kuuawa, marra ataamru watu kumfunga, wampeleke mtoni, panapo dindi, lenyi mamba wengi, marra watamtosa. ma'ana zamani killa mkhálifu hutoswa katika maji, illa mchawi, ndiye anayechomwa moto.

kažálika iwapo si mtu wa kuuawa — atafungwa,

---

Huhn, ferner chooko-Bohnen und kunde-Bohnen zusammen gekocht werden. Dann werden solche Wurzeln in heissem Wasser abgekocht und mit ugali wa mtama Hirsebrei vermengt. Beide Speisen werden gleichzeitig gegessen und zwar 7 Tage lang von Frau sowohl wie von dem Manne. Sie dürfen jedoch auch andere Speisen essen, diese gilt nur als Medicin. Die Frau muss dazu die Zeit ihrer Menstruation abwarten.

ma'ana ḥokumu ya kuuawa namna mbili. ya kwanza yule aliyeua, ba'adá ya kwisha kuua, pazi huwashauri wenyi ndugu yao, aliyeuawa — ya kama: „huyu ameua, nanyi mtakaje? auawe, ao mnataka dia?" wale wenyi ndugu, aliyeuawa, wakitaká dia — hauawi. ataamru watu kumfungá yule, aliyeua, ḥatta walete feḍḍa jama'a zake.

ao ikawa aliyeuawa mtumwa, każálika aliyeua akiwa mungwana — hauawi, illa itatoka dia themani ya yule mtumwa.

każálika kifungo cha zamani mkhálifu, aliyeua, hufungwa gogo katika shingo, na mikononi hutiwa pingu za mti, na miguuni hutiwá pingu na mti katti-katti. jina lake kifungo hicho kongora ao malinda kozi, lakini sasa tangu kujá vifungo vya sirkali, nao wameviwacha vifungo hivo. mkhálifu aliyeua, akipatikana, pazi hawezi kumweka kwake, marra atampeleka mjini katika nyumba ya shauri. imekwisha ḥokumu ya kuua.

### namna ya kurithi.

zamani mtu akifa, naye amewácha nduguze na mama na baba amewacha na mpwawe na mkewe, akiwa na mali, yatafanyizwa sehemu mbili. ya kwanza atapewa mkewe, ya pili atachukua mpwawe, lakini sehemu ya mpwa ndio kubwa. waliwobaqi mama na baba na ndugu hawapati kitu. tenna watamfanyiza yule mpwa ndiye mshauri wao, killa wakiona ḥaja waitakayo — watakwenda kwake.

lakini siku anayorithishwa yule mpwa, hujikusanya jama'a zake, wakenda barazani kwá pazi, kunako fanyizwa maneno ya urithi. ḥatta anapokwisha kurithi, huwagawia wale jama'a zake, killa mtu kwa qádiri yake.

na yule maiti akiwa ámekosa mpwa, mali atarithi

ndugu yake. każálika mtoto wa suria hapati wárithi áṣili.

lakini sasa wàtu wote wamekuwá werevu tangu ilipoingia sirkali katika Afrika, hapana mtu anayequbali kupunjwa. mwanzo wa ḥokumu watakwenda kwa pazi, iwapo mameisikia ḥokumu ya pazi wote — maneno yamekwisha. na kama hawakuisikia — watakwenda mjini. na mpwa hawaqubali arithi sasa. iwapo amekufa mtu, amewacha mtoto na ndugu, watarithi kama sheri'a ya watu wote. na mtoto wa suria sasa anapata kurithi kama mtoto wa mke. imekwisha khabari ya wárithi.

## dasturi za Wazaramu.

### dasturi ya kuzàliwa mtoto.

mwánamke siku ya kushikwa na uchungu wa uzazi, qabla hajazaa, kwanza huitwa mumewe na wazee wa yule mke kuja kumwaga mchele, apate kujifungua mkewe. naye mwanamke awapo hakujifungua upesi, bibi zake na mama zake watamwuliza: „umefanyiza neno gani nje? usitufiche sisi, twambie!" na yule mwanamke akaona ta'abu nyingi, kama amefanyiza neno, husema — ya kama: „mimi nimezini na fulani". bassi iwapo ndugu za yule mume hawakusikia maneno yale, hutolewa mtu hima, akenda kuitwa jama'a ya yule mwanamume, aliyezini naye, kuja kumwaga mchele kwa faragha. na kama pale, panapo uzazi, nduguze mume wapo, wamesikia maneno yale, itakuwa da'awa. mtoto akizaliwa — hawamlei, amekuwa mtoto wa ugoni. sababu desturi waanawake wa kizaramu, akiwa na mume, si desturi yao kuzini na mwanamume mwingine, huchelea kuzaa mtoto wa ugoni, illa mwanamke asiye mume.

kažálika yule mume iwapo amemwaga mchele, marrâ mwanamke amejifungua, juu yake mume kutafuta ubeleko. na ubeleko, unaobebewa mtoto, áṣili ni nguo, aliyokuwa akivaa yule mwanamke zamani, alipokuwa na mimba. ma'ana mwanamke akiwa na mimba, ba'ada ya miezi saba' hununuliwa shuka mwanamke, akajifunga tumboni. lakin kwanza hupika togwa la kufundishwa yule mtoto mwanamke mambo ya mimba kama atakáyoyaona. ba'ada ya kwisha kufundishwa hufungwa hiyo shuka, jina lake mkowa.

wa kažálika iwapo qaribu ya kuota meno, roḥo zao huingiwa na shughuli sana kutafuta waganga, kumfunga meno yule mtoto, yasiote vibaya, ma'ana yasitangulie meno ya juu kuota. yakitángulia meno ya juu kuota — mtoto hawamlei, watamwua ao watatafuta mtu, wanayemjua katika mji, wampe kumlea, sababu kwao si dasturi kumlea. lakin kumtoa kwake huyu mtoto sherṭi kwa taguzo [1]). hukutana wazee wa yule mwanamke na wazee wa mwanamume, wakafanyiza kitara [2]) cha sababu ya yule mtoto kutolewa kwake, na ma'ana ya kitara kuuliza khabari — amri iliyo juu ya yule mtoto. na hicho kitara huwa siku mbili ao tatu, ḥatta wote wajue, ya kama huyu mtoto anatolewa, kwa sababu ameota meno vibaya, ao amri nyingine.

tenna humchukua yule mtoto, kama hawataki kumwua, ḥatta wakapata mlezi humpa. na yule mlezi humfundisha miko [3]) yake yule mtoto, ma'ana kitu kaža

1) Zusammenkunft. — 2) = shauri. — 3) mwiko pl. miko eigentlich Löffel, hier „verbotene Speise". Jeder Familienstamm hat ein bestimmtes Fleisch oder gewisse Fleischstücke eines Thieres oder gewisse Fische, die sämmtliche Familienangehörigen nicht essen dürfen. Der betreffende sagt z. B. mwiko wangu kidali (Bruststück) oder mzio wangu mkundaji (der mkundaji-Fisch).

wa każa vibaya hali, na nyama każa wa każa hali, na kulla miko ya tangu udogo wake hatta ukubwa wake. wakesha kumfundisha yote, watamwachia mtoto kabisa, wende zao. imekwisha khabari ya mtoto kutangulia kuota meno kwa Wazaramu.

### dasturi ya kuzaliwa watoto wawili pacha.

Wazaramu watoto wawili pacha shidda kuwalea ao kuwapa watu kuwalea, roḥo zao huwa na khofu sana, lakin huwaua kwa faragha, asijue mtu illa wale makungwi [1]). kisha pale alipozalia yule mwanamke — ndipo wanapowazika. na mtu akauliza khabari ya uzazi „amejifungua ao bado", makungwi hujibu: „amejifungua, lakini watoto si riziqi, wamerudia nyumbani", ma'ana yake wamekufa.

na iwapo watawalea, sherṭi kwa dawa zilizo nyingi kufanyiziwa watoto na mamie mtu, lakin atakufa mamie mtu ao watakufa watoto. ma'ana mamie mtu anapowalea wale watoto, moyo wake umejaa khofu, na mji mzima watu wanata'ajjabu, ya kuwa fulani amezaa watoto pacha akawalea. katika inchi ya Zaramu hawapatikani sana watoto pacha.

na iwapo watawalea, vyakula vyao hutiliwa katika kitunga, hawalishiwi katika ṣaḥani ao mkungu. huo mzio wao. wafanyapo mambo kama hayo, watoto hao kukua kwao hukuwa na maraḍi, hutokewa na madonda mwili mzima.

każālika wanapokatiwa nguo, sherṭi wote wavae namna moja, si dasturi kupewa killa mtu nguo rangi namna nyingine. na wakiugua, hupelekwa wote pahali panapo njia panda kwenda kutambikiwa [2]). huja watu

1) Frauen, die der Wöchnerin bei der Geburt beistehen. — 2) tambika die Seele der Verstorbenen anrufen.

wakemba nyimbo za tambiko ya wale watoto kupata uzima. huchukua mahindi na jungu, lililo kubwa, na kuni za mpingo, wakapika kande[1]) yale mahindi. wakesha hutia hatika ungo, wakaja watu wakala. hiyo ndio tambiko yao.

na katika watoto hao mmoja akifa, na wa pili hana maʿisha. na kuzikwa kwao hawatiwi katika sanda ya bafta, sanda yao jani la mgomba ao majani ya mnyonyo. wala hawapelekwi katika maqabri ya watu wakubwa, huzikwa katika ua, iwapo amekufa kwa ʿomri wa mwaka mmoja. na kama amekufa katika kuzaliwa, huzikwa mle katika chumba alichozaliwa. hiyo ndio khabari ya watoto pacha.

namna ya kulea watoto waanaume wa Wazaramu.

watoto waanaume baʿada ya kupata miaka kumi, ḥufundishwa kutega nyavu za kuwindia nyama katika mwitu. wakijua kazi hiyo, hufundishwa kutega migono ya kuvulia samaki mtoni. kisha huoneshwa dawa za nyoka iwapo amemwuma mtu. ḥatta akapata miaka thenʿashar, hufundishwa kutaguza[2]) maneno, maʿana killa panapo kitara[3]) huchukuliwa kufundishwa wanavotaguza. maʿana hiyo taguzo kwao mfano wake kama ḥokumu. katika Zaramu mtu kama hajui kutaguza, humfanya huyu hajui ḥokumu. akijua kutaguza, tenna hushika kazi ya jembe, akenda shamba pamoja na wazee wake kuwasaʿidia kulima, sababu wao hawendi chuoni kusoma.

każālika na kumbini wanapelekwa, lakini katika hizi zama za sasa, zamani hawakuwa wakipeleka wa-

1) kande ya mahindi oder purre ya mahindi sind ganze Maiskolben, die in Wasser gekocht worden sind. — 2) = hokumu oder amua. — 3) shauri.

toto wao kumbini. na siku wanayopelekwa katika kumbi, usiku hucheza manyago, usiku kucha ḥatta aṣ-ṣubuḥi kwimba na kucheza. aṣ-ṣubuḥi ndipo wanapoṭahiriwa. lakini manyago wa kwanza wazee wao wakicheza hawana furaḥa, sababu mle katika kumbi hukaa sana qadri ya mwezi, hutokea marra nyingine wale watoto wakapata maraḍi, ndio maʿana wasiwe na furaḥa. lakin marra ya pili huchezwa manyago ya kutokea nje watoto — hayo ndio yenyi furaḥa. hufanyizwa pombe nyingi ya ʿajabu, wakaalikwa watu killa mitaa, na vyakula vingi hupikwa. bassi usiku huanza manyago ḥatta aṣ-ṣubuḥi. saʿa ya kwanza wale watoto hunyolewa nywele, na wazee wao huwanunulia mavazi yaliyo mazuri. na mtoto mwenyi jamaʿa wengi, killa mtu humletea vazi lake, ikawa kitambi ao kanzu. bassi tenna wale watoto hufunikwa ukingo wasionekane, tenna hupelekwa kwa wazee wao, na huko watu wanakwimba nyimbo, na wazee wao wanafuraḥi na kumwaga mchele katika njia na vigelegele. na wengine wanatoa mapesa kuwatunza wale wanaokwimba. hio ndio khabari ya kulea kwao watoto Wazaramu na kuwapeleka kumbini.

### khabari ya mtoto mwanamke kuwa mwari[1]).

mwanamke akiwa mwari, kwanza hupika pombe ya kupelekwa muyomboni[2]) kwenda kufundishwa mizungu[3]) na desturi za kujua koga, sababu waanawake wanapo-

---

1) mwari wird jedes junge Mädchen mit Beginn der ersten Menstruation genannt. Sie behält diesen Namen bis sie geboren hat. Dann heisst sie gewöhnlich mamiye Mtoro, etc. — 2) muyombo-Baum, unter dem ihr alle auf die Menstruation bezüglichen Regeln mitgetheilt werden. — 3) Verstand. Meist ist für Verstand jetzt das arab. Wort ʿaqili in Gebrauch, doch hört man auch häufig ana mizungu mingi er hat viel Verstand. Hiervon ist das Wort Wazungu „Europäer“ abgeleitet d. h. die Leute, welche viel Verstand besitzen.

kuwa wari, sherṭi wapewe mizungu hiyo. ba'ada ya mwaka hupikwa marra ya pili pombe, na kucheza ngoma ya muhagata siku saba'. tenna yule mtoto mwanamke hupewa mikononi mwake mwana sesere[1]), ma'ana yake mtoto wa mti akipika na akitwanga huwa naye pamoja, ma'ana akiolewa apate kuzaa. naye mwari hasemi na mtu killa siku illa bibi yake ao watoto waanawake, walio wadogo, ndiwo anawozungumza nawo. na nje hatoki kwenda ngomani wala kutembea, hukaa nyumbani mudda wa miaka miwili. na bikra yake haipotezi, illa kwa mume atakáyemwoa. akiwa nyumbani huwa na khofu kuzini, huchelea kupata mtoto wa ḥaramu.

na kuposwa kwake huposwa ndani ya nyumba aliyomo. na huyu mchumba wake humletea maṣurufu chakula na nguo na kulla tunu ḥatta atoke nje.

na kungwi lake humfundisha adabu ya kukaa na mume katika nyumba. sababu iwapo ameolewa, na yule mwanamke anafanyiza mambo, yasiyo njia, mumewe akiqaṣirika, huenda kwa kungwi lake, akamwambia „mwari wako hukumfundisha kitu". yule kungwi huqaṣirika sana. huenda kwa mwari wake, akampa maneno yaliyo mabaya, ma'ana Wazaramu, na watu walio katika mji[2]) waanawake huogopa makungwi zao kuliko wazee wao. na raḍi za makungwi zao wanapenda kuzipata. mwanamke akikosa raḍi za kungwi lake, wenziwe wote humcheka, tenna humwambia ana wazimu. naye shidda kupata mume. tussi la mwanamke, ukitaka kumqaṣiri, mwambie: „wewe msungo, hukwenda muyomboni". bassi akiwa mwanamke mwenziwe, watapigana mchana kutwa, hawishi ugomvi wao. na akiwa ameambiwa na mumewe, siku hiyo atamwacha. na

1) Puppe. — 2) d. h. die Suaheli.

ma'ana ya hili jina la msungo ni mwanamke, asiyejua maḥaba ya kuzungumza na mume, wala asiyejua mambo ya katika unyago. waanawake wa kizaramu na wengine hukaa na waume zao kwa vema kwa kuchelea kupelekwa mashitaka kwa makungwi zao. imekwisha khabari ya mtoto mwanamke kuwa mwari.

### dasturi ya kuoana kwao.

Wazaramu wakitaka mke, kwanza huenda kwa mjomba wa yule mwanamke, akampa khabari — ya kama: „mimi namtaka mpwa wako kumwoa". na yule mjomba humjibu: „vema, lakin nataka mkalio wangu wa maneno, ndipo nikujue kama wewe mkwe wangu". bassi yule mume hutoa reale moja ao mbili, akampa yule mjomba mkalio wake. tenna huenda kwa babiye mtu, akampasha khabari — ya kama: „mtoto wako ametokea mchumba anataka kumwoa". babiye mtu hujibu: „miye sina mashauri, maneno yote yako kwenu". tenna hurudi kwake yule mjomba kumsikiliza siku atakáyokuja yule mchumba. dasturi ya Wazaramu babiye mtu hana ízini juu ya mtoto wake, illa amri ya mtoto wa kizaramu killa neno juu ya wajomba zake. atakápokuja yule mchumba, atatoa feḍḍa ampe mjomba, naye ataweta ndugu zake na jama'a zake, wagawane feḍḍa. ma'ana yake dasturi ya Wazaramu mtoto hurithi kwa wajomba, kwa baba yake hapati kitu.

khalafu watamwoza yule mtoto mume. na kuoza kwao hawendi kwa mw'allim kufunga khútuba, illa huoza kwa mila yao na lugha yao, humwambia: „nnakupa mwanangu wewe, ndiwe mumewe, mkae mkisikilizane". na mume huitikia maneno yale. na 'arusi hawafanyizi karamu kupika wali na kuchinsha n̄gombe, illa hufanya pombe, wakaalika watu kuja kunywa. kaẓálika killa ngoma huja — kibende, sangara, kum-

furaḥia ʿarusi. wala hawana dasturi ya kutembeza bikra kuonesha killa mtu, illa yule mume, baʿada ya kupewa mkewe, humla bikra taratibu, kama siku anazotaka mwenyewe. illa iwapo hafai, killa siku anamtazama macho, tenna hampati baʿada ya miezi sitta, atashitaki mwanamke kwa mapazi, ya kama huyu mwanamume hafai.

na wakesha oana, hawana desturi sana ya kuwachana, hukaa miaka mingi, wakazaa watoto na wajukuu. na mumewe akifa, haolewi na mume mwingine, illa ndugu ya mumewe, ao ndugu za mumewe wawe raḍi kuolewa na mume mwingine, huko ndiko kuoana kwao Wazaramu.

### dasturi za kuachana kwao.

mwanzo wa ugomvi katika nyumba mwanamume huwa kazi ya kufanyiza kupata maṣurufu ya kumpa mwanamke kula na nguo hana, na kulima shamba hawezi. yule mwanamke huvumilia siku nyingi. akiona taʿabu sana, humwambia; „wewe mwanamume kama huniwezi niwache". na mume hukataa kumwacha, mwanamke hushitaki kwa pazi, akasema, kama ʿaibu aliyo nayo mwanamume. tenna atamwacha, lakin anapomwacha — asitokee mume marra kumwoa, itakuwa daʿawa kubwa, maʿana atasema: „huyu mwanamke asingalitaka kuachwa, illa wewe — ndiye uliyemfitini".

namna ya pili mwanamke kutaka kuachwa, akimwona mwanamume hafai, killa siku wanakula wakilala, marra atataka kuachwa. ao mwanamume ametoka kufanyiza biʿashara, amepata feḍḍa, na ile feḍḍa hamwonyeshi mkewe, killa siku anaifukia katika shimo, ao hutia katika mfuko, akajifunga kiunoni, bassi mwanamume huyo hawana siku nyingi wataachana.

na kuachana kwao kama kuoana kwao. hawendi

kwa mw'allim kuandika ṭalaqa, illa yule mwanamume, akiona użia mwingi, huenda kule kwa mjomba wake akamwambia: „mimi na mke wangu hatupatani". bassi akiweza kuwapatanisha — atawapatanisha. na kama hawezi, mwanamume atasema: „mimi mwanamke amenishinda, sasa pokea mwanao, amefika kwako". hiyo ndio ṭálaqa yao. yamekwisha maneno ya ṭálaqa.

### dasturi ya Wazaramu kama mtu amekufa.

nao wanakwenda kuzika kule mazikoni, sherṭi wende na masikitiko. ḥatta wakafika qaribu ya nyumba ya yule mtu, aliyekufiwa, huanza kulia na mkono kushika kichwani. khalafu atakuja mtu kumshika mkono, ampeleke panapo ufuo[1]), wampe kata ya maji, amwagie yule maiti maungo mazima. na kulla atakáyekuja — hufanya kama hivo, lakini sherṭi watu waliomkhuṣṣi.

na kama aliyekufa ni mtu mkubwa katika ule mji, pazi atakuja kuzika. akiwáṣili qaribu ya nyumba, huamru mazunguri[2]) kupigwa. pazi yuko mbele na mazunguri nyuma. watu wakasikia mazunguri yanalia, watu wote huzidi kulia. na hayo mazunguri hapigiwi mtu illa aliyezaliwa katika upazi.

wanapotaka kuzika watauliza: „maiti huyu hana ndugu, waliwokuja kumzika? sababu tunataka kushona sanda". killa mtu aliyechukua sanda yake atatoa, wengine huchukua doti ya bafta, wengine huchukua riale, na wengine huja na mbuzi, killa mtu kwa qádiri yake. na killa mtu husema: „hii ndio sanda yangu". wakesha ámri ile hukata sanda hushona. tenna huweka sehemu ya watu, waliwochimba qabri, na waliwochimba ufuo,

---

1) unter die Bettstelle, auf der der Tote beim Waschen ruht, wird ein Loch gegraben, in welches das Wasser abläuft. Dieses heisst ufuo. — 2) ngoma.

na watu waliwoosha maiti, wote hupewa ʿada yao. tenna humtia sandani maiti, wakenda kuzika. nao hulaza[1]) tanga siku sabaʿ.

każālika mtu anayekwenda kuzika mkwe wake, sherṭi aliye machozi yamtoke. na kama hakulia machozi kumtoka, watu humfanya yeye ndiye mchawi. na mtu anayekwenda kuzika, kama ana nywele — asinyoe kichwani, si desturi kama anakwenda tangani. akafanya mambo kama hayo, watamkamata wamwulize: „sababu ya kuja tangani kunyoa nywele? wewe ndiwe mchawi uliyemroga maiti huyu“. hiyo ndio dasturi ya kuzikana kwao Wazaramu.

## kuzikwa kwake pazi.

pazi akifa, marra hutolewa watu, wakenda kuwambia mapazi. wanapokuja killa mtu huchukua sanda yake. wanapowāṣili wale mapazi, marra huamru ngoma kupigwa, na watu kwenda kumwosha. na wale wosha, wakiingia ndani, huvua kofia. marra watakuja watani, watataka ʿada yao. wakipata watakwenda qaburini kuchimba qaburi. wataamrishwa watu kushona sanda, na wanaposhona — sherṭi wapige ngoma ya mazunguri. każālika maiti akichukuliwa kupelekwa qaburini, lakini waqati huo ghāzia nyingi. magoma yanalia na watu wanalia, na watani wanafanyiza kelele zao, siwa na mazumari yanalia hatta qaburini.

lakini akiwa na mke, waqti wa jeneza linapotoka, huja mtu mwanamke akambeba yule mke wake ḥatta panapo mlango, lilipowekwa lile jeneza. tenna yule mke husema: „buriani, mume wangu“. lakini akiona lile jeneza ya mumewe hulia sana. marra hurudishwa,

1) Causatif von lala.

vilevile amebebwa, na jeneza likachukuliwa kwenda qaburini.

wakesha zika, atakuja kibirikizi kuuliza khabari ya tanga. likiwapo pazi atajibu, naye kibirikizi atawambia watu wote, ya kama usiku pana tanga. wanaolala tanga vijana na waanawake. na tanga lao hawalali juu ya vitanda, wanalala chini tangu siku aliyekufa ḥatta siku ya kuondoka tanga. nao hawajui kusoma khítima ya kuondolea tanga, illa waliwofuata mażehebi ya kiislamu. mapazi wanalala katika nyumba zao, illa wanakuja aṣ-ṣubuḥi kuamkia na siku ya karamu.

baʿada ya mwaka huenda qaburini kujenga panga. na hilo panga huchonga mabao, wakaweka mwanzo wa qabri ḥatta mwisho — ndilo panga. lakini siku ya kwenda kusimika hilo panga hufanya karamu.

### khabari ya kuhani kwao.

wanapokwenda kumhani mwenzao, aliyefiwa, hawavai nguo zilizo nzuri, wala hawapakai mafuta. każálika huchukua killa mtu qádiri ya kitu alicho nacho, tangu feḍḍa hatta náfaqa, humletea yule mfiwa. nao huanza vilio tangu njiani, na waliwo nyumbani wakisikia vilio — nao hulia. tenna huja mtu na baquli la maji kuwafuta machozi na kuwabembeleza wasizidi kulia. kisha humpeleka panapo qaburi kumwonyesha.

### dasturi nyingine baʿada ya kuzika.

każálika mashambizo[1]) aliyooshewa yule maiti — hugawana, wakapewa jamaʿa zake wa kuumeni na wa

1) Sobald jemand gestorben, wird er mit neuen Kleidern (Tüchern) bekleidet, die mashambizo genannt werden. Diese behält die Leiche bis nach der Waschung an. Alsdann wird er mit sanda „den Leichentüchern“ bekleidet.

kukeni, illa mali yake na mashamba hurithi mpwawe. lakini desturi hiyo yalikuwa zamani ya kurithi mpwa. na waliwoshika mażehebi ya kiislamu, killa mwaka humsomea khítima, na kupika wali, wakala watu. na walioshika mażehebi yao, hufanyiza pombe killa mwaka. na mṣiba wao mudda wa mwaka ndipo wanapokwisha. khaṣṣa ikawa mke amefiwa na mumewe, ao mume amefiwa na mkewe — mwaka mzima halimi wala hasafiri. hutumia vyakula vyake, vikesha — jama'a zake humsa'idia kumpa ḥatta atakápolima.

### mila ya mizimu na khabari za uganga na za uchawi kwa Wazaramu.

wao hawana dini, illa wameshika mila ya mzimu na tambiko. mtu akiwa hawezi, humwambia: „wewe unauguzwa na mizimu ya wazee wako, siku nyingi hujatambika". bassi hufanyiza pombe, akaweta watu, wakamtambikia tambiko ya gombo. hiyo tambiko kubwa ya Wazaramu. husema katika ile tambiko — ya kama: „ninyi mmetangulia qaburini na huyu kijana hana uzima. sasa amekwenga pombe, kukumbuka majina yenu. sasa kwa fáḍila zenu, kama ninyi ndivo mnaomwuguza, tambiko igone, apate uzima".

na kama hakupona kwa ile tambiko, hutafuta mganga akaja kutezamia. tenna mganga atabashiri — ya kama: „wewe umerogwa", ao wenyi ḥosuda wanakwambia „unapata sana", ao „mkeo kuna mtu anamtaka, naye hampati, anataka kukuua". bassi yule mgonywá huuliza: „mwisho wake nini"? humjibu: „tafuta mtu akuchomoe, vitolewe vitu vilivyo ndani ya mwili". yule mgonywa hujibu: „mtambua ndwele [1]) ndiye mganga". tenna yule mganga atafungua mkoba wake, atoe chuku [2]),

1) Krankheit. — 2) Schröpfhorn.

wembe na mavumba, akesha atamchansha, amwumike, khalafu itatoka damu katika mwili. ndani yake itakuwa na vunge la nywele, ao litatoka jino la bin Adam, ao shindano na vitu vingine. bassi yule mgonywa akiona mambo yale yametoka katika mwili wake, atataʿajjabu sana. tenna mganga atamwambia: „umeona vitu vilivotaka kukuua“? naye ataṣadiqi kweli. baʿada ya siku haba atakuwa mzima.

na kama atakufa — watamzika, lakin baʿada ya kwisha kuzika watakwenda kwa mganga mwingine, jina lake mpiga mbizi [1]), watachukua na ushanga mweupe kumpelekea yule mganga. naye atakuwa katika inchi nyingine. bassi wakifika kwa yule mganga, hawatamwambia, ya kama sisi tumefiwa tunakotoka, watampa ule ushanga waliochukua, kisha watakwenda kulala wote. maʿana huo ushanga ndio njozi [2]) zake, wanawita kiñgalu. ḥatta aṣ-ṣubuḥi watakwenda kumwamkia mganga, tenna watampa khabari — ya kama: „sisi tumekuja kutezamia kwako“. yule mganga atatoa kiko chake, atie tumbako na mavumba avute. khalafu baʿada ya kwisha kuvuta, atatoa khabari ya uganga wake, atawambia: „ninyi kweli kwangu mmekuja kutaka kutezamia“. kwanza atawapa khabari ya mwanzo wa safari yao, walivotoka katika mji wao, na mambo waliyoyakuta njiani. atasema yule mganga, kama wamekutana mtu mmoja njiani — atawambia, na kama wamekuta nyoka njiani — atawambia, kama kitu walichokiona — atawapa khabari. nao wataitikia „táile“ [3]). khalafu atawabashiria — ya kama: „mnakotoka — kwenu, mmefiwa na mwanamume. kama mwekundu

1) mbizi eine kleine Schelle. — 2) Traum, ndozi im kiamu. — 3) suah. = kweli, jedoch wird táile nur zum mganga gesagt, um ihn zu erfreuen, wenn er seine Sache richtig gemacht und man mit ihm zufrieden ist — táile mganga.

atawambia. nao wataitikia watasema: „kweli“. tenna atawapa sababu ya maiti kufa kwake na ugonywa aliougua. na kama amekufa kwa uchawi atasema: „ndugu yenu ameuawa na mkewe, na sababu mwanamke hamtaki mwanamume, ao sababu nyingine. kama yeye mwanamke ndiye aliyemwua nafsi yake — atawambia, ao amepewa na mtu mwingine uchawi kumletea katika chakula — yote atayasema, ma'ana sherṭi ajue bayana zote yule mganga. nao wenyewe waqubali yote, hapo ndipo watakapo kumqirri, ya kama anajua kutezamia.

tenna wakirudi, iwapo mkewe ndiye aliyemwua ao mtu mwingine, watapeleka maneno kwao — ya kama: „ndugu yenu ametuulia ndugu yetu“. nduguze watauliza: „kwa dalili gani“? watatoa khabari kama khabari iliyotoka kwa mganga. ikawa thábiti ndio aliyoua — hawana maneno. iwapo ndio mkewe aliyomwua — naye watamwua.

na kuua kwao hawaui kwa bunduqi ao kwa kisu. kwanza humfunga kamba yule mchawi, wakamwuliza: „ba'ada ya huyu nani mwingine umeua“? naye hukataa. tenna hukata kuni za mkuruti, kisha wakamchukua nje ya mji yule mchawi, tenna zile kuni huzipanga, naye wakamtia kattikatti ya kuni. wakesha wakamchoma moto, tenna ataungua ḥatta moto ukafika qaribu ya kiunoni, husema mwenyewe kama watu aliowaua. na kama uchawi wake anao mwenyewe — atasema: „uchawi wangu sikumpa mtu“. na kama ana mtu mwingine amempa, atasema: „mwanafunzi wangu fulani“.

na huo uchawi namna nyingi. kuna mwingine wa kiume, mwingine wa kike. lakini uchawi wa kike mbaya. wanauficha katika matako yao. mwanamke aliye mchawi, akitaka kumroga mtu, hutwaa punje ya mahindi ao ya mtama, zamani anapoingia katika ḥeḍi

ule muhindi, huutia katika tundu yake ya uchi, akachanganya na dawa zake nyingine katika chakula, akampa mumewe ao mtu mwingine, humwambia: „kula pekeyako“. bassi yule mtu atakula, akiondoka hapo — mgonywa, hana siku nyingi atakufa. na uchawi huo jina lake maḥema. ao huvimba tumbo mfano wa bunju [1]), kama mwanamke mwenyi mimba, lakini hawi na maʿisha — atakufa. labda apate waganga, wanaojua sana pale alipokula, marra wamfanyizie dawa.

### mifano ya nywele zao Wazaramu.

nywele zao wanasuka waȧnaume na waanawake, lakini huzidia udongo mwekundu na mafuta ya nyonyo, ndipo wanapozisuka. na wanaosuka waanaume waliwo vijana na waanawake vijana, lakini wazee hawasuki wananyoa. na kusuka kwao kàma mfano wa punje za muhindi. na wanapokwisha kusuka, hufunga kitambaa juu ya kichwa, kilicho chekundu, kuzuia zile nywele, zisipate mchanga ao vumbi. nazo wanazita mburunge ao kikonge. lakini wanaofanyiza mambo hayo, ni wale waliwoshika mażehebi yao, wasiwokwenda kumbini, wala wasiwoingia katika njia ya Uislamu, maʿana hio ndio ʿalama yao. watu wote wakiwaona namna hiyo katika inchi ya Zaramu, killa mtu atajua, huyu amekataa kwenda kumbini. tenna hayumo katika njia ya Uislamu. hio ndio namna ya nywele zao Wazaramu.

### meno yao ya Wazaramu.

hawayachongi — huyawacha kama yanavoota. lakini huyasukua meno yao sana na mswaki. na mswaki ni mti, katika matawi ya mti hukata vijiti, hufanya miswaki, sababu miswaki hiyo ina kiini kizuri. amma

1) dicker runder Fisch.

wengine hutwaa matawi ya mchikichi, wakafanya mswaki, lakini si sana — kwa kukosa ule mswaki nafsi yake.

nguo zao za wäanaume na waanawake.

waanaume wanavaa vitambi, watu wanaojiweza, kitambi barawaji ao kitambi kareati. na wasiojiweza wanavaa shuka moja na kanzu, hawana kofia, illa watu, waliwo wakubwa, huvaa mavazi ya kámili na kofia za alfia [1]).

kažálika waanawake nguo zao mno huvaa kaniki ao kitambi. nao ni katika wanaojiweza, waume zao [2]) hununua vitambi, vilivo vikubwa, kimoja chini na kimoja cha kujitanda. hawavai ukaya, illa wanajifunika ushungi [3]). na wengine huvaa kaniki moja bass na upande wa kujitanda. wengine hujifunga nguo moja kiunoni ḥatta miguuni, kifuani hawana kitu. hayo ndio mazoea yao, anachelea maziwa yake kuanguka. kažálika waanaume, waliwo watu wazima, hupenda kuvaa kunguru [4]), ao shuka ya matamvua [5]) ya kibarawa, hujitupia mabegani wanapotembea. imekwisha khabari ya mavazi yao Wazaramu.

khabari ya nyumba zao.

nyumba zao wanapotaka kujenga, kwanza hukata miti ya mkuruti, sababu migumu sana. wakesha hukata pau [6]) za kufungia mapaa, tenna hukata fito za kufungia viwambaza vya mbele na vya nyuma. marra hureje'a tenna mwituni kuchuna kamba za kufungia. vinapokwisha tumia vitu hivo, marra hupima kiwanja, wakachimba mashimo yote ya nyumba, tenna hutia nguzo za mbele katika baraza, hufunga viwambaza vya mbele na vya nyuma.

1) Jumben-Mützen. — 2) neben waume wao. — 3) Tuch über dem Kopf zu tragen, so dass nur das Gesicht frei ist. — 4) grosses carriertes Tuch. — 5) Fransen. — 6) upau pl. pau Dachbalken.

marra hukata vyumba, wakakata na kumbi zote mbili. linapokwisha boma [1]) huzimika nguzo za katti, ndizo za kusimamishia mwamba [2]) wa kufungia paa. na nyumba zao hujenga za mgongo [3]). wao si mno nyumba za mapáa manne. na baraza zao hawajengi zikainuka, mtu anayetaka kuingia ndani ya nyumba sherṭi ainame sana. illa wengine hujenga nyumba yenyi kirubu [4]) kikubwa, na kirubu chake huweza kuingia wima barazani. na ua hawajengi, illa wakitaka hufanyiza ukomea mdogo wa kogea na kwendea ḥajá ndogo.

nyumba inapokwisha, wakitaka manyasi ya kuezekea, każálika wanapotaka kukandika — huwambia wenziwe — ya kama: „siku każa wá każa mimi nataka nyasi na udongo kukandikia nyumba yangu". nao humsikia amri yake, huja kumsá'idia. wakesha kazi ile, huwapa karamu yao. hii khabari ya majengo yao.

### khabari ya miji yao.

miji yào hawajengi katika mwitu, wao wanapenda paḥali palipo qaribu ya maji, ndipo wanapojengea miji yao, lakin sherṭi kwa zindiko [5]) la khaṭari ya kulla mnyama tangu nyoka ḥatta simba. wala hawajengi boma katika miji yao, na nyumba zao hawajengi zikashikana. ukawa mji mmoja, killa paḥali hutokea zi-

---

1) Holzgerüst des Hauses ohne Dach. — 2) Tragebalken, deren es gewöhnlich 5 im Hause giebt. — 3) Haus mit Dach nach vorn und hinten nur, nicht auch nach den Seiten. Ersteres auch nyumba ya mcheche genannt, während ein Haus mit Seitendach nyumba ya mapaa manne heisst. — 4) Entfernung von der Erde bis zum Dach d. h. Stockwerk, da die Häuser alle einstöckig sind = arab. ghorfa. — 5) Schutzmittel in Gestalt eines Steines, den sie mit der dazu nöthigen dawa zum Schutz gegen wilde Thiere am Eingang des Dorfes an einem Kreuzweg eingraben, so dass er aber zu sehen ist. Oder sie nehmen an Stelle des Steines eine Holzkeule mit der Nachbildung eines menschlichen Gesichtes.

kạwa nyumba kumi na pengine tano, lakini jina la mji hujulikana yule mkubwa.

kaẓálika katika miji yao kifuu cha nazi mzio mkubwa, hakitiwi katika jiko kupikiwa, sababu ya zindiko lao walilozindikia simba na nyoka. kaẓálika katika miji yao hawaweki chuguu kama Wadoe.

wengine nyumba zao wanajenga qaribu ya kivuko katika mto. huwa na kàmba na ngogo [1]) wengi, hufanyiza vimvaba [2]) vya kuvulia kamba, wakafanya kitoweo. ao huweka mtumbwi, mtu akipita kutaka kuvuka, humpa pesa moja, ao kama amechukua chumvi, humpa kidogo. lakini pana ta'abu ya mbu pale panapo kivuko waqti wa masika, mtu mwingine hawezi kulala. na mvua zinapokuwa nyingi, mto hujaa ḥatta nyumba zao huelea, zikawa juu kwa juu. ào marra nyingine maji yakiwa na nguvu, huzichukua zile nyumba, na watu wakafa. lakini wanajenga kwa 'aqili na ḥáẓari ya maji ya masika.

kaẓálika hapo qaribu ya mto wanapapenda, kwa sababu ya mashamba ya mpunga na mahindi yanastawi. lakini waqti wa kuamia ndege — sherṭi juu ya madungu [3]). wakiamia — chini mamba anawangoja, ma'aná hutoka kàtika mto, akaja inchi kavu maqṣudi kungoja watu, watakáoshuka juu ya madungu awakamate. na usiku hutoka viboko katika mto kwa wingi kuja juu ya mashamba kutafuta vyakula, nao hukaa katti ya njia kungojea watu, wanaopita, huwakata na meno pande mbili. ndiwo u'ádui wao, lakini juu ya hayo Wazaramu wamependa kufanyiza mji qaribu ya mto, kwa sababu hufuata manfa'a hayo tuliyoyasema. hii khabari ya miji yao.

---

1) kleiner Fisch. — 2) Reuse. — 3) Gestell auf 4 Stangen ruhend, oben ein Platz zum Sitzen oder Stehen.

**kazi ya waanaume na kazi ya waanawake.**

katika Zaramu waanaume kazi zao huchimba sandarusi. hupatikana kwa ta'abu sana, ma'ana huchimba mashimo kwa majembe. na paḥali panapopatikana hiyo sandarusi — inchi yake kavu sana, wanapofukua kwa mikono yao — kucha zote huwakatika. nayo huichimba waqti wa jua, zamani za masika haipatikani.

na wengine hugonga mpira. nao mpira ta'abu kuupata. ma'ana mpira mti, kwanza huukatakata ule mti, ukatoka utomvu, ukavuja utomvu ḥatta ukesha. tenna huutoa ule utomvu, wakaviringa katika matumbo yao ao mikononi. mudda wa siku kumi ao záyidi wamo katika mwitu, wanagonga mpira, ḥatta vikanda vyao killa mtu vijae.

na waanaume wengine kazi zao kujenga majumba, na wengine hukata miti wakiuza, wengine hutafuta kamba mwituni, illa wazee, wasiwo nguvu, husuka vitanga[1]) na vikapu na majamvi. na wengine kazi zao huchonga ngoma za madogori na muhágata na zumari na vijiko na pawa.

kažálika wengine huchukua mkoba wa dawa, akipita killa panapo mgonywa — humwita, akafanyiza dawa zake, kiisha humpa kitu kidogo akenda zake. hii kazi ya waanaume.

kazi ya waanawake: aṣ-ṣubuḥi akiamka, kwanza hushika ufyagio, akafyagia nyumba yake tangu ndani ḥatta uanja. akisha huosha vyungu na mikungu na mitungi, marra huenda kisimani kuteka maji, akajaza mitungi yote tangu maji ya kunywa ḥatta maji ya koga. akisha kazi hiyo, hushika kazi nyingine, hutwaa kanda la muhogo, akatwanga unga, akauweka katika vikapu,

---

1) runde Matte, die als Unterlage für Getreide dient oder auch als Tablett beim Essen gebraucht wird.

ukawa ṭayyari. marra huenda mwituni kutafuta kuni. akirudi kunako kuni, huenda shamba kuchuma mboga ya kufanya kitoweo. kisha huichambua akaipika. na iwapo mfinanzi, ataponda udongo, afinange vyungu na mitungi. na kama msusi, atasuka mkeka, lakin si mno waanawake wa kizaramu kusuka mikeka.

na wengine kazi yao kuumika [1]) waanawake wenzao. na namna ya kuumika mtu, humchansha chale mbili, akaleta chuku, akamwumika pale alipomchansha, ma'ana ndani ya chuku huwa na tundu juu, akainyonya, na damu ya mtu inakuja. huyacha ile chuku mudda wa nuṣṣu sa'a, kiska huzibua.

na wengine wana kazi ya kuzalisha, lakini wenyi kazi ya kuzalisha waanawake wäzee, sababu wanasema, mwanamke akiwa kijana akizalisha, macho yake huḥaribika hima kwa kutezama kunga, ma'ana ya kunga damu. hii ndio kazi za waanawake.

### kulima kwao Wazaramu.

Wazaramu hulimia jembe na mundu. jembe ndilo linalolima, na mundu kazi yake unakata masiki [2]). na ba'ada ya kwisha kulima shamba, likawa jeupe, hupanda muhogo na mbazi na kunde pamoja na maboga, każálika chooko na mahindi. lakini muhogo unakawa sana kupatikana rizqi yake, lakini chooko na mahindi na vingine, tulivotangulia kuvitaja, havina siku nyingi. hivo ndivo vyakula vyepesi kuota, ba'ada ya siku khamsini wanaweza kuvila, lakini muhogo sherṭi miezi sitta. na mbegu [3]) yao kubwa ya ukulima muhogo, lakini mtama na mahindi wanapenda sababu ya kuuza. na mashamba yao hawalimii mbali na miji, illa nyuma

---

1) schröpfen. — 2) siki pl. mas. Wurzelrest, Gestrüpp. — 3) Ertrag.

ya nyumba, ndiko kunako shamba lake. sababu akilimia mbali, hapati kitu kwa wizi, waliwo wengi. lakini juu ya hayo shamba kuwa qaribu ya nyumba hawawachi kwiba. zamani mwaka juzi, njaa ilipokuwa nyingi, wameuawa watu wengi Zaramu katika mashamba, na wengine hupigwa mishare, wasiweze kuondoka, wakaja kukamatwa na vikapu vya muhogo.

namna ya mavuno yao.

ba'ada ya miezi sitta muhogo unapokuwa mkubwa, huenda shamba wakaung̃oa. tenna wakauanika juani mudda wa siku tano, hushona makanda wakautia, mwingine huweka matumizi yao. każálika kunde na chooko na mbaazi vilevile huzitia katika makanda, lakini mbaazi huzipika kwanza, tenna wakázianika, zisioze, ndipo wanapozitia katika makanda, ma'ana huzitumia mudda wa mwaka, huzifanyiza chakula ao kitoweo wanapokikosa.

mtama wanapouvuna, wanakata mabua yake, kisha huuwacha siku tano ao sitta katika mashamba ḥatta ukakauka. tenna huenda na makapu wakautia, wakaupeleka majumbani, wakauputa ḥatta ukawa ṣafi. tenna huutia katika vikanda.

illa mahindi wanayavuna namna mbali. ba'ada ya kutoka shamba yale mahindi huyafunga kosa [1]) qádiri zitakázotokea. kisha huzifunga zile kosa juu ya mwamba wa nyumba palipo qaribu na moto, ma'ana ule moshi ukipata katika yale mahindi hayaọzi.

każálika vyakula vikawa vingi zamani za mavuno, hualika watu kwenda kumsa'idia kuvuna. na vyakula vipya hawali, illa kwa mavumba, sababu Wazaramu wengi wana pepo wa kinyamkera. akila billa ya ma-

1) Bund von 60 Maiskolben.

vumba, atashikwa na ḥoma, usiku pepo wake atapanda kichwani, apige kelele nyingi sana, ḥatta aje fundi wake, alete dawa ampe, ndipo makelele yatakápokwisha.

ao hujengea kibanda cha kinyamkera zamani za mavuno, hupika kijungu cha wali, wakapeleka njia panda, wakaweka kile kijungu na wali, wakenda zao.

## vyakula vyao.

wanakula muhogo, huutwanga katika kinu, wakauchunga unga, tenna huusonga ugali. na kitoweo ni huo muhogo. ma'ana majani yanayotoka katika muhogo hufanyiza mboga ya kisamvu, wakaipika wakatowea ugali. Wazaramu hawapendi chakula kingine kushinda ugali wa muhogo. ma'ana wengine hulima muhogo ukawa haukustawi ule muhogo, na nyumbani mwake mna mpunga, atatoa mpunga ao mtama, akabadili na muhogo. ma'ana wali wa mpunga ao mtama Wazaramu wakila, hawauoni tamu kuliko ugali wa muhogo kwa nguru ao kwa samaki wa maji baridi ndohe ao pere ao samaki wengine wa maji baridi.

namna ya pili ya chakula cho muhogo, huutokosa muhogo mbichi pamoja na mbaazi. lakini chakula hicho kifungua kinywa [1]) ao anaporudi shamba. kaźálika nao hawali ndani ya nyumba, chakula hukitoa barazani, killa mtu, atakáyepita, akiwa na njaa, huja akala. na mgeni akitokea kwao, wakimwona hana kitu cha kutumia, hapo atakápofikia, atakula chakula ḥatta siku atakázoondoka hawamwambii tunataka kitu kaźa wa kaźa. na iwapo ndio kwanza wanavuna, na mgeni anakwenda zake, watampa qádiri ya vitu wanavovuna. ukiwa mpunga ao mtama ao muhogo — muradi haondoki mikono mitupu.

1) erstes Frühstück.

namna ya pombe na togwa.

pombe yao namna wanavopika: kwanza huroweka[1]) mtama mudda wa siku saba' ḥatta ukatoa miche[2]) ule mtama. ba'ada ya siku saba' huutoa kátika maji, wakautwanga, wakauchunga unga. wakisha hutwanga muhogo, wakachunga unga, marra waanaume huenda mwituni kukata kuni, kuwaletea waanawake. ḥatta aṣ-ṣubuḥi huanza kupika pombe. na mwanzo wao huteleka mitungi jikoni na maji, ḥatta yale maji yakawa moto. tenna hutia unga wa muhogo katika yale maji, ba'ada yake hukoroga[3]) mchana kutwa, ḥatta ule unga na maji uive. tenna huipua, wakawacha ikapoa ḥatta aṣ-ṣubuḥi, hutia unga wa mtama, wakaipika marra ya pili, ḥatta ule unga wa mtama uive. tenna huipua marra ya pili, wakaiwacha mudda wa siku mbili ikapoa. ḥatta siku yake huja na kamo[4]) za kuchujia[5]) makapi ya ule unga wa muhogo pamoja na mtama. bassi huikamua ḥatta ikawa ṣafi. lakin siku ya kwanza kukamua, wanapokunywa hawaipendi, ma'ana imekuwa baridi kama mfano wa togwa, illa siku ya tano na siku ya sitta wanapokunywa marra huwalevya, huwa kali sana.

kaẑálika khabari ya togwa inapikwa kama pombe, lakini togwa halilevi. kwanza hutwanga kimea, na kimea ma'ana yake ni huo mtama uliowekwa kama khabari ya maneno ya pombe, lakin togwa hupikwa mtama mtupu pasipo unga wa muhogo. kwanza hupika chēnga[6]) za kile kimea, tenna huipua, wakawacha ḥatta ukapoa. usiku hutia kimea, unga kidogo, kàtika lile togwa. kisha wakafunika, likalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, wa-

1) nass machen, anfeuchten. — 2) mche Keim. — 3) umrühren. — 4) Sieb. — 5) durchseien. — 6) die harten Körner, die beim Mahlen übrig geblieben sind.

kanywa huwa baridi, tenna li tamu sana. wanaokunywa pombe, togwa hawalipendi, sababu li tamu mno. hii ndio khabari ya pombe pamoja na togwa.

### silaḥa zao.

wanashika mishare na nyuta tangu zamani, hawajui silaḥa nyingine. illa sasa zilipoingia bunduqi, nao wanashika, lakini si mno kutumia kwao. nayo wanaitumia na sumu hiyo mishare. kaẓālika mikuki wanashika, lakini hawawezi kuitumia katika mapigano, illa watu wȧwinda, wanaowinda viboko, ndiwo wanawojua silaḥa ya mikuki.

silaḥa nyingine ni kisu. hufanyiza kisu, kilicho kirefu, ncha yake nyembamba, hujifunga vyunoni. na vingine namuna kama hivo, lakini hivyo kazi yake huulia mamba. navo vina ncha kali, maʿana, wakitaka kuua mamba, sherṭi humchoma katika jicho, katikȧ mwili kisu hakiingii, magamba yake magumu sana.

### namna ya vita vyao.

iwapo zamani mmoja amemwʿaṣi mwenziwe, anataka vita, marra hawapigani, illa kwanza hupelekeana salāmu. na salāmu zȧo husema: „sababu nini wewe fulani umeniʿaṣi? sasa nakuʿarrifu, nataka uwe kȧtika amri yangu. na kama hutaki amri yangu, bassi katika vitu viwili hivyo nnakuletea, chagua kimoja wapo“. na katika vitu hivo humpa mshare na jembe. maʿana ya mshare — vita, na jembe — ukulima. iwapo anataka vita, atachukua mshare, akiupokea — marra atauvunja, amrejeshee vijiti vitupu. bassi marra atajua, ya kama anataka vita.

naye atapeleka khabari kwa watu wake, apige ngoma ya vita. wakija watawambia, ya kama fulani ametuʿaṣi, anataka vita na sisi. nao wakisikia maneno

yale, killa mtu atajifunga kwa zana ya vita. watakwenda kwa mkubwa wao wote, marra watajizindika maungo yao [1]), wote wende kunako vita.

na vita vyao huenda usiku, wakifika katika mji, huuzunguka wote. marra mtu mmoja atapiga bunduqi ya kuwaamsha. ḥatta wakiamka katika usingizi, marra wanaingia katika mji, wanachoma moto majumba. bassi yule waliyemwendea, iwapo naye ana nguvu za kuweza kupigana, watapigana huo usiku. akimwona mwenziwe ana nguvu záyidi kuliko yeye — atakimbia, awache mji. marra wale wa vita watateka vitu vyote, wamwache maskini. kule atakakokimbia, ʿaqili ikamrudi, marra atatoa mtu kumpelekea yule aliyemshinda — ya kama: „mimi bassi vita, nataka amani". vita vyao havina siku nyingi.

### khabari ya amani.

baʿada ya kupigana, mmoja akashindwa, atakwenda kwa mwenziwe kuanguka miguu, atasema: „mimi katika amani yako, na kulla amri utakayo mimi ni pamoja nawe, wala sikumbuki miaka yote kutaka vita na wewe". baʿada ya kwisha maneno haya, hamṣadiqi maneno yake, atarejeʿa. baʿada ya siku haba ataleta mshenga. na yule mshenga, aliyetumwa máneno yale ya amani, katika mikono yake hupewa ushanga mweupe kupeleka, maʿana huo ushanga ndio ʿalama ya amani. kama hana ushanga wala hawaqubali amani yao, hujua ya kama hawa waongo, hawataki amani. iwapo ámequbali amani yao, atawambia: „mimi sherṭi — mle mchanga" [2]). nao watariḍia kula mchanga. watasema

---

1) sie machen überall am Körper kleine Ritze in die Haut und reiben dawa hinein, die sie vor Pfeilschüssen und Speerstichen bewahren soll. — 2) vergl. folgenden Bericht über die Blutsbrüderschaft.

katika shuruṭi zao za yamini: „tunakula mchanga na fulani hatuna vita naye tangu sisi ḥatta tunacho kizaa sisi, tukawazá kufanyiza u'ádui naye — tufe". bassi wakesha shuruṭi hizo — beina yao huwa udugu ma'isha yao. imekwisha khabari ya amani.

### khabari ya udugu wao.

udugu wao wanawotakana katika mkutano wa pombe ao katika safari. katika pombe iwapo amekuja moja katika ule mji wenyi pombe mgeni, hana mtu anayemjua, hutokea mmoja mwenyeji wa mji, killa marra humtilia kibaba cha pombe, akampa, na kukaa naye pamoja akazungumza. na njaa ikamwuma, marra humpeleka nyumbani kwake, akiwa na mke, humwambia mkewe: „fanyiza chakula hima, mgeni ale". yule mwanamke hufanyiza chakula, akisha akampelekea maji chooni koga, marra humpa chakula akala na kumwonyesha kitanda, akiwa na usingizi akalale. tenna akiona eḥsani nyingi, humwambia: „somo, mimi nakutaka urafiqi, tuwe pamoja mimi nawe". naye huqubali, marra huwambia wazee wake — ya kama: „huyu mimi ananitaka urafiqi". nao wanamjibu: „kama unamtaka — fanyeni". marra hukamata kuku, wakamchinsha, wakatoa ini lake, wakafanyiza shuruṭi kama tulizotangulià kuzisema katika urafiqi wa kidoe[1]).

namna nyingine — hula mchanga wa Mzia. na mchanga huu unatoka Pangani, paḥali panakwitwa Mzia. na kama pazi wao hana ule mchanga na wao hawawezi kwenda kule Pangani, hupeleka mtu kwa majumbe wa Bagamoyo ao wa Daressalama, amma wa mji mwingine, humwambia — ya kama: „pazi anataka mchanga wa

1) vergl. safarí yangu ya Udoe ḥatta Uzigua im Kapitel khabarí ya udugu wao.

Mzia". nao huwapa burre, wakampelekea pazi. hutiwa ule mchanga ndani ya bakuli na maji, hunywa pamoja na maji na mmoja atasema: „mimi, kama nitamḍuru rafiqi yangu, ao akitaka kitu nikamnyima, mchanga wa Mzia uniyayushe kama maji". na wa pili husema kama hivo. bassi killa mtu amemwamini mwenziwe, ya kama huyu ndugu yangu. hii khabari ya udugu wao Wazaramu.

### khabari ya vyapo vyao.

wakitaka kumpa mtu kiapo, hupika maji ya moto, wakamwambia yule mwizi kutia mkono katika maji. iwapo mwizi — mkono utachubuka, kama si mwizi — hauchubuki. ao humwambia yale maji kunywa. iwapo ni mwizi — humwunguza yale maji.

namna nyingine ya kiapo: hupepea mundu ao shoka katika moto, na ule mundu huupaka mavumba. ukesha kupata moto sana, huja mwizi atasema: „mimi kama mwizi — kiapo nigwie, na kama si mwizi — nihongeze". yule mtu huramba ule mundu, kama si mwizi — haungui.

namna nyingine ya kiapo cha sanga. sanga ni hiyo shindano, kuja mganga, akamtia mwizi katika jicho. kaẓálika akiwa mwizi, shindano huingia. na khalafu huimbiwa wimbo — ikatoka. na kama si mwizi husalimika salama.

hii khabari ya vyapo vyao. lakini desturi hii yalikuwa zamani, sasa wameiwacha, sasa wanaogopa, sababu yule mwizi, iwapo amechubuka ulimi ao jicho — hutaka kwenda mjini kushitaki, husema „mimi si mwizi, wamenipa kiapo, nami sikuchukua kitu".

### namna ya sumu yao.

katika mishare wanatia sumu. na hiyo sumu wa-

naipika uchungu [1]). kwanza mti wa msunguti wanachuna magome yake, wakayapika ḥatta yakawiva, tenna magome huyatupa, maji yaliyotoka katika magome — ndio wanayofanyiza sumu. ma'ana yale maji huyapika pekeyake ḥatta yakaganda, yakiwa kama mfano wa mafuta. marra huyatia katika vibuyu wakafunika. hawaweki katika nyumba, wanajenga kibanda mwituni, ndiko wanakoficha sumu zao, illa ya kutumia kidogo hutia katika kibuyu. na kulla mwaka ukisha huipika marra ya pili, huchanganya ya zamani na mpya, wakaipika pamoja, ma'ana huzidi kuwa kali. ndio khabari ya sumu yao.

### kuwinda kwao.

wanawinda na nyavu ao mikuki. nyavu wanawindia nyama za mwitu, tohe ao paa ao parahara. kwanza huchimba shimo, kisha wakazungusha nyavu upande moja wa shimo, marra wakawasaka walikolala wale nyama. tenna huwafukuza, wakenda kufikia katika nyavu, tenna huwakamata, wakawapiga kwa mikuki, wakafa. na wasioingia katika nyavu — huingia katika mashimo.

illa viboko na mamba huwapiga na mikuki, na hiyo mikuki wanayowindia huitia sumu. na kuwinda kwao viboko waqti wa usiku, ma'ana viboko wanatoka wengi kwenda mashamba kula majani. wakiwaona huwapiga kwa mikuki ile yenyi sumu. na akifa humtoa meno. wengine hula nyama ya kiboko, lakini wenzao hawataki kukaa nao pamoja, sababu wanasema, nyama ya kiboko inanuka sana. bassi wale wawinda wakipata nyama ya kiboko, hujenga kibanda katika mwitu, wakala nyama yao kule ḥatta ikesha. khalafu hureje'a katika mji.

---

1) Gift.

na wengine hula nyama ya mamba. każālika ni kama wanaokula nyama ya kiboko, hawaingii katika mji.

wengine wanawinda na mishare, lakini si mno kuliko nyavu na mikuki. waqati wa masika maji yakiwa mengi, wanawinda billa ya mikuki, wala nyavu hawana, illa wanakaa katika mikondo, wanayopita nyama wadogodogo tangu tohe ḥatta funo na wengine, wakipita huwapigia makelele wale nyama, watu wengine huwaziwia kwa mbele na wengine nyuma, ḥatta wakipata kattikatti huwapiga. sababu waqati wa masika nyama hao hawana nguvu, wala hawawezi kukimbia. hiyo ndiyo khabari ya mawindo yao Wazaramu.

### namna ya kuvua samaki.

kwanza wanakata miti mirefu, mfano wake kama mianzi, lakini miembamba, wakesha husuka machachȧ [1]), yaliyo marefu. khalafu huenda katika tambiko, wakatambika. marra wanakwenda katika mto wenyi maji mengi kusimamisha ile miti na yale machacha. lakini kwanza sherṭi atangulie fundi kuzama katika maji. sababu huyu fundi anapokwenda katika maji, huchukua dawa za kuwafumba macho mamba na majoka yaliyomo, wasiḍurike. akishȧ fanyiza dawa zake, ndipo wanapoingia watu kufunga hayo machacha ya kutegea samaki. tenna mamba wanakutana nao katika maji — ḥawawaḍuru. na wakiwa katika maji hawataji jina la „mamba", wanataja „gogo [2])" ao „mkonge" [3]). bassi wakesha kazi ile, hutoka katika maji, wakakaa ḥatta usiku, huingia marra ya pili katika maji, samaki wameingia ao bado. iwapo wameingia, huwachȧ wakalala

---

1) lange dünne Stange. — 2) Baumstumpf. — 3) Ast vom mkonge-Baum.

ḥátta aṣ-ṣubuḥi, ndipo wanapowatoa samaki. nao huwapata wengi sana. killa samaki huwamo, wanawoliwa na wasiwoliwa. wakesha watoa, hugawana mafungu wale sàmaki. fungu moja humpa fundi, na fungu moja hupewa mwenyi áṣili ya ziwa, ndio tambiko yake. sababu desturi ya kuvua katika mito, iliyo mikubwa, sherṭi kwa tambiko. huenda yule mwenyi áṣili ya ziwa, akatambika kwa wazee wake, ndipo anapowapa rukhṣa kuvua. na kama watavua min gheri ya yule mwenyi mto, hakuwa raḍi, watapata samaki, lakini si wengi. hutokea baʿaḍi ya siku watu wengi kukhasirika na mamba. imekwisha khabari ya kuvua kwao samaki katika mito.

### namna ya hérizi zao.

wao hawaandiki ḥérizi kwa ḥarufu za qorani kàma Wasuaḥeli, illa, wanapotaka ḥérizi, huenda kwa mganga, akamwambia: „mimi nataka ḥérizi“. naye mganga humwuliza: „unataka ḥérizi ya namna gani?“ atajibu: „nataka ḥérizi ya macho ya watu, ao ḥérizi ya simba nyikani asiniḍuru, ao ḥérizi ya vita, nendapo vitani usiniḍuru mshare wala riṣaṣi, ao ḥérizi ya uchumi nipate fàyida“. bassi akisha mwambia mganga, atasema: „kwanza nataka mchele wangu“. watapatana mwanzo wa reale moja ḥatta tano kwa mtu mweza. marra mganga atakwenda mwituni kuṭafuta mzizi wa ḥérizi aliyoitaka. marra atakuja nao, tenna atatoa kibuyu kinacho mavumba, atoe na kitambaa cheupe. na mle katika kibuyu kingine huwa na asali ya nyuki pamoja na mafuta ya nyonyo, ndio wino wa kuandikia. bassi ule mzizi ataupaka yale mafuta na asali pamoja na mavumbà, akisha atashona ḥérizi. na siku atakayompa, kwanza atamchansha katika uso na mkononi na kiunoni, kisha atamwambia „vaa“. marra atamtoa khofu moyo

wake. na yule mganga atampa shuruṭi zote — ya kama: „mimi nakupa ḥérizi yangu, iwapo umesema na mtu, nawe umeḍurika, niletee khabari". każálika mzizi anaochimba yule mganga, jina lake kamila kumbwene. hii ndio ḥérizi ya macho ya watu.

wa każálika ḥérizi ya vita mzizi wake namna mbali, unakwitwa ndugo. vilevile huenda kwa mganga, akamwambia: „nataka ḥérizi ya vita". watapatana na khalafu atafanyiza ḥérizi, aishone na kitambaa, na ndani atie mavumba. vilevile ikisha atamchansha maungo mazima, killa paḥali chale moja. tenna atampa ḥérizi, atamwambia: „iwapo utakwenda vitani, mshare haukupati. illa utadunga katika mwili, marra utaanguka, lạkini angalia — ukenda kwako, mudda wa siku mbili usilale na mwanamke".

aiḍa ḥérizi ya uchumi ni kama hizo tulizotangulia kuzisema sherṭi zake, lakini hiyo hujifunga kiunoni killa siku. jina lake unakwitwa mkili.

każálika ḥérizi ya simba — wasafiri na wawinda sherṭi huwa nayo. na kuandikwa kwake sherṭi upatikane uso wake simba na ḥérizi yake ya mtu aliyemwua. wenyewe waganga wanaijua paḥali ilipo, sababu wao husema: simba anapokamata mtu, ḥérizi yake huitema, akala nyama ḥatta ikesha, tenna huimeza. nayo shidda watu kuipata, illa hutokea bakhti kupatikana. iwapo simba ameuawa, huchuna kipanda uso chake, wakapata na ḥérizi yake, hiyo ndiyo wanavoandikia watu ḥérizi, wakawapa. lakini ghali sana, wananunua kwa feḍḍa nyingi tangu riale kumi ḥatta khamustʿashara.

wenyewe waganga wa simba wakikutana na simba njiani, hawaḍuru, illa humtukana, humwambia: „mtu mzima wewe, huna ḥaya? unataka nini njiani? watoto wanataka kupita". yule simba akasikia maneno ya yule mganga, marra ataguna ataingia mwituni. mganga

anaijua dawa za simba — hamwogopi katika njia. hii khabari ya ḥérizi.

maneno ya uganga wa nyoka.

Wazaramu desturi yao — wengi katika miguu yao wamechansha dawa ya nyoka, sababu asiwaume. na kuchanshwa kwao — kwanza humwua nyoko, aliye mkubwa, nondo ao chatu ao futa amma vuvi, hayo ndio majoka makubwa. wakesha na katika majoka hayo tuliyoyataja, marra hutoa nyongo yake na meno yake, każálika na ngozi yake, lakini meno na nyongo huyaunguza katika moto, ḥatta yákawa majivu. hiyo ndiyo dawa, jina lake unakwitwa usira yale majivu. każalika ngozi yake ndio kiti cha kukalia mtu anapotaka kuchanshwa dawa ya nyoká. akisha chanshwã, marrá hupákwa yale majivu pale alipochanshwa. kwa desturi yao Wazaramu mtu aliyo chanshwa dawa ya nyoka asimwume — hamwumi. na iwapo atamwuma — hawi na uchungu, marra patanyamaza pale alipoumwa. akisha mwuma hawi na ma'isha yule nyoka, marra atakufa. każálika akimwuma, husimama, hakimbii, humwambia: „reje'a marra ya pili". yule nyoka humwuma marra ya pili, hiyo ndiyo sumu yake. bassi endako — yule nyoka atakufa. naye akenda kwake, hasemi „nimeumwa na nyoka", husema „nimegombwa na nyoka".

namna ya kuomba mvua.

katika Zaramu mvua iwapo imepotea, vyakula vinakauka, marra watu wanakwenda kwa mapazi kuwambia — ya kama: „mna mashauri gani? vyakula hamna mashamba". nao huwajibu: „tufanyeje?" wale watu huwajibu mapazi: „tutambike kunako mizimu". nao mapazi, iwapo wana nafasi ya kwenda kunako mizimu ya Ukami, watakwenda, ao watakwenda kunako maqa-

buri ya wahenga[1]) wao, waliwowatangulia, hupeleka shuka na bendera na kaniki katika maqaburi, husema ya kama: „tumekuja sisi watoto wenu, sababu mwaka huu vyakula, tukipanda, haviji juu. leo tumekuja kwenu, wazee wetu, kufyagia katika maqaburi yenu, muungu atushushie mvua, vyakula viote, tukapata vyakula. killa mwaka tutakuja katika maqabri". na wakisema maneno hayo hupiga magoti wakafyagia kwa mikono. nao hawavai kofia, wala hawendi na nguo mbili. ba'ada ya kwisha tambiko, muungu atakapo kuwakumbuka, huwashushia mvua kwa wingi. husema: „tambiko zetu zimegona". huko ndiko kuomba kwao mvua.

### khabari ya pepo.

katika Zaramu watu wengi wana pepo. na pepo wao mno kinyamkera. mtu akishikwa na ḥoma, huja mganga na mavumba, akampa yule mgonywa. na maraḍi yakazidi juu ya mwezi, mganga husema: „huyu kinyamkera kimemshika". jama'a zake humwuliza mganga: „tufanyeje sasa?" mganga hujibu: „kwanza tumpike nyungu ya mawe". marra huenda mwituni, wakatafuta mawe ya vidurazi, wakakata na mizigo ya kuni. ḥatta usiku huchimba shimo, wakakoka moto, marra huyatia yale mawe katika moto, marra hufunga jamvi kuziwia moshi usitoke. ḥatta mawe yanapowiva, huja yule mgonywa, akawekwa juu ya kiti qaribu ya lile shimo, lililotiwa mawe, marra huleta mtungi wa maji kuyazima yale mawe. naye humfunika nguo maungo yote, ule moshi humwingia mwilini. ḥatta yakesha kuzimika mawe, humtoa ndani ya nyungu, marra huenda kulala.

aṣ-ṣubuḥi mganga huleta jimbo la koga na kupakaa,

---

1) Vorfahren.

ma'ana jimbo la majani, mudda wa siku saba'. marra hufanya mashauri ya kumpunga madogori[1]). wakesha patana mashauri, yule mganga huenda kualika waganga wenziwe na waanafunzi wake. ḥatta usiku huleta ngoma zake na ngoma za madogori, jumla yake ngoma saba'. ngoma nne hupiga mtu mmoja, na mbili hupiga mtu mwingine, na moja hupiga mtu moja. marra huletwa mgonywa, wakampaka mavumba usoni, wakamremba killa rangi — nyeupe, nyeusi, nyekundu. tenna hupiga ngoma mwanzo wa usiku ḥatta aṣ-ṣubuḥi, na mwele[2]) anacheza, na wasiwo pepo wote wanacheza. na wengine wanajiwa[3]) na pepo, huanguka uanjani kwa mshindo wa ngoma. mtu mwenyi kinyamkera kama mwenyi wazimu. anapocheza pepo wake, usimwonyeshe kidole, akiona kidole, atakufukuza. akikupata atakikata na meno. khabari ya pepo — wale waganga watapunga usiku kucha, ḥatta aṣ-ṣubuḥi watamkomoa pepo, wampe újira wake mganga, ende zake. imekwisha khabari ya pepo.

### mambo ya watu wenyi ukoma na maraḍi mengine.

watu wenyi maraḍi katika Zarâmu ndui, buba, tego, yote maraḍi hayo hawayakhofu, illa ukoma wanaukhofu sana. lakini wanakaa naye mwenyi ukoma katika mji moja. maraḍi wasiyoyapenda mabalanga, ma'ana maraḍi hayo huchubuka mtu mwili mzima, akiwa mwekundu. na akila chakula, huyayuka mikono yake. na áṣili ya kutoa kumpenda yule mwenyi maraḍi — zamani akula naye chakula pamoja hutokea kumṣibu mtu yale maraḍi.

wa kaẓâlika mtu mwenyi wazimu wanamfunga gogo

1) kumfanyizia ngoma ya madogori. — 2) Kranke. — 3) passiv von kuja.

miguuni, wakampa chakula na maji, hapo walipomfunga, hawamwachi kutembea ovyo, sababu huchoma moto majumba ya watu na kuwapiga watoto, ndio ma'ana wakamfunga.

kaẓálika maraḍi ya kifafa [1]) wanakula naye pamoja, lakini maji anayokunywa, akazaza katika kata, maji hayo mtu mwingine hayanywi. ma'ana maraḍi hayo mabaya kama mfano wa maraḍi ya pumu [2]). áṣili yake mtu hukohoa, na pumuzi killa marra huja juu, khaṣṣa siku za mvua, hawezi kufanyiza kazi mwele wa pumu. ḥii ndio khabari ya watu wenyi maraḍi.

1) Fallsucht. — 2) Schwindsucht.

# Safari yangu ya Russia na ya Sibirien

## niliyofanya pamoja na bwana wangu Dr. Bumiller

ya

**Selim bin Abakari.**

bismillah er-raḥman er-raḥim!

katika safari yangu ya barra Russi sene elfu thalatha mia u arbʿatʿashara mwezi mfunguo tatu nimeondoka na bana wangu doktor Bumiller Berlin Friedrichstrasse Nordexpress kwenda Königsberg. tulipofika Königsberg sikuwa na khaṭṭi ya múhuri[1]), bana wangu akafanza sim Berlin kutiwa katika múhuri wake. tulipofika katika mpaka wa Deutschi na Russi, tukaipata simu — ya kuwa — rukhṣa niingie katika inchi ya Russi, kwani qawaʿida ya Russi, hakuna mtu kuingia katika inchi yake — shurṭi awe na múhuri. katika Ulaya zote mtu anaweza kusafiri kulla inchi billa kuwa na múhuri, lakini Russi na Turki huwezi kuingia katika inchi zao billa kuwa na múhuri. katika inchi hizo zote nimekwenda, lakini Russi imezidi katika múhuri wake. tulipokwenda katika inchi ya Turki, sikuwa na múhuri, lakini nimeweza kuingia. na inchi ya Russi ingalikuwa

1) Pass.

sikutiwa katika múhuri wa bana wangu, singaliweza kuingia katika inchi yao.

bana wangu alipata barua ya serkali, ya kuwa yeye hana ʿushuru. kulla inchi tunayopita, hapana rukhṣa kuutoza ʿushuru, wala haiḥitaji kufungua vitu vyake. tulipofika katika mpaka wa Russi, nikaondosha barua yake ya serkali kuonyesha watu wa forḍani, wapate kunirukhuṣu na mizigo yangu, lakini, walipoiona, wakanena: „hii haifai, lázima utafungua mizigo yako". bana wangu akakataa akanena: „sifungui mizigo yangu, kwani nna khaṭṭi ya waziri wetu, ya kuwa sitozwi ʿushuru". na siye tulikuwa na mizigo mingi, mizigo khamso u arbaʿini, hatuwezi kufungua marra moja. nasi tumefanza użia sana, hawakuqubali kutuwachia.

bana wangu akawambia: „sasa sina wasaʿa kufungua mizigo, lakini nipeni mizigo mitatu, iliyo na nguo zangu naitaka kuvaa siku mbili ḥatta mizigo mingine ikija". tukaacha mizigo yetu yote katika mpaka wa Russi na wa Deutschi, tukachukua mizigo mitatu, iliyokuwa na nguo zetu, tukawambia: „mizigo yetu tupelekeni Petersburg, tutakuja kuchukua forḍani, hapa hatuwezi kufungua, maʿana tukikaa kufungua mizigo arbaʿin na mitano, hatutapata nafasi kusafiri na gari hili. bassi mizigo yetu ileteni nyuma, siye tunatangulia, tukachukue mizigo mitatu". tukasafiri tukenda zetu Petersburg.

tulipowáṣili Petersburg, marra nimepata fíkira, kama sasa tuko katika inchi nyingine. na mavazi ya kule namna nyingine kuliko inchi za Ulaya, na magari namna nyingine. katika magari yao madogo sana, na mavazi ya masais [1]) kama waanawake wazee. kweli mtu akiwa katika safari, huʿallam maneno mengi, na mtu huingia aqili nyingi.

1) Kutscher.

tukatoka forḍani, tukenda zetu Hotel Europa. tulipokwenda kule tukapumzika. khalafu bana wangu akaondoka, akenda kutembea, kanambia, nikisha kazi yangu, nikisha kula, nende zangu nikatembee. nilipokwisha kazi yangu, nikenda zangu mezani kwenda kula. na miye sijui maneno ya kirussi, nikitaka kuuliza kitu, hawasikii maneno yangu. nikaondoka nikenda kuita mkulimani wa kideutschi. akaja kuwambia vitu nnavotaka, ndivo walivoelewa.

na wale watu maboi wa katika hotel mno si qabila ya Russi, sana watu wa kideutschi amma Tartari. na hawa Tartari islamu. watu walikuwa maboi katika meza yetu wote wislām. nilivouliza vyakula vyangu na kitu nnachokitaka kunywa — walistaʿajjabu: „kwa nini huli nguruwe, amma hunywi wein"? nikawambia: „mimi sinywi wein, wala sili nguruwe, kwani miye islām". nao wakanijibu, — kama nao wislām. nikat͟hanni wananiḍiḥaki, nikanena: „itakuwaje nyīe kuwa wislām katika inchi hii?" wakanambia: „sisi qabila yetu huitwa Tartari, na Tartari huwa islām". sikuṣadiqi. nikat͟hanni wanasema uwongo. nikaondoka, nikenda zangu katika nyumba yangu, nikaipiga kengele, akaja boi, anajua kideutschi. nikamwuliza: „hawa watu gani, wanaofanza kazi katika meza yetu?" akanambia: „hawa Tartari." kamwambia: „dini yao dini gani?" kanambia: „islamu." nikastaʿajjabu sana! kuwa katika inchi ya Wazungu pana wislām namna hii.

nikaondoka nikenda kutembea katika mji, na miye sijui maneno, sijui mtu. nikenda zangu kwa bawabu wa katika hotel yetu, nikamwuliza paḥali, mtu anapoweza kwenda kutazama mchezo amma kutembea. akanieleza kulla paḥali penyi mchezo. nikamwambia: „nipe barua moja, uniandikie maneno ya kirussi, na

kienda kulala, lázima husujudia ile picha ya ʿIsa, ndio shahada yao katika mkubwa na mdogo, ṭabiʿa yao ni moja.

siku moja nimekwenda katika nyumba za machezo na bustani [1]. na mtu hawezi kuingia katika Ulaya zote billa kutoa mapesa, lakini Russia wale ʿaskari, wanaotwaa zile barua za mapesa, ukimpa mapesa kidogo kwa faragha — utaweza kuingia katika machezo. maʿana nilipokwenda nimetoa rubel nne kuingia. mudda wa nuṣṣu saʿa nimeona watu wengine wamekuja hawana khaṭṭi ya kuingilia katika nyumba ya machezo, khalafu wakamkonyeza, wakamwambia yule ʿaskari: „hatuna khaṭṭi ya kuingilia hapa, na siye tunataka kutazama machezo, bassi chukua roboʿ moja, utuweke paḥali". yule ʿaskari marra moja akachukua ile roboʿ, akaweka wale watu watatu paḥali panapo beʿi yake rupia nne. nimestaʿajjabu sana, kwani katika Ulaya huwezi kufanza namna hivo, ukifanza namna hiyo huḥokumiwa vibaya sana, na yule ʿaskari atapata ʿaẓabu záyidi kuliko wale, sababu ni kama uivi.

na Moskov ndio mji wa áṣili wa Russia, zamani ndio mji wa ʿezi, lakini sasa mji mkubwa wa Russia ni Petersburg. lakini Moskov kuna ʿafya kuliko Petersburg, sababu Petersburg ḥoma nyingi katika mji, lakini katika mashamba ya Petersburg kuzuri sana. záyidi watu wakubwa wa Petersburg hukaa mashamba, sababu mabardi wa kule nzuri kuliko mjini.

na mji wa Moskov wa zamani uliungua. wenyewe Warussia wametia moto maqṣudi, kwa ájili ya Wafranza walipokwenda kupigana kule. sasa umejengwa mpya, mzuri záyidi kuliko mji wa zamani.

na mji wa Moskov mji wa biʿashara sana, záyidi

1) Theater.

ya Petersburg, ma'arufu katika dola zote kuliko Petersburg. bi'ashara ya kule mno inatoka barra ya Shami[1]) na barra ya 'Ajam[2]) na Bukara[3]). watu wa kule huleta vitu vyao Moskov mabassati na ngozi za kondoo na ngozi za nyama wa mwitu huja kuuza Moskov, ma'ana mabazazi wa katika Ulaya zote huja hununua vitu kule Moskov. kulla mwaka kuna musim[4]) mkubwa sana, bi'ashara kubwa sana hufanya Moskov, ma'ana mabazazi hutoka Ulaya hununua vitu rakhiṣi kule, vinavyotoka barra yote, huenda kuuza ghali sana Ulaya kule.

na katika mji wa Moskov ndio wenyi mapádiri[5]) makubwa wa Russi. na makanisa yao mazuri sana. lakini dini yao namna nyingine, huabudu mtume moja kama Wazungu. na wako wislamu wengi sana kule Moskov. na wislamu wa kule vyakula vyao nyama ya frasi. nilista'ajjabu sana, kwani siye kwetu nyama ya frasi makruḥ, lakini kwao ḥalali. na islamu wao Sunni, huṣali sana na kusoma.

na tenna wao mabazazi sana. uchuzi wao hubadilisha vitu nguo kukuu na nguo mpya na ngozi, kulla aina ya vitu hubadilisha, wapate fayida. ukimpa kitu kikukuu hubadilisha upate kipya. na wale Tartari bi'ashara yao kama Wahindi, kofia zao kama Wahindi vilevile, wanajua bi'ashara kuliko hawa Warussi wenyewe, ndio watu naḍifu kuliko Warussi wenyewe.

siku moja tumenunua vitu vyetu kufunga, tukataka kwenda Sibirien. tumefunga killá kitu, ma'ana Sibirien hakuna kitu kununua kule. na ukenda kule, kulla mtu atakwambia: „ununue dawa ya kunguni na dawa za chawa". kuna wadudu sana kule Sibirien, sababu watu wachafu sana.

---

1) Asien. — 2) Persien. — 3) Buchara. — 4) Messe. — 5) Geistlichkeit.

tulipoondoka Moskov, tukenda Nishinovka, vilevile mji wa musim. na watu wa kule záyidi ni Tartari. kuna meskiti mingi sana. tumekaa siku moja, tukaingia katika stima katika Wolga kwenda Samara. na mto ule mkubwa sana. tukasafiri siku nne ḥatta kufika Samara.

na katika stima, tuliyoingia, wale maʿabiria Russia kulla mtu huwa na chayi yake na sukari, kulla mtu huchukua vyombo vyake vya kufanza chayi na kunywa chayi, kwani wagumu sana. nao katika stima hununua maji ya moto bassi kufanza chayi yao. alikuwa mwanamke moja na watoto wake wamekaa tangu saʿa nane ya aṣ-ṣubuḥi na sufuria ya maji ya moto wamekunywa chayi ḥatta saʿa tisʿa ya usiku, kikombe hakiondoki midomoni kabisa, kazi — hunywa chayi. nimekaa kuwatazama watu wale, nikat͟hanni watachoka waondoke wakapumzike amma walale — lakini hawaondoki, birika ya chayi ikisha huingiza maji ya moto. ḥatta mimi nimechoka, nimekwenda kulala mudda wa saʿa tatu tangu saʿa sabaʿ ḥatta saʿa kumi, nimeondoka nikenda mezani, nikawakuta vilevile wanakunywa chayi. nikauliza mtu mmoja, nikamwambia: „hawa hawachoki kunywa chayi?“ akanena: „hii desturi ya Russia, kazi yao hunywa chayi, hawachoki“. na kulla mtu huwa na kipande cha sukari mkononi, huuma kwa meno, khalafu akinywa chayi, hawatii katika vikombe. kipande kimoja cha sukari ataweza kunywa vikombe sitta vya chayi. nimestaʿajjabu sana.

na katika magari na stima ukisafiri katika inchi ya Russia — utazame sana vitu vyako, huiba sana wao. pana watu husafiri maqṣudi kufuatana maʿabiria kwiba vitu vyao.

kule Samara tulipofika, watu walishtuka sana, walipoona mtu mweusi. wakasema, kama hawakupata

kuona mtu mweusi billa miye. nikenda tembea katika njia — hunikimbia, huthanni sheṭani ameshuka kwao. wazee na watoto wakiniona wote hunikimbia.

tulipoondoka Samara kwenda Omskow, wakatwambia watu, tutazame sana vitu vyetu, sababu njia ile ina wevi sana. miye lázima nikae juu ya mizigo na mkulimani wetu. mmoja akilala — shurṭi mmoja awe na zamu, haifai kulala watu wawili, tukilala sote — vitu vyetu vitaibiwa vyote.

na waqati ule tulipoondoka Samara, bwana wangu alikuwa hawezi sana, alishikwa na ugonywa wa tumbo. mudda wa siku nne hakuweza kula chakula. na siye tuko katika gari. nataka nimtazame bana wangu, na mizigo isiibiwe — nikiondoka kwenda kumtazama — lázima mkulimani akae juu ya mizigo yetu. ugonywa wake wa bana wangu — alikula samaki wa kule. mtu akisafiri katika Sibirien, ajiḥáżari sana, asile samaki wa kule, maʿana huḍuru watu wengi. hatukujua sababu ya ugonywa kule, katwambia mtu moja, tuliofuatana naye, baʿada ya kumwuliza, kama hakula samaki, kasema, kama amekula, lakini samaki wa huko haifai kula kulla mtu, sababu kulla tumbo haliwezi kustaḥimili kwa samaki wa kule.

njia ya Samara ḥatta Omskow ndio njia [1]) nzuri niliyoiona katika Sibirien. mwitu wa kule mzuri sana na hewa nzuri sana. ndio paḥali panapogawa Shami na Ulaya. tulipofika Omskow, tukafanyiwa ḥéshima sana na Guverneri wa kule, maʿana áṣili yake Mdeutschi, jina lake Taubẹ. tumekaa mudda wa siku mbili katika hotel, na hapo ndio tulipoanza kuumwa na kunguni.

na katika magari yao mtu hawezi kuchukua mizigo mitatu, kulla gari huchukua mizigo miwili na mtu

---

1) Gegend.

mmoja. tuliposhuka katika gari la moshi Omskow, tumechukua magari sitt'ashara ya frasi kupakia vitu vyetu kwenda katika hotel. na njia ḥatta katika hotel matope mengi, mtu hawezi kwenda kwa miguu, shurṭi aingie katika gari amma apande frasi.

tulipoondoka Omskow ḥatṭa Ob, bana mkubwa na bana Bumiller walitaka gari lao pekeyao, wametaka kwa Guverneri. Guverneri akawambia: „vema, tafanza wasa'a mwe na gari lenu pekeyenu". tulipoondoka tukasafiri, wakatufuatisha 'askari wawili na frasi, na mahobsa [1]) wawili kutupeleka forḍani. na wale mahobsa wakenda kutengeneza gari la bana mkubwa. tulipofika forḍani, hatukupata maḥali pa kukaa, gari limesheheni watu wengi sana. tulitaka sisi kureje'a kulingojea gari jingine, lakini wale mahobsa wakatufanzia wasa'a tupate kukaa. mwisho tukaingia katika gari tukenda Ob.

tumekwenda mwendo wa sa'a nne, tukafika forḍa ya kwanza. tulipofika hapa, wakaingia wevi katika gari letu, walitaka kwiba mizigo yetu. na mkulimani wetu alikuwa akijua ṭabi'a ya watu wa kule, akanambia — kama: „hawa wevi, tukae zamu sisi watu wanne". na wale walikuwa wakituandamia — tukilala webe vitu vyetu. khalafu tukafanza kelele, tukawafukuza katika gari letu, tukawambia: „ninyi mnataka kwiba vitu vyetu". tulipoambia vile, wakajua kama wevi, marra ile wakaondoka wakakimbia.

tulipofika Ob, kwa siku ya pili tumefika, pana mji mdogo, ndio mwisho wa gari la moshi. tukakaa siku mbili katika hotel, hatukuweza kulala kwa kunguni katika hotel ile. naliuliza paḥali pa koga. wakenda wakanitia katika chumba, ambacho mtu hawezi kustaḥamili kwa jasho. nikaingia mudda wa daqiqa mbili

---

1) **Offizier; verstümmelt aus dem engl. Officer.**

— sikuweza kutoa pumzi kwa moto mwingi. nilista'ajjabu sana, watu wa kule wana bardi sana, nao wanaweza koga maji ya moto záyidi kuliko watu weusi.

watu wa kule maskini sana. huchukua viṣanduqu vyao, hufunga tumboni, wakiombea mapesa. wengine wanakuja kuomba mapesa ya kanisa.

na nyumba za kule nyumba za miti, nyumba ndogo kabisa, vyumba viwili na jiko ndani. na watu hulala pamoja — chumba kimoja — na nyama wao. nasta'ajjabu katika 'ajabu niliyoona — watu, walioko katika inchi ya bardi, na paḥali walipolala, siwezi kulala miye mtu mweusi kwa moto. wao hustaḥamili jasho sana, hustaḥamili na baridi sana.

na mvinyo yao kama mafuta ya taa, ukiwasha — moto huwaka kama taa. nao hunywa tele ya mafuta haya.

siku ya pili tumeondoka kuingia katika stima[1]) kwenda Bernaūl. na katika mto, tulioingia, zamani kulikuwa żahabu nyingi sana na feḍḍa nyingi sana. ḥatta siku ya pili tukafika Bernaūl, tukenda katika hotel. ule mji wa Bernaūl kuzuri kidogo. na Bernaūl hapana gari la moshi, lázima kusafiri na gari la frasi. na watu wa kule vilevile wakaniogopa, hawakupata bado kuona mtu mweusi.

tumekaa siku tatu Bernaūl, tukataka kuonana na yule guverneri wa inchi ile, apate kutupa múhuri wa kusafiria, ma'ana kama mtu hakupata múhuri wa guverneri, hawezi kupata frasi na gari. akaja bana mkubwa wa Bernaūl kuja kumtazama bana Wissmann. bana Wissmann akamwambia, kama ataka múhuri. kamwambia: „la, miye siwezi kufanza múhuri, múhuri shurṭi uende Domskow, khalafu utapata múhuri“. na bana

1) engl. steamer.

mkubwa hakuweza kureje'a Domskow, sababu mbali. yule bana wa Bernaūl akamwambia: „tafanza sim kuleta ṣaḥiḥi ya mkono wake, khalafu utapata barua ya watu wa shamba wakupe farasi". ma'ana yule guverneri wa Domskow ndiye anayeḥokumu watu wa mashamba, naye huḥokumu 'askari, na 'askari huitwa Kosaki. bana Wissmann alikuwa na múhuri wa sulṭani wa Russia, kapata rukhṣa kulla paḥali apewe frasi anayotaka, lakini watu wa Sibirien hawasikii amri ya sulṭani, wanasikia záyidi ya guverneri. ukionyesha khaṭṭi ya guverneri, marra hukupa frasi na magari.

khalafu akatuletea sim guverneri wa Domskow, tupate barua ya safari. tukanunua vitu vyetu Bernaūl, tukanunua mikate na biskuti na mboga na jokho za baridi za ngozi za kondoo — vitu vya miezi miwili, kwani kule juu Altai hapana vyakula, shurṭi watu wanunue vyakula kule Bernaūl amma Biskow. tukagawa mizigo yetu. mingine tukapeleka mbele Semipalatschinski na mingine tumechukua. tukaingia katika magari ya frasi, na kulla gari moja frasi sitta, huenda sana kama upepo. kulla mwendo wa sa'a tatu ukifika mjini — lázima utapata frasi wapya. na wale watu wa mji wa kwanza hawana rukhṣa kupita na frasi wao mji wa pili.

na katika vivuko vya mitoni wana mashua zao, hupakia magari na frasi katika duwara. na ile duwara huzungushwa na frasi ḥatta huvukia n̄gambo ya pili.

tukenda ḥatta mji wa mwisho, tukataka maḥali pa kulala. wakatupeleka katika nyumba ya serkali kwenda kulala, na mizigo yetu wameiweka nje, wakaweka mtu wa serkali kukaa zamu. na kulla mji wa Sibirien una nyumba ya serkali na mtu wa serkali wa kutazama vitu vya wageni. na katika nyumba zile za serkali havitozi qo'odi, illa utalipa kitu chakula kwa mwanamke,

anayekaa katika nyumba kutengeneza vitu vyote vya nyumba. na mwanámke huyu na manamme wake wamewekwa kwa ḥokumu ya serkali. na yule mtu anatafutia frasi, analeta magari kwa watu wageni. aṣ-ṣubuḥi tulitaka kulipa ḥesabu yetu, yule mwanamke tukamwuliza: „qiasi gani?“ akasema: „kama mwataka“. na mtu akimpa reale mbili amma reale tatu hufuraḥi sana.

tukaondoka tukasafiri kwenda Biskow, ḥatta siku ya tatu tukafika. na mji huo ndio mwisho wa posta na sim[1]. tumekaa siku mbili vilevile, tukasafiri Biskow kwenda zetu vilima vya Altai. na farasi wa kule Biskow wakenda sana kama upepo juu ya vilima, na katika mito ya maji hupita na magari yao. na kulla gari hutiwa frasi tis'a na watu wawili wa kupanda. mwendo wa daqiqa kumi kulla frasi huḥesabiwa kopeken tatu qo'odi yake. nasi tulikuwa kulla marra huchukua frasi themánie u 'asherīn, na siku moja hupata frasi settīn.

na kule tumeona watu walevi sana, khaṣṣa wa mashamba. kulla juma' a mosi na juma' a pili hawana kazi illa kunywa mvinyo, wao na waanawake wao hulewa pamoja ḥatta na watoto wao. hupita njiani wakipiga makelele, mtu hawezi kulala kabisa.

na watoto wao — mtoto wa miaka minne — hupanda frasi pekeyake. mno huenda kwa frasi. frasi wengi sana kule, lakini frasi wao si wazuri kama frasi wa Ulaya. na kulla frasi themani yake utapata tokea rubel kumi ḥatta 'asherīn. na vitu vyote vyao huchukua juu ya frasi, ḥatta kondoo na mbuzi wao, amma hufunga miti nyuma ya frasi, hupakia kondoo huburura.

na watu wale Semski hawasikii neno la mtu amma ḥokumu ya mtu billa guverneri wao. nao hawamjui

1) Post und Telegraf.

guverneri, huḥokumiwa na watu wanatoka kwa guverneri. nao wapumbavu sana. ukiwaonyesha barua, kama inatoka kwa guverneri amma kwa sulṭani, japokuwa haikutoka kwao, huṣadiqi, ma'ana hawajui kusoma. bakhti kulla mji ukiona mtu mmoja, ajuaye kusoma na kuandika.

na feḍḍa ya safari feḍḍa ya qarṭasi. na kama feḍḍa hiyo mpya, hawachukui, husema: „hii si ya sulṭani". hawakujua kama sulṭani mwingine sasa, wao hujua sulṭani Alexander bassi.

na ta'abu katika gari la frasi huumiza mbavu sana, kwa jissi wanavopanda katika vilima na mawe. shurṭi ukae katika mito, uweke katika gari na mbavuni.

na katika safari hii tulipopita na magari, tukipita mashamba, bana wangu akitangulia, walipomwona watu wa shamba, humwamkia, lakini si záyidi kama miye, miye huniamkia sana kama miye sulṭani, sababu humwona bana wangu mweupe kama wao, lakini miye mweusi, hawakumwona bado, wakat͟hanni miye ndio mwenyi safari.

tukenda ḥatta tukafika inchi ya Kalamik. hawa Kalamik ṣura zao kama China. nao hawana nyumba katika inchi yao. dini yao huabudu sheṭani. na makazi hukaa juu ya vilima, hunena kama sheṭani hukaa juu ya vilima, kulla kilima kina sheṭani. nao hukaa juu ya vilima vilevile, hulala ndani ya ḥema ndogo sana za magunia. nao hawakai paḥali siku mbili — kama Wamassai, wao hufuata paḥali penyi majani na mbuzi wao na kondoo na frasi. na maḥali wanapokaa, huchinsha farasi, huchuna ngozi yake, hutungika juu, husema ndio kanisa lao. hurekebisha katika kilima, husema ndio penyi sheṭani, huabudu ile ngozi na sheṭani.

nao Kalamik hawajui kulima. wala hawajui koga. ma'isha yao hawashiki maji, wala hawanawi uso. wao

hunuka sana, tenna hapana watu wenyi chawa kama wao.

vyakula vyao nyama ya kondoo na nyama ya frasi na nyama za mwitu. na wakiwa na nyama hupakia juu ya frasi, huweka katika matandiko yao ya frasi, hukalia juu yake. huenda kulla paḥali wanapotaka kuchunga frasi na kondoo. ḥatta jua likichwa, wanajenga viḥema vyao, wanalala pale. hulala kulla maḥala wanapofika, hawana mji illa moja tu. na mji wao Angudai wapata nyumba thelathīn, ndio mji mkubwa wa Kalamik. hapo lázima tukaanza kupànda frasi kwenda vilimani. alikuwa hawezi sana bana wangu, siku tatu hawezi ḥoma. tukapanga frasi kusafiri kwenda Altai. na wale Kalamik wakiniona — hunisujudia, hawakupata kuona mtu mweusi. wao wanaabudu sheṭani, wakathanni miye ndiye sheṭani wao, aliyeshuka vilimani.

na ṭabiʿa kule mwanamme huweza kuoa kwa miaka kumi na mwanamke kwa miaka minane. na mtu hawezi kujitahidi kukaa nao pamoja ḥatta asipàte chawa. hawawezi kwenda chini, kulla maḥali huenda kwa frasi na n̈gombe, ḥatta watoto wa miaka mitatu na waanawake pia juu ya frasi. frasi zao ndogo kama punda. kulla mtu huweza kupanda kwa kuwa taratibu sana. hapana frasi dunyani kupanda vilimani kama frasi za Kalamík.

tenna nimeona kule n̈gombe — nuṣṣu frasi nuṣṣu n̈gombe, na mkia wake wa frasi.

mno hupiga nyama za mwitu hao Kalamík. nyama za kule sala [1]) na kondoo, lakini kondoo wa mwitu wa kule ana pembe kubwa kuliko mbogo. na tenna simba Ulaya [2]), na simba hawa hawakai paḥali illa penyi barafu.

na ukiona paḥali palipolimwa, ujue kama pana Russi, lakini Kalamik hawajui kulima kabisa.

1) Hirsch. — 2) Eisbär.

guverneri, huhokumiwa na watu wana
neri. nao wapumbavu sana. ukiwaon
inatoka kwa guverneri amma kw
haikutoka kwao, huṣadiqi, ma
bakhti kulla mji ukiona mtu
kuandika.

na feḍḍa ya safari feḍḍ
hiyo mpya, hawachukui
hawakujua kama sulṭan
ṭani Alexander bassi.

na ta'abu katik
kwa jissi wanavop
ukae katika mito

na katika
mashamba, be
wa shamba . . . mpaka wa Russia
miye huni . . . Warussi wakakaa zamu ya
mwona . . . mwisho wa Kalamik, inaanza Mon-
mweus . . . Wakirgisi wislamu, lakini ṭabi'a zao
mwer . . . Kalamiki, na mavazi yao kama Kalamiki. wa-
. . . mbia wakulimani wetu, ya kuwa hawa islamu —
K . . . ṣadiqi. nikawambia: „huku hapana islamu, pahali
. . . bali kama hapa islamu atakujaje hapa?“ wakulimani
wakanambia: „waulize ismu yake islamu“. nikawa-
piga: „salām 'aleikum“. wakanijibu: „'aleikum salām“.
nao wakasta'ajjabu sana, ya kuwa miye islamu. kha-
lafu nikatambua tenna, ya kuwa wao wislamu katika
kofia zao na kuṣali kwao.

wakatuqurubisha katika nyumba zao, wakatufanzia
vyakula, wakachinsha mbuzi na kondoo, tukala. waka-
tupangisha na frasi zao za kupigia nyama, wakatupa
na watu wa kuchunga frasi.

na maziwa yao Kalamiki na Kirgisi maziwa ya
frasi, hupenda sana. na mtu akinywa bilauri moja,

hulewa mtu kama mvinyo. Kirgisi walinipa ninywe — nikakataa, nikawambia kama hiyo mvinyo. wakasema: „hakuna, siye wislam". nikawambia: „haifai kunywa, sababu inalewa.

ḥatta tulipofika vilima, tukenda kupiga kondoo. tukenda tukajenga kambi juu ya barafu, tukakaa ḥatta siku ya pili, tukaondoka al-fajiri kwenda piga nyama vilimani. tumepanda frasi tangu saʿa hedʿashara alfajiri ḥatta saʿa tatu ya aṣ-ṣubuḥi, tukafika juu ya kilima. tukakuta kondoo wakubwa sana, tukataka kuwapiga. Kalamiki wakatwambia: „bado msipige, ngojeni, maʿana sasa wamelala kondoo, na wakilala, haifai kupiga". maʿana kondoo wa kule wakilala, wawili amma watatu huwa na zamu, hutazama kama wanakuja watu na hunusa ʿarufu za watu sana. wakijua, kama pana kuja watu — huwaamsha wale wengine, wakakimbia. Kalamiki wakatwambia — kama: „tukae ḥatta waamke wote — wanakula, waqati ule hawashiki zamu, kulla nyama hutazama kula, huendea mbele kunatokea upepo".

tumekaa pale mudda wa saʿa sabaʿ ḥatta walivoamka wanakula. wakatwambia Kalamik: „sasa rukhṣa pigeni". tukapiga moja, tukarejeʿa kwenda kambini. na ukipiga nyama, Kalamik hufanza kelele sana kwa furaḥa ya nyama, wao hutaka nyama bassi, hawajui kama pembe zao ndio mali.

nao wana ʿilimu kwenda kupiga nyama. huchukua fupa la nyama, hutia moto, khalafu hujua, kana mtu atapiga amma hapigi. tulipokwenda, tumekaa siku sitta, hatukupiga nyama. siku moja huyu mpiga nyama akachukua fupa, katia moto, akanambia: „nataka tazama, kama bana wako atapiga nyama". alipoondosha lile fupa katika moto, akanambia: „kesho bana wako atapiga nyama mkubwa".

ḥatta al-fajiri walipoondoka kupiga nyama, wakenda vilimani vya katika barafu, wamekaa mudda wa saʿa thenʿashara — hawakuona kitu. ḥatta walikuwa wakirejeʿa kuja zao kambini, wakashuka kilimani maghribi — marra wakakuta kondoo, bana wangu kampiga kondoo mkubwa sana na pembe zake nzito sana. ndivo nilivoṣadiqi ʿelimu yao kama kweli.

ḥatta siku ya pili akanambia: „vilevile atapiga nyama, lakini hana pembe". walivokwenda wakapiga kondoo mwanamke, hakuwa na pembe, ndogo sana pembe zake.

siku moja bana wangu akanambia, atakwenda piga nyama mbali sana. akanambia hajui, kama atarudi siku hiyo kambini, amma atalala huko. na bana von Wissmann akaenda China. nikamwambia bana wangu: „nitakuja na weye pamoja, kama utalala huko". nikachukua sufuria moja na nyama kidogo na chumvi na pilipili na vifya vya kupikia. tukapanda frasi zetu, tukenda zetu kupiga nyama. tulipokwenda mwendo wa saʿa tatu, ikatokea upepo wa bardi, unanyesha barafu [1]) — hatukuweza kwenda mbele wala hatukuweza kurejeʿa nyuma. Kalamik wakatwambia — kama: „hatuwezi kwenda mbele, pigeni frasi upesi, twende maḥali penyi majani, tupate kuwasha moto". tulipofika maḥali penyi majani, pana kijuto kidogo, lakini maji yake si mengi. tukashuka juu ya frasi, Kalamik wakaanza kutafuta kuni kuwasha moto. miye na bana wangu tukatafuta mawe na majani kujenga ukuta kuzuilia upepo wa barafu. tukajenga ukuta wapata żiraʿa mbili, tukakaa pale. marra ile ikaja barafu sana na upepo mbaya sana — mtu hawezi kuona mbele. ilipopita saʿa mbili, ikanyamaza kidogo, tukapanda frasi zetu kwenda mbele.

1) schneien.

mwisho tukafika hapo paḥali penyi nyamà, tukafanya kambi hapa.

tuliposhuka, bana wangu akachukua Kalamik moja, wakapanda vilimani kwenda kutafuta kondoo. nikabaqi miye na watu wawili kutafuta kuni kuwasha moto. haikupata mudda wa saʿa, ulirudi upepo mbaya sana. bana wangu akarudi upesi. tukaanza kujenga ukuta wa mawe na udongo kutengeneza paḥali pa kulala. na siye hatukuwa na ḥema, hatukuweza kurudi kambini, tukafanza ukuta kidogo wa żiraʿa moja a nuṣṣ kuzuilia upepo na barafu. tukachukua matandiko ya frasi, tukatandika chini, hatukuwa na nguo za kujifunika illa makoti zetu za baridi. nikapika uji kidogo na nyama ya kondoo, kulla mtu akapata kikombe kimoja — bana wangu na miye na wale Kalamik, tukalala. lakini sisi hâtukuweza kulala kwa bardi, na Kalamik wakalala zamu kuwasha moto na kutazama frasi. na kule khaṭari sana kwa simba ya Ulaya na mbwa wa mwitu, ndio nyama wabaya sana. lakini mwenyʿezimuungu atujaʿalia, hätukuona nyama mbaya.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka kwenda tafuta nyama tupige, lakini hatukupata. tumeondoka tangu saʿa tatu, ḥatta saʿa kumi tumefika kambini. tuliona taʿabu sana katika vilima vya Altai. na siye tumekaa siku arbʿatʿashara kule kambini kwa ájili kupiga nyama.

khalafu tukarejeʿa tukenda zetu Kashkashi. bana wangu akanipa frasi moja, akasema: „panda frasi huyu“. na frasi yule amefundishwa kupiga nyama, frasi wa Kirgis, huenda kama tiyyara. ukisema neno kidogo — marra hukimbia. na miye sikujua, kamà frasi wa kupiga nyama. tulipokwenda mwendo wa nuṣṣu saʿa, tukaona paḥali pana pembe. akanambia bana wangu: „nenda katazame, labda ile ya nyama wetu tuliyopiga“. nikampiga frasi kwenda kutazama, nikakuta si pembe

yetu. na bana wangu amekwisha kwenda mbali sana. mimi nimekaa nyuma, nikataka kumpiga shoti, aende upesi frasi, nimfikie bana wangu, lakini frasi wa Sibirien ukiwapiga — hawaendi, wenyewe wana maneno yao wanayosema na frasi. na frasi ukisema naye neno la kwendea upesi, ma'ana „tshu", hukimbia sana. na miye nikasema „tshu!" frasi akakimbia mbio katika vilima ḥatta nikamfika bana wangu. nilipomfikia bana wangu, nalitaka kumzuia frasi, sikuweza kumzuia, tukampita bana wangu. akawacha njia, akapanda vilima, tukenda mbali sana. bana wangu akat͟hanni, kama atanitupa frasi. nikamwachia kutazama huko anakotaka kwenda. ḥatta tukafika mbali kwenyi majani na miti, nikafanya 'aqili. kwani nilikaza zile khatamu zake ḥatta zikataka kukatika, lakini hasikii kabisa, nikamrejeza kama nikimtaka rudisha upande mwingine — akanyamaza. bana wangu akasimama kuningojea, na wale Kalamik walikuja kunitafuta. niliporudi, bwana wangu akanicheka, akanambia — kama: „sasa unajua ta'abu ya frasi". waqati ule nalijua, kama frasi yule kweli frasi wa kupigia nyama.

nilipowambia wenyewe Kirgis, wakanambia, kama frasi wa kukamatia mbwa wa mwitu. wakenda na wale frasi kupiga nyama, hawaḥitaji kupiga bunduqi, huwafukuza ḥatta wakakanyagwa na frasi.

ḥatta tulipofika paḥali, tukafanya kambi. ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka, tukafunga mizigo yetu. bana wangu akanambia: „tunataka mudda wa sa'a tatu tufike Kashkashi". na kutoka ile kambi ḥatta kufika Kashkashi mwendo wa sa'a saba'. tukaacha safari yetu nyuma, tukapiga frasi wetu, na pamoja na kirongozi wetu tukenda mbio sana, ḥatta mwendo wa sa'a tatu tukafika Kashkashi.

tumekaa siku moja Kashkashi, bana mkubwa akatangulia mbele, akatwambia, ajenge kambi, atungojee. na siye tukafunga mizigo yetu na pembe zetu, tulizopiga,

tupeleke Moskov, na mkulimani moja atangulie na vitu vyetu. na siye tukapita njia nyingine kwenda Semipalatshinski. tukaondoka al-ʿasiri miye na bana wangu, tukenda ḥatta magharibi — hatukuona mtu. tukafika paḥali bana mkubwa alipotwambia, kama atatungojea, lakini hatukumkuta paḥali hapo. tukasema: „twende mbele, labda tutamkuta“. tukenda mwendo wa saʿa tatu saʿa nne za usiku — tusimpate. tukapiga bunduqi na kupiga makelele — lakini hatukumwona. na siye hatuna ḥema, wala hatuna kitu cha kulalia billa silaḥa zetu na frasi wetu bassi.

kirongozi akachukua frasi wake, akenda mbele kwenda kuwatafuta. alipokwenda – hakuona mtu, akarejeʿa paḥali tulipokuwa. na upande ule hapana mtu ḥatta moja, wala hapana nyumba paḥali, kule vilima vya barafu bassi.

tukarejeʿa nyuma, tukenda paḥali tukakuta ḥema moja na kondoo wengi sana na ñgombe na frasi za Kirgis. tukenda tukawaamsha wale Kirgis katika ḥema yao, tukauliza, kama hawakuona safari yetu. wakanena hawakuiona. tukawambia watufanzie paḥali pa kulala. wakatuqurubisha katika ḥema yao.

na wale Kirgis wake wao na watoto wao katika ile ḥema, na ñgombe wadogo na kondoo wadogo wakalala pia ndani ya ḥema. na mlangoni huwa paka wa mwitu kutazama watu. na wale watu wana chawa sana na kunguni. wakatupa nguo zao kujifunika, wakachukua sufuria kubwa sana, wakatia maji kupika, wakachukua chayi. na chayi yao kama jiwe, ngumu sana, hukata kwa visu amma kwa shoka. hupika na chumvi, ndio sukari yao, wakachanganya na maziwa, hupika pamoja. nayo huwa nzito kama uji. wakampa bana wangu kikombe kimoja na miye kikombe kimoja, tunywe, lakini tuliona uchafu sana, hatuwezi kunywa. lakini tukikataa kunywa wataqaṣirika. kulla mtu akanywa kidogo, na

tamu yake kama kinini [1]). tukafikiri tufanye nini ḥatta tusinywe hii chayi! tukafanza kama tunalala na kunywa, tukaimwaga wasione, tukawapa vikombe vitupu wakatupa marra ya pili, tukakataa, tukawambia: „hii yatosha". nao wanaweza kunywa kulla mtu vikombe sitta, hawaoni uchungu.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi tukaondoka tukawapa pauni [2]) moja, wakakataa, kwani hawajui żahabu yao, wala hawajui feḍḍa, illa feḍḍa yao qarṭāsi. nikasema nao kwa kibubu, kuonesha hii záyidi kuliko qarṭasi, khalafu wakachukua. na wale Kirgis waṭaw'a sana, desturi yao ya ṣala hawaachi kabisa, huṣali sana.

tukapanda frasi zetu kwenda kumtafuta bana mkubwa. tukamkuta mtu moja njiani, akaja kututafuta. tukenda ḥatta tukafika kambi ya bana mkubwa, na kule ndio mwisho wa Kalamik. tenna tukaingia katika inchi ya Kirgis. tukenda mwendo wa siku tatu, tukafika katika mwitu wa sala. na sala wa kule wakubwa sana kama frasi. na hawa wapiga nyama wana zumari yao ya mio la sala ya kuitia sala, ma'ana hulia kama sala. sala akisikia huja kama ana wazimu.

bana mkubwa alikwenda kupiga sala, akafuatana na mpiga nyama Kalamik. walipofika mwituni, wamekaa paḥali, akapiga zumari yake marra tatu. marra wàkaona sala, anakuja mkubwa kama frasi, na pembe zake kubwa sana, yapata frásila moja u nuṣṣu. àkampiga, wakareje'a kambini. wakaondosha watu, wakenda kumchukua nyama. nao hufunga na miti, huburura na frasi.

tumekaa siku nne katika kambi kule ya sala, tukaondoka kwenda mbele. na katika inchi ya Kirgis na Kalamik shidda sana kuona mji, huku hapana miji

---

1) Chinin. — 2) pound, ein Goldstück.

kabisa. kazi yao hukaa mwituni na maporini kuchunga nyama wao. nao hawajui paḥali panapozaliwa, sababu huzaliwa maporini.

ḥatta siku ya pili hatuwezi kutazama mbele kwa upepo na barafu. tukajenga kambi juu ya barafu. na shidda moto kuwaka katika ile barafu. tukakaa ḥatta siku ya pili, tukaondoka kwenda zetu. tukenda mwendo wa siku mbili, tukafika paḥali panapo nyumba za Russia na za Kirgisi, wanazokalia, mpaka wa Russia na China. ndipo paḥali tulipokuta watu. hapo haijambo, tulipata vyakula kidogo. kuna barafu sana, ḥatta mito imeganda kwa baridi, huweza mtu kutembea juu ya barafu, asiweze kuanguka ndani ya maji.

tukakaa siku mbili, tukaondoka kwenda zetu Alteiski. tulipoondoka hapo bana wangu alikuwa hawezi sana. nikabaqi nyuma mimi naye, bana mkubwa ametangulia mbele. akenda akajenga kambi, na siye tumebaqi nyuma na Kirgis moja. kulla robo' sa'a hushuka juu ya frasi, hawezi kupanda jissi alivokuwa hawezi. tukenda ḥatta jioni, hatukufika bana mkubwa. tukashikwa na baridi sana. tukenda polepole ḥatta la 'esha, tukakuta watu, walioondoshwa na bana mkubwa, kuja kututafuta. tukafika kambini, tukakaa ḥatta aṣ-ṣubuḥi.

ḥatta siku ya pili mji wa kwanza tukafika ni Alteiski. na Russia wa kule huitwa Kosaki. na ma'ana ya Kosaki — lázima hutumikia serkali ma'isha yake. kwanza anafanya kazi ya 'askari miaka mitatu, khalafu hupata shamba lake la kulima, lakini vilevile huwa katika 'askari. na Kosaki akiwa 'askari, lázima achụkue frasi wake mwenyewe, anunue nguo zake mwenyewe, lakini rukhṣa kulla waqati akitaka, huvuo nguo za serkali.

hapa Alteiski ndio mji wa kwanza tulipokuta gari la frasi. tukaondoka Alteiski kwenda Sikukuminagosko.

walitwambia, kama tutaweza kufika kwa siku kumi, lakini siye tulifanza kwa siku sitta, ma'ana tulikuwa tukenda usiku na mchana. na frasi wa kule wanakwenda sana, ukimpa sais mapesa kidogo bakhshishi huenda sana. lakini walevi sana, kulla mji unaokwenda wamelewa waanawake wao ḥatta watoto wao, hupiga makełele njiani. ḥatta siku moja tumefika paḥali mji mdogo, tukakuta watu wote wamelewa. tulipofika katika nyumba tunamolala, tukawakuta wote wamelewa. akachukua mtu mmoja taa, akataka kumchoma banȧ wangu moto machoni jissi alivolewa. na Mrussia akilewa — hasikii maneno ya mtu.

lakini jissi wanavokwenda katika gari lao la frasi — wana machachare sana. mtu hawezi kutazama mbele kwa vumbi — jissi wanavokwenda upesi, na frasi hawaonekani kwa vumbi. wana maneno yao wakitaka kusema kwenda upesi, akisema „nōnō“ — frasi huenda kama tiyyara.

tulipofika Sikukuminagosko, ndio mji wa kwanza tulipokuta posta na simu. na kutoka mji huu tukaanza kusafiri kwa posta. huweza kununua mtu barua — kulla paḥali utapata frasi, ukilipa paḥali pamoja, ḥatta ufike paḥali utakapo. lakini katika barua hizo użia sana, ma'ana ukenda katika mji — hukupata frasi za posta, huwezi kuondoka, shurṭi ungoje frasi wengine waje. na ukichukua kulla paḥali mapesa, kama hukupata frasi za posta, huweza kuchukua za watu wa shamba, lakini hushika ghali be'i yȧo. na mtu akipewa barua ya frasi tis'a, huweza kutaka frasi thelit'ashara, kulla frasi wa tatu hukuzidishia moja záyidi, na kama hakukupa, huweza ta'arraḍia.

na watu wa kule katika Sikukuminagosko watu wemȧ záyidi kuliko upande mwingine wa kule Altai, wepesi katika safari zao. na maakuli kule mema zá-

yidi kuliko Altai. na hewà kule hubadilika upesi sana, marra utaona jua kali kama kule barra Afrika, na marra huona mvua huona barafu — ni khabari ya ʻajabu kubwa mno. na katika upepo wa kule mbaya sana, unaḏuru watu. kutoka Semipalatshinski ḥatta kufika Werne ḥatta Aulyata ule upepo wa kule wakiona kama unakuja — hawaqubali kusafiri. na ule upepo huitwa „burani".

kutoka Semipalatshinski tukenda siku nne ḥatta mji mwingine. na kulla gari frasi tisʻa. na katika inchi hizi Warussia na Islamu. na mavazi yao ya wale Kirgis ni nguo za ngozi za kondoo min ájili ya bardì nyingi sana. na waanawake hupiga vilemba vya mḥaruma vyeupe. na vyakula vyao ni mno hufanya maandazi ya kiʻarabu. na maji yao ni maziwa ya frasi, jina lake kūmis. na kazi yao kazi ya frasi, n̄gombe na mbuzi, ndio mali yao. na tenna kazi yao kuibiana frasi, wakibadilisha rangi zao. nao wanajua kuandikà kiʻarabu, na kusoma, na kuṣali. na mażehebi yao Hámbali na Hánefi. wao hupenda sana wakiona mtu aliyokhuṣṣa dini yao, amma akitoka katika barra ʻarab — humpenda sana, hutaka kumweka mwʻallimu, ili kuwasomesha. hapana mtu ana rukhṣa ya kuvaa kilemba, illa amekwenda Makka. na inchi yao imeanza tangu Altai ḥatta kufika Werne ḥatta Aulyata, ndio mpaka. nao hawakài sana mjini, hukaa záyidi katika pori na nyama wao. na ʻajabu — ngamia za kule migongo miwili, na kondoo za kule wana pembe kubwa.

kḥalafu tukafika Atropol. kule tumeona vitu vya zamani katika tempel yao. tukakaa siku mbili, khalafu tukaondoka tukenda Kapal. na tulipofika hapo, ṭabiʻa yao ya Kirgisi wa hapa ningine, wao wana biʻashara zao nzuri za maduka. na katika waqati wa ṣala hufunga maduka yao mpaka waṣáli, ndipo wafungue.

nasi tumefika katika nyumba ya sherifu mmoja, na huyu sherifu ndio luwali wa Kapal. alitushika vizuri sana.

tumekaa siku nne, tukasafiri, tukenda zetu Werne. na Werne ni mji mkubwa kidogo kuliko miji hii mingine. na Werne ndio mji wa guverneri. hapa tukakuta watu, waliosema kideutschi, wakatufanzia ḥéshima. na yule guverneri alitufanzia ḥéshima vilevile.

na kutoka Werne ḥatta kufika Taschkend, inaanza užia wa frasi. na tenna njia mbaya sana. tuliposafiri — kulla paḥali tunapofika, tukitaka frasi - hufanziwa užia sana, kwani watu wa kule wanaṭamaʿani sana kupata mapesa. ijapokuwa frasi wako nyumbani, atesema „frasa hapana, kwani hutaka ukae siku nyingi, apate fáyida ya vyakula. walakini kama mtu akiwa na ʿaqili, akifikiri, haqubali kukaa. shurṭi ufanze vishindo ḥatta akupe frasi. na mtu asipokuwa na pass ya guverneri, hawezi kuondoka kabisa katika ile miji, kwani hawampi frasi. na katika safari yetu tulikuwa watu watatu. bana mkubwa huenda mbele mudda wa siku moja, khalafu bana wangu humfuatia nyuma, na miye ndiye nilikuwa wa mwisho, kwani ni kungoja ḥatta wakitangulia mbele na frasi wao. na kulla nnapofika, nikitaka frasi, hunambia — kama: „hapana“. hunambia: „utakaa siku moja ao siku mbili“? na miye nimewafanzia nguvu ḥatta kupata frasi waqati ule niloutaka. miye hujitia wazimu, huwatukana kwa maneno ya kisuaḥeli, humsukuma yule mkulimani kutazama ḥatta tupate frasi.

na Aulyata katika inchi ya Bukhara. na watu wa kule huvaa wote vilemba na juba. nao waṣalḥina sana. nao mashamba yao hulima sana pamba na ḥariri. na kazi yao hufanza mazulia. na katika mazulia mazuri, tuliyoyaona, hutoka upande kule wa inchi ya Bukhara.

kutoka Aulyata kwenda Taschkend waqati ule tukapata njia nzuri ḥatta tumefika Taschkend. katika ule mji mkubwa wana ṭabi'a kidogo ya Ulaya. nao wana bi'ashara sana ya mazulia na vitambaa vya ḥariri.

tukaondoka tukenda Samarkand. tukaona kuna majumba ya zamani ya majáhil, wamefanza meskiti sasa. na qabila za kule zimechanganyika sana. wako Bukhara, ndio wenyi inchi, lakini watu wanaofanya bi'ashara ni Warussia, Kirgisi, Tartari, Turkestani, Ajam, na Farsi. ndio mji tuliopata gari la moshi. tukaingia kwenda Bukhara. Bukhara tukakaa siku tatu. kule huweza kupata watu husema kideutschi na ki'arabu. na kule ndipo anapokaa Amiri wa Bukhara. lakini huyu Amiri sasa hana nguvu sana sababu ya Warussia. na watu wa kule wana bi'ashara nzuri, matájiri; bi'ashara yao mazulia na ngozi za kondoo ndogo [1]). na inchi yao nzuri sana, hawa wa kule nzuri sana.

tukasafiri kule tukenda baḥari Kaspisch, baḥari ya maji ya bardi, lakini ina mawimbi sana. tukasafiri katika meli, tukenda mji wa Baku. na kule Baku ndio paḥali penyi mafuta Ulaya. yanatoka katika arḍi. na ule mji wa Baku áṣili ya watu wa Fars. na ile dini yao ya Farsi, wanaokaa barra hindi, dini yao ya moto, wameanza kule Baku. na katika haya mafuta Ulaya, paḥali panapotoka, viko visima vyapata sitta, nayo hutoka kwa nguvu sana yapata żira'a thelatha mia. nao wamejengea minara ya miti ya kuzuilia nguvu za mafuta yasipotee na upepo. na kulla siku katika yale mafuta wanayopata hupata vibabà kari tatu, ma'ana millioni tatu.

kutoka Baku tumesafiri tukenda Kaukasus, tuka-

1) Persianer.

nasi tumefika katika nyumba y… …kasus ndio vilima huyu sherifu ndio luwali wa K… ya Sham. na katika sana. …ma vizuri sana — ndio

tumekaa siku nne, tr… kule huitwa Tscherkessen, na Werne ni mji mku… waita Búrgia. na kazi yao gine. na Werne nd… sana kufua. nao hodari sana kuta watu, walio… mtu akitupa rupia chini, humpigá na yule guver… inama, akaichukua.

na kut… hapa tukenda Moskau kwa gari la užia wa … kwa njia ya Warschau ḥatta tukafika — ku… ndio khabari yangu ya safari yangu ya užie… ya Sibirien.

* * *

na katika safari zangu zote furaḥa zangu na ta'abu zangu nilizoziona nyingi, lakini miye nikastaḥamili, sababu mwisho wake nimeona ma'ana yake. na miye nimejua khabari nyingi katika dunya, nami nimeona vitu vingi, nisivyopata kuviona katika barra yetu, amma kuvisikia. na sasa namshukuru mweny'ezimuungu na bana doktor Bumiller, niliyokaa naye miaka kumi na miwili, aliyonionyesha dunya. ma'ana safari kama hii na safari zote nilizozifanya naye pamoja — eḥsani kama hiyo asingeweza kunifanzia baba yangu mwenyewe, ijapokuwa ana mali — asingalifanza. wala hawezi kufanya kulla mtu mwenyi mali, yataka mtu mwenyi roḥo njema na imani. na miye tangu kuzaliwa kwangu nimekaa na watu wengi, wamenifanzia njema nyingi na fáḑili, lakini sikupata mtu, aliyonifanzia fáḑili ya bana doktor Bumiller. na aḥsánte yake mweny'ezimuungu ndio atakáyemlipa fáḑili aliyonifanzia, ma'ana mweny'ezimuungu ndio anayeweza kulipa njema, lakini bin Adam hawezi kulipa.

# Orḍa ya khabari zilizomo zote.

(Inhaltsverzeichniss.)

Seite.

Safari yangu ya barra Afrika ya Slēmān bin Mwenyi Tshande bin Mwenyi Ḥamisi esh-Shirazi . . . . . . . . . . 1

Safari yangu ya Nyassa waqati bwana Major von Wissmann alipopeleka stima katika juto la Nyassa ya Selim bin Abakari. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 50

Safari yangu ya Ulaya toka Daressalama ḥatta Berlin ya Selim bin Abakari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106

Safari yangu ya Udoe ḥatta Uzigua na khabari za Wadoe na mila yao inatoka kwa Mtoro bin Mwenyi Bakari. . . . 126

Safari yangu ya Afrika toka baḥari ya suaḥeli ḥatta baḥari ya pili katika safari ya bwana Graf von Götzen ya 'Abdallah bin Rashid . . . . . . . . . . . . . . . . . . 181

Khabari ya inchi ya Wazaramu na dasturi za Wazaramu kama zilizotungwa na Mtoro bin Mwenyi Bakari . . . . . . 205

Safari yangu ya Russia na ya Sibirien niliyofanya pamoja na bwana wangu Dr. Bumiller ya Selim bin Abakari . . . 253

RETURN TO the circulation desk of any
University of California Library
or to the
NORTHERN REGIONAL LIBRARY FACILITY
Bldg. 400, Richmond Field Station
University of California
Richmond, CA 94804-4698

ALL BOOKS MAY BE RECALLED AFTER 7 DAYS
2-month loans may be renewed by calling
(510) 642-6753
1-year loans may be recharged by bringing books to NRLF
Renewals and recharges may be made 4 days prior to due date

DUE AS STAMPED BELOW

MAR 29 1993

APR 27 1995

OCT 23 1998

U.C. BERKELEY LIBRARIES

C020859659